**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23

**MACHI, 2022**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ASA | Wakala wa Mbegu za Kilimo |
| ASDP II | Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo |
| ATC | Chuo cha Ufundi Arusha |
| ATCL | Shirika la Ndege Tanzania |
| ATMIS | Mfumo wa Kutoa Leseni na Vibali |
| BRELA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni |
| BSAAT | Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa Chuo cha |
| BTI | Mafunzo ya Ufugaji Nyuki |
| BTIP II | Backbone Transmission Investment Project - II |
| CAMARTEC | Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini |
| COASCO | Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika |
| CoEATO | Kituo cha Ubora katika eneo la Uendeshaji wa Anga na Usafirishaji |
| COSTECH | Tume ya Sayansi na Teknolojia |
| CPB | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko |
| CUPPS | Mfumo wa kuhudumia Abiria |
| DCF | Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo |
| DIT | Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam |
| DITF | Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam |
| DMDP | Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam |
| DMI | Chuo cha Bandari Dar es Salaam |
| DUCE | Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Dar es Salaam |
| EAC | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| EACOP | Bomba la mafuta ghafi la Uganda –Tanzania |
| e-CAS | Mfumo wa Kukusanyia Takwimu za Uvuvi |
| e-GA | Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| e-HRP | Mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimali Watu |
| EIA | Tathmini ya Athari za Kimazingira |
| EMIS | Mfumo wa Usimamizi wa Elimu |
| e-OPRAS | Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi |
| EP4R | Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu |
| EPZA | Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi |
| ERPP | Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga |
| ESIA | Tathmini ya athari kwa mazingira na jamii |
| ETH | Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi |
| FETA | Taasisi ya Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi |
| FORVAC | Mradi wa Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu |
| FRS | Mfumo wa Kusajili Wakulima |
| GePG | Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali |
| GST | Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania |
| HCMIS | Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya |

| | |
|---|---|
| | Mishahara |
| HESLB | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu |
| HGA | Mkataba wa Nchi Hodhi |
| IDRAS | Mfumo wa Kodi za Ndani |
| IJA | Chuo cha Uongozi wa Mahakama |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| ISTA | Shirika la Kimataifa la Kupima Ubora wa Mbegu |
| JDS | Mfumo wa Uratibu wa Mwenendo wa Mashauri |
| JNIA | Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere |
| KIA | Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro |
| KILP | Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro |
| KNMTC | Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa |
| LITA | Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo |
| LNG | Gesi Asilia (Kimiminika) |
| LSP II | Program ya Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili |
| MMEM | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MTAKUWWA | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto |
| MTDS | Mkakati wa Kusimamia Madeni katika Muda wa Kati |
| MUCE | Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Mkwawa |
| MUSE | Mfumo wa Uhasibu Serikalini |
| MUST | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya |
| NBM | Rajamu ya Taifa |
| NEDF | Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali Wananchi |
| NEEC | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| NEMC | Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira |
| NFRA | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula |
| NIC | Shirika la Bima la Taifa |
| NIDC | Kituo mahiri cha kuhifadhi Data |
| NIT | Chuo cha Taifa cha Usafirishaji |
| NMNAP | Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Lishe |
| NMTC | Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa |
| NPMIS | Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo |
| NSC | Kamati ya Mbegu ya Taifa |
| OECD | Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo na Uchumi |
| OSC | Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja |
| PFMRP | Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma |
| PPP | Ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi |
| PSSSF | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma |
| RBF | Mpango wa Malipo kwa Ufanisi |
| REA | Mfuko wa Nishati Vijijini |

| | |
|---|---|
| REGROW | Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini |
| SELF | Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha |
| SEZ/EPZ | Kanda Maalumu za Kiuchumi |
| SGR | Reli kwa Kiwango cha kimataifa |
| SHA | Mkataba wa Ubia |
| SIDO | Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo |
| SMMRP | Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Madini |
| STAMICO | Shirika la Madini la Taifa |
| SUA | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine |
| SWIOFish | Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi |
| TADB | Benki ya Maendeleo ya Kilimo |
| TAEC | Tume ya Nguvu za Atomiki |
| TAFICO | Shirika la Uvuvi Tanzania |
| TAFIRI | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania |
| TAFICO | Shirika la Uvuvi Tanzania |
| TALIRI | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania |
| TAMCO | Eneo la Kongano la Viwanda |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania |
| TASAF | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii |
| TATC | Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania |
| TBC | Shirika la Utangazaji Tanzania |
| TBS | Shirika la Udhibiti Ubora wa Bidhaa Tanzania |
| TCRA | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| TCRF | Jukwa la Haki za Watoto Tanzania |
| TDCs | Vituo vya Kuendeleza Teknolojia |
| TEA | Mamlaka ya Elimu Tanzania |
| TEMDO | Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo |
| TESP | Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu |
| TGC | Kituo cha Jimologia |
| TIRDO | Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania |
| TOSCI | Taasisi ya Uthibiti wa Mbegu |
| TPRI | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki |
| TPSF | Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini |
| TSHTDA | Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai |
| TTCL | Shirika la Mawasiliano Tanzania |
| UTT - AMIS | Unit Trust of Tanzania – Asset Management and Investment Services |
| UVIKO-19 | Ugonjwa wa Virusi vya Korona - 19 |

## YALIYOMO


SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.1 Usuli ..... 1
1.2 Miradi ya Kipaumbele ..... 1
1.3 Mawanda ya Mpango ..... 1
1.4 Ushirikishwaji wa Wadau ..... 2
1.5 Mpangilio wa Kitabu ..... 2

SURA YA PILI ..... 3
HALI YA UCHUMI ..... 3
2.1. Utangulizi ..... 3
2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi ..... 3
2.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia ..... 3
2.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ..... 3
2.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ..... 3
2.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ..... 4
2.2.5. Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ..... 4
2.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa ..... 5
2.3.1. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ..... 5
2.3.2. Mfumuko wa Bei ..... 6
2.3.3. Sekta ya Nje ..... 8
2.3.4. Deni la Serikali ..... 9
2.3.5. Sekta ya Fedha ..... 10
2.4. Maendeleo ya Watu ..... 14
2.4.1 Ongezeko la Idadi ya Watu ..... 14
2.4.2 Viashiria vya Maendeleo ya Watu ..... 14
2.4.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ..... 15
2.4.2.2 Upatikanaji wa Chakula ..... 15

SURA YA TATU ..... 17
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ..... 17
3.1 Utangulizi ..... 17
3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22 ..... 17
3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ..... 17
3.3.1 Miradi ya Kielelezo ..... 17
3.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ..... 21
3.3.2.1 Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma ..... 21
3.3.2.2 Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ..... 38
3.3.2.3 Mapinduzi ya TEHAMA ..... 46
3.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ..... 48
3.3.3.1 Uzalishaji Viwandani ..... 48
3.3.3.2 Huduma za Biashara ..... 53

3.3.3.3 Masoko ... 54
3.3.3.4 Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II ... 55
3.3.3.5 Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia ... 66
3.3.3.6 Huduma ... 66
3.3.4 Kukuza Biashara na Uwekezaji ... 73
3.3.4.1 Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji ... 73
3.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu ... 75
3.3.5.1 Afya ... 75
3.3.5.2 Ustawi na Maendeleo ya Jamii ... 85
3.3.5.3 Elimu ... 88
3.3.5.4 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ... 95
3.3.5.5 Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ... 96
3.3.5.6 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ... 98
3.3.5.7 Usimamizi wa Maafa Nchini ... 101
3.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu ... 102
3.3.6.1 Ujuzi na Uwezeshaji ... 102
3.3.7 Maeneo Mengine Yaliyopewa Kipaumbele ... 103
3.3.7.1 Utamaduni, Sanaa na Michezo ... 103
3.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ... 104
3.3.7.3 Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma ... 105
3.3.7.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ... 105
3.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo ... 106
3.4.1 Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2021/22 ... 106
3.4.2 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2021/22 ... 106
3.4.3 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto ... 107

SURA YA NNE ... 108
MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2022/23 ... 108
4.1 Utangulizi ... 108
4.2 Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ... 108
4.2.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ... 108
4.2.2 Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2022/23 ... 108
4.3 Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2022/23 ... 108
4.3.1 Miradi ya Kielelezo ... 108
4.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi ... 111
4.3.2.1 Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji ... 111
4.3.2.1.1 Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma ... 111
4.3.2.2 Mapinduzi ya TEHAMA ... 130
4.3.2.3 Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi ... 132
4.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma ... 138
4.3.3.1 Uzalishaji Viwandani ... 138
4.3.3.2 Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia

ASDP II ........................................................................ 143
4.3.3.3 Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia ........ 152
4.3.3.4 Huduma........................................................................ 152
4.3.4 Kukuza Biashara na Uwekezaji ........................................... 155
4.3.4.1 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji .. 155
4.3.4.2 Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi............................. 156
4.3.4.3 Kukuza Sekta Binafsi........................................................ 156
4.3.4.4 Huduma za Biashara na Masoko ........................................ 157
4.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu .......................................... 158
4.3.5.1 Afya ............................................................................. 158
4.3.5.2 Ustawi na Maendeleo ya Jamii........................................... 162
4.3.5.3 Elimu ........................................................................... 165
4.3.5.4 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ....... 172
4.3.5.5 Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira .............................. 173
4.3.5.6 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ...................................................................... 176
4.3.5.7 Hifadhi ya Jamii ............................................................. 178
4.3.5.8 Usimamizi wa Maafa Nchini .............................................. 178
4.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu ............................................... 179
4.3.7 Maeneo Mengine ya Kipaumbele ......................................... 180
4.3.7.1 Utamaduni, Sanaa na Michezo .......................................... 180
4.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ................................. 182
4.3.7.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ..................... 183

SURA YA TANO ............................................................................ 184
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2022/23 .................. 184
5.1 Utangulizi.............................................................................. 184
5.2 Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2022/23 .. 184
5.3 Mikakati ya Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2022/23184
5.3.1 Mapato ya Ndani.................................................................. 184
5.3.1.1 Mapato ya Kodi na Yasiyo Kodi.......................................... 184
5.3.2 Mikopo na Misaada ya Nje..................................................... 185
5.3.2.1 Misaada ya Nje................................................................ 185
5.3.2.2 Mikopo ya Nje................................................................. 186
5.3.3 Mikopo ya Ndani ................................................................. 186
5.4 Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo............. 186

SURA YA SITA ............................................................................. 188
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA.................................... 188
6.1 Utangulizi.............................................................................. 188
6.2 Misingi ya Ufuatiliaji na Tathmini .............................................. 188
6.3 Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ............................................................. 189
6.4 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini.............................................. 189

6.5 Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ........................................ 190
6.6 Mgawanyo wa Majukumu ........................................ 190
6.6.1 Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu (IMTC) ........................................ 190
6.6.2 Wizara ya Fedha na Mipango ........................................ 190
6.6.3 Ofisi ya Taifa ya Takwimu ........................................ 190
6.6.4 Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma ........................................ 190
6.6.5 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) ........................................ 191
6.6.6 Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia ........................................ 191

SURA YA SABA ........................................ 192
VIHATARISHI NA HATUA ZA KUKABILIANA NAVYO ........................................ 192
7.1 Utangulizi ........................................ 192
7.2 Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo ........................................ 192

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli
Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni ya Pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 wenye dhima ya *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu* ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2021/22. Lengo la Mpango huu ni kuendeleza juhudi za kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuweka mkazo katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu.

Mpango umeandaliwa kwa mujibu wa matakwa ya Ibara ya 63 (3) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 116 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020.

Aidha, Maandalizi ya Mpango yamezingatia miongozo mbalimbali ya kisera, kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo ni: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 2050; Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

## 1.2 Miradi ya Kipaumbele
Miradi itakayotekelezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni miradi katika maeneo matano (5) ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa ambayo ni (i) Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi (ii) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma (iii) Kukuza Biashara na Uwekezaji (iv) Kuchochea Maendeleo ya Watu na (v) Kuendeleza Rasilimali Watu. Msisitizo umewekwa katika miradi ya kielelezo ambayo ni ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), ujenzi wa mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115, Bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga eneo la Chongoleani na Ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania.

## 1.3 Mawanda ya Mpango
Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 yanajumuisha: Malengo na shabaha za Mpango na Bajeti ya 2022/23; miradi ya kipaumbele kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; mfumo wa ugharamiaji; wajibu wa sekta ya umma na binafsi na mgawanyo wa majukumu katika utekelezaji; na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango.

## 1.4 Ushirikishwaji wa Wadau

Maandalizi ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 yameshirikisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, Washirika wa Maendeleo wameshirikishwa kupitia majadiliano katika maeneo mahsusi ya ushirikiano, ufadhili wa miradi ya maendeleo na programu za kisekta.

## 1.5 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mpango kimegawanyika katika sura saba (7): Sura ya kwanza ni utangulizi; Sura ya pili inaainisha mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya tatu inaelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2021/22; Sura ya nne inaelezea miradi ya kipaumbele kwa mwaka 2022/23; Sura ya tano inaelezea ugharamiaji wa Mpango; Sura ya sita inaainisha mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango; na Sura ya saba ni vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na hatua za kukabiliana navyo.

## SURA YA PILI

## HALI YA UCHUMI

### 2.1. Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa muhtasari mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi, maendeleo ya watu katika mwaka 2021 na mwelekeo kwa mwaka 2022. Mwenendo wa viashiria hivi unajenga msingi wa malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Baadhi ya viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: Pato la Taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo idadi ya watu na hali ya umaskini nchini.

### 2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi

#### 2.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa Dunia ilipungua kutoka ukuaji wa asilimia 2.8 mwaka 2019 hadi ukuaji hasi wa asilimia 3.1 mwaka 2020. Sababu kubwa ya kushuka kwa ukuaji wa uchumi wa dunia ilisababishwa na athari za Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19) ambako ilipelekea kwa nchi nyingi kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege za abiria na kupiga marufuku mikusanyiko ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa. Hali hii ilisababisha kuvurugika kwa mfumo wa biashara, uzalishaji na uhitaji wa huduma. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Januari 2022, uchumi wa dunia uliimarika na kufikia ukuaji wa asilimia 5.9 mwaka 2021 na unatarajiwa kuwa asilimia 4.4 mwaka 2022. Kuimarika kwa uchumi wa dunia kutatokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na nchi mbalimbali katika kuimarisha uchumi, ikiwemo utekelezaji wa sera za fedha na bajeti zinazochochea shughuli za uchumi zilizoathirika na kuendelea kuimarishwa kwa huduma za afya ikiwemo usambazaji wa chanjo kwa lengo la kupunguza athari za UVIKO-19.

#### 2.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea ilipungua kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2019 hadi ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2020. Aidha, nchi zilizoendelea zinatarajiwa kuimarika kiuchumi na kufikia ukuaji wa asilimia 5.0 mwaka 2021 na asilimia 3.9 mwaka 2022. Matarajio hayo yanatokana na sera za kifedha na kibajeti zenye lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi pamoja na kuimarika kwa usambazaji wa chanjo ya UVIKO-19 hivyo kuwezesha raia wengi kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

#### 2.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi uliporomoka kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2019 hadi ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2020. Aidha, uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi unatarajiwa kuimarika na kufikia asilimia 6.5 mwaka 2021 na asilimia 4.8 mwaka 2022.

Vile vile, ukuaji wa uchumi katika nchi za Asia Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ikijumuisha China na India ulikuwa asilimia hasi 0.8 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2019. Nchi hizo zinatarajia kuwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2021 na asilimia 5.9 mwaka 2022 mtawalia.

### 2.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ilipungua kutoka ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2019 hadi ukuaji hasi wa asilimia 1.7 mwaka 2020. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari za mlipuko wa UVIKO-19 pamoja na kushuka kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia mwanzoni mwa mwaka 2021 hivyo kuathiri nchi ambazo chumi zake zinategemea mafuta kuingiza mapato. Matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2021 na ukuaji wa asilimia 3.7 mwaka 2022. Matarajio haya yanatokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa ili kuimarisha ukuaji wa uchumi ikiwemo kuboresha huduma za afya. **Jedwali 2.1** linaonesha mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia.

**Jedwali 2.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Matarajio**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | | Matarajio (asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
| Dunia | 3.8 | 3.5 | 2.8 | -3.1 | 5.9 | 4.4 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.4 | 2.2 | 1.7 | -4.5 | 5.0 | 3.9 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 4.8 | 4.5 | 3.7 | -2.1 | 6.5 | 4.8 |
| Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara | 2.9 | 3.3 | 3.1 | -1.7 | 4.0 | 3.7 |

***Chanzo:** Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Januari, 2022*

### 2.2.5. Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2020 katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki haukuathiriwa kwa kiwango kikubwa na mlipuko wa UVIKO-19 ikilinganishwa na kanda nyingine. Kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutoka ukuaji wa asilimia 5.4 mwaka 2019 hadi asilimia 2.3 mwaka 2020. Kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutokana na mwenendo usioridhisha wa biashara na shughuli za kiuchumi kulikosababishwa na hatua zilizochukuliwa na baadhi ya nchi wanachama kukabiliana na mlipuko wa UVIKO-19. Sababu hizo ni pamoja na kuzuia safari za ndege za abiria, kuhimiza watu kubaki majumbani, kufunga mipaka ya nchi na kupiga marufuku mikusanyiko ya watu. Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2020 zilikuwa na kasi ya ukuaji wa uchumi kama ifuatavyo: Tanzania asilimia 4.8; Rwanda asilimia hasi 3.4; Uganda asilimia hasi 0.8; Burundi asilimia hasi 1.0; Sudani Kusini asilimia hasi 6.6; na Kenya asilimia hasi 0.3. Uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unatarajiwa kukua na kufikia asilimia 4.6 mwaka 2021. Hii ni kutokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na nchi wanachama ikiwemo za kisera na kuboresha huduma za afya ili

kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19.

**Jedwali Na.2.2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

| Nchi | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 |
| Tanzania | 6.8 | 7.0 | 7.0 | 4.8 |
| Kenya | 3.8 | 5.6 | 4.9 | -0.3 |
| Uganda | 6.8 | 5.6 | 9.5 | -3.4 |
| Rwanda | 4.0 | 8.6 | 3.1 | -1.7 |
| Burundi | 0.5 | 1.6 | 1.8 | -1.0 |
| Sudani ya Kusini | -5.6 | -1.9 | 0.9 | -6.6 |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Ofisi za Takwimu za Nchi husika*


## 2.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 2.3.1. Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Ukuaji wa uchumi wa Taifa katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2021 ulikuwa asilimia 4.9 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2020 (**Kielelezo Na. 1**). Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji kumetokana na jitihada mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo utekelezaji wa mpango wa kukabiliana na athari hasi za UVIKO-19 na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Baadhi ya shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa katika kipindi hicho ni pamoja na madini (asilimia 10.9), habari na mawasiliano (asilimia 10.2), huduma nyingine za kijamii (asilimia 9.8), umeme (asilimia 9.7) na maji (asilimia 7.0). Shughuli zilizokuwa na ukuaji mdogo katika kipindi hicho ni pamoja na kilimo (asilimia 2.7) na biashara na matengenezo (asilimia 3.6). Shughuli nyingi za kiuchumi zimeendelea kuwa na viwango chanya vya ukuaji ingawa kasi yake ilipungua ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2020.

**Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa Katika Kipindi cha Januari hadi Septemba (2017 – 2021)**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### 2.3.2. Mfumuko wa Bei

**(a) Mfumuko wa Bei Nchini**


Mfumuko wa Bei umeendelea kuwa ndani ya lengo la wigo wa asilimia 3 hadi 5. Mwaka 2021, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.7 kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 katika kipindi cha mwaka 2020. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Msingi[1] *(Core Inflation)* kufikia asilimia 4.1 mwaka 2021 kutoka asilimia 2.3 mwaka 2020. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.2 Desemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.2 Desemba 2020.

Wastani wa Mfumuko wa Bei wa Bidhaa za Vyakula na Vinywaji Baridi ulipungua hadi asilimia 4.2 mwaka 2021 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2020. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za vyakula kwenye masoko ya ndani. Vile vile, Mfumuko wa Bei usiojumuisha vyakula na nishati ulifikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na asilimia 2.3 mwaka 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula na nishati zikiwemo saruji na mafuta ya kupikia kulikosababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa hizo nchini.

---

[1] Mfumuko wa Bei wa bidhaa za msingi hukokotolewa kutoka Fahirisi za bei za msingi zinazoandaliwa kwa kutojumuisha bidhaa za vyakula zisizochakatwa; nishati na ankara za maji. Kutojumuisha bei za bidhaa ambazo zina sifa ya kubadilika mara kwa mara kwenye Fahirisi za bidhaa na huduma zote, hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa Watunga Sera.

**Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini (Januari 2020 hadi Desemba 2021)**




Chanzo: *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Aidha, hali inayoendelea ya kuongezeka kwa bei za bidhaa mbalimbali imechangiwa na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali ikijumuisha:

(i) Kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia kutokana na athari za UVIKO-19;

(ii) Kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la ndani kutokana na kuongezeka kwa bei na gharama za usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka nje, hususan bidhaa za petroli, mafuta ya kula, mbolea, chuma na malighafi za viwandani. Mathalan, bei za bidhaa za mafuta ghafi (crude oil) ilifikia dola za Makerekani 87.4 kwa pipa Januari 31, 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani 72.6 kwa pipa Julai 1, 2021. Hata hivyo mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuongezeka kutoka na vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine;

(iii) Kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma, hususan vifaa vya ujenzi ikilinganishwa na uwezo wa uzalishaji katika viwanda vya ndani; na

(iv) Kupungua kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya ndani kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli.

Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti mfumuko wa bei katika soko la ndani, ikiwemo:

(i) Kuchochea na kuhamasisha uzalishaji na usambazaji wa mazao ya muda mfupi, hususan maharage, mbogamboga, mbegu za mafuta ya alizeti na pamba;

(ii) Kuchochea na kuhamasisha uzalishaji na usambazaji wa baadhi ya vifaa vya ujenzi katika viwanda vya ndani ili kuendana na mahitaji ya soko;

(iii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sera za bajeti na fedha ili kudhibiti mzunguko wa fedha katika uchumi;

(iv) Kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mnyororo wa uzajishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma katika soko la dunia ili kufungamanisha na mahitaji ya soko la ndani; na

(v) Kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ili kupunguza gharama za usfirishaji wa bidhaa na huduma; na

(vi) Kuongeza na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji ili kupunguza utegemezi wa mvua katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

**(b) Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki**

Mfumuko wa bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipungua kutoka wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2020 hadi asilimia 4.1 mwaka 2021. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulitokana na kuimarika kwa uzalishaji wa chakula kwa baadhi ya nchi wanachama na kupungua kwa mahitaji ya mafuta. Aidha, viwango vya mfumuko wa bei vya nchi wanachama vilikuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko usiozidi asilimia 8. **Jedwali Na. 2.3.** linaonesha Mfumuko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**Jedwali Na. 2.3: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2020 na 2021**

| **Nchi** | **Mfumuko wa Bei (Asilimia)** | |
|---|---|---|
| | **2020** | **2021** |
| Tanzania | 3.3 | 3.7 |
| Uganda | 3.7 | 2.2 |
| Kenya | 5.4 | 6.1 |
| Rwanda | 8.6 | 0.8 |
| Burundi | 7.4 | 7.5** |
| Sudani ya Kusini | NA | NA |
| **Wastani kwa Afrika Mashariki*** | 5.7 | 4.1 |

**Chanzo**: *Ofisi za Taifa za Takwimu za Nchi Husika*

**NA**: Hakuna takwimu

***** Wastani kwa Afrika Mashariki bila kujumuisha nchi ya Sudani ya Kusini.

****** Wastani kwa nchi ya Burundi mwaka 2021, umekokotolewa kufikia Oktoba 2021.

### 2.3.3. Sekta ya Nje

**(a) Urari wa Malipo ya Kawaida**

Urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 2,032.3 mwaka 2021, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,122.0 mwaka 2020. Hii ilitokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

**(b) Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma**

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 9,918.6 mwaka 2021, kutoka dola za Marekani milioni 8,555.5 mwaka 2020.

Mauzo ya bidhaa zisizo asilia yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 5,763.0 kutoka dola za Marekani milioni 5,253.3 mwaka 2020 kutokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani, mbogamboga, na bidhaa nyinginezo. Aidha, mauzo ya dhahabu nje ya nchi yalikuwa dola za Marekani milioni 2,743.1 mwaka 2021 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,957.5 mwaka 2020, hali iliyochangiwa zaidi na kupungua kwa bei katika soko la dunia. Mauzo ya bidhaa asilia yalipungua na kufikia dola za Marekani milioni 627.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 808.1 mwaka 2020.

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 11,744.4 mwaka 2021 kutoka dola za Marekani milioni 9,181.0 mwaka 2020. Hali hii ilichangiwa zaidi na kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa mafuta kutoka nje kufuatia kuongezeka kwa bei katika soko la dunia.

**(c) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosheleza kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Desemba 2021, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 6.4, kiasi kinachotosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 6.6. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, pamoja na lengo la miezi 6.0 kwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

### 2.3.4. Deni la Serikali

Hadi Desemba 2021, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 68,520.79 ikilinganishwa na shilingi bilioni 58,684.4 kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 16.8. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 47,399.46 na deni la ndani ni shilingi bilioni 21,121.33. Mwenendo huu wa deni ulitokana na kupokelewa kwa mikopo kutoka vyanzo vyenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya. Aidha, ongezeko hilo la deni pia limetokana na kutolewa kwa hatifungani maalumu yenye thamani ya shilingi bilioni 2,176.74 kwa ajili ya kulipa deni la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) linalohusu michango ya watumishi waliokuwa kwenye utumishi kabla ya mwaka 1999.

Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Novemba 2021 imeonesha kuwa pamoja na uwezo wa nchi wa kubeba deni (country’s debt carrying capacity) kushuka kutoka strong performer kuwa moderate, deni la Serikali ni himilivu katika muda mfupi, wa kati na muda mrefu. Aidha, kushuka kwa uwezo wa nchi kubeba deni lake kwa kiasi kikubwa ni kutokana na kushuka kwa uchumi wa dunia kwa ujumla ambapo karibu nchi zote za kusini mwa Jangwa la Sahara uwezo wa kubeba deni umeshuka. **Jedwali Na. 2.4** linaonyesha Matokeo ya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni kwa Mwaka 2021.

**Jedwali Na. 2.4: Matokeo ya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni kwa Mwaka 2021**

| Viashiria | Ukomo Kabla ya Mapitio | Ukomo | 20/21 | 21/22 | 22/23 | 23/24 | 24/25 | 25/26 | 26/ 27 | 31/ 32 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Deni la Nje (Asilimia)** | | | | | | | | |
| Uwiano wa thamani halisi ya Deni kwa Pato la Taifa | 55 | 40 | 18.8 | 18.8 | 18.7 | 18.8 | 18.8 | 18.5 | 18.4 | 20.2 |
| Uwiano wa thamani halisi ya Deni kwa Mauzo ya Nje ya Nchi | 240 | 180 | 142.4 | 132.9 | 117.4 | 108.5 | 102.8 | 96.9 | 93.7 | 95.7 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mauzo ya Nchi | 21 | 15 | 14.8 | 14.9 | 11.5 | 9.4 | 9.2 | 9.2 | 7.7 | 9.4 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | 23 | 18 | 14.6 | 14.2 | 12.1 | 10.6 | 10.9 | 11.3 | 9.6 | 12.1 |
| | | **Deni la Ndani na Nje (Asilimia)** | | | | | | | | |
| Uwiano wa Thamani Halisi ya Deni kwa pato la Taifa | 70 | 55 | 31 | 31.8 | 31.8 | 31.5 | 30.7 | 29.4 | 29 | 33 |
| Uwiano wa Thamani Halisi ya Deni kwa Mapato | N/A | N/A | 224.9 | 206.2 | 201.9 | 198.3 | 191.8 | 181.8 | 179.4 | 199.3 |
| Uwiano wa Ulipaji wa Deni kwa Mapato | N/A | N/A | 36.2 | 32.4 | 31.2 | 27.4 | 25.6 | 23 | 20.6 | 26.3 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha na Mipango, 2022*

### 2.3.5. Sekta ya Fedha

### (a) Ujazi wa Fedha na Karadha

Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha kwa ajili ya kufanikisha malengo mapana ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali ikiwa ni pamoja na utulivu wa mfumuko wa bei na kudumisha ukuaji wa uchumi shirikishi. Katika mwaka 2021, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye mfumo wa kibenki ili kukidhi mahitaji halisi ya kiuchumi na kupunguza athari za janga la UVIKO-19 kwenye uchumi. Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha, pia ulilenga kuwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza utoaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi na kudumisha utulivu wa riba kwenye masoko ya fedha.

Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, ujazi wa fedha umeendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha, kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha iliyosaidia kufufua shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizodorora kutokana na UVIKO-19. Katika kipindi hicho, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikuwa kwa wastani wa asilimia 10.2 ikilinganishwa na asilimia 8.8 mwaka 2020. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na ongezeko la rasilimali fedha za kigeni katika sekta ya benki na kuendelea kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

### (b) Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi

Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua, ijapokuwa kwa kasi ndogo kwenye baadhi ya biashara na shughuli za uwekezaji kutokana na athari za UVIKO-19. Katika mwaka 2021, wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulikuwa asilimia 4.7, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2020. Aidha, kasi ya ukuaji mikopo kwa sekta binafsi imeanza kuimarika katika miezi ya hivi karibuni na kufikia asilimia 10.0 kwa mwaka ulioishia Desemba 2021. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kunatokana na utekelezaji madhubuti wa sera wezeshi ya fedha yenye kuongeza ukwasi katika uchumi kwa gharama nafuu, pamoja na hatua za ziada za kisera zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kupitia Benki Kuu. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuelekezwa kwenye shughuli binafsi (shughuli za wajasiriamali wadogo na

wa kati), biashara, uzalishaji viwandani, pamoja na kilimo.

Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi unatarajiwa kuendelea kuimarika katika kipindi cha mwaka 2022, sanjari na utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi, sheria ya bajeti, pamoja na utekelezaji wa hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu mwezi Julai 2021 kwa lengo la kuchochea ukuaji wa mikopo na kushusha viwango vya riba za mikopo kwa sekta binafsi.

**(c) Mwenendo wa Viwango vya Riba**

Kufuatia mwendelezo wa utekelezaji wa sera ya fedha yenye kuongeza ukwasi kwenye uchumi, wastani wa riba za mikopo inayotolewa na benki na taasisi za fedha imeendelea kupungua. Riba ya mikopo imepungua na kufikia wastani wa asilimia 16.59 katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 16.66 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, riba ya mikopo ilifikia asilimia 16.37 mwezi Desemba 2021, ikilinganishwa na asilimia 16.74 Desemba 2020. Kupungua kwa riba za mikopo kumechangiwa na usimamizi wa hatua mbalimbali za kupunguza riba na mikopo chechefu, ikiwemo matumizi ya kanzidata ya taarifa ya kumbukumbu za wakopaji, pamoja na usimamizi wa maadili ya kiutendaji ya watumishi kama yalivyoainishwa na Chama cha Mabenki Tanzania. Wastani wa riba za amana katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, ilikuwa asilimia 6.85 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.70 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Aidha, riba za amana ilifikia asilimia 6.79 mwezi Desemba 2021, ikilinganishwa na asilimia 7.09 Desemba 2020.

**(d) Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya sarafu za nchi washirika wakuu wa kibiashara katika kipindi chote cha kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2021. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na utulivu wa bei nchini, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa urari wa biashara ukichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu nje ya nchi, kuendelea kuimarika kwa shughuli za utalii pamoja na kuwepo kwa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.13 ikilinganishwa na shilingi 2,305.58 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

**(e) Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki**

Sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Viwango vya amana na rasilimali vimeendelea kuongezeka na kuimarisha sekta ya benki dhidi ya misukosuko ya ndani na nje. Uwiano wa mtaji wa msingi wa sekta ya benki ukilinganishwa na jumla ya rasilimali ilifikia asilimia 19.5 Desemba 2021, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha kisheria cha asilimia 10.0 na asilimia 17.2 Desemba 2020. Aidha, uwiano wa ukwasi wa sekta ya benki kiujumla *(Liquid Assets to Demand Liabilities)* umeendelea kubakia kwenye kiwango cha juu kutosheleza mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kubaki katika wastani wa zaidi ya asilimia 30 katika kipindi chote cha mwaka 2021 na 2020, ikilinganishwa na kiwango cha chini cha

kisheria cha asilimia 20.0. Sekta ya benki imeendelea kutengeneza faida, ambapo faida ya benki itokanayo na mali ilikuwa asilimia 2.8 Desemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 1.9 Desemba 2020. Vile vile, faida ya benki itokanayo na mtaji iliongezeka kufikia asilimia 11.6 Desemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 7.1 Desemba 2020.

**(f) Mikopo Chechefu**

Ubora wa rasilimali za benki umeendelea kuimarika, kutokana na kupungua kwa uwiano wa mikopo chechefu kwenye mikopo yote kufikia asilimia 8.2 mwezi Desemba 2021, kutoka asilimia 9.8 Desemba 2020. Hali hii ilichangiwa zaidi na ongezeko la urejeshaji wa mikopo pamoja na kufutwa kwa baadhi ya mikopo chechefu. Hata hivyo, pamoja na kupungua kwa kiwango cha mikopo chechefu, bado kiwango hicho ni kikubwa zaidi ya kiwango kinachokubalika na Benki Kuu cha asilimia 5. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kupunguza kiwango cha mikopo chechefu ikijumuisha kuzitaka benki na taasisi za fedha kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo, kuwasilisha mkakati wa kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zenye uwiano mkubwa; na kuhamasisha matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji *(credit reference system)* katika utoaji wa mkopo. Aidha, hatua za sera za fedha na bajeti zilizotekelezwa katika kupunguza athari za UVIKO-19 katika uchumi zilijumuisha utoaji wa unafuu wa mahitaji ya usimamizi katika kufanya marekebisho ya marejesho ya mikopo *(loan restructuring)*. Vile vile, Benki Kuu ilitoa tamko Februari 2021 kuzielekeza benki za biashara kusitisha utoaji wa gawio au motisha (bonuses) kwa wanahisa au wafanyakazi endapo mikopo chechefu itazidi asilimia 5.0 ambalo limeendelea kusimamiwa kikamilifu. Lengo ni kuhakikisha sekta ya benki inaongeza ufanisi katika uendeshaji wa shughuli zake, kuongeza matumizi ya teknolojia na kupunguza gharama ambazo nyingi hubebwa na wateja kupitia riba hali ambayo imekuwa ikisababisha kuongezeka kwa mikopo chechefu.

**(g) Soko la Upili la Hatifungani**

**Hatifungani za Serikali**

Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 20.70 na kufikia shilingi trilioni 2.56 katika kipindi cha mwaka kilichoishia Desemba 2021 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi trilioni 2.12 katika kipindi cha mwaka kilichoishia Desemba 2020. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Serikali kumechangiwa na ushiriki wa wawekezaji kwenye masoko ya mitaji nchini kufuatia elimu inayotolewa kwa umma kuhusu fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji. Aidha, kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Serikali kumetokana na wawekezaji kuhamisha uwekezaji kutoka kwenye uwekezaji unaoweza kupata athari za kiuchumi *(perceived economic risk)* na kuwekeza kwenye uwekezaji salama zaidi yaani *risk free* ambao unahusisha hatifungani za Serikali.

**Hatifungani za Kampuni *(Corporate Bonds)***

Mauzo ya hatifungani za Kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1.45, sawa na ongezeko la asilimia 11.05

katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.31 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020. Ongezeko hilo lilitokana na wawekezaji kupata elimu ya masuala ya uwekezaji na fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji na dhamana.

**Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Collective Investment Schemes) katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 ulikuwa wa kuridhisha. Thamani ya uwekezaji katika mifuko sita (6) ya uwekezaji wa pamoja inayoendeshwa na kampuni ya UTT AMIS iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 744.93 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 476.98 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020 sawa na ongezeko la asilimia 56.18. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji. **Jedwali Na. 2.5** linaonesha mwenendo wa uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

**Jedwali Na. 2.5: Mwenendo wa Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

| | **31 Desemba 2020** | | **31 Desemba 2021** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jina la Mfuko | Thamani ya Mfuko (TZS Bilioni) | Bei ya Kipande | Thamani ya Mfuko (TZS Bilioni) | Bei ya Kipande | Ongezeko la Thamani ya Mfuko (%) | Ongezeko la Bei ya Kipande (%) |
| Umoja Fund | 237.36 | 675.96 | 269.46 | 776.68 | 13.52 | 14.90 |
| Wekeza Maisha | 1.43 | 530.57 | 2.54 | 659.45 | 77.62 | 24.29 |
| Watoto Fund | 3.68 | 404.81 | 4.60 | 483.45 | 25.00 | 19.43 |
| Jikimu Fund | 17.96 | 140.53 | 17.32 | 151.52 | -3.56 | 7.82 |
| Liquid Fund | 152.62 | 263.63 | 304.34 | 302.44 | 99.41 | 14.72 |
| Bond Fund | 63.93 | 107.70 | 146.67 | 111.65 | 129.42 | 3.67 |
| Jumla | **476.98** | | **744.93** | | **56.18** | |

*Chanzo: UTT AMIS Plc*

**Mwenendo wa Masoko ya Mitaji**

Mwenendo wa biashara katika soko la hisa hupimwa kwa kuzingatia viashiria vya ufanisi wa soko. Viashiria hivyo ni pamoja na: Thamani ya Mauzo ya hisa; Mtaji wa Soko (Market Capitalisation); Fahirisi za Soko (Share Index); na ushiriki kwenye Soko la Hisa.

Katika kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Desemba 2021 Soko la Mitaji na Dhamana limeendelea kufanya vizuri ambapo thamani ya mauzo ya hisa na hatifungani za Serikali na kampuni yameongezeka. Aidha, mtaji wa Soko na Fahirisi za Soko zimeongezeka. Ufanisi huo umetokana na juhudi kubwa za Serikali katika kutoa elimu ya masuala ya uwekezaji na fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji na dhamana.

**Mtaji wa Soko**

Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani (Domestic Market Capitalisation) katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 uliongezeka na kufikia shilingi trilioni 9.45, sawa na

ongezeko la asilimia 3.17 ikilinganishwa na shilingi trilioni 9.16 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020. Aidha, Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa (Total Market Capitalisation) katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 uliongezeka kufikia shilingi trilioni 15.81 ikilinganishwa na shilingi trilioni 15.09 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020 sawa na ongezeko la asilimia 4.73. Ongezeko la Mtaji wa Soko limechangiwa na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa.

**Fahirisi ya Soko *(Market Index)***

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani (Domestic Market Index) iliongezeka kwa alama 80.85 na kufikia alama 3,565.18 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 ikilinganishwa na alama 3,484.53 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2020. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa.

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote (All Share Index) iliongezeka kwa alama 79.83 na kufikia alama 1,896.71 katika kipindi kilichoishia Desemba 2021 ikilinganishwa na alama 1,816.88 katika kipindi kilichoishia Desemba 2020. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa.

## 2.4. Maendeleo ya Watu

### 2.4.1 Ongezeko la Idadi ya Watu

Makadirio ya Idadi ya watu kwa mwaka 2022 yanaonesha kuwa idadi ya watu Tanzania Bara itaongezeka kutoka watu 57,724,380 mwaka 2021 hadi watu 59,517,754 mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.1. Kati ya idadi hiyo, wanawake ni 30,325,507 sawa na asilimia 51.0 na wanaume ni 29,192,247 sawa na asilimia 49.0. Aidha, idadi ya nguvu kazi yenye umri wa miaka 15 – 64 inakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 3.3 kutoka watu 31,124,653 na kufikia watu 32,157,786 sawa na asilimia 54.0 ya idadi ya watu wote mwaka 2022. Ongezeko hili linaendelea kuwa fursa kubwa kimtaji kwa nchi hususan katika shughuli mbalimbali za uzalishaji pamoja na masoko katika sekta zote za huduma na uzalishaji.

### 2.4.2 Viashiria vya Maendeleo ya Watu

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo katika jamii ikiwemo: usambazaji wa umeme mijini na vijijini; uboreshaji wa huduma za afya; utoaji wa elimu msingi bila ada; utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi; na utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Matokeo chanya katika viashiria mbalimbali vya maendeleo yametokana na jitihada za Serikali katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo. Viashiria hivyo vinajumuisha:

(i) Kuongezeka kwa wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 66.0 (2020) hadi miaka 66.6 (2021) na makadirio ya wastani wa miaka 67.2 kwa mwaka 2022. Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, unakadiriwa kuwa miaka 69.6 kwa wanawake na miaka 64.7 kwa wanaume mwaka 2022;

(ii) Kuongezeka kwa idadi ya Watanzania wanaonufaika na mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutoka 4,403,581 Juni 2020 hadi wanufaika 4,550,207 Juni 2021

sawa na ongezeko la asilimia 14.87 kwa mwaka;

(iii) Kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka 1,631,085 mwaka 2020 hadi wanafunzi 1,680,365 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 3.0;

(iv) Kuongezeka kwa idadi ya watu waliofikiwa na huduma ya haki nchini kufikia asilimia 65 mwaka 2021 kutoka asilimia 55 mwaka 2020;

(v) Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 (2015/16) hadi 45 (2020/21) kwa kila vizazi hai 1,000;

(vi) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2014/15 hadi vifo 250 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020/21;

(vii) Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imeimarika kutoka wastani wa asilimia 70.1 Juni 2020 hadi wastani wa asilimia 72.3 Juni 2021. Aidha, kwa upande wa mijini hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeongezeka kutoka asilimia 84 Juni 2020 hadi asilimia 86 Juni 2021; na

(viii) Idadi ya vijiji vilivyounganishwa na umeme vimeongezeka kufikia vijiji 8,587 sawa na asilimia 70 ya vijiji vyote vya Tanzania bara.

#### 2.4.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

Katika kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, jumla ya kaya 886,724 zilifanyiwa uhakiki kutoka Vijiji/Mitaa/Shahia 10,293 kwenye maeneo 186 ya utekelezaji. Kati ya hizo, kaya 781,342 zilikuwa na sifa na kaya 105,382 zilibainika kutokuwa na sifa za kuendelea katika Mpango kwa sababu mbalimbali zikiwemo vifo, kuhama, kuchaguliwa kuwa viongozi kujitoa kwa hiari na kuwa na uraia tata.

Aidha, utambuzi na uandikishaji wa kaya kwa kutumia vishikwambi ulifanyika katika Vijiji, Shehia, na Mitaa 7,217 ambavyo havikufikiwa katika Kipindi cha Kwanza cha Mpango. Jumla ya kaya 602,672 zilitambuliwa ambapo, kaya mpya 498,091 ziliandikishwa. Hadi Desemba 2021 Mpango ulikuwa na jumla ya kaya 1,279,433. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 289.7 zimelipwa kwa walengwa 1,279,325 kwenye maeneo 186 ya utekelezaji wa Mpango katika Halmashauri 184 pamoja na Wilaya zote za Zanzibar. Malipo haya yamejumuisha Vijiji, Mitaa na Shehia zilizotambuliwa na kuandikishwa kutoka katika asilimia 30 ya Vijiji, Mitaa na Shehia ambayo haikufikiwa kipindi cha Kwanza cha Mpango. Aidha, Mpango umeendelea na utekelezaji wa miradi ya ajira za muda katika maeneo 51 ambapo miradi 3,124 yenye thamani ya shilingi bilioni 12.16 imetekelezwa. Vile vile, Mpango umeendelea kuibua miradi 3,094 katika maeneo mengine 72 na kufanya jumla ya miradi itakayotekelezwa kufikia 6,218 katika maeneo 123 ya Utekelezaji.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: Kujengea Uchumi wa Wanakaya kwa kuhamasisha uanzishaji wa Vikundi vya Kuweka Akiba ambapo jumla ya Vikundi 30,648 vyenye Wanachama 421,353 vilianzishwa katika Maeneo 78 ya Utekelezaji; kujenga na kuimarisha uwezo wa Kaya za Walengwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uzalishaji wenye tija; Kutoa mafunzo kwa Kaya yanayohusu stadi za maisha; Kuweka akiba na ujasiriamali; na kuhamasisha Walengwa kujiunga katika Vikundi vya kuweka akiba.

#### 2.4.2.2 Upatikanaji wa Chakula

Taarifa ya Tathmini ya Awali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula Msimu wa 2020/21 na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka 2021/22 inaonesha kuwa, hali ya uzalishaji wa chakula katika msimu wa 2020/21 imefikia tani 18,425,250 kwa mlinganisho wa nafaka *(Grain Equivalent) ambapo* mazao ya nafaka ni tani 10,639,990 na mazao yasiyo nafaka ni tani 7,785,260.

Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/22 ni tani 14,796,751 ambapo tani 9,417,888 ni mazao ya nafaka na tani 5,378,864 ni za mazao yasiyo nafaka. Hivyo, nchi imezalisha ziada ya tani 3,628,499 za chakula ambapo tani 1,222,103 ni za mazao ya nafaka na tani 2,406,396 ni za mazao yasiyo nafaka.

Kwa kuzingatia Kigezo cha Upimaji wa Kiwango cha Utoshelevu *(Self Sufficiency Ratio – SSR),* matokeo yanaonesha kuwa kwa mwaka 2020/21, nchi imekuwa na kiwango cha utoshelevu cha asilimia 126, ambacho ni cha juu zaidi kupatikana. Kiwango hiki kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/20 ambapo nchi ilijitosheleza kwa asilimia 118.

# SURA YA TATU

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 hadi kufikia kipindi cha nusu ya mwaka. Aidha, inaainisha bajeti ya maendeleo iliyotengwa, kiasi cha fedha kilichotumika hadi Januari 2021 na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo.

## 3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2021/22

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 14,977.6, sawa na asilimia 39.4 ya Bajeti ya Serikali ambapo, shilingi bilioni 10,723.0, sawa na asilimia 71.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 4,254.6, sawa na asilimia 28.4 ni fedha za nje.

Hadi Januari 2022, ridhaa ya matumizi ya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo iliyotolewa ni shilingi billioni 8,546.3. Kati ya kiasi hicho, shilingi billioni 6,163.14 ni fedha za ndani na shilingi billioni 2,383.2 fedha za nje. Aidha, baadhi ya maeneo ya kipaumbele yaliyopatiwa fedha katika kipindi husika ni kama ifuatavyo:

(a) Shilingi bilioni 981.49 kwa ajili ya Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji – MW 2,115;
(b) Shilingi bilioni 897.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja kwenye barabara kuu, barabara za mikoa pamoja na barabara na madaraja ya vijijini na mijini;
(c) Shilingi bilioni 742.82 kwa ajili ya ununuzi wa ndege mpya na ukarabati wa ndege;
(d) Shilingi bilioni 421.84 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa *(Standard Gauge Railway)*;
(e) Shilingi bilioni 351.8 kwa ajili ya kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;
(f) Shilingi bilioni 292.51 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini;
(g) Shilingi bilioni 235.5 kwa ajili ya mradi wa usambazaji umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini;
(h) Shilingi bilioni 289.76 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara Vijijini (TARURA);
(i) Shilingi bilioni 188.39 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Reli;
(j) Shilingi bilioni 133.61 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;
(k) Shilingi bilioni 44.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; na
(l) Shilingi bilioni 13.37 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa meli na vivuko.

## 3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 3.3.1 Miradi ya Kielelezo

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo ni kama ifuatavyo:

**(a) Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95.32, kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) asilimia 81.09 na kipande cha Mwanza – Isaka (km 341) asilimia 4.02; kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Makutupora – Tabora (km 368); kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Tabora – Isaka (km 165); kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa na vifaa vya matengenezo ya njia; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli za Tabora – Kigoma (km 411), Uvinza – Musongati - Gitega (km 282) na Kaliua – Mpanda – Karema (km 321) kwa kiwango cha *Standard Gauge*. Jumla ya shilingi bilioni 421.84 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa tuta kuu la bwawa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53.4, njia za kupitisha maji ya kufua umeme asilimia 66.16, nyumba ya mitambo ya kufua umeme asilimia 40.04, kingo za bwawa asilimia 35.89, kituo cha kupokea na kusafirisha umeme kV 400 asilimia 64.39, daraja la kudumu la kuvuka Mto Rufiji asilimia 81.11, barabara za kudumu asilimia 14.41 na nyumba 39 za makazi ya kudumu ya wafanyakazi asilimia 59.13. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 55.3. Jumla ya shilingi bilioni 981.49 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa malipo ya mwisho ya ununuzi wa ndege tatu (3) kati ya hizo, ndege moja (1) ni aina ya *De Havilland Dash 8-Q400* iliyopokelewa Julai, 2021 na ndege mbili (2) aina ya *Airbus A220-300* zilizowasili nchini tarehe 8 Oktoba, 2021; kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege tano (5) mpya ambapo ndege moja (1) aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege mbili (2) aina ya *Boeing 737-9*, ndege moja (1) aina ya *De Havilland Dash 8-Q400* na ndege moja (1) ya mizigo aina ya *Boeing 767-300F*; kukamilika kwa ufungaji wa jenereta, ukarabati wa mfumo wa umeme, kuendelea na ukarabati wa karakana ya matengenezo ya ndege ya KIMAFA katika kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro (KIA); kukamilika kwa ununuzi wa jozi ya injini ya ndege aina ya *Dash 8-Q400* na vipuri muhimu vinavyoambatana na ndege mpya; kununuliwa kwa vifaa vya kuiwezesha ATCL kuhudumia abiria na mizigo kiwanjani (ground handling services); kulipa bima za ndege za *Boeing 787-8 Dreamliner* na *Dash 8 Q400*; na kutoa mafunzo kwa marubani 73 na wahudumu 128 wa ndani ya ndege (Cabin Crew). Aidha, ATCL imefanikiwa kuanza safari katika vituo vya Arusha, Geita, Mwanza na kurejesha safari za Mtwara na Songea, na kurudisha safari za kikanda katika vituo vya Bujumbura, Entebbe, Harare, Lusaka na Hahaya (Comoro) pamoja na kuanzisha vituo vipya vitatu (3) vya kikanda ambavyo ni Lubumbashi, Nairobi na Ndola. Vile vile, ATCL imefanikiwa kurudisha safari za kimataifa (Mumbai) pamoja na kuanzisha safari za mizigo za kwenda Guangzhou. Jumla ya shilingi bilioni 742.82 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 3165: Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na tathmini ya mahitaji ya gharama za miundombinu

wezeshi (barabara, umeme, maji, mawasiliano na makazi); na kuendelea kuhuisha upembuzi yakinifu na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii katika eneo la mradi.

**(e) Mradi Na. 3167: Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na tathmini ya mahitaji ya gharama za miundombinu wezeshi (barabara, umeme, maji, mawasiliano na makazi); na kuendelea kuhuisha upembuzi yakinifu na tathmini ya athari kwa mazingira na jamii katika eneo la mradi.

**(f) Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa kimiminika *(Liquefied Natural Gas - LNG)* – Lindi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi katika maeneo ya Likong'o na Masasi ya Leo; kupatikana kwa hati na uwekaji wa mipaka kuzunguka eneo la mradi; kuendelea na utoaji wa elimu kwa wananchi na wadau kuhusu mradi wa LNG kupitia mikutano ya jamii pamoja na vyombo vya habari; kuendelea na stadi za kisayansi (geo-science) na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi; kukamilika na kuendelea kuboreshwa kwa nyenzo zitakazotumika katika majadiliano (Host Government Negotiation Brief) ya Mkataba wa Nchi Hodhi (Host Goverment Agreement - HGA) kati ya Serikali na wawekezaji; kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor) wa masuala ya sheria, fedha, biashara, uchumi na masoko; na kuendelea na majadiliano ya Mkataba wa HGA kati ya Serikali na wawekezaji. Jumla ya shilingi bilioni 15.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ulipaji fidia katika maeneo ya kipaumbele ya mradi ambapo jumla ya shilingi bilioni 2.29 zimelipwa kwa wananchi 351; kusainiwa kwa Mkataba kati ya nchi hodhi na wawekezaji (Host Government Agreement – HGA); kusainiwa kwa Mkataba wa Wanahisa wa Mradi (Shareholders Agreement - SHA); kukamilika kwa stadi za kijiolojia na kijiofizikia kwa eneo lote la mradi; kukamilika kwa tathmini ya athari ya mazingira na jamii; kufikiwa kwa maamuzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mradi wa EACOP kwa asilimia 15; kutangazwa kwa maamuzi ya mwisho ya uwekezaji (Final Investment Decision) na Wanahisa wa kampuni ya EACOP tarehe 1 Februari 2022; na kuendelea na ununuzi wa wakandarasi wa ujenzi wa mradi.

**(h) Mradi Na. 3115: Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia**

**(i) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mshauri Mwelekezi wa uchorongaji wa visima (Drilling Management Consultant); kukamilika kwa uhuishwaji wa moduli za kiuchumi na fedha; na kukamilika kwa kazi ya kuchakata na kutafsiri taarifa za kimtetemo za 3D katika eneo la kilomita za mraba 132. Jumla ya shilingi milioni 27.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika kitalu cha Eyasi Wembere:**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa tafiti za awali za kijiolojia na kijiofizikia; kuandaliwa kwa moduli ya mfumo wa 3D utakaotumia data za kijiofizikia; kuendelea na tafiti za kina za miamba pamoja na kijiofizikia; kukamilika kwa uchorongaji wa visima vifupi vitatu (3) vya utafutaji vilivyopo maeneo ya Luono – Iramba (Singida), Kining'inila – Igunga (Tabora) na Nyalanja – Meatu (Simiyu). Jumla ya shilingi milioni 208.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(i) Mradi wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mbigiri**

**Mkulazi II – Mbigiri Estate**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa mfumo wa usambazaji maji mashambani; kukamilika kwa mabwawa manne (4) ya kuvuna na kuhifadhi maji yenye uwezo wa kuhifadhi maji ya mita za ujazo 1,750,000; kuongezwa kwa eneo la shamba lililolimwa na kupandwa miwa kutoka hekta 2,061 hadi hekta 2,755 za miwa zenye uwezo wa kutoa tani 220,400 za miwa na sukari tani 13,000; kusajiliwa kwa wakulima 245 wa nje ya kiwanda wenye uwezo wa kulima hekta 745 za miwa zinazoweza kuzalisha tani 5,000 za sukari. Hadi Januari 2022, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 75 kwa upande wa mashamba ya miwa na asilimia 23 kwa upande wa ujenzi wa kiwanda. Jumla ya shilingi bilioni 111.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(j) Mradi Na. 4015: Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 ambapo ujenzi umefikia asilimia 34.9. Jumla ya shilingi bilioni 29.96 zimetumika hadi Januari 2022.

**(k) Mradi Na. 4191: Daraja Jipya la Selander (Tanzanite Dar es Salaam)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja jipya (km 1.03) na barabara unganishi zenye urefu wa km 5.2 ambapo limeanza kutumika. Jumla ya shilingi bilioni 13.40 zimetumika hadi Januari 2022.

**(l) Mradi Na. 1122: Magadi Soda - Engaruka**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uthamini na uhakiki wa ardhi na mali za wananchi; kukamilika kwa *Techno-Economic Study* inayojumuisha upembuzi yakinifu katika eneo la Magadi Soda; na Tathmini ya Athari za Kimazingira (Enviromental Impact Assessment - EIA) na utafiti wa masoko ya Magadi Soda; kuendelea na ulipaji wa Leseni za Utafiti (Prospecting Licence); na kufanyika kwa maombi ya leseni 29 kwa ajili ya uchimbaji (Mining Licence). Jumla ya shilingi milioni 145.17 zimetumika hadi Januari 2022.

**(m) Mradi Na. 3171: Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Mradi Na. 3161: Chuma – Liganga**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na majadiliano kati ya Serikali na mwekezaji kuhusu uanzishwaji wa mgodi wa makaa ya mawe na chuma pamoja na ujenzi wa kiwanda cha chuma; na kupatikana kwa vibali vya kutumia maji ya mito jirani na mradi. Jumla ya

shilingi milioni 12.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(n) Uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi**

**Mradi Na. 4920: Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na majadiliano na wawekezaji watakaowekeza kwenye miradi ya msingi mitatu (3) ambayo ni Bandari ya kisasa (Modern Seaport Component), Sehemu ya Kanda Maalum kwa ajili ya mizigo na usafirishaji (Logistics Park) na Sehemu ya Mji wa Viwanda (Port side Industrial City); kukamilika kwa majadiliano baina ya Mamlaka ya EPZ na TARURA kwa ajili kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani katika eneo lenye viwanda; na kutolewa kwa leseni kwa Kampuni 11 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za uwekezaji katika eneo la viwanda (Bagamoyo SEZ).

### 3.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 3.3.2.1 Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma

**A. Reli**

**(i) Mradi Na. 4216: Ukarabati wa Njia Kuu za Reli**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka (km 970) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 58; kukamilika kwa usanifu kwa ajili ya ukarabati wa vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka; kupokelewa kwa vichwa vya treni vitatu (3), mabehewa 44 ya mizigo na mtambo wa kupima ubora wa njia ya reli; na kuendelea na majaribio ya vifaa hivyo.

**(ii) Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa njia ya reli ya Tanga – Moshi - Arusha (km 470); kuendelea na ukarabati wa njia ya reli katika eneo la Kilosa - Gulwe; kukamilika kwa ukarabati wa mabehewa ya mizigo 200 ambayo yanatumika kutoa huduma ya usafiri kwa njia ya reli ya *Meter Gauge* iliyopo; kukamilika kwa uundaji wa vichwa vya injini vya sogeza saba (7); kusaini mkataba wa ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na mabehewa 37 ya abiria yatakayotumika kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo; kusaini mkataba wa ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria yatakayotumika katika njia ya reli iliyopo; na kuendelea na upembuzi na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli ya treni ya mjini katika jiji la Dodoma (*Dodoma Commuter train*). Jumla ya shilingi bilioni 188.39 zimetumika hadi Januari 2022.

## B. Barabara na Madaraja

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi:**

**(a) Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 68) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 49.5; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396). Jumla ya shilingi bilioni 6.42 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 4113: Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220) kwa kiwango cha lami.

**(c) Mradi Na. 4148: Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 365.98)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara sehemu ya Tabora – Sikonge (km 30); Usesula - Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8) na Kasinde – Mpanda (km 107.68). Jumla ya shilingi bilioni 47.05 zimetumika hadi Januari 2022.

Aidha, katika kipande cha Ipole – Rungwa (km 172) hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**(d) Mradi Na. 4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Makutano – Sanzate (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 92; Mto wa Mbu – Loliondo sehemu ya Waso – Sale Jct (km 50) asilimia 90.3; Sanzate – Natta (km 40) asilimia 9; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Natta – Mugumu (km 45) na Tarime – Mugumu (km 85) ambapo zabuni kwa sehemu yenye urefu wa km 25 zimetangazwa. Jumla ya shilingi bilioni 3.11 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 4130: Barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora (km 259.75)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami sehemu za Tabora – Nyahua (km 85); Nyahua – Chaya (km 85.4) na Manyoni - Itigi - Chaya (km 89.35). Jumla ya shilingi bilioni 11.280 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83.5; na kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 25.09 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 4193: Handeni - Kibaya – Singida (Km 460)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza hatua za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 20 kwa kiwango cha lami.

**(h) Mradi Na. 4195: Barabara ya Dodoma – Iringa (km 273.3)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3) kwa kiwango cha lami ambapo mita 450 zimekamilika; na kuendelea na kazi za uimarishaji wa matabaka katika barabara ya Iringa – Dodoma (km 266) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 45.

**(i) Mradi Na. 4196: Barabara ya Dodoma – Babati (km 243.8)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kuendelea na kazi ya usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati - *Babati Bypass* (km 15.5).

**(j) Mradi Na. 4188: Mbeya – Makongolosi – Manyoni Road (km 528)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Mbeya – Lwanjilo (km 36) na Lwanjilo – Chunya (km 36) na sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 39). Taratibu za ununuzi za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa sehemu za Mkiwa – Itigi - Noranga (km 56.9) na Mbalizi – Makongolosi - Noranga (km 50) zinaendelea.

**(k) Mradi Na. 4112: Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Daraja la Kikwete (Malagarasi) na barabara za Kidahwe – Uvinza (km 76.6), Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 51.98), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Urambo - Kaliua (km 28); na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chagu – Kazilambwa (km 36) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30 na kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 4.61 zimetumika hadi Januari 2022.

**(l) Mradi Na. 4002: Barabara ya Mtwara - Newala - Masasi (km 210)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210); sehemu za Mtwara – Mnivata (km 50); Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 258.2); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa sehemu za Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi (km 160) na Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji.

**(m) Mradi Na. 4003: Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

**(n) Mradi Na. 4107: Barabara za kuelekea kwenye Mradi wa Kufua Umeme wa Maji katika Mto Rufiji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Bigwa – Matombo – Mvuha (km 70); kuendelea na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kilometa 10 kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya

Maneromango - Vikumburu - Mloka (km 100); na kuendelea na ukarabati kwa kiwango cha changarawe na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi - Mvuha - Kisaki - Mtemele *Junction* (km 178).

**(o) Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Kimara – Kiluvya (km 19.2) na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 94; na kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kiluvya – Msangani (km 6.5). Jumla ya shilingi bilioni 16.37 zimetumika hadi Januari 2022.

**(p) Mradi Na. 4004: Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Jumla ya shilingi milioni 631.55 zimetumika hadi Januari 2022.

**(q) Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuendelea na ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45) na Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40. Jumla ya shilingi bilioni 1.29 zimetumika hadi Januari 2022.

**(r) Mradi Na. 4197: Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) sehemu yenye urefu wa kilometa 35 na kulipa madai ya makandarasi na wahandisi washauri wa ujenzi wa barabara ya Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66).

**(s) Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tanga - Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji umefikia asilimia 19; kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami pamoja na daraja la Pangani. Jumla ya shilingi bilioni 6.29 zimetumika hadi Januari 2022.

**(t) Mradi Na. 4152: Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kumlipa Mkandarasi wa barabara ya Puge – Tabora na kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri na Mkandarasi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65).

**(u) Mradi Na. 4186: Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni - Mafinga (km 234.8)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) kwa kiwango cha lami; kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi

wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152); kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Mafinga – Igawa (km 137.9) na kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga – Mgololo (km 78). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kufanya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Junction - Mangae/Melela - Mikumi – Iyovi (km 158.45). Jumla ya shilingi bilioni 8.44 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Mradi Na. 4199: Barabara ya Igawa – Songwe –Tunduma na Mchepuo wa Mbeya - Mbeya Bypass (km 273.5)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) na ujenzi wa mchepuo wa Mbeya (Uyole – Songwe (km 49); na kuanza usanifu wa kina wa barabara ya Iwambi – Mbalizi (km 6.5) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 1.43 zimetumika hadi Januari 2022.

**(w) Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Njombe – Moronga (km 53.9); kuendelea na ujenzi sehemu ya Moronga – Makete (km 53.5) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75.6; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) kwa kiwango cha lami.

**(x) Mradi Na. 4194: Barabara ya Makambako – Songea (km 295)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass) na kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea.

**(y) Mradi Na. 4123: Dumila – Kilosa Road (km 141)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika ujenzi wa sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45); kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Rudewa - Kilosa (km 24) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 50) kwa kiwango cha lami yanaendelea.

**(z) Mradi Na. 4023: Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na uthamini wa mali zitakazoathiriwa na mradi kwa ajili ya fidia.

**(aa) Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 152)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyiwa mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152) na Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200) kwa kiwango cha lami.

**(bb) Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara sehemu ya Kyaka – Bugene (km

59.1) kwa kiwango cha lami; kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Kumunazi - Bugene – Kasulo na Kyaka - Mutukula (km 163); na kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Bugene – Chato - Burigi (km 60) kwa kiwango cha lami.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(a) Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112.0); na kukamilika kwa usanifu wa kina wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) ambapo hatua za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Matai – Tatanda (km 25) kwa kiwango cha lami zinaendelea.

**(b) Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 84.8)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu za Sanya Juu – Elerai (km 32.2) na KIA – Mirerani (km 26); kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Machame *Junction* (km 16) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95.

**(c) Mradi Na. 4129: Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 242.2)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa sehemu ya Isaka – Ushirombo (km 132) na Ushirombo – Lusahunga (km 110). Kazi nyingine ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero (km 150) na kuanza hatua za ununuzi wa Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Jumla ya shilingi bilioni 1.86 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 4111: Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141)**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32.

**(e) Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65). Kazi nyingine ni kuanza kwa taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Vikonge – Uvinza (km 159), sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) na Kibaoni – Sitalike (km 71.0), sehemu ya Kibaoni – Mlele (km 50) kwa kiwango cha lami; na kuanza maandalizi ya ujenzi wa Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31).

**(f) Mradi Na. 4155: Barabara ya Nyanguge – Musoma/Kisesa Bypass (km 202.25)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu ya Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass, km 16.35) kwa kiwango cha lami na ukarabati wa sehemu ya Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5).

**(g) Mradi Na. 4141: Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**
Hatua iliyofikiwa ni**:** Kukamilika kwa ujenzi sehemu ya Kisorya - Bulamba (km 51) kwa kiwango cha lami; na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bulamba (km 56.4) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 33. Jumla ya shilingi bilioni 4.46 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Mradi Na. 4162: Barabara ya Mwigumbi** - **Maswa - Bariadi** - **Lamadi (km 121)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu za Bariadi – Lamadi (km 71.8**),** Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na Maswa - Bariadi (km 49.7); na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10).

**(i) Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25**)
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sehemu za Kidahwe - Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50). Kazi nyingine ni kuendelea na utekelezaji wa sehemu za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 13.6, Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35) asilimia 21.3, Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5) asilimia 34.9 na Nduta *Junction* – Kibondo (km 25.9) asilimia 15.93; na kuanza taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa Kibondo – Mabamba (km 35), sehemu ya Kibondo – Kibondo Airstrip (km 10) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 21.50 zimetumika hadi Januari 2022.

**(j) Mradi Na. 4025: Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa sehemu ya Mpemba – Isongole (km 51.2); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21) na Katumba Songwe - Kasumulu - Ngana – Ileje (km 90.1) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 3.84 zimetumika hadi Januari 2022.

**(k) Mradi Na. 4103: Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 174)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara za Geita – Bulyanhulu *Junction* (km 58.3), Bulyanhulu *Junction* – Kahama (km 61.7) na Uyogo - Nyamilagano – Nyandekwa - Kahama (km 54).

**(l) Mradi Na. 4138: Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Kimara Baruti – Msewe –

Changanyikeni (km 2.6), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola, (km 14.7) sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2), Ardhi – Makongo – Goba (sehemu ya Goba – Makongo km 4) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (sehemu ya Mbezi Mwisho – Goba km 7), Wazo Hill (Madale) – Goba (km 5), Wazo Hill – Madale Section (km 9) na upanuzi wa barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3). Aidha, ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (sehemu ya Ardhi - Makongo km 5) umefikia asilimia 40 na usanifu wa kina wa sehemu ya Mloganzila – Makondeko (km 1) unaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 5.87 zimetumika hadi Januari 2022.

**(m) Mradi Na. 4132: Barabara za Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukarabatiwa kwa km 6.55 za barabara kwa kiwango cha lami na km 55.11 kwa kiwango cha changarawe; na kuendelea na ujenzi wa madaraja ambapo utekelezaji umefikia asilimia 27.3. Jumla ya shilingi bilioni 52.14 zimetumika hadi Januari 2022.

**(n) Mradi Na. 4285: Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam)**

**(i) Awamu ya Kwanza**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha eneo la Jangwani kwa kujenga daraja la juu na tuta.

**(ii) Awamu ya Pili**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa *Lot 1* inayohusisha barabara zenye urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu), Bendera Tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Barabara ya Kawawa – Barabara ya Morogoro (Magomeni), Barabara ya Chang'ombe – Barabara ya Kilwa) ambapo ujenzi umefikia asilimia 44; na kukamilika kwa ujenzi wa *Lot 2* inayohusisha ujenzi wa majengo (vituo 2, yadi 1 na vituo mlisho vinne (4). Jumla ya shilingi bilioni 65.77 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Awamu ya Tatu na Nne**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi wa ujenzi wa Awamu ya Tatu inayohusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya kilometa 23.6 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA ambapo kibali cha Benki ya Dunia '*No Objection"* kinasubiriwa kwa ajili ya kusaini mkataba wa ujenzi. Aidha, usanifu wa kina wa awamu ya nne inayohusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi na Bagamoyo hadi Tegeta pamoja na barabara ya Sam Nujoma (Ubungo - Mwenge) zenye jumla ya km 25.9 imekamilika.

**(o) Mradi Na. 4161: Ujenzi wa Barabara za Juu Jijini Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutumika kwa barabara ya Juu ya Kijazi (Kijazi Interchange); kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Selander (Ali Hassan Mwinyi/*UN Road Junction*); Mbezi mwisho,

Buguruni na Morocco na kuanza maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

**(p) Mradi Na. 4146: Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Ihumwa - Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12) na barabara za Ikulu (Chamwino) - km 15.1; na kuanza ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Mtumba – Veyula – Nala – Matumbulu – Mtumba (km 112.3). Kazi nyingine ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kongwa Junction – Ng'ambi – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98); na kuanza usanifu wa Dodoma *inner ring roads* kuanzia Makulu Jct – Ntyuka Jct – Image *Round About* – Bahi Jct (km 6.3). Jumla ya shilingi bilioni 4.11 zimetumika hadi Januari 2022.

**Barabara za Vijijini na Mijini**

**Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na matengenezo ya kawaida ya miundombinu ya barabara zenye urefu wa kilomita 24,878.71; ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 356.92; ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kilomita 13,710; na ujenzi wa madaraja 729; jumla ya kilomita 19,257.76 zimefanyiwa matengenezo ya kawaida; na kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 98.5, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kilomita 2,951.25 pamoja na ujenzi wa madaraja 93. Jumla ya shilingi bilioni 444.93 zimetumika hadi Januari 2022.

**Ujenzi wa Madaraja**

**(a) Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja ya Mara (Mara), Magara (Manyara), Magufuli (Kilombero), Momba (Songwe), Sibiti (Singida), Mlalakuwa (DSM), Lukuledi (Lindi), Ruhuhu (Ruvuma) na Nyerere (DSM) na kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Kitengule (Kagera) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90; Msingi (Singida) asilimia 70, *Lower* Malagarasi asilimia 65, Kiyegeya (Morogoro) asilimia 95; na kukamilika kwa usanifu wa daraja la Mkundi (Morogoro), Godegode na Mtera. Jumla ya shilingi bilioni 12.69 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 4020: Daraja Jipya la Wami (Pwani)**
Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja na barabara unganishi (km 3.8) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 72.1. Jumla ya shilingi bilioni 5.96 zimetumika hadi Januari 2022.

**Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Serikali**
Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: Ujenzi wa nyumba za Magomeni Kota - Dar es Salaam; ukarabati wa nyumba 28 za viongozi; kuendelea na ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi jijini Dodoma ambapo utekelezaji upo katika hatua za ukamilishaji; kuendelea na

ujenzi wa nyumba 100 za watumishi wa umma jijini Dodoma; na ukarabati wa nyumba 272 Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 24.26 zimetumika hadi Januari 2022.

**C. Usafiri Majini**

**(i) Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za *New* Butiama Hapa Kazi Tu na *New* Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85; kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo ya kujengea na kukarabatia meli katika Bandari ya Mwanza; kusainiwa kwa mkataba wa ukarabati wa meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika; kuanza ujenzi wa meli nne (4) mpya na ukarabati wa meli mbili (2) zinazojumuisha ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mizigo katika Ziwa Victoria, ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo tani 2,800 katika Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo tani 2,700 katika Bahari ya Hindi na ukarabati wa meli ya MV. Liemba na MV Umoja katika Ziwa Victoria. Jumla ya shilingi bilioni 12.22 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Vivuko**

**(a) Mradi Na. 4125*:* Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika vituo 10 vya vivuko (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakarilo, Maisome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma na Kinesi) uko katika hatua za ununuzi. Vile vile, ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome upande wa Bukondo umekamilika na upande wa Zumacheli upo katika hatua za ununuzi. Ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia upande wa Nyamisati umekamilika na upande wa Mafia ujenzi unaendelea; ukarabati wa maegesho ya vituo vinne (4) vya vivuko (Bugolora - Ukara, Rugezi - Kisorya, Nyakarilo - Kome na Kigongo – Busisi) umekamilika; kuendelea na ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya Ijinga – Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Ukerewe), Iramba – Majita (Mara) na Kayenze – Kanyinya (Kagera) na Muleba – Ikuza (Kagera). Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 4139*:* Ujenzi wa Vivuko Vipya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia, Chato - Nkome na Bugolora – Ukara; kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa kivuko kipya cha Kisorya – Rugezi upo katika hatua ya maandalizi ya ujenzi pamoja na taratibu za ununuzi wa *fiber* boti mpya moja (1) kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo upo katika hatua za ununuzi. Jumla ya shilingi milioni 918.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 4144*:* Ukarabati wa Vivuko**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vivuko vya MV Kigamboni, MV Tegemeo, MV KIU na MV Mafanikio na kuendelea na ukarabati wa MV Misungwi, MV Kilombero II, MV Nyerere na MV Kome II. Aidha, miradi ya ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Tanga, MV Mara na MV Ujenzi upo katika hatua mbalimbali za kuanza ukarabati. Jumla ya shilingi milioni 98.34 zimetumika hadi Januari 2022.

**D. Bandari**

**(a) Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

**(i) Bandari ya Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uboreshaji wa gati Na. 1 – 7 kwa kuongeza kina hadi kufikia mita 14.5; na kukamilika kwa ujenzi wa gati maalumu la kuhudumia meli za magari (RoRo); kukamilika kwa ujenzi wa yadi ya kuhudumia makasha; kuendelea na kazi za kuchimba na kupanua lango la kuingilia meli bandarini na sehemu ya kugeuzia meli ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5; kuendelea na hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya uboreshaji wa gati Na. 8 – 11. Jumla ya shilingi bilioni 29.64 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Bandari ya Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uongezaji wa kina cha lango la kuingilia meli kutoka mita nne (4) hadi mita 13 pamoja na kuweka vifaa vya kuongozea meli; kuendelea na awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari ya Tanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya gati la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani (Tanga). Jumla ya shilingi bilioni 60.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Bandari ya Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa gati moja (Multipurpose Terminal) lenye urefu wa mita 300; kuendelea na ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 600. Jumla ya shilingi bilioni 11.69 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iv) Bandari Kavu katika eneo la Ruvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bandari kavu ya Kwala - Ruvu ambapo kazi zinazoendelea ni: kukamilisha utwaaji wa eneo lenye ukubwa wa hekta 502; ujenzi wa mchepuo wa reli kutoka reli ya kati kwenda Kwala/Vigwaza; ujenzi wa yadi na sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65; na barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 18 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Vigwaza/Kwala ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40.

**(b) Bandari za Maziwa Makuu**

**(i) Ziwa Victoria**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Nyamirembe, Magarine, Lushamba, Bukoba, Ntama, Chato awamu ya kwanza, Muleba, pamoja na gati mbili (2) za majahazi katika bandari ya Mwigobero; kununuliwa kwa vifaa vya kuhudumia mizigo na meli (*forklifts*); kuendelea na ukarabati wa majengo na ofisi za bandari ya Ziwa Victoria; kuboreshwa kwa eneo la kushukia abiria katika bandari ya Mwanza *North*; na kukamilika kwa ukarabati wa 'Link Span' ya bandari ya Mwanza South. Jumla ya shilingi bilioni 1.28 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Ziwa Tanganyika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa magati ya Kagunga, Sibwesa na Kabwe (Nkasi); kukamilika kwa ujenzi wa bandari ya Lagosa; kuendelea na ujenzi wa bandari ya Karema ambapo utekelezaji umefikia asilimia 73; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa bandari ya Kigoma, chumba cha abiria katika bandari ya Kibirizi na eneo la kuegeshea meli katika bandari ya Ujiji ambapo kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 60; kuendelea na upanuzi wa bandari ya Kasanga ambapo utekelezaji wake umekamilika (Substential Completion) na hatua inayofuata ni ukaguzi (Technical Inspection). Jumla ya shilingi bilioni 17.19 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Ziwa Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa sakafu ngumu katika bandari za Kiwira na Itungi; kuendelea na ujenzi wa sehemu ya kuegesha meli *(ramp)* katika bandari ya Kiwira; kuendelea na ujenzi wa gati na miundombinu yake katika bandari ya Ndumbi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96. Jumla ya shilingi bilioni 7.64 zimetumika hadi Januari 2022.

**E. Usafiri wa Anga**

**(a) Mradi Na. 6267: *Institutional Support***

**(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA TB III) na Kuboresha Huduma katika Viwanja vya Ndege**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uendeshaji na uwekaji wa miundombinu katika jengo la tatu la abiria (JNIA TB III) unaohusisha matengenezo (preventive maintanance) ya mitambo na mifumo mbalimbali (*switchgears 33 kV*, *lift* 14, eskaleta saba (7), *travelators* mbili (2) za abiria, mashine 20 za ukaguzi wa abiria na mizigo, mifumo ya tiketi za abiria, na mifumo ya TEHAMA); kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa usalama katika kiwanja cha ndege cha Mwanza; na kazi ya ukarabati wa Jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Arusha imefikia asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 8.36 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Ununuzi wa Rada Saba (7) za Hali ya Hewa**

**(i) Mradi Na. 4290: Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kufungwa kwa rada tatu (3) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Mtwara; kufanya malipo ya asilimia 90 ya rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Mbeya na Kigoma; kufanya malipo ya asilimia 80 kwa ajili ya ununuzi wa rada mbili (2) zitakazofungwa katika Mikoa ya Dodoma na Kilimanjaro; kuwezesha mafunzo ya kiwandani kwa wahandisi 10 na wataalamu wa hali ya hewa 16 kuhusu matumizi ya rada nchini Marekani; kukamilika kwa ufungaji wa jenereta na ununuzi wa gari kwa ajili ya uendeshaji wa kituo cha utabiri wa Hali ya Hewa Mtwara; na ukarabati wa vituo vinne (4) vya Hali ya Hewa upo katika hatua mbalimbali ambapo Tabora (asilimia 85), Singida (asilimia 89), Dodoma (asilimia 38) na Mpanda (asilimia 10).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuanza kwa ufungaji wa Mkongo wa Taifa katika vituo vya rada; kununuliwa kwa vifaa na mitambo mbalimbali ikiwemo vifaa vya kutambua matukio ya radi, mitambo miwili (2) inayohamishika ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe, vifaa 15 vya kupima mgandamizo wa hali ya hewa, mitambo minne (4) ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe; seti iliyokamilika ya vifaa vya kuandaa utabiri wa hali ya hewa; mitambo nane (8) ya kutoa huduma za hali ya hewa kwa ajili ya usafiri wa anga; mitambo 13 ya kupima hali ya hewa ambayo ni mahsusi kwa sekta ya kilimo; vifaa 10 vya kupima upepo; na kuendelea na ukarabati wa majengo ya Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa (National Meteorological Training Centre - NMTC). Jumla ya shilingi bilioni 6.28 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 4309: Mradi wa Afrika Mashariki wa Ujuzi wa Mabadiliko na Ujumuishaji wa Kikanda (EASTRIP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanzishwa kwa Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji; kukamilika kwa usanifu wa majengo matano (5) yatakayojengwa katika kampasi ya Mabibo; kuendelea na tathmini ya mazingira kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne (4) ya KIA; kuendelea na ununuzi wa vifaa maalumu vya mafunzo ya uhandisi matengenezo ya ndege (Aircraft Engineering System Trainers na Virtual Maintenance Trainer (VMT) na Cabin Crew Mock Up); kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya TEHAMA na vitabu 2,231; kuandaliwa kwa mitaala mitano (5) ya mafunzo ya urubani na usafiri kwa njia ya reli na maji; na kuwapeleka masomoni wanataaluma 13 nje ya nchi ikijumuisha wakufunzi wa urubani wanne (4) na wahandisi matengenezo ya ndege wanne (4). Jumla ya shilingi bilioni 2.25 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 6377: Kuboresha Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia**

**(i) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji - NIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege mbili (2) za kufundishia marubani aina ya *Cessna Skyhawk* - 172 na kifaa cha mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege (Full Motion Cabin Crew Mock –up); kuendelea na tathmini ya ujenzi

wa awamu ya tatu ya Kituo cha Rasilimali Mafunzo (Maktaba); na kuanzishwa kwa Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani. Jumla ya shilingi bilioni 5.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezeshwa kwa wanataaluma 17 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu pamoja na wanataaluma watano (5) kuhudhuria mafunzo baharini (sea-service training); na kukamilika kwa ukarabati wa vyumba vya madarasa (Hall I, II na III) na miundombinu ya Chuo.

**(e) Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani na kufungwa kwa taa za kuongozea ndege. Aidha, usanifu wa Ujenzi wa jengo la abiria umekamilika na taratibu za kuanza kazi zinaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 4.03 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4220: Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, viungio, maegesho ya ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani pamoja na maegesho ya magari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 86. Jumla ya shilingi bilioni 2.46 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake ikiwemo mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ufungaji wa taa, ujenzi wa kituo cha uchunguzi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Jumla ya shilingi bilioni 1.46 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Jumla ya shilingi shilingi milioni 11.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(i) Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na ufungaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege. Jumla ya shilingi milioni 25 zimetumika hadi Januari 2022.

**(j) Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na: Ukamilishaji wa jengo jipya la abiria pamoja na mifumo na vifaa vyake; ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege; ufungaji wa taa za kuongozea ndege, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (Run End Safety Area – RESA) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95. Jumla ya shilingi bilioni 15.32 zimetumika hadi Januari 2022.

**(k) Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa njia ya kutua na kuruka ndege na kufungwa kwa mfumo wa kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege Dodoma; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Geita na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa kiwango cha changarawe katika kiwanja cha Nachingwea; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Songea (asilimia 96), Iringa (asilimia 38), na Musoma (asilimia 4). Jumla ya shilingi bilioni 18.46 zimetumika hadi Januari 2022.

**(l) Kiwanja cha Ndege cha Lindi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa njia ya kuruka na kutua ndege kutoka kiwango cha changarawe *(gravel)* kwenda kiwango cha lami. Kiwanja kina njia tatu (3) ambazo ni: *Runway* Na. 1 (2810) yenye urefu wa mita 1,383 na upana wa mita 46; *Runway* Na. 2 (1634) yenye urefu wa mita 1,847 na upana wa mita 46; na *Runway* Na. 3 (0422) yenye urefu wa mita 1,609 na upana wa mita 46.

**(m) Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wakazi walioathiriwa na utekelezaji wa mradi na kukamilika kwa maandalizi ya kuanza ujenzi ambapo: Mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi Awamu ya Kwanza wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na jengo la abiria ulisainiwa Septemba 2021. Jumla ya shilingi milioni 450.23 zimetumika hadi Januari 2022.

**(n) Mradi Na. 4158: Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa usanifu wa jengo la abiria.

**(o) Mradi Na. 4159: Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, jengo jipya la abiria, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Jumla ya shilingi milioni 5.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(p) Mradi Na. 4210: Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uongezaji wa urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita 200; na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege, uzio wa usalama,

barabara mpya ya kuingilia kiwanjani na ukarabati wa maegesho ya magari.

**F. Nishati**

**Miradi ya Kufua umeme**

**(a) Mradi Na. 3164: Kinyerezi I *Extension* (MW 185)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa mkandarasi mpya wa kukamilisha kazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 84. Mkandarasi mpya amekabidhiwa mradi mwezi Desemba 2021 na unatarajiwa kukamilika tarehe 31 Oktoba 2022.

**(b) Mradi Na. 3169: Kufua Umeme wa Maji Rusumo (MW 80)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na uchimbaji wa handaki la kupitisha maji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 100, ufungaji wa mitambo asilimia 74 na ujenzi wa kituo cha kuongeza nguvu ya umeme (switch yard) asilimia 98 Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 87. Jumla ya Dola za Marekani milioni 3.92 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 3168: Kufua Umeme wa Maji Kikonge (MW 300)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na kuidhinishwa kwa Tathmini ya Mazingira na Jamii (Strategic Environmental & Social Assessment – SESA).

**Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**
**(a) Mradi Na. 3113: Usambazaji wa Umeme Vijijini**
Hatua iliyofikiwa ni kuunganishwa kwa jumla ya vijiji 8,587 kati ya vijiji 12,345 vya Tanzania Bara. Jumla ya shilingi bilioni 235.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 3157: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa – Singida – Shinyanga (*Backbone Transmission Investment Project* - BTIP II)**
Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupooza umeme vya Singida na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.

**(c) Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 - North West Grid Extension (Iringa – Mbeya - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi)**
**Awamu ya Kwanza (Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga):**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa mapitio na uhuishaji wa taarifa zilizoandaliwa awali kuhusu mazingira; kukamilika kwa mpango wa kuhamisha wananchi wanaopisha mradi (Resettlement Action Plan – RAP) katika maeneo ya Iringa hadi Mbeya; na kuandaa zabuni kwa ajili ya kuwapata Mtaalamu Mshauri; Mkandarasi Mjenzi wa mradi; na wataalamu wengineo wa mradi.

**Awamu ya Pili (Kigoma hadi Nyakanazi)**:
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ulipaji wa fidia katika eneo la Kidahwe kwa asilimia

99; kuhuishwa kwa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi; kukamilika kwa Maandalizi ya ununuzi wa Mkandarasi wa njia za usafirishaji na usambazaji umeme; na kuanza taratibu za kumpata Mkandarasi wa vituo vya kupoza umeme.

**Awamu ya Tatu (Kigoma – Mpanda – Sumbawanga):**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri atakayehuisha upembuzi yakinifu na kuandaa taarifa ya mazingira.

**(d) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na shughuli za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ambapo utekelezaji umefikia asilimia 61. Ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi umefikia asilimia 95.

**(e) Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida - Arusha – Namanga**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na shughuli za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme; kujenga vituo vya kupoza umeme jijini Arusha na Singida; na kuendelea na usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 96.1.

**(f) Mradi Na. 3179: Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Kinyerezi - Dodoma**
**Awamu ya kwanza (Rufiji - Chalinze)**: Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa njia ya usafirishaji wa umeme wa kV 400 na barabara za mradi (asilimia 48.45). Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, ujenzi wa mradi umefikia asilimia 8. Jumla ya shilingi bilioni 23.71 zimetumika hadi Januari 2022.

**Awamu ya pili (Chalinze – Dodoma na Chalinze - Kinyerezi)**: Hatua iliyofikiwa ni: Kufanya majadiliano na mkandarasi ili kupanga upya mawanda ya mradi kwa kuzingatia mahitaji ya sasa; kuendelea na malipo kwa wananchi wanaopisha mradi kati ya Kinyerezi na Chalinze; na kukamilika kwa tathmini ya athari za mradi kwa mazingira na jamii (ESIA). Jumla ya shilingi bilioni 7.84 zimetumika hadi Januari 2022.

**Miradi ya Usambazaji wa Gesi Asilia**
**(a) Mradi Na. 3162: Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utandazaji wa miundombinu (mabomba na vituo vya kupunguza msukumo wa gesi) jijini Dar es Salaam; kuendelea na uunganishaji wa nyumba 515 katika maeneo ya Sinza na Polisi Barracks - (Kurasini); kuendelea na uunganishwaji wa gesi asilia viwandani katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara; na kukamilika kwa miundombinu ya usambazaji na uunganishaji wa gesi asilia kwa nyumba 200 katika Mkoa wa Lindi. Jumla ya shilingi million 133.2 zimetumika hadi Januari 2022.

#### 3.3.2.2 Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi

**A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**

**(i) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Bunge**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Bunge uliohusisha ununuzi wa vipuri vipya vya mfumo wa umeme, ukarabati wa mfumo wa kupoza ukumbi wa Bunge. Jumla ya shilingi bilioni 1.37 fedha za ndani zilitumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge**
Hatua iliyofikiwa ni kuanza ujenzi wa makazi ya viongozi pamoja na ukarabati wa mifumo na mitambo ya usalama. Jumla ya shilingi bilioni 2.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Mradi Na. 6216: Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili (LSP II)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, utungaji wa sheria na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge; kuandaliwa kwa miongozo ya uendeshaji wa shughuli za Bunge ambayo ni Mwongozo wa Utungaji wa Sheria, Muswada Binafsi wa Sheria, usikilizaji wa maoni ya wadau, ziara za Kamati za Bunge, hoja binafsi na uchambuzi wa Bajeti. Jumla ya shilingi milioni 122.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iv) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi katika masuala ya kodi; kufanyika kwa utafiti ili kubaini mchango na athari za michezo ya kubahatisha katika uchumi; ununuzi wa vifaa (*video conferencing equipments*, *kompyuta mpakato* na *smart board)* kwa ajili ya kituo cha habari. Jumla ya shilingi milioni 398.01 zimetumika hadi Januari 2022.

**B. Kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma**

**Utumishi wa Umma na Utawala Bora**
**(i) Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa**
Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa ukuta pembeni mwa bahari ili kuzuia mmomonyoko baharini (retaining wall for the beach/cliff mitigation) katika nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassani Mwinyi; na kujengwa kwa uzio (fence) katika nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Jumla ya shilingi milioni 574.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho ya Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**

**(a) Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki – e-OPRAS**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki (e-OPRAS) na kuanza kwa majaribio ya Mfumo katika Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na kutolewa kwa mafunzo kwa watumiaji 420 wa mfumo. Jumla ya shilingi milioni 150 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimali Watu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimali Watu (e-HRP); na kuendelea na shughuli za uwekaji wa mfumo (installation) ili uanze kutumika ikiwemo kufanya majaribio ya mfumo. Jumla ya shilingi milioni 100 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mfumo wa Utumishi Mtandao (Watumishi e – Service Portal and Digital Repository)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza usanifu wa mfumo na kubadili nyaraka za kiutumishi kwa kuzifanyia ‘scanning’ ili kurahisisha upatikanaji wa nyaraka kwa njia ya kielekroniki; kupitia Mwongozo wa Uanzishaji wa Tovuti ya Serikali wa Mwaka 2014 ili uendane na mahitaji ya sasa ya TEHAMA; na kupitia miundo na mifumo ya TEHAMA serikalini. Jumla ya shilingi milioni 100 zimetumika hadi kufikia Januari 2022.

**(d) Mfumo wa Maadili na Mfumo wa kushughulikia malalamiko**

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa maboresho ya mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumishi na wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na Taasisi za Umma; na kuendelea na usanifu na ujenzi wa mfumo wa maadili na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa mfumo. Jumla ya shilingi milioni 338 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 6282: Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara - Home Grown HCMIS**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuunganishwa kwa Mfumo wa HCMIS na mifumo mingine ya Serikali ikiwemo mifumo ya PSSSF, HESLB na Mfumo wa Usaili; kuendelea na uunganishaji wa mfumo wa HCMIS na mifumo ya MUSE, Planrep, na mifumo ya Benki za kibiashara (NMB,CRDB n.k); kukamilika kwa ununuzi wa vifaa vya TEHAMA vikiwemo *server*, kompyuta, ‘*Firewall Licenses*, *Antivirus*, *UPS*, *Electronic na Signature Pad*; kuhamishwa kwa taarifa kutoka katika mfumo wa zamani wa HCMIS (Lawson) kwenda Mfumo Mpya wa HCMIS; na kuwajengea uwezo maafisa TEHAMA 15 katika uandaaji wa taarifa za kiutumishi. Jumla ya shilingi milioni 500.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**C. Mfuko wa Mahakama**

**(i) Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe,

Katavi, Lindi na Mahakama za wilaya sita (6) za Bahi, Chemba, Rungwe, Makete, Wanging'ombe na Bunda; na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Hakimu Mkazi Songwe na Mahakama za Wilaya nane (8) za Nanyumbu, Namtumbo, Same, Tandahimba, Kilindi, Sikonge, Mwanga na Ngara. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 6311: Ujenzi na Upanuzi wa Jengo la Chuo cha Uongozi wa Mahakama - Lushoto (IJA)**

**Ujenzi wa Bweni la Wavulana Lushoto**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa awamu ya pili ya ujenzi wa bweni la wavulana Lushoto ambapo jumla ya shilingi milioni 232 zimetumika hadi Januari 2022.

**(a) Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa Majengo ya Mahakama za Mwanzo sita (6) za Matiri (Mbinga), Hydom (Mbulu), Ngerengere (Morogoro), Mtae (Lushoto), Kibaigwa (Kongwa), Lugarawa (Ludewa); na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo sita (6) za Chanika (Ilala), Kabanga (Ngara), Kimbe (Kilindi), Nyakibimbili (Bukoba), Mlimba na Mang'ula (Morogoro). Jumla ya shilingi milioni 729 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6314: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama Kuu**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kwa ukarabati wa Jengo la Mahakama Kuu Tabora ambapo jumla ya shilingi milioni 349 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

**Nyumba za Majaji na Mahakimu**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa nyumba mbili (2) za Mahakimu Loliondo – Arusha ambapo jumla ya shilingi milioni 51 zimetumika hadi Januari 2022.

**Ujenzi wa Jengo la Kuhifadhi Kumbukumbu, Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa jengo la kuhifadhi kumbukumbu ambapo jumla ya shilingi milioni 126 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa boma (main structure) ambapo jumla ya shilingi bilioni 10.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 6215: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Mahakama *(Citizen Centic Judiciary Modernisation Project)***

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa: Vituo vitano (5) Jumuishi vya utoaji Haki katika Mikoa ya Dar es Salaam (Temeke na Kinondoni), Dodoma, Arusha na Morogoro; kuendelea na

ujenzi wa jengo la kituo kimoja (1) jumuishi cha utoaji Haki katika Mkoa wa Mwanza ambacho kipo katika hatua za mwisho; na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za wilaya 18 katika wilaya za Kakonko, Buhingwe na Uvinza (Kigoma), Butiama na Rorya (Mara), Itilima na Busega (Simiyu), Songwe (Songwe), Mbogwe na Nyang'wale (Geita), Kyerwa na Misenyi (Kagera), Gairo, Mvomero na Kilombero (Morogoro), Mkinga (Tanga), Tanganyika (Katavi) na Kaliua (Tabora). Jumla ya shilingi bilioni 9.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**D. Utawala wa Sheria**

**(a) Mradi Na. 6201: Haki Mtandao (e-justice)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa usanifu wa Mfumo wa Usimamizi wa Uangalizi wa Utajiri na Maliasilia za nchi; ununuzi wa vifaa vya TEHAMA vitakavyotumiwa na jeshi la magereza kwenye mikoa ya Singida na Dodoma; kukusanywa kwa mahitaji kwa ajili ya mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa haki za binadamu; na kuendelea kuboresha kwa kuunganisha mifumo ya kielektroniki ya Sekta ya Haki mtandao iliyopo ikiwemo kanzidata ya wanasheria serikalini, mfumo wa kusajili watoa huduma za masuala ya upatanishi, maridhiano, mashauriano na usuluhishi, mfumo wa kuchakata huduma za utoaji haki na mfumo wa kusajili watoa huduma ya msaada wa kisheria. Jumla ya shilingi milioni 429.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6517: Haki ya Mtoto na Mwanamke**

**(i) Kuimarisha Haki za Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: kusajiliwa kwa vizazi 739,498, kati ya hivyo vizazi 654,740 vilisajiliwa kupitia Mpango wa usajili wa watoto wa umri chini ya miaka mitano katika mikoa ya Mwanza, Rukwa na Katavi: kuanza kwa usajili wa watoto 523,090 wa umri chini ya miaka mitano katika Mkoa wa Tabora; kutolewa kwa hati 15 za kuasili watoto sawa na asilimia 75 ya lengo la kuasili watoto 20; kuandaliwa na kuhifadhiwa kwa wosia 86 kati ya wosia 90 sawa na asilimia 95 ya lengo. Jumla ya shilingi bilioni 1.35 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Kuimarisha Haki za Watoto na Wanawake**

Hatua iliyofikiwa ni: kutolewa kwa mafunzo kwa wadau 22 wanaosimamia haki za wanawake na watoto katika Mkoa wa Kigoma; kutolewa kwa mafunzo kwa watumishi 56 kuhusu usimamizi wa masuala ya kijinsia, pamoja na miradi ya kijinsia; kutolewa kwa mafunzo kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria (mawakili na wanasheria) 15, watakaofanya kazi katika madawati ya huduma ya msaada wa kisheria yaliyoanzishwa katika Mahakama Jumuishi (Integrated Justice Centre) Mkoa wa Mwanza, Morogoro, Dodoma na Arusha, na vituo jumuishi (One Stop Centre) vilivyoanzishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni na Temeke; kukusanya maoni juu ya marekebisho ya Sheria ya Ndoa hususan kuhusu umri wa mtoto wa kike kuolewa; kufanyika kwa tathmini ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto katika wilaya ya Kasulu (Kigoma), Wilaya ya Sengerema (Mwanza), Wilaya ya Ngorongoro (Arusha) na Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam; kutengenezwa kwa mfumo wa kupokea taarifa kutoka kwa

wadau wanaotekeleza afua kuhusu wanawake na taarifa za wanawake waliopokea huduma ya msaada wa kisheria kutoka kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria; na kuzinduliwa kwa kamati za uratibu wa huduma za msaada wa kisheria katika mikoa mitatu ya Kilimanjaro, Mara na Katavi. Jumla ya shilingi milioni 668 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 5501: Kuimarisha Upatikanaji wa Haki za Binadamu**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa andiko la Mfumo wa Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Binadamu katika kipindi maalumu na kuiwasilisha katika kikao cha Umoja wa Mataifa. Jumla ya shilingi milioni 138.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 5502: Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa andiko la awali la Sera ya Taifa ya Mashtaka. Jumla ya shilingi milioni 104.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 6207: Kuboresha Uwajibikaji na Kuongeza Upatikanaji wa Haki**
Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria kwa mwaka 2021. Jumla ya shilingi milioni 288 zimetumika hadi Januari 2022.

**Serikali Kuhamia Dodoma**

**(i) Uhamisho wa Watumishi**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuhamishwa kwa watumishi 18,300 na vifaa vya ofisi kwenda Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 162.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Ujenzi wa Majengo ya Serikali**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Wizara katika mji wa Serikali Mtumba baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kiasi cha shilingi bilioni 300 zimetengwa na Wizara zimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi. Jumla ya shilingi bilioni 81.8 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Ujenzi wa Miundombinu**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya awali katika Mji wa Serikali Mtumba ikiwemo maji, umeme, mawasiliano na barabara. Aidha, ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 51.2 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 82. Jumla ya shilingi bilioni 50.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**Mradi Na. 6351: Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu**

Hatua iliyofikiwa: Kuendelea na ufungaji wa umeme kuzunguka uzio katika Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu – Mlimwa; na kuendelea na ufungaji wa taa kuzunguka ukuta. Jumla ya shilingi milioni 453.67 zimetumika hadi Januari 2022.

## E. Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi

**Ofisi na Makazi ya Viongozi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa majengo mawili (2) ya ofisi za Halmashauri za Wilaya (Kibaha Mji na Malinyi); kuendelea na ujenzi wa majengo 94 ya ofisi za Halmashauri; kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi 24 na nyumba 16 za Wakuu wa Wilaya; kuendelea na ujenzi wa Ikulu Ndogo nne (4) (Musoma, Ludewa, Hanang' na Mufindi), nyumba za Wakuu wa Mikoa nne (4) (Ruvuma, Iringa, Songwe na Njombe), Ofisi za Wakuu wa Mikoa sita (6) (Mbeya, Simiyu, Songwe, Katavi, Geita na Njombe), nyumba za Makatibu Tawala wa Mikoa tatu (3) (Katavi, Njombe na Songwe), nyumba za Wakuu wa Wilaya 13 (Songea, Bariadi, Songwe, Ruangwa, Mufindi, Kiteto, Kyerwa, Simanjiro, Dodoma, Kibiti, Butiama, Liwale na Ilemela) na nyumba kumi (10) za Maafisa Tarafa katika Mikoa ya Katavi (Tarafa 6), Songwe (Tarafa 2) na Iringa (Tarafa 2).

Aidha, shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi Nane (8) za Wakuu wa Wilaya (Igunga, Nzega, Karatu, Arumeru, Kwimba, Kilindi, Pangani, na Korogwe); na kuendelea na ukarabati nyumba 28 za Wakuu wa Wilaya (Hai, Mwanga, Iramba, Manyoni, Singida, Rombo, Chunya, Mbarali, Rungwe, Kyela, Mbeya, Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe, Rufiji, Mafia, Ngorongoro, Longido, Karatu, Monduli, Magu, Misungwi, Kwimba, Nyamagana, Kilindi, Tanga, Korogwe, na Lushoto), Ofisi za Wakuu wa Wilaya tatu (3) (Lindi, Arusha na Ngorongoro), Ofisi za Wakuu wa Mikoa 11 (Mara, Kilimanjaro, Lindi, Mwanza, Iringa, Ruvuma, Kigoma, Singida, Manyara, Pwani na Dodoma), nyumba mbili (2) za Makatibu Tawala wa Mikoa (Lindi na Iringa) na nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya tano (5) (Ileje, Kibaha, Arusha, Tanga na Rukwa). Jumla ya shilingi bilioni 79.9 zimetumika hadi Januari 2022.

## F. Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika majimbo ikiwemo miradi ya ujenzi wa vituo vya afya, vyumba vya madarasa, vyumba vya maabara na miundombinu ya maji na umeme. Jumla ya shilingi bilioni 11.0 zimetumika hadi Januari 2022.

## G. Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi
Shughuli zilizotekelezwa ni: Kujenga nyumba za wakuu wa idara 45 katika Halmashauri 33 zilizohamia kwenye maeneo mapya ya utawala na nyumba za wakurugenzi 55; kuendelea na ujenzi wa majengo 82 ya utawala na majengo ya utawala mapya katika Halmashauri 14 zenye majengo yaliyojengwa zamani; kuendelea na ukarabati wa majengo ya zamani ya utawala katika ofisi 4 za Mikoa (Kigoma, Kilimanjaro, Mara na Shinyanga), nyumba 5 za Wakuu wa Mikoa (Ruvuma, Lindi, Pwani, Iringa, Kigoma), nyumba 10 za Makatibu Tawala wa Mikoa (Pwani, Iringa, Rukwa, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mwanza, Singida na Ruvuma), majengo ya utawala 20 ya zamani katika ofisi za Wakuu wa Wilaya (Kibaha, Mafia, Rufiji, Bagamoyo, Kasulu, Kibondo, Kigoma, Moshi, Same, Siha, Musoma, Tarime, Bunda, Sengerema, Serengeti, Rorya, Kinondoni, Ilala, Temeke, Makete na Ludewa) na nyumba 11 za Makatibu Tawala wa Wilaya

(Mpanda, Itilima, Buhigwe, Uvinza, Moshi, Lindi, Musoma, Tarime, Rorya, Shinyanga, Kahama).

Aidha, shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika ofisi sita (6) za Wakuu wa Mikoa (Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Mbeya, na Songwe), majengo ya utawala manne (4) katika ofisi za Wakuu wa Wilaya (Mbogwe, Nyangh'wale, kahama na Kishapu); na ujenzi wa nyumba za Makatibu Tawala wa Mikoa (Simiyu, Geita na Songwe), majengo ya utawala mapya 11 katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya (Kibiti, Kondoa, Kongwa, Uvinza, Hai, Kahama na Kishapu, Hanang', Uyui na Handeni) na nyumba 12 za Makatibu Tawala wa Wilaya (Kibaha, Mafia, Kibiti, Hai, Same, Kilwa, Liwale, Ruangwa, Mbozi, Momba, Songwe, na Serengeti).

**H. Mradi Na. 6580: Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 5.38 na mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa km 6. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 92. Jumla ya shilingi bilioni 55.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**I. Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa**
Shughuli zilizotekelezwa ni: kuendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu, ambapo jumla ya watu 303,248 wamesajiliwa, wageni wakaazi 2,116 na wakimbizi 34,837 wamesajiliwa na kufanya jumla ya raia wa Tanzania waliosajiliwa kufikia 22,840,419, wageni wakaazi 34,366 na wakimbizi 234,879 katika mikoa na wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar.

Aidha, Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) 306,698 zilizalishwa na kupelekea jumla ya NIN zilizozalishwa kuwa 19,238,469; vitambulisho 2,556,314 vilizalishwa ambapo 2,452,883 vimesambazwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 10,708,319 na vitambulisho vilivyosambazwa kwa wananchi kufikia 9,928,742.

Vile vile, taasisi nane (8) zimeunganishwa katika Mfumo wa Usajili na Utambuzi na kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa na mfumo kufikia 58; kuendelea kuunganisha na kuboresha miundombinu ya mtandao wa mawasiliano kati ya Ofisi za Usajili za Wilaya na Makao Makuu ambapo jumla ya ofisi 130 zimeunganishwa; na kuundwa na kuboreshwa kwa mifumo ya ndani 12 (modules) kwa ajili ya kusaidia Mfumo wa Usajili na Utambuzi. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**J. Usalama wa Raia**

**(i) Mradi Na. 6302: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara**
Shughuli zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Mkuu wa Kikosi cha kutuliza ghasia mkoani Singida; kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa kutenganisha eneo la Makao Makuu ya Polisi/CID na eneo la RPC Dodoma; kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja ”C” na ujenzi wa nyumba za

makazi ya askari Ludewa ambao ulikuwa umesimama tangu mwaka 2012; kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja “A” katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma ambapo umefikia asilimia 65; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja “A” Kigamboni (Dar es Salaam) ambapo umefikia asilimia 61. Jumla ya shilingi milioni 1,303.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 6303: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Zanzibar**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkokotoni ambao umefikia asilimia 95 na ujenzi wa Kituo cha Polisi Kizimkazi ambao umefikia asilimia 65. Jumla ya shilingi milioni 539.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**K. Magereza**

**(i) Mradi Na. 1201: Uimarishaji wa Viwanda vya Magereza**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa kwa michoro na makadirio ya ujenzi (BOQ) wa jengo la kuuzia bidhaa za samani katika kiwanda cha samani Msalato pamoja na kuundwa kwa kamati za kusimamia mradi na kupata kibali cha kutekeleza mradi huo kwa utaratibu wa *Force Account*.

**(ii) Mradi Na. 6308: Ukarabati wa Magereza Makuu**

Shughuli zilizotekelezwa ni kuandaliwa kwa makadirio ya ujenzi (BOQ), kuundwa kwa kamati za utekelezaji wa mradi pamoja na kupata kibali cha kutekeleza mradi kwa kutumia utaratibu wa *Force Account* kwa ajili ya ukarabati wa magereza ya Isanga, Mkuza, Maweni, Lindi, Mbozi, Mpanda, Songwe, Kibondo na Kondoa.

**(iii) Mradi Na. 4428: Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuandaliwa taratibu za ununuzi wa zana za kilimo na pembejeo; na kuandaliwa kwa michoro ya majengo na makadirio ya ujenzi (BOQ) wa maghala ya kuhifadhi mazao.

**L. Zimamoto na Uokoaji**

**Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa nyumba za familia 80 za Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji eneo la Kikombo (Dodoma) ambapo umefikia asilimia 65; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Nzuguni (Dodoma) ambapo umefikia asilimia 75; na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Chamwino ambapo umefikia asilimia 96; ununuzi wa magari matatu (3) ya kuzima moto kutoka Shirika la Nyumbu linalomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuendelea na ujenzi wa kituo cha zimamoto na uokoaji kilichopo eneo la Mchicha, Tazara Jijini Dar es Salaam ambapo ujenzi umefikia asilimia 75.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: kukamilika kwa taratibu za uandaaji wa mkataba wa ununuzi wa magari mawili (2) ya kuzima moto na vifaa vya kuzima moto na uokoaji; na ukarabati wa kituo cha zimamoto na uokoaji cha Ilala (Dar es Salaam).

**M. Uhamiaji**

**Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji Mikoa**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 55; kuendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53; kuendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25; na kuendelea kwa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65 ya utekelezaji wake.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa Kambi ya Mafunzo ya Uhamiaji - Boma Kichakamiba Wilayani Mkinga (Tanga) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 26.93; na kuanza kwa taratibu za ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara kwa kutumia utaratibu wa *Force Account*. Jumla ya shilingi bilioni 3.70 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.2.3 Mapinduzi ya TEHAMA

**A. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**(i) Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa kilomita 409 katika mgawanyo ufuatao: kilomita 72 za kuunganisha nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala katika Mkoa wa Mtwara na kukamilika kwa kituo cha kutoa huduma za mawasiliano; kilomita 72 za kuunganisha watumiaji wa mwisho (Last mile connectivity) katika Ofisi za Serikali za Msalato, Mtumba na Kikombo Dodoma; na kilomita 265 awamu ya kwanza Manyoni – Kambi Katoto (Chunya).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kupitia miundombinu ya TANESCO; kununuliwa kwa magari saba (7) na vitendea kazi vingine kwa ajili ya kuhudumia shughuli za Mkongo wa Taifa; kukamilisha usanifu wa Mfumo wa Uratibu wa shughuli za Wizara unaojumuisha Moduli ya Vibali vya usimikaji wa Miundombinu ya Mkongo; na kukamilika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya kupata mahitaji ya kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na DRC Congo. Jumla ya shilingi bilioni 27.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 4234: Anuani za Makazi na Postikodi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa Mkakati wa miaka mitano (2021-2025) wa kuharakisha utekelezaji na matumizi ya mfumo; kuwekwa kwa nguzo 5,300 za majina ya barabara/mitaa katika Kata 18 za Halmashauri ya Jiji la Mwanza; kubandikwa kwa vibao 78,138 vya namba za nyumba katika kata 18 za Halmashauri ya Jiji la Mwanza; kukusanywa kwa taarifa kwa taarifa za anwani 98,801 kwa Makazi na Wakazi kwa kutumia Programu Tumizi; kukamilika kwa uandaaji wa ramani za mipaka ya kiutawala katika Halmashauri 20 za Majiji ya Ilala, Tanga, Mwanza, Mbeya na Dodoma, Manispaa za Tabora, Morogoro, Bukoba, Lindi, Shinyanga, Songea, Moshi, Kigamboni, Kinondoni,

Temeke, Ubungo, Singida, Iringa, Kigoma Ujiji, na Sumbawanga ambapo mipaka yake imetasfiriwa kwa mujibu wa Matangazo ya Serikali (GN).

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa ramani za kidijitali katika Halmashauri tisa (9) za Tabora MC, Shinyanga MC, Ilemela MC, Mbeya CC, Iringa MC, Tanga CC, Dodoma CC, Arusha CC & Bukoba MC; kutolewa elimu kwa umma sambamba na kutolewa kwa mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makazi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa mikoa yote ya Tanzania Bara na Wajumbe wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), watalaamu kutoka Halmashauri 196 (184 Tanzania Bara na 12 za Tanzania Visiwani) kutoka mikoa yote nchini wamefanyiwa mafunzo ya utekelezaji na usimamizi wa Mfumo; kuandaliwa kwa rasimu ya Sheria Ndogo (Uniform By law) kuhusu utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makazi na Postikodi ambayo itatumiwa na Halmashauri zote nchini; na kukamilika kwa maboresho kwenye Wavuti (Web Portal) na Program Tumizi (Mobile App) sambamba na kuunganisha Mfumo wa Anuani za Makazi na Mifumo ya NIDA, HFR, TRA & BRELA. Jumla ya shilingi bilioni 13.27 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa tathmini ya kutambua maeneo ya vijijini ambayo hayana mawasiliano ili kujenga minara ya mawasiliano sambamba na kutambua maeneo yanayopaswa kuboreshwa kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G/4G ili kuwezesha huduma za mkondo wa mawasiliano ya kasi (broadband) nchini; kukamilika kwa tathmini ya ununuzi wa vifaa na maboresho ya vituo mahiri vya kuhifadhi Data (National Internet Data Center - NIDC and Government Data Center - GDC) ili kuongeza uwezo wa vituo hivyo katika kutunza *data*; kukamilika kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo (Training Needs Assesment) kwa watumishi wa umma wa kada ya TEHAMA ili kuwatambua watumishi wenye sifa ya kupewa mafunzo kulingana na mahitaji ya Taasisi za Serikali wanakotumikia; na kukamilika kwa maandalizi ya Mkakati wa Mawasiliano wa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Jumla ya shilingi bilioni 6.4 fedha za ndani zimetumika hadi Januari 2022.

**B. Mradi Na. 4279: Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kituo cha kurushia matangazo ya masafa ya FM katika kituo cha Kisaki mkoani Morogoro; kukamilika kwa ujenzi na ufungaji wa mitambo ya kituo cha Redio ya Jamii Makao Makuu Jijini Dodoma; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa wazabuni wa kufunga mitambo ya masafa ya FM katika mikoa mipya ya Njombe, Songwe na Simiyu, sambamba na wilaya za Kilwa, Serengeti pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba; kuboreshwa na kufungwa kwa mitambo yenye vifaa vya kisasa katika studio za redio zilizoko Barabara ya Nyerere; kuendelea na ufungaji wa mitambo ya masafa ya FM katika Wilaya za Karagwe, Same, Bunda, Kasulu, Kahama, Nkasi na Sikonge ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 80; kuendelea na ujenzi wa mitambo ya masafa ya FM katika Wilaya za Ngara, Kyela, Ruangwa, Kilombero na Ludewa ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 95; kuendelea na ujenzi wa mitambo ya masafa ya FM katika wilaya za Tanganyika/Mlele, Makete, Uvinza, Mbinga na

Ngorongoro ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 70; kukamilika kwa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi 45 waliopisha eneo la ekari takriban 53 kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya TBC katika eneo la Vikonje Jijini Dodoma; kununuliwa na kufungwa kwa mitambo miwili (2) ya kurushia matangazo kwa njia ya Satelaiti (FLY AWAY) pamoja na mtambo wa kurushia matangazo mubashara ya redio kwa njia ya mtandao (LIVE U); ununuzi wa magari manne (4) kwa ajili ya shughuli za utangazaji; na kukamilisha ujenzi wa jengo la Studio na ununuzi wa vifaa vya Chaneli ya Televisheni ya TBC 2 katika ofisi za Mikocheni Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**C. Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo kamera, kompyuta na visaidizi *(accessories)*; kuandaliwa kwa video fupi, vibango na makala maalumu kwa ajili ya matangazo ya televisheni na mitandao ya kijamii pamoja na makala maalumu zilizochapishwa kwenye magazeti mbalimbali na jarida maalumu; na ukusanyaji na usambazaji wa habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Serikali katika Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Miji na Majiji nchini. Jumla ya shilingi milioni 236.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**D. Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utaratibu wa kuwapata washauri elekezi wa ujenzi wa kiwanda na uandaaji wa michoro, makisio ya gharama na usimamizi wa ujenzi wa kiwanda; na kuandaliwa kwa vigezo/sifa za kuwapata watengenezaji wa mitambo (pre-qualification).

### 3.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 3.3.3.1 Uzalishaji Viwandani

**(i) Mradi Na. 6103: Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania (Tanzania Automotive Technology Centre - TATC)**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa magari mawili (2) ya zimamoto kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; kuanza kwa maandalizi ya uundaji wa magari matatu (3) mapya ya zimamoto; kutolewa kwa mitambo na vipuri vilivyowasili Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya mradi wa kuzalisha nguzo za chuma na viambata vyake kwa matumizi ya Shirika la Umeme Tanzania; kununuliwa kwa mashine na mitambo na kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kuhifadhi mitambo; kuboreshwa kwa karakana kwa ajili ya tafiti kwa kununua vipuri na kukarabati mitambo; na kufanyika kwa utafiti na uhawilishaji wa teknolojia katika nyanja za kilimo, madini na usafirishaji na kutengeneza zana mbalimbali zikiwemo *Power Tillers, Brake drums and blocks* za treni na vipuri vya pampu za maji. Jumla ya shilingi bilioni 8.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 6260: Mradi wa Kusaidia Taasisi**

**(a) Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mtambo wa kuchemsha vyuma (Galvanizing plant) ambao umefikia asilimia 98; kukamilisha maandalizi ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa tanuru la kuyeyusha chuma (Foundry), na kusimika *overhead crane*; kununuliwa kwa vifaa vya tanuru la kuyeyusha chuma na malighafi za uzalishaji wa awali; kukamilika kwa tathmini ya mfumo wa umeme ili kupata gharama halisi za kufanya ukarabati ambapo kazi hiyo imefanywa na TEMESA; kuendelea na ukarabati wa mashine za kiwanda; na kukamilika kwa mazungumzo kati ya NDC na TANESCO kuhusu uzalishaji wa minara *(Lattice Towers)* na vipuli. Jumla ya shilingi millioni 158.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa mita 580 kuelekea Kiwanda cha Kuzalisha Betri; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa kujenga barabara yenye urefu wa mita 230 kuelekea kwenye kiwanda cha Hester Bioscience(Viuatilifu road); kuanza kwa uzalishaji katika Kiwanda cha Kuunganisha Magari cha *GF Trucks Motors* ambapo jumla ya magari 245 yameunganishwa; kukamilika kwa usanifu wa mahitaji ya maji na umeme kwa eneo la TAMCO; kukamilika kwa ununuzi wa mkandarasi wa kufanya usanifu wa barabara za ndani (design of internal road network) katika eneo lote la TAMCO; na kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha *Hester Bioscience* katika eneo la ekari 201.6 kwa ajili ya kuzalisha chanjo za wanyama. Jumla ya shilingi milioni 29.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Kuendeleza Mashamba na Viwanda vya Mazao ya Mafuta ya kupikia**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa mwekezaji kutoka Korea ya Kusini (GF Oil Company Limited) ambapo Serikali kupitia Ubalozi wa Tanzania Nchini Korea imesaini Makubaliano ya Awali (Memorandum of Understanding) na Kampuni hiyo; kukamilika kwa Mpango Kazi wa Kampuni hiyo na Kuwasilishwa NDC; na kuendelea na utafutaji wa ardhi katika Mkoa wa Kigoma kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

**(d) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa mashine (fork lift) itakayoboreshwa kwa lengo la kurahisisha kazi ya kuvuna chikichi; kufanyika kwa majaribio ya awali (on-station testing) ya mashine ya kutenganisha viini vya chikichi na maganda yake baada ya kubanguliwa; kuboreshwa na kutengenezwa kwa kipandio cha mazao ya aina mbalimbali ambacho kinavutwa na trekta; kufanyika kwa *design optimization* ya sampuli kifani ya mashine 10 za kulima, kupanda, kupura na kuongeza thamani ya mazao; kuwezeshwa kwa wajasiriamali watano (5) kubuni na kutengeneza sampuli kifani za mashine ya kukaushia mbogamboga na matunda, mashine ya kuchakata mazao kwa kutumia *Power Tiller*, mashine ya kuchakata viazi vitamu kwa ajili ya michembe, mashine ya kupura mtama na uwele, mashine ya kukatakata majani (forage chopper) na mashine ya kufunga majani (Bailer) na trekta dogo linaloendeshwa kwa injini ya Pikipiki; kuratibiwa kwa shughuli za kuanzisha Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (Engineering Technology Hubs-ETH) katika

kijiji cha Mwandete Halmashauri ya Wilaya ya Maswa; na kubuniwa kwa aina 10 ya teknolojia mbalimbali kwa matumizi ya *Hub*.

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: kutolewa kwa mafunzo na uwezeshaji kwa wajasiriamali ya kutengeneza teknolojia zilizothibitishwa na zinazohitajika na wadau ambazo ni  mashine za kukatakata malisho ya mifugo (Forage chopper) na kufunga majani kwa ajili ya mifugo (Bailer) na mashine ya kupura mtama na uwele inayokokotwa na Wanyamakazi; kufanyika kwa majaribio ya awali (*piloting)* kwa wadau wa teknolojia za kukatakata na kufunga malisho ya mifugo katika Wilaya ya Karatu; kuhawilisha teknolojia za kukatakata  na kufunga malisho ya mifugo katika Wilaya ya Hai; kufanyika matengenezo ya mashine za Karakana; kuwezeshwa kwa watumishi sita (6) kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (2), Shahada ya uzamili 2(), Shahada ya kwanza (2) na Stashahada (1); na kuwezeshwa kwa watumishi 20 kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi nje ya Kituo. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Usimikaji wa mitambo katika kiwanda cha kukoboa mpunga cha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) Mkuyuni, Mkoani Mwanza umefikia asilimia 90; ujenzi wa majengo ya kiwanda cha kusindika ngozi (tannery) cha Karanga – Moshi umefikia asilimia 93; kutengenezwa kwa ramani za viwanda nchini kwa kuanza na mfano wa Pwani (*industrial mapping*); kufanyika kwa tafiti sita (6) zenye lengo la kuongeza thamani katika malighafi na mazao nchini; na kuatamiwa (*incubation*) kwa wabunifu sita (6) akiwemo mgunduzi wa dawa ya COVIDOL katika kupambana na janga la UVIKO-19.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kupimwa kwa bomba kubwa la mafuta la TPA lililopo bandarini ili kubaini ubora wake; kununuliwa kwa vifaa vya maabara kwa ajili ya tafiti mbalimbali zikiwemo za mazao ya korosho na chikichi; kuhakikiwa kwa ubora wa sampuli 244 za bidhaa mbalimbali za chakula na maji; kuhakikiwa kwa ubora wa makaa ya mawe yanayozalishwa nchini; kubuniwa na kutengenezwa kwa mashine kwa ajili ya kiwanda cha mfano cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua kilo 300 kwa saa; kutolewa kwa mafunzo kwa wadau 350 wa mnyororo wa thamani wa zao la ngozi kuhusu uzalishaji ngozi bora kwa ajili ya soko la ndani na nje; kutolewa kwa mafunzo ya uongezaji thamani katika zao la mwani yaliyofanyika Pemba na kutekeleza mradi wa ubunifu na usambazaji wa vitofali lishe vya kuzalishia uyoga wenye virutubisho *(mushroom substrate blocks);* kuendelea na ujenzi wa jengo la Utawala; na ununuzi wa magari manne (4). Jumla ya shilingi bilioni 1.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa karakana ya TEMDO pamoja na ukarabati wa sehemu ya Ofisi za Ubunifu; kufanyika kwa tafiti tatu (3) za kuendeleza, kuongeza thamani na kubiasharisha mazao ya alizeti, parachichi na chikikichi; kufanyika kwa usanifu wa vifaa vya afya vikiwemo *nommal hospital beds*, *drip stand, examination bed, delivery bed, theatre trolleys, hospital screens* na *bed side lockers* ambavyo

vimepitishwa na Mamlaka za TMDA na MSD*;* kuendelea kutengeneza chasili cha Mtambo wa kutengeneza sukari kwa kiwango cha mjasiriamali wa kati (sugar processing mini-plant); kuendelea na usanifu wa mtambo wa kuchakata zao la mkonge kwa kiwango cha upatikanaji wa nyuzi za katani zinazokidhi viwango vya soko la nje; kutengenezwa na kusimikwa kwa mtambo wa kuchakata alizeti katika Wilaya ya Ngara; kuendelea kuboresha kwa kusanifu upya mtambo wa kuchomea taka kwa ajili ya Hospitali za Wilaya za Nyasa, Bukoba, Busekelo, Chunya, Uhuru Dodoma pamoja na uwanja wa ndege wa Julius Nyerere (JNIA); na kukamilika kwa usanifu wa majokofu ya kisasa mawili ya kuhifadhia maiti ambapo moja lina uwezo wa kuhifadhia maiti tatu (3) na lingine la kuhifadhi maiti sita (6). Jumla ya shilingi bilioni 1.88 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo (SIDO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa ushauri wa kiufundi na biashara kwa wajasiriamali 15,988; kutolewa kwa mikopo 1,366 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.39 ambapo asilimia 48 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa wanawake. Mikopo hiyo ilizalisha fursa za ajira 3, 458. Aidha, wastani wa urejeshaji wa mikopo umefikia asilimia 92; kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya viwanda katika mikoa ya Morogoro (majengo 2); Mwanza (Jengo 1) na Katavi (majengo 2); kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara, mifumo ya majitaka na safi, umeme na kukamilika kwa ujenzi wa uzio katika maeneo ya SIDO kwenye mikoa ya Kagera, Geita, na Kigoma; kuagizwa kwa mashine na mitambo ya kisasa kwa ajili ya Kituo cha Uendelezaji wa Teknolojia cha Iringa; kuzalishwa kwa mashine 1,465 za aina mbalimbali kupitia Vituo vya Kuendeleza Teknolojia (TDCs) kwa ajili ya viwanda vidogo; na kutolewa kwa mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara, kuongeza tija viwandani na hati miliki kwa wajasiriamali 21,610 kupitia kozi 729.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa michoro na makadirio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya kujenga majengo ya viwanda *(industrial sheds)* katika mikoa ya Dodoma, Simiyu, Mtwara, Tanga na Shinyanga; na kuunganisha mikoa mingine 10 ya Lindi, Dar es Salaam, Iringa, Ruvuma, Shinyaga, Kigoma, Geita, Mwanza, Kilimanjaro na Tanga kwenye mtandao unganifu. Jumla ya shilingi milioni 731.89 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Katika Uchumi wa Viwanda**

**Kilimanjaro International Leather Industries Co Ltd (KLICL)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi inayojumuisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya kiwanda cha kuchakata ngozi, ghala na nyumba ya kufua umeme pamoja na ufungaji wa mashine za kutengeneza viatu; kuendelea na majaribio ya mashine pamoja na mafunzo ya waendeshaji wa mashine; kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi inayojumuisha kiwanda cha kuchakata ngozi, jengo la maabara, kantini na miundombinu ya chanzo cha maji ya chemichemi na mtambo wa kutibu maji taka (Effluent Treatment Plant - ETP). Jumla ya shilingi bilioni 118.96 zimetumika hadi Januari 2022.

**Kiwanda cha Nyama cha Nguru - Morogoro**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la kiwanda; kukamilika kwa

maboresho ya mfumo umeme na ufungaji wa mitambo ya kuchinjia; kukamilika kwa utengenezaji wa majokofu; kukamilika kwa ufungaji na uunganishaji wa umeme; na kuendelea na ufungaji wa mashine. Jumla ya shilingi bilioni 8.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi cha 'Mamba Ginger Factory Limited'**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya kiwanda; kukamilika kwa uunganishaji wa umeme mkubwa na ufungaji wa mashine; kuendelea na majaribio ya mashine na mafunzo kwa waendeshaji mashine. Jumla ya shilingi bilioni 1.55 zimetumika hadi Januari 2022.

**Kiwanda cha Chai cha Mponde - Tanga**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la kiwanda, sehemu ya usindikaji na karakana; na kuendelea na taratibu za ununuzi wa vipuri na vifaa vya ujenzi ili kukamilisha ukarabati wa mashine na mitambo. Jumla ya shillingi 250 milioni zimetumika hadi Januari 2022.

**(i) Maeneo Mengine Maalumu ya Uwekezaji (SEZ/EPZ)**

**Mradi Na. 4933: Uendelezaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi**

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Tanga**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utambuzi wa mipaka, upimaji na uthamini wa eneo; ulipaji wa sehemu ya fidia; na kuendelea na taratibu za kuzuia uvamizi wa eneo.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Kigoma**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe wa uendelezaji wa eneo; upimaji wa viwanja 401 vya uwekezaji katika eneo la hekta 691; kukamilika kwa upatikanaji wa hati pamoja na kuendelea na kutafuta wawekezaji. Vile vile, Kampuni tatu (3) zimepewa leseni na kuanza uwekezaji katika eneo hilo ambazo ni *Third Man Limited* kwa ajili ya uchakataji wa asali na nta, *Next Gen Solawazi Ltd* ya uzalishaji wa nishati ya umeme wa nguvu ya jua na *SGC Investment Ltd* inayochakata zao la chikichi.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Kahama**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upimaji wa eneo na kuidhinishwa kwa michoro; na kukamilika kwa andiko la mradi pamoja na kutangazwa rasmi kwa eneo kuwa Eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi na kupewa leseni ya Mamlaka ya EPZ.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Bunda**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upimaji na kuweka mipaka ya eneo la mradi. Aidha, taratibu za upatikanaji wa hati zinaendelea kutekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa utambuzi wa maeneo yanayopendekezwa kuwa Kanda Maalum za Kiuchumi; kuendelea na majadiliano baina ya Uongozi wa Mkoa na TBA ili kulitangaza eneo la ekari 600 lililopo Tunduma, Wilaya ya Momba linalomilikiwa na TBA kuwa Ukanda Maalum wa Kiuchumi; na kutolewa kwa mafunzo kwa Viongozi na wataalamu 15 wa Mkoa wa Songwe kuhusu uendelezaji wa Maeneo Maalumu ya Kiuchumi.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Manyara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upimaji wa mipaka ya eneo la mradi na kupitishwa na Mamlaka husika; kukamilika kwa uwekaji wa alama za mipaka kuzunguka eneo la mradi lenye Hekta 511 katika pande zote zinazopakana na kijiji cha Kandasikra (Simanjiro); kukamilika kwa taratibu za kukabidhi eneo lenye ukubwa wa ekari 250 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro lilotengwa kwa ajili ya kuwezesha shughuli za biashara ya uuzaji, ununuzi, ukataji na ung'arishaji wa madini ya Tanzanite na madini mengine ya vito yanayopatikana Mirerani; na kukamilika kwa tathmini ya nyaraka za zabuni ili kumpata mtaalamu mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu na kuandaaa Mpango Kabambe wa eneo la mradi.

**Eneo Maalumu la Uwekezaji Mtwara *Free Port Zone***

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara za ndani ya eneo la mradi yenye urefu wa kilomita moja (1.06); na kukamilika kwa usanifu wa jengo la Kituo cha Pamoja cha Huduma *(*One Stop Center Building*)*.

**(j) Mradi Na. 4486: Uzalishaji Viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa msingi na kuendelea na ujenzi wa kuta za jengo la viwanda kwa ajili ya wajasiriamali; kufanyika kwa kongamano la wadau wa Alizeti Mkoani Singida; na kuendelea kuhamasisha utengaji wa maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vya mafuta ya kupikia.

### 3.3.3.2 Huduma za Biashara

**Mradi Na. 4933: Kituo cha Biashara na Ugavi Kurasini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa malipo ya fidia kwa wakazi watatu (3) ambao hawakulipwa awali; kupatikana kwa hati ya eneo la mradi; kukamilika kwa ujenzi wa uzio wa muda na kuanza ujenzi wa ukuta wa kudumu ambapo tayari ujenzi wa msingi mita 1,025 umekamilika kati ya mita 2,636; kuendelea na utangazaji wa eneo kwa lengo la kualika makampuni ya kitaifa na kimataifa kuendeleza eneo la Kurasini *Industrial, Trade and Logistic Park*; kupatikana kwa Mshauri Elekezi (Consultant) kwa ajili ya kuandaa Mpango Kabambe, kufanya tathmini ya Kimkakati ya Athari za Mazingira (SEA) na Usanifu wa Kina wa Miundombinu. Jumla ya shilingi milioni 337.2 zimetumika hadi Januari 2022.

#### 3.3.3.3 Masoko

**(a) Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa jumla ya leseni 38 za waendesha ghala ambapo leseni 33 kwa zao la korosho ambazo ziliwezesha ukusanyaji wa kilo 229,851,869, leseni nne (4) kwa zao la dengu na kuwezesha kukusanya kilo 646,130.50 na leseni moja (1) kwa zao la kakao zilizofanikisha kukusanywa kwa kilo 3,631,140; na kutolewa miongozo miwili ya Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi ya Mwaka 2021/22 Toleo la kwanza na Mwongozo wa Biashara kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala wa Mwaka 2021 kwa mazao ya Choroko, Soya, Ufuta, Mbaazi na Dengu.

**Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) - TANTRADE**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuratibiwa kwa Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(Dar es Salaam International Trade Fair - DITF)* ambayo yalijumuisha washiriki 3,002 (2,926 wa ndani na 76 kutoka nchi 17); kuzinduliwa kwa Mfumo wa utoaji wa Taarifa za Biashara (Trade Information Portal) kwa njia ya mtandao ambapo mfumo umelenga kuwezesha upatikanaji wa taarifa na taratibu za kufuata kupata leseni na vibali mbalimbali vya biashara za kimataifa (*Export, Import and Transit Procedures and Documentation*). Mfumo huo una jumla ya watumiaji 70,258 na watembeleaji 217,528 kutoka ndani na nje ya nchi; kuzinduliwa kwa Duka Mtandao (e-commerce shop) ambapo jumla ya wafanyabiashara 130 wamejiunga na mfumo huo; kuzinduliwa kwa Nembo ya Taifa ya Viungo; kufanyika kwa uratibu wa mikutano ya wafanyabiashara kwa wafanyabiashara kwa njia ya mtandao (B2B) ambapo sekta ya mazao ya matunda (parachihi na zabibu), Nyama, viungo vya chakula na Ngozi vilijadiliwa; na kuhudumia wafanyabiashara 121 kupitia Kliniki ya Biashara ambapo changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyabiashara zilishughulikiwa.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Maonesho ya Sita ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania yaliyofanyika Mjini Unguja Zanzibar ambapo jumla ya viwanda 131 vilishiriki kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini na kuwakutanisha wenye Viwanda na wanunuzi; kuratibiwa kwa kampuni 382 kushiriki misafara minne (4) ya biashara, Kongamano moja (1) na Maonesho mawili (2) ya kibiashara nje ya nchi katika nchi za Kenya, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uturuki, Uingereza, Afrika Kusini na Saudi Arabia; na kuandaliwa kwa rasimu ya awali ya Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Nje.

**Ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya EXPO - DUBAI**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezeshwa kwa ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Dunia ya Expo 2020 Dubai Kuanzia Octoba 1, 2021 hadi Marchi 31, 2022 ambapo jumla ya taasisi 18 za umma na kampuni 11 kutoka sekta binafsi zinashiriki kutangaza fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji katika sekta za Madini, Utalii na kilimo; kuwezeshwa kwa upatikanaji wa masoko ya uhakika na endelevu ya bidhaa zinazozalishwa nchini ambapo kampuni nane (8) za Kitanzania zimefanikiwa kuingiza bidhaa zao kwenye mtandao wa *World Souq* kwa ajili ya mauzo kupitia soko la mtandao; na kuratibiwa kwa mikutano 53 na programu 11 zinazohusisha sekta mbalimbali na kutoa fursa kwa wadau

kujenga mitandao ya kibiashara na uwekezaji pamoja na maeneo mbalimbali ya ushirikiano. Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa - TBS**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa vifaa vya maabara 142 vya aina mbalimbali, seti 17 za vifaa vya kukagua magari yaliyotumika hususani *portable/mobile motor vehicle Inspection equipment*; kuwajengea uwezo wataalamu 94 wa maabara na udhibiti ubora wa bidhaa kupitia mafunzo ya ndani na nje ya nchi; na kutolewa kwa mafunzo na semina 176 kwa washiriki 11,809 kuhusu kuhamasisha matumizi ya viwango vya ubora, sayansi, teknolojia na ubunifu kwa wazalishaji mbalimbali na waagizaji wa bidhaa.

### 3.3.3.4 Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II

### A. Kilimo

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II**

**(i) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika skimu tatu (3) za Mkombozi (Iringa), Idudumo (Nzega) na Ilemba (Sumbawanga); kufanyika kwa Tathmini ya Athari ya mradi kwa Mazingira katika skimu ya Mkombozi; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa skimu za Kirya (Mwanga) na Endagaw (Hanang') ambazo utekelezaji wake umefikia asilimia 25 na 3.6 mtawalia; kuendelea na taratibu za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa skimu za Usense (Nsimbo) na Misufini (Morogoro); kuanzishwa na kusajiliwa kwa vyama 27 vya umwagiliaji katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Tanga, Kilimanjaro na Kigoma na kutolewa mafunzo ya kuandaa kanuni ndogo ndogo za uendeshaji wa vyama hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 (2013) na kanuni zake; kusambazwa kwa miongozo ya uanzishaji na usimamizi wa vyama vya umwagiliaji kwenye skimu 70 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe na Ruvuma; kutolewa kwa mafunzo ya ukusanyaji wa ada za huduma za umwagiliaji kwa wataalamu 49 (DAICOs), wahandisi wa mikoa na wilaya kutoka katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Iringa na Mbeya; na kutolewa kwa mafunzo ya ukusanyaji wa ada na tozo za umwagiliaji kwenye skimu 450 katika mikoa 11. Jumla ya shilingi milioni 349.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Kuwezesha Uanzishwaji wa Mashamba Makubwa ili kuwa Kitovu Cha Teknolojia Bora kwa Wakulima Wadogo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuhakikiwa kwa mashamba 67 yenye ukubwa wa hekta 205,432.45 ambayo kila moja lina ukubwa wa kuanzia hekta 50; kuhakikiwa na kutambuliwa kwa mashamba manne (4) ya NAFCO yaliyopo Kilimanjaro (Jouney's end - ekari 1,670, Fosters - ekari 727, Harlingto - ekari 1,237, Kanamodo - ekari 2,203) na Manyara (Basuto ekari 13,142.5); kuanishwa kwa mashamba 50 yenye ukubwa kuanzia ekari 50 katika bonde la mto Kilombero katika Halmashauri za mji Malinyi, Ulanga na Mlimba; na kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima na wadau 265 kuhusu teknolojia za matumizi bora

ya ardhi ya kilimo ikiwemo hifadhi ya maji na udongo mashambani. Jumla ya shilingi milioni 28.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo ya maafisa ugani 40, kuhusu namna ya kujumuisha shughuli za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi kwenye mipango ya Halmashauri katika Wilaya za Mkalama, Manyoni, Ikungi na Iramba (Singida) na Busega, Bariadi, Meatu na Maswa (Simiyu) na kusambazwa kwa Mwongozo wa mabadiliko ya tabianchi katika halmashauri hizo; kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima 250 katika vijiji 10 vya halmashauri ya wilaya ya Karatu kuhusu mazingira, kuwawezesha kuibua changamoto za kimazingira zinazotishia uhifadhi wa Ziwa Manyara na kuwasaidia kutengeneza mipango ya usimamizi wa mazingira na jamii (ESMPs) ili kutatua changamoto hizo; na kuendelea na hatua za ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya uchimbaji wa visima vitatu (3) vya umwagiliaji katika halmashauri ya Mpwapwa. Jumla ya shilingi milioni 21.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iv) Kuimarisha Huduma za Ugani na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

**Kuongeza Matumizi ya Teknolojia Bora katika Uzalishaji wa Mazao ili Kuongeza Uzalishaji na Tija**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupitishwa kwa aina mpya 28 za mbegu bora na Kamati ya Mbegu ya Taifa; kuendelea na taratibu za ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya kituo cha Kilimo Anga; kusajiliwa kwa viuatilifu vipya 83 ambavyo ni viuadudu 38, viuagugu 19, viuatilifu vya kudhibiti ukungu 22 na visaidizi vya mbolea (growth regulators); na kusajiliwa kwa wadudu marafiki tisa (9) kwa ajili ya utafiti. Jumla ya shilingi milioni 16.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Kuimarisha Vituo vya Utafiti, Utafiti wa Mbegu Bora, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima na Huduma za Ugani**

**(a) Kuimarisha Vituo vya Utafiti**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa mkandarasi wa kujenga ofisi na nyumba tatu (3) za TARI Kihinga- Kigoma; kununuliwa kwa vifaa na vitendanishi vya maabara ya udongo ya TARI Mlingano; na kupatiwa ufadhili kwa watafiti 43 wa masomo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi, kati ya hao 19 ni shahada ya uzamivu, 19 shahada ya uzamili na watano (5) shahada ya kwanza. Jumla ya shilingi milioni 349.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Utafiti wa Mbegu Bora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupendekezwa kwa aina za mbegu 21 kati ya 28 na kuwasilishwa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu - TOSCI kwa ajili ya uhakiki kabla ya kupelekwa kamati ya Mbegu ya Taifa kwa maamuzi, kati ya mbegu hizo 11 ni za ngano, mbili (2) mpunga, tano (5) maharagwe na tatu (3) mchicha; kuzalishwa kwa miche 7,445,602 ya mazao ya parachichi, korosho, miembe, michungwa, michikichi, mkonge na minazi;

kuzalishwa na kusambazwa kwa wakulima mazao mengine ya miti yenye ukinzani dhidi ya magonjwa; na kuzalishwa kwa jumla ya tani 135.4 za mbegu za ngano. Jumla ya shilingi milioni 53.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(vi) Kuimarisha Huduma za Ugani na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

**(a) Kuimarisha Vyuo vya Mafunzo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa ufadhili kwa wanafunzi 2,450 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo; kuendelea na ukarabati wa majengo ya vyuo vya kilimo vya Uyole, Inyala, KATC, KATRIN, Ilonga na Mubondo; kuendelea na taratibu za ununuzi wa trekta na zana zake kwa vyuo vya kilimo vya Uyole, Tumbi, Mlingano, Ilonga na Mtwara; kuendelea na tathmini na taratibu za ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa vyuo vya kilimo vya Uyole, Ilonga, Tumbi na Ukiriguru; kuwezeshwa kwa wakufunzi 12 na wakufunzi sita (6) katika mafunzo ya shahada ya uzamili na shahada ya kwanza mtawalia; kuendelea na utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa udahili wa wanafunzi kwa ajili ya vyuo 14 vya mafunzo ya kilimo ambapo mfumo huo upo katika hatua za majaribio; kuwezeshwa kwa wakufunzi kilimo 113 kuhudhuria katika mafunzo ya muda mfupi, kuhusu mbinu za kufundishia. Jumla ya shilingi milioni 332.8 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Kuimarisha Huduma za Ugani na Vituo vya Mafunzo ya Wakulima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa maafisa ugani 1,795 kuhusu kilimo bora cha alizeti na pamba katika mikoa ya Dodoma, Singida, Simiyu, Kilimanjaro, Kigoma na Manyara; kuendelea na taratibu za ununuzi wa pikipiki 2,000 kwa ajili ya maafisa ugani; na kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa simu janja 384, kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya ugani 3,483 (Sprayers, Gumboots na Overcoats) na kifaa cha kupima Afya ya Udongo (Agrocares Scanner) 143 katika mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu. Jumla ya shilingi milioni 120.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(vii) Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Zana za Kilimo na Pembejeo**

**(a) Zana za Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarishwa kwa mfumo wa upatikanaji wa zana za kilimo na pembejeo kupitia Mfuko wa Pembejo (AGITF) ambao umewezesha kutoa mikopo 18 ambapo mikopo ya matrekta ni miwili (2), pembejeo miwili (2), mitambo ya kuongeza thamani ya mazao mmoja (1) ujenzi wa miundombinu ya shamba miwili (2), ufugaji na uvuvi minne (4), *powertiller* moja (1) na uendeshaji mmoja (1); kuandaliwa kwa Sheria ya zana za kilimo ambayo ipo katika hatua ya kupata maoni ya wadau; kutambuliwa kwa mahitaji ya zana za kilimo katika Halmashauri za Wilaya za Korogwe, Mvomero na Kilosa hususan katika hatua za upandaji, upaliliaji na uvunaji; kukamilika kwa taratibu za ununuzi wa matrekta mawili (2) na zana zake, mashine mbili (2) za kupandia, mashine (2) za kunyunyuzia dawa na mashine mbili (2) za kuvunia; kutolewa kwa mafunzo ya matumizi bora ya zana za kilimo katika uzalishaji wa zao la alizeti kwa maafisa ugani 258 katika Halmashauri 18 za Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara; na kufanyika kwa tathmini ya mahitaji ya malighafi ya viwanda vya kusindika mafuta (alizeti) katika Mikoa ya Singida, Dodoma na Manyara kwa ajili ya viwanda vidogo. Jumla ya shilingi milioni 833.0

zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mbegu Bora za Mazao**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa mbegu bora tani 29,137.65 ambazo ni nafaka, kunde, mbegu za mafuta na mboga ambapo tani 14,968.50 zimezalishwa hapa nchini, tani 10,746.4 zimeagizwa kutoka nje ya nchi na tani 3,422.80 ni bakaa ya msimu uliopita; kuzalishwa kwa vipando vya mihogo 12,307,837; kuhakikiwa ubora *(standard seed*) na kusambazwa kwa wakulima kwa jumla ya tani 2,088 za mbegu za alizeti kupitia ASA; na kufunguliwa kwa maeneo mapya ya mashamba yakuzalisha mbegu yenye jumla ya hekta 2,100 kupitia ASA ambayo ni 100 (Namtumbo), 50 (Bugaga), 100 (Msungura), 3,000 (Kilimi), 300 (Mwele) na 1,250 (Msimba). Jumla ya shilingi bilioni 2.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mbolea**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa mbolea tani 409,232 sawa na asilimia 59% ya mahitaji ya tani 698,260 ya msimu wa 2021/22, kati ya tani hizo, tani 259,170 zimeingizwa kutoka nje, tani 32,162 zimezalishwa ndani na tani 117,900 ni bakaa ya msimu wa 2020/21; kuuzwa kwa mbolea tani 173,957 ndani na tani 43,175 nje ya nchi, na kuendelea kuuza tani 192,100; kuhakikiwa kwa jumla ya vibali 59 vya kusafirisha mbolea nje ya nchi vyenye jumla ya tani 43,175 za mbolea katika mipaka ya Tarakea, Holili, Horohoro, Namanga, Tunduru, Kabanga na Rusumo; kusajiliwa kwa wafanyabiashara 1,583 na kukaguliwa kwa wafanyabiashara 2,031 Tanzania Bara kwenye eneo la leseni na ubora wa mbolea; kutolewa kwa mafunzo ya uhifadhi ubora wa mbolea kwa wafanyabiashara wa mbolea 2,988 Tanzania Bara; na kuendelea na ujenzi wa maabara ya mamlaka ya usimamizi wa mbolea – TFRA katika hatua ya kumwaga sakafu ya kwanza (suspended slab) ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 38. Jumla ya shilingi milioni 8.9 fedha ndani zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Viuatilifu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukaguliwa kwa maduka 233 na shehena za viuatilifu 149 ili kutathmini aina na ubora wa viuatilifu vinavyouzwa; kutolewa kwa vibali 681 kwa wafanyabiashara wa viuatilifu; kununuliwa kwa mashine *Microwave Plasma - Atomic Emission Spectrometer* (MP-AES) yenye uwezo wa kuchambua sampuli za mbolea, maji na udongo katika Mamlaka ya Usimamizi wa Afya ya Mimea na Madawa Tanzania - TPHPA; kufanyika kwa majaribio 88 ya kisayansi (bioefficacy field trials) kwa viuatilifu vipya; kutolewa kwa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima, maafisa ugani na wauzaji wa viuatilifu 306 kutoka maeneo mbalimbali nchini; kutolewa kwa mafunzo ya matumizi sahihi ya mabomba ya kunyunyizia na vinyunyizi kwa wadau wa kilimo. Jumla ya shilingi milioni 978.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(viii) Kuimarisha Miundombinu ya Kuhifadhi Mazao ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa ghala la Kiteto lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao; kukamilika kwa ukarabati wa vihenge Arusha vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 38,000 na ghala la Mbugani - Dodoma lenye uwezo wa kuhifadhi

tani 30,000 za nafaka; na kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kiwanda cha kukoboa mpunga Mwanza. Jumla ya shilingi milioni 891.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ix) Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuchakatwa kwa tani 2,990.26 za mahindi na tani 1,099.70 za alizeti ambapo jumla ya tani 4,089.96 za nafaka zilioongezewa thamani; kukamilika kwa usimikaji wa kiwanda cha kusindika mpunga Mwanza ambacho kipo katika hatua za majaribio; na kuzalishwa kwa bidhaa zitokanazo na korosho (*Roasted cashew kernels, White cashew kernels* na *Cashew apple wine)* ambazo zimekidhi viwango vya kimataifa. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(x) Upatikanaji wa Masoko ya Ndani na Nje ya Nchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa tani 23,132.07 za mahindi kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; kuuzwa kwa jumla tani 183.22 za maharagwe, tani 215.96 za mchele, tani 1,023.70 za mbegu za alizeti; kufunguliwa kwa kituo cha mauzo katika mji wa Juba - Sudan Kusini na masoko katika nchi za DRC, Kenya, Zimbabwe, Rwanda, Burundi na Comoro; kupatikana kwa ghala Lubumbashi (DRC) lenye ukubwa mita za mraba 680 kwa ajili kuhifadhi mazao yatakayopelekwa sokoni; kufanyika kwa tathmini ya mwelekeo wa bei za mazao ya ufuta na mbaazi katika minada kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara na kuonyesha ongezeko la shilingi 2,100 mwaka 2020/21 hadi shilingi 2,800 mwaka 2021/22 kwa kilo; kuongezeka kwa mapato yatokanayo na *CESS* katika zao la ufuta na kufikia shilingi bilioni 3.8 na shilingi milioni 320 katika mikoa ya lindi na Mtwara; kuongezeka kwa uuzaji wa soya katika nchi za China, India, Rwanda na Kenya na kufikia tani 53,594.35 mwaka 2020/21 ikilinganishwa na tani 2,647 mwaka 2019/20; kusainiwa kwa hati ya makubaliano ya miaka mitano na Kampuni ya *Smart Import and Export* ya Misri ili kuwauzia mahindi ya njano kiasi cha tani 1,000,000; na kuuzwa kwa tani 214, 445 za zao la korosho, tani 144,405 za zao la pamba na tani 6,367.8 zao la kakao. Jumla ya shilingi bilioni 2.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xi) Kuboresha Mifumo ya Kitaasisi, Bodi na Sheria**

**(a) Sera, Sheria na Mikakati ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa tathmini ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2013; kuandaliwa kwa rasimu ya muundo wa taasisi na kanuni zake kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya mwaka 2020; na kuendelea na hatua za kufufua Kampuni ya Mbolea Tanzania na Mkakati wa Ubinafsishaji wa Mashamba ya Kilimo yaliyokuwa chini ya Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula. Jumla ya shilingi milioni 86.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mifumo ya Kielektroniki ya kutoa huduma katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarishwa kwa matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma za ugani na masoko kwa kutumia mfumo wa M-Kilimo na kutolewa huduma za biashara ya mazao kwa kutumia mfumo wa *Agriculture Trade Management Information System* (ATMIS); kutolewa mafunzo kwa maafisa ugani 1,375 kuhusu Matumizi ya mfumo; kusajiliwa kwa wakulima na wanunuzi 147,303 wa mazao kwenye mfumo na

kutoa ushauri kwa wakulima 6,659 juu ya kilimo bora kulingana na maswali yaliyoulizwa kupitia mfumo; kuboreshwa kwa mfumo wa ATMIS na kupatikana muda wote na ambao umewezesha utoaji wa huduma bora kwa wateja; kupatikana kwa mawasiliano ya huduma ya Intaneti kwa vituo vyote vya PHS vilivyopo mipakani na vitendea kazi vya TEHAMA; na kutolewa elimu kwa watumiaji wa mfumo na kutatua changamoto mbalimbali. Jumla ya shilingi milioni 260.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuundwa kwa kamati ya viongozi ya kushughulikia upatikanaji wa mitaji katika sekta ya kilimo kwa kupunguza riba ya mikopo. Matokeo ya kamati hiyo ni Benki Kuu kuongeza ukwasi wa shilingi trilioni moja (1) katika mabenki ya biashara, hatua hiyo imewezesha NMB kutenga bilioni 100 kwa ajili ya kukopesha wajasiriamali katika sekta ya kilimo kupitia matawi yake 225 nchini; kufanyika kwa mapitio ya sera ya mikopo katika mfuko wa pembejeo; na kuendelea na utafiti wa kubaini maeneo yenye changamoto na kushauri mikakati ya kukabiliana nayo.

**(d) Bima ya Mazao**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa tathmini ya bima ya mazao kwa wakulima wadogo wa zao la mahindi katika mikoa ya Manyara (Babati na Kiteto), Dodoma (Mpwapwa na Kongwa), Singida (Ikungi na Iramba) na Morogoro (Kilosa na Mvomero). Lengo ni kupata taarifa halisi za wakulima wadogo zitaazoiwezesha Serikali na wadau wengine kuzingatia changamoto halisi za wakulima wadogo katika kuandaa mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwemo huduma ya bima ya mazao; na kuendelea na mikakati ya kupata uzoefu wa huduma ya bima ya mazao kwa wakulima ili kuboresha huduma ya bima ya mazao nchini.

**(xii) Kuimarisha Usimamizi wa Maendeleo ya Ushirika**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukaguliwa na kuchukuliwa kwa hatua stahiki kwa vyama 6,095 vya ushirika na Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika – COASCO; kuandaliwa kwa andiko la uuzaji wa mazao jamii ya mikunde (choroko na dengu) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, katika mikoa ya kanda ya ziwa; kutolewa kwa mafunzo kwa watendaji na viongozi wa vyama vya ushirika Dodoma ili kuwajengea uwezo katika utafutaji wa fursa za masoko na biashara pamoja na taratibu za kusafirisha bidhaa nje ya nchi; kuendelea na ufufuaji wa viwanda vya kukamua mchuzi wa zabibu katika vyama vya ushirika vya CHABUMA, GAWAYE na UWAZAMAA ili kuongeza thamani na bei ya zabibu; kufufuliwa kwa viwanda vya kuchakata Pamba vya vyama vikuu vya ushirika vya KACU - Kahama, Chato - Geita na Mbogwe - Bukome; kutolewa mafunzo kwa maafisa ushirika 83 kuhusu usimamizi wa vyama vya ushirika; kutolewa leseni kwa SACCOS 164 zilizokidhi matakwa ya sheria ya huduma ndogo ya fedha ya mwaka 2018; kutolewa kwa mafunzo na kuhamasisha washirika 1,703 kuhusu taratibu za kuanzisha chama cha ushirika kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya ushirika; kufanyika kwa upembuzi yakinifu wa uhamasishaji wa uanzishaji wa vyama vya ushirika vya ufugaji nyuki na viwanda vidogo vya kuchakata mazao ya asali katika Tarafa ya Ngorongoro iliyopo ndani ya hifadhi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na jumla ya vikundi 60 vya ufugaji

nyuki vimefikiwa ndani ya hifadhi hiyo; kutolewa mafunzo kwa wana kikundi 800 wafugaji ndani ya Tarafa ya Ngorongoro kuhusu ufugaji nyuki na jumla ya Mizinga 1,476 imetolewa kwa vikundi vyote. Jumla ya shilingi milioni 958.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 4499: Kudhibiti Sumukuvu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengwa kwa maghala 14 katika mikoa 10 ya Kigoma, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Ruvuma, Tabora, Manyara, Geita, Simiyu na Morogoro yenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500 za mahindi na karanga ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 16 na 70 mtawalia; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Kibaiolojia - Kibaha ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 59; na kutolewa kwa mafunzo kuhusu madhara ya sumukuvu kwa wakufunzi (*TOT*) na wadau 252 wakiwemo Wabunge kutoka Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kikundi cha Wabunge vinara wa usalama wa chakula na lishe, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, maafisa wa sekretarieti ya bunge, wakuu wa idara na vitengo - Wizara ya Kilimo na maafisa ugani. Jumla ya shilingi bilioni 4.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4497: Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka**

Hatua iliyofikiwa ni: Kujengwa kwa vihenge (silos) kwa ajili ya kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kutoka tani 251,000 hadi tani 501,000 katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga Babati, Mpanda, Sumbawanga na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88.64; na kuendelea na ukarabati wa maghala katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga Babati, Mpanda Sumbawanga na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65.38. Jumla ya shilingi bilioni 12.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**B. Mifugo**

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

**(a) Kuimarisha Huduma za Ugani**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa gari moja (1) ajili ya uratibu wa ugani na pikipiki 300 kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kuboreshwa kwa mfumo wa kielektroniki wa M-Kilimo kwa kujumuisha mahitaji ya ugani wa sekta ya mifugo. Jumla ya shilingi milioni 864 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Kuimarisha Huduma za Tafiti**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na tafiti na tathmini za teknolojia bora saba (7) za ng'ombe chotara wa maziwa uliowezesha kuzalishwa kwa ng'ombe bora 14 chotara wa maziwa; kufanyika kwa utafiti wa teknolojia bora sita (6) za ng'ombe chotara kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na kuwezesha kuzalisha ng'ombe 45; kufanyika kwa utafiti wa teknolojia bora tatu (3) za mbuzi kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na maziwa ambapo jumla ya mbuzi chotara 40 aina ya *MalyaBlended, Gogowhit*e, Buha, *Norwegian* na *Parewhite* walizalishwa; na jumla ya sampuli 2,113 zimekusanywa kutoka kwa ng'ombe kwa ajili ya kufanyika uchambuzi wa vinasaba (DNA Genotyping); na kununuliwa kwa gari moja (1)

kwa ajili ya kuwezesha masuala ya utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) makao makuu, Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 340 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Kuimarisha Tiba na Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa majosho 95 katika mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa; kuanza kwa ujenzi wa majosho 73 katika halmashauri 58; kununuliwa kwa vifaa vya maabara kwa ajili ya jengo jipya la maabara ya Taasisi ya Chanjo Tanzania - TVI; kuanza kwa ujenzi wa jengo la maabara ya kituo cha Wakala wa Maabara za Veterinari Tanzania – TVLA, Iringa ambapo jengo limeshapauliwa, uwekaji wa vyuma vya milango na madirisha (gril) unaendelea; kuendelea na hatua za uzalishaji wa mbegu kuu ya chanjo ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65; kuzalishwa na kusambazwa kwa dozi 43,409,600 za chanjo dhidi ya magonjwa ya Mdondo, Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Homa ya Mapafu ya Mbuzi, Kimeta, Chambavu, Mchanganyiko wa Kimeta na chambavu na Kutupa Mimba. Jumla ya shilingi bilioni 1.805 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Kuboresha Huduma ya Uhimilishaji Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa basi dogo kwa ajili ya kuwezesha mafunzo na mazoezi ya uhimilishaji kwa vitendo katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji- *NAIC*; kuzalishwa kwa jumla ya dozi 50,261 za mbegu za mifugo na kusambazwa kwa dozi 31,380 katika mikoa 19 kwa ajili ya uhimilishaji. Jumla ya shilingi milioni 502.09 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kulimwa hekta 500 za malisho ya mifugo katika ranchi ya Kongwa, Ruvu na West Kilimanjaro; kuzalishwa kwa jumla ya ndama 1,939 katika Ranchi za Kikulula (45), Misenyi (70), Kongwa (1,274), Ruvu (117), Mkata (13), West kilimanjaro (99), Mzeri (27) na Kalambo (294); kuuzwa kwa jumla ya ng’ombe 1,812 ambapo Misenyi (186), Kongwa (819), Ruvu (477), Mkata (35), West Kilimanjaro (109) na Kalambo (186); na ununuzi wa gari moja kwa ajili ya ofisi ya NARCO makao makuu. Jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Kujenga Machinjio ya Kisasa na Minada ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa machinjio ya Dodoma hususan sehemu ya kuchinjia mifugo. Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya mifugo katika minada 18 ya Pugu (Dar es Salaam), Wasso (Arusha), Gendi (Manyara), Meserani (Arusha), Horohoro (Tanga), Ndelema (Tanga), Chamgoi (Pwani), Kizota (Dodoma), Igunga (Tabora), Ipuli (Tabora), Nyamatala (Mwanza), Malampaka (Simiyu), Kirumi (Mara), Magena (Mara), Lukole (Kagera), Mutukula (Kagera), Buhigwe (Kigoma) na Kileo (Kilimanjaro) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 25. Jumla ya shilingi milioni 326.71 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa mabwawa ya Chamakweza (Pwani), Kimokua (Longido) na Narakauo (Simanjiro); kuanza kwa ujenzi wa malambo manne (4)

katika maeneo ya Kimambi Liwale Lindi (1); Matekwe Nachingwea Lindi (1); Msaginia Nsimbo Katavi (1) na Mhanga Itigi Singida (1); kuanza kwa uchimbaji wa visima vitano (5) katika maeneo ya Makatapola (Iringa), Matanzi (Pwani), Kinamwigulu (Simiyu), Muhukulu Lilai (Ruvuma) na Lwami (Kilimanjaro). Jumla ya shilingi milioni 255 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Kuboresha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa vyumba viwili (2) vya mihadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 240 katika Kampasi ya Tengeru ambapo ujenzi umefikia asilimia 70; kuendelea na ujenzi wa hosteli mbili (2) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 208 kila moja katika Kampasi za Mpwapwa na Morogoro ambapo ujenzi umefikia asilimia 60 na 40 mtawalia; na kukamilika kwa ukarabati wa majengo ya utawala na mabweni katika Kampasi za Buhuri, Morogoro, Madaba na Mabuki. Jumla ya shilingi milioni 334 zimetumika hadi Januari 2022 kwa upande wa ujenzi wa vyumba viwili vya mihadhara katika kampasi ya Tengeru na shilingi milioni 980 kwa ajili ya ujenzi wa hosteli mbili katika kampasi za Mpwapwa na Morogoro.

## C. Uvuvi

**Mradi Na. 4702: Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kubainishwa kwa eneo la ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko lililopo katika Halmashauri ya Kilwa; kukamilika kwa upembuzi wa awali; kuundwa kwa Kamati ya Watalaam ya Usimamizi wa mradi; na kukamilika kwa tathmini ya athari ya mazingira na kijamii.

**Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa tathmini ya hali ya majengo ya makao makuu ya TAFICO; kukamilika kwa Mpango Biashara wa ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ambao umeainisha miradi 10 ya kimkakati; kuanza kwa ukarabati wa ofisi za Shirika ikiwemo jengo la sasa la utawala; kuandaliwa kwa michoro na makadirio ya gharama za jengo la mtambo wa kuzalisha barafu, maghala ya kuhifadhi samaki, karakana ya nyavu za uvuvi na gati la kuegesha meli. Jumla ya shilingi milioni 76.03 zimetumika hadi Januari 2022.

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)**

**(a) Kuimarisha na Kuendeleza Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Mazingira**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa ofisi tatu (3) za ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi za Nyakalilo (Sengerema), Sota (Rorya) na Busega (Simiyu); kuimarishwa kwa vituo vitano (5) vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Mwanza, Simiyu, Ukerewe, Kanyigo na Geita kwa kuvipatia injini moja (1) kila kituo, kuvipatia magari vituo vitatu (3) vya Mwanza, Kigoma na Tanga; kuendeshwa kwa operesheni moja maalumu katika Mkoa wa Mwanza na doria zenye siku kazi 3,251; kufanyika kwa operesheni mbili (2) katika Ziwa Victoria, Bwawa la Mtera na Bahari ya Hindi kwa kushirikiana na kikosi kazi cha Kitaifa cha Kupambana na Uhalifu wa

Kimazingira; kuimarishwa kwa vikundi vya Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kujenga ofisi tano (5) katika Halmashauri tano (5) za Pangani, Jiji la Tanga, Mkinga, Bagamoyo na Lindi Vijijini; kutolewa kwa mafunzo kwa wadau wa uvuvi 120 kuhusu usimamizi wa uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira; na kufanyiwa mapitio ya Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi; kufanyika kwa kaguzi 1,863 za kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao ya uvuvi kwenye viwanda vya kuchakata samaki, mialo, magari ya kusafirisha samaki, maghala ya kuhifadhi samaki na masoko ya samaki; na kutoa elimu kwa wadau 750 kuhusu uwekezaji katika Sekta ya uvuvi hususan uchakataji wa mazao ya uvuvi. Jumla ya shilingi milioni 802.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Kujenga na Kuimarisha Miundombinu ya Uvuvi (Mialo na Masoko)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa mialo ya Kayenze - Ilemela, Igombe – Ilemela na kuendelea na ujenzi ya mialo mitatu (3) ya Ihale (Busega), Chifunfu/Kijiweni (Sengerema) na Igabiro (Bukoba) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90; kuendelea na ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay (Nyasa) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90; kufanyika kwa tathmini ya hali ya mialo ya Mchinga (Lindi) na Chato (Geita) kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mialo hiyo. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Uzalishaji wa Mazao ya Uvuvi kwenye Maji ya Asili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarishwa kwa ukusanyaji wa Taarifa za uvuvi wa Samaki kwa kugawa simu 100 zenye Programu ya e-CAS (*electronic – Catch assessment system*) kwa vikundi shirikishi vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi;kuvuliwa kwa tani 276,798.92 za samaki zenye thamani ya shilingi trilioni 1.6; kuuzwa nje kwa tani 20,437.56 za samaki na Samaki hai 111,378 wa mapambo wenye thamani ya shilingi bilioni 256.98 wameuzwa. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Kujenga na Kukarabati Miundombinu ya Ukuzaji Viumbe Maji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa ofisi za kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira (Morogoro); kukamilika kwa uezekaji wa majengo sita (6) ya utawala, kitotoleshi, mgahawa, bweni na nyumba mbili (2) za makazi, mfumo wa maji safi na maji taka na mfumo wa umeme; kuendelea na ujenzi wa ghala na kukamilisha kazi ya kurekebisha mabwawa makubwa matatu (3) yenye ukubwa wa mita za mraba 2,016 na madogo sita (6) yenye ukubwa wa mita za mraba 442 kwa kuotesha nyasi na kujenga mifumo ya kuingiza na kutoa maji katika kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Rubambagwe (Geita); kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kituo cha Ruhila (Songea); kuanza kwa ujenzi wa kitotoleshi na ukarabati na upanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji cha Nyengedi – Lindi na kituo kipya cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Bahari Ruvula – Mtwara. Jumla ya shilingi bilioni 1.38 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa hosteli mbili (2) katika kampasi ya Gabimori (Mara) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 64; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Utawala la Kampasi ya Kigoma; kuandaliwa michoro ya majengo ya kampasi mpya kwa

ajili ya Chuo cha Nyegezi na Mbegani; kutengenezwa kwa mitambo miwili (2) ya kutotoleshea vifaranga vya samaki katika kampasi za Mbegani na Nyegezi na kuendelea na matengezo ya kitotoleshi katika Kampasi ya Kigoma; kukamilika kwa ukarabati wa meli moja (1) ya mafunzo ya vitendo ya wanafunzi katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza) na kuendelea na taratibu za ununuzi wa magari mawili (2) kwa ajili ya Kampasi ya Mbegani (1) na Kampasi ya Nyegezi (1); na kuanza kwa taratibu za ukarabati wa Kituo cha Mikindani (Mtwara). Jumla ya shilingi milioni 469.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa utafiti wa athari za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la tindikali baharini; kufanyika kwa utafiti wa chakula bora cha samaki na kufanya utafiti wa mbegu bora za samaki wanaofaa kufugwa; kufanyika kwa utafiti wa njia bora za kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa na kuongeza thamani katika mavuvi; kufanyika kwa utafiti wa wingi na mtawanyo wa samaki katika Ziwa Victoria; kuchunguza viashiria vya kimazingira na kutambua maeneo yanayofaa kuvua kwenye maji ya kitaifa katika Bahari ya Hindi na EEZ kwa kutumia satelaiti; kuchunguza baiolojia na ikolojia ya samaki aina ya Jodari (Tuna) na kutambua maeneo ya mazalia na makulia katika maji ya Tanzania; kufuatilia ubora wa maji katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria; kufuatilia na kuelewa mnyororo wa thamani wa samaki aina ya dagaa na migebuka wa Ziwa Tanganyika kupitia mradi wa FISH4ACP. Jumla ya shilingi bilioni 1.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (Agriculture and Fisheries Development Programme - AFDP)**
**(a) Ununuzi wa Meli na Kuendeleza Uvuvi katika Ukanda wa Bahari Kuu**
Hatua iliyofikiwa: Kuandaliwa kwa msawazo (*specifications)* kwa ajili ya ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi kati ya nne (4) zilizopangwa kununuliwa; na kuendelea na utambuzi wa maeneo yanayofaa kuweka vifaa kwa ajili ya kukusanyia samaki kwenye maji (Fish Aggregating Devices).

**Mradi Na. 4701: Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi – (South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth – SWIOFish)**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa ofisi tano (5) za Vikundi vya Ulinzi na Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika halmashauri tano (5) zinazotekeleza mradi huo ambazo ni Bagamoyo, Lindi Vijijini, Mkinga, Pangani na Chalinze; kujengwa kwa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam; na kuendelea na hatua za ujenzi wa ofisi ya utawala ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu Mafia. Jumla ya shilingi bilioni 3.1 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.3.5 Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia

**(i) Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini (Sustainable Management of Mineral Resources Project- SMMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vitatu (3) vya umahiri katika masuala ya madini vya Chunya, Songea na Mpanda; kuendelea na ujenzi wa ghala la kuhifadhia sampuli za miamba choronge (Core shed) lililopo eneo la Kizota mkoani Dodoma; kununuliwa kwa vifaa vya mbalimbali vya maabara na utafiti, magari manne (4) ya *field* na mtambo mmoja wa kuchimba madini (excavator) katika mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira; kukamilika kwa ufungaji wa mtambo wa kutengeneza makaa ya mawe ya kupikia nyumbani (Rafiki Coal briquettes); kukamilika kwa ujenzi wa Mtambo wa kusafisha dhahabu wa Mwanza (Mwanza Precious Metal Refinery); kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vingine vya usafishaji wa dhahabu (Gold Refineries) katika Mikoa ya Geita na Dodoma; kukamilika kwa mikataba ya uwekezaji mkubwa na wa kati katika uchimbaji wa madini na utiaji saini wa mikataba minne (4) ya ubia baina ya wawekezaji na Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kununuliwa kwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha masoko ya madini; kuanzishwa kwa masoko mapya manne (4) ya madini katika maeneo ya Kiteto (Manyara), Mirerani (Manyara), Mangaka (Mtwara) na Soko la Vito na Dhahabu Moshi (Kilimanjaro); kuanzishwa kwa vituo vipya nane (8) vya ununuzi wa madini vikijumuisha Nyang'wale (Geita), Segese (Kahama), Ifwenkenya na Mwembeni (Songwe), Masasi (Mtwara), Mbugani, Kiwanja, Mwaoga na Mkola (Chunya), hivyo kufanya jumla ya masoko ya madini kuwa 42 na vituo vya ununuzi wa madini kufikia 66 kutoka vituo 58 vilivyokuwepo Juni 2021; kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya Ofisi ya Tume ya Madini na kufanikisha upatikanaji wa magari 40; kufanikisha upatikanaji wa vifaa vya utafiti wa jiosayansi kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST); na kukamilishwa kwa Ripoti ya TEIT kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 ya malipo ya kodi kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia. Jumla ya shilingi bilioni 3.1 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.3.6 Huduma

**A. Maliasili na Utalii**

**(a) Utalii**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje kufikia watalii 544,132 kutoka watalii 262,093 katika kipindi kama hicho mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 107.6 Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2021; huduma za malazi zinazokusanya tozo ya kitanda siku (bed night levy) ziliongezeka kutoka 1,815 mwaka 2020 hadi 8,681 mwaka 2021; Hifadhi ya Taifa Serengeti imeendelea kuwa hifadhi bora duniani kwa miaka mitatu (3) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021; Hifadhi ya Taifa Serengeti ilitangazwa na shirika la *Mainland Aggregates Limited* la nchini Marekani mwaka 2021 kuwa mshindi wa pili barani Afrika na wa 12 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa mtandao wa

kijamii wa instagram; kuendelea kuheshimika kimataifa katika uhifadhi ambapo hifadhi tatu (3) za Serengeti, Kilimanjaro na Tarangire zilipewa tuzo ya kuwa hifadhi bora kati ya hifadhi bora 20 za kwanza duniani; na kuendelea kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi ili kuwezesha maeneo hayo kufikika kwa urahisi katika kipindi chote cha nusu mwaka.

Shughuli nyingine zilitokelezwa ni: Kuendeleza *Programu ya Royal Tour*; kusafishwa kwa jumla ya kilomita 133 za njia za asili na kilomita 27 za barabara za kuingia hifadhi za misitu ya mazingira asilia; kuongezeka kwa idadi ya watalii waliotembelea hifadhi za misitu ya mazingira asilia kufikia watalii 67,677 mwaka 2021 ikilinganishwa na watalii 31,564 katika kipindi kama hicho mwaka 2020; na Tanzania kuwa mwenyeji katika Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Regional Tourism Expo - EARTE 2021) lilofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 9 hadi 16 Oktoba, 2021.

**(b) Mradi Na. 5203: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient natural resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa usanifu na tathmini ya athari za kimazingira kwa ujenzi wa km 2,051 za barabara, km 132.5 za njia za utalii wa miguu, majengo 80, madaraja na viwanja vya ndege 14 katika hifadhi za Taifa za Mikumi, Ruaha, Nyerere, Udzungwa na Hifadhi Asili ya Kilombero; ununuzi wa mitambo nane (8) kwa ajili ya ujenzi na kuiwasilisha katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na kuendelea na hatua za ununuzi wa malori 17, boti za upepo (airboat) mbili (2) na magari mawili (2) ya kuoneshea sinema; kukamilika kwa uandaaji wa mkakati wa kutangaza utalii katika nyanda za juu kusini; kutekelezwa kwa utafiti wa wanyamapori na kukusanya takwimu za mtawanyiko wa wanyamapori katika Hifadhi za Taifa za Nyerere na Ruaha; kukamilika kwa mwongozo wa mafunzo ya Utalii wa Nyuki (Api-tourism); kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi wa kituo cha tafiti Iringa; kufanyika kwa mapitio ya miongozo ya kushughulikia migogoro baina ya wanyamapori na binadamu pamoja na kukamilika kwa utoaji wa mafunzo ya utalii wa nyuki (Api-tourism) na matumizi ya ardhi kwa hifadhi za Nyerere na Ruaha.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Uwezeshaji wa utambuzi wa shughuli za kiuchumi za jamii ambazo zimesaidia kuimarisha uhifadhi na kuwaongezea kipato mfano ufugaji (samaki, nyuki, kuku) na kilimo cha hifadhi shadidi endelevu (mbogamboga, mpunga, kilimo kinachotumia maji kidogo); kufanyika kwa utambuzi wa wawezeshaji Jamii katika vijiji vyote 15 vya kipaumbele kwa awamu ya kwanza; kutolewa kwa mafunzo ya maendeleo ya jamii, usimamizi wa ushirika pamoja na mafunzo elekezi kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya mradi kwa watumishi 18 wa mradi, wawezeshaji 15 wa jamii, maafisa watendaji wa vijiji 15 na wasimamizi saba (7) wa wilaya zinazotekeleza mradi; kuendelea kuboresha skimu ya umwagiliaji ya majaribio ya Madibira; kukamilika kwa shughuli za ujenzi, ufungaji wa miundombinu ya kupima maji na utandazaji wa mifereji ambapo ujenzi umefikia asilimia 22; na kutolewa kwa mafunzo na vitendea kazi kwa watekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 13.78 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 4812: Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara kwa watumishi 110 kutoka Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili *(National Taskforce Anti-poaching – NTAP na Kanda 10 za Kiikolojia za Kupambana na Ujangili (Tasking and Coordination Groups – TCG);* kufanyika kwa doria za ki-intelijensia za siku watu 422 katika ikolojia ya Ruaha - Rungwa; kuandaliwa kwa Mwongozo wa Utendaji wa Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili; kufanyika kwa tathmini ya uwezo na mahitaji ya NTAP na TCG; na kuendelea na uhuishaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; na kuendelea na hatua za ununuzi wa magari 10 kwa ajili ya TCGs. Jumla ya shilingi milioni 598 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 4647: Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa huduma za ugani (kuhusu udhibiti wa moto, uanzishaji na utunzaji wa mashamba ya miti, uchakataji na uzalishaji wa mazao ya misitu) zilizowafikia wakulima wa miti na wadau 6,422 katika vijiji 80 ambapo vijiji 27 vipo katika kongano ya Njombe, vijiji 20 vipo kongano ya Mafinga na vijiji 33 vipo kongano ya Makete; kutolewa kwa mafunzo rasmi kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati 698 kuhusu namna ya ukaushaji mbao, njia za uchakataji mazao ya misitu, uanzishaji na utunzaji vitalu vya miti na uzalishaji wa mkaa endelevu; kuwezeshwa kwa wanachama 60 kuhusu uandaaji wa Katiba za Umoja wa Wakulima wa Miti (Tree Growers Association – TGA); na kupatiwa mafunzo kwa wananchi 1,558 kuhusu namna bora ya kuzuia moto katika mashamba ya miti.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutolewa kwa mikopo shillingi million 90 kupitia halmashauri za wilaya ya Mufindi (milioni 75) na Njombe (milioni 15) kwa ajili ya kuwawezesha wakulima na wajasiriamali wadogo na wa kati; kuandaliwa kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 6 (wilaya ya Njombe vijiji vya Iyembela na Wanginyi na wilaya ya Ludewa vijiji vya Ilininda, Ilawa, Manga na Mangalanyene); kutolewa kwa hatimiliki za kimila za ardhi 869 katika Kijiji cha Ibaga wilaya ya Makete. Jumla ya shilingi bilioni 1.03 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 4650: Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme – (FORVAC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupandwa kwa aina 61 za miti kwenye eneo la misitu lenye ukubwa wa hekta 2,118 wilayani Nachingwea katika kijiji cha Matekwe; kuwekwa kwa mipaka kwenye misitu yenye urefu wa Kilometa 17 Wilayani Liwale kijiji cha Ngumbu; kuandaliwa na kupitishwa kwenye ngazi ya kijiji maeneo ya ardhi yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za misitu katika vijiji vya Mikuyu, Ngunja, Ngongowele, Mihumo, Turuki na Darajani; kufanyika kwa mapitio na kudurufu sheria ndogo za usimamizi wa misitu ya vijiji; kuandaliwa kwa mpango wa uvunaji mbao katika maeneo ya hifadhi za misitu Wilayani Liwale katika kijiji cha Ngumbu; kukamilika kwa ufuatiliaji wa maendeleo ya misitu ya vijiji

11 Wilayani Nachingwea ambapo matokeo yanaonesha kuwa mita za ujazo 311 za mbao zilivunwa zenye thamani ya shilingi milioni 129.88; usimikaji wa vigingi 60 kwenye maeneo ya hifadhi za misitu wilayani Namtumbo; na kutolewa kwa pikipiki saba (7) katika kongano ya Ruvuma kwenye wilaya tano (5) kwa ajili ya kurahisisha shughuli za mradi na kufanya doria.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kuhusu shughuli za misitu kwa washiriki 252 wilayani Liwale;  kutolewa kwa mafunzo ya mazao ya mbao kwa washiriki 43 wa Wilaya ya Ruangwa katika kijiji cha Nahanga; kutolewa kwa mafunzo kuhusu ukataji bora wa magogo ya miti na usimamizi wa umri sahihi wa uvunaji kwa washiriki 34 Wilayani Nachingwea kwenye kijiji cha Kiegei ‘A’; na kutolewa kwa mizinga ya nyuki 42 kwa wanachama 27 wa kikundi cha Nyusa *Enterprise* Wilayani Liwale wanaofanya shughuli za ufugaji nyuki. Jumla ya shilingi bilioni 3.8 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4651: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki - BEVAC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ununuzi wa magari matatu (3) na pikipiki 17 za mradi, ununuzi wa vifaa vya kitafiti katika Maabara ya Utafiti wa Nyuki Njiro na maandalizi ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) – Tabora; kukamilika kwa ukarabati wa vyumba saba (7) na ununuzi wa vifaa vya ofisi ya uratibu wa Mradi iliyopo Mkoani Tabora na ofisi ndogo ya uratibu iliyopo Mkoani Kigoma; na kukamilika kwa maandalizi ya mpango wa utekelezaji wa mradi kwa mwaka wa kwanza. Jumla ya shilingi milioni 326.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 4816: Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio - MICE**

Hatua iliyofikiwa ni: kulipwa kwa gharama za upimaji wa eneo la mradi wa Kigamboni lenye ukubwa wa hekta 22.44; na kuanza upembuzi yakinifu katika eneo la mradi. Jumla ya shilingi milioni 14.22 zimetumika hadi Januari 2022.

**B. Sekta ya Fedha, Biashara na Masoko**

**(a) Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa miradi 12 ambayo ni: Ujenzi wa Soko la Kisasa la Chifu Kingalu - Morogoro, Soko la Mpakani Muhange – Kakonko, Soko la Mburahati, Kisutu na Magomeni, Ghala la Kuhifadhia Mazao Ruangwa, Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Stendi ya Mangaka, Machinjio ya Kisasa ya Vingunguti, Maegesho ya Malori Mpakani mwa Tanzania na Rwanda na Kiwanda cha Chaki na Vifungashio Maswa. Aidha, miradi 26 inaendelea katika Halmashauri nane (8) na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Jumla ya shilingi bilioni 18.24 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uundaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa wastaafu; kupatiwa mafunzo kwa watumishi 957 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) kutoka mashirika ya umma 468; kupatiwa mafunzo kwa wahasibu 440 kuhusu mfumo wa Uhasibu na Ujumuishaji wa Hesabu za Serikali (GACS); kukamilika kwa mfumo wa kielektroniki wa uchambuzi na utekelezaji wa Kamati ya uangalizi (LAAC); kujengewa uwezo kwa wakaguzi wa ndani 205 wa halmashauri kuhusu matumizi ya Ukaguzi wa Mfumo (System Audit); na kuunganishwa na kufungamanishwa kwa mifumo sita (6) ambayo ni MUSE na GePG, MUSE na PlanRep – TRO, MUSE na PlanRep – LGA, MUSE na CBMS, MUSE na ERMS, MUSE na mifumo ya benki za biashara (CRDB na NMB); kuandaliwa kwa mfumo wa ukuasanyaji mapato katika ngazi ya Halmashauri na kutumiwa katika Halmashauri zote 184; kuanzishwa kwa Mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Hazina; na uaandaaji wa maabara ya kiuchunguzi (forensic laboratory) katika Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali umekamilika. Mfumo wa ukaguzi kwa Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (GIAMIS). Jumla ya shilingi bilioni 8.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Benki za Maendeleo**

**Benki ya Maendeleo TIB**

Benki ya Maendeleo (TIB) imeendelea kutekeleza majukumu yake katika kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo na kuongeza tija kwenye ukuaji wa Pato la Taifa. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, Benki ilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 652.95 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 634.29 iliyotolewa katika mwaka 2020. Kati ya mikopo iliyotolewa, maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: madini ya dhahabu na ujenzi (shilingi bilioni 188.66), kilimo (bilioni 166.70), utalii (bilioni 76.19), uzalishaji viwandani (bilioni 70.07), majengo (bilioni 46.83), biashara (bilioni 26.46), umeme (bilioni 15.58), hoteli (bilioni 14.43), elimu (bilioni 15.23), taasisi za fedha (bilioni 9.55), usafirishaji na mawasiliano (bilioni 4.09), mikopo binafsi (bilioni 6.92), huduma nyingine (bilioni 2.72), maji (bilioni 8.55), ukodishaji mali (bilioni 0.86) na uvuvi (bilioni 0.33). Jumla ya miradi 111 ilinufaika na mikopo hiyo na idadi ya mikopo binafsi ilikuwa 156.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo – TADB**

Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ilifanikiwa kutekeleza yafuatayo katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 122.09 katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe na Tanga.

Vile vile, TADB imedhamini benki za biashara kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 61.7 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima (SCGS) katika mikoa ya Arusha,

Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinganya, Simiyu, Singida, Tabora na Tanga kwenye shughuli za uzalishaji, uhifadhi na utunzaji wa mazao, uchakataji na usindikaji, ununuzi na uuzaji mazao, ununuzi wa pembejeo za kilimo, na ununuzi wa mitambo ya kilimo, ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao, ukarabati wa maghala ya mazao, unenepeshaji wa ng'ombe wa nyama.

**(d) Huduma za Bima**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandikishwa na kutolewa kwa leseni 1,122 zikijumuisha makampuni ya bima 31, madalali wa bima 70, wakala wa bima 938 na benki wakala (bancansurance) 20, watakwimu bima wanne (4), madalali bima mtawanyo watano (5) na wakadiriaji hasara wa bima 52; kufanya ukaguzi kwa watoa huduma za bima ambao ni makampuni ya bima 28, matawi ya kampuni 22 za bima, madalali wa bima sita (6) na mawakala wa bima 210; kufanya ukaguzi wa bima kwa vyombo vya moto 20,986; na kupokea malalamiko 272 kutoka kwa wananchi wanaotumia huduma za bima (policyholders) ambapo kati ya hayo malalamiko 77 yalipatiwa ufumbuzi, malalamiko 19 yalipelekwa kwa Msuluhishi wa Migororo ya Bima (TIO), malalamiko 157 yanaendelea kufanyiwa kazi, malalamiko 29 yamekataliwa na malalamiko tisa (9) yamepelekwa mahakamani.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa usanifu wa awali wa jengo la Ofisi za Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Dodoma; kukamilika na kuanza kutumika kwa Mfumo wa TIRA-MIS unaowezesha ukataji wa bima kwa njia ya kielektroniki; na kutolewa kwa elimu ya masuala ya bima kwa wananchi 518,734 kutoka katika makundi mbalimbali kwa kupitia semina, luninga na warsha.

**(e) Huduma Ndogo za Fedha**

Utoaji wa huduma ndogo za fedha katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Juni 2021 ni kama ifuatavyo: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 38.88 kwa wajasiriamali wadogo 18,505 kutoka Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF ambapo wanawake ni 9,808 na wanaume 8,697. Mikopo hiyo imeelekezwa katika sekta za kilimo (shilingi bilioni 3.2) na viwanda vidogo na biashara (shilingi bilioni 35.68).

Shughuli nyingine ni: Benki Kuu imefanya uhamasishaji kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la nne kufanya usajili wa vikundi katika kanda zote nchini, kutoa mafunzo kwa watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili kuhusu sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha pamoja na mafunzo juu ya ujazaji na uwasilishaji wa taarifa za utendaji za watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili. Benki Kuu imeandaa mfumo wa uwasilishaji wa taarifa za watoa huduma ndogo za fedha na kuwataarifu watoa huduma ndogo za fedha kuwasilisha taarifa za utendaji kama ilivyoainishwa katika fomu maalum kwa kipindi kilichoishia tarehe Desemba 2021. Benki Kuu imeendelea kupokea taarifa za usajili na uandikishwaji wa watoa huduma ndogo za fedha walio katika daraja la tatu na nne kutoka kwa mamlaka kasimishwa ambazo ni Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Serikali za Mitaa mtawalia. Aidha, Benki Kuu imetoa leseni 692 kwa ajili ya watoa huduma ndogo za fedha kwa daraja la pili, leseni 580 kwa watoa huduma za fedha daraja la tatu (SACCOS) na kusajili watoa huduma za fedha daraja la nne wapatao 23,705 (CMGs).

**(f) Huduma Jumuishi za Fedha**

Benki Kuu imeendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake chini ya Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa mwaka 2018 - 2022. Hatua iliyofikiwa katika mwaka 2021 ni pamoja na: kuzinduliwa na kuanza kutekelezwa kwa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21 – 2029/30 na Mpango Kazi wa utekelezaji wake; kuzinduliwa na kuanza utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Fedha wa Mwaka 2021 - 2025 na nyenzo za kufundishia elimu ya fedha; kuundwa kwa Kamati ya Wanawake ya Huduma Jumuishi za Fedha kwa lengo la kuongeza idadi ya wanawake wanaofikiwa na kutumia huduma rasmi za fedha; kutekeleza mikakati ya Mpango wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa mwaka 2018-2022 ikiwa ni kuundwa kwa Kamati ya Wanawake wa Huduma Jumuishi za Fedha kwa lengo la kuongeza idadi ya wanawake; na kusajili watoa huduma za fedha nchini.

**(g) Mifumo ya Sekta ya Fedha**

Benki Kuu imeendelea kusimamia mifumo ya malipo ambayo imeendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi.

**(i) Mfumo wa malipo ya papo kwa hapo (Tanzania Instant Payment Systems – TIPS).**

Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mradi wa TIPS upo katika majaribio tangu tarehe 29 Agosti 2021 na kutarajia kuhitimishwa majaribio hayo mwezi Februari 2022. Majaribio ya awamu ya kwanza yameshirikisha watoa huduma watano ili kuangalia ufanisi wa mfumo, pamoja na kuboresha masuala yanayojitokeza kwenye matumizi ya mfumo. Mfumo huu unatoa aina mbili za matumizi ambazo ni malipo baina ya mtu kwa mtu na malipo kati ya mtu na wafanyabiashara. Awamu ya pili inatarajiwa kuanza mwezi Machi 2022 ambapo watoa huduma wengine wataendelea kujumuishwa kwenye mfumo, pamoja na kuunda mahitaji mengine ya matumizi. Kukamilika kwa mfumo huu kutaongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za fedha kwa kuongeza ushirikiano kati ya watoa huduma za fedha kidigitali na kuchochea kupungua kwa gharama za miamala ya fedha kwa njia ya kidigitali.

**(ii) Kanzidata ya watoa huduma za Kifedha(FSR)**

Awamu ya kwanza ya uandikishwaji wa watoa huduma za fedha nchini kote imekamilika ambapo vituo (outlets) 101,819 vikiwa na jumla ya huduma mbalimbali 230,401 vimekwishasajiliwa. Taasisi za kutoa huduma za fedha zinaendelea na uhakiki wa taarifa kwenye mfumo pamoja na kusajili vituo vipya vya huduma zao. Halikadhalika, awamu ya pili ya uandikishwaji ilianza Desemba 2021 na inatarajiwa kukamilika Februari 2022. Awamu hii imelenga kukamilisha mapungufu yaliyoainishwa wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza.

**C. Masoko**

**(a) Soko la Bidhaa Tanzania – TMX**

Hatua iliyofikiwa ni:

(i) Zao la choroko: kufanyika kwa mauzo katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga,

Tabora na Simiyu ambapo bei ya juu ilikuwa shilingi 1,809 kwa kilo ikilinganishwa na wastani wa bei ya shilingi 900 kwenye mifumo isiyo rasmi;

(ii) Zao la chai: Kukamilika kwa asilimia 95 ya mfumo wa mauzo wa kielektroniki; kuandaliwa kwa kitabu kinachoainisha taratibu na kanuni za uuzaji chai (Tea Rule Book) na kuandaliwa kwa *Memorundum of Understanding* baina ya Wadau wa Sekta Ndogo ya Chai nchini ili Mnada wa chai uweze kuanza;

(iii) Zao la Mkonge: Kukamilika kwa Mfumo wa mauzo wa kielektroniki wa zao la mkonge;

(iv) Zao la Kakao: Kufanyika kwa mauzo ya zao la kakao katika Mkoa wa Morogoro ambapo wakulima wamefaidika kwa ongezeko la kipato kwa asilimia 100 ambapo bei ya kununulia imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 2,000 hadi shilingi 5,000. Jumla ya tani 260 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.29 zimeuzwa;

(v) Zao la Ufuta: Kuendelea kufanyika kwa mauzo ya zao la ufuta katika Mkoa wa Songwe na Manyara ambapo bei imeongezeka kutoka wastani wa shilingi 1,400 hadi shilingi 2,574. Jumla ya tani 310 zenye thamani ya shilingi milioni 754 ziliuzwa;

(vi) Zao la Mifugo Hai na Ngozi: Kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Mauzo ya mifugo hai na ngozi kwa ajili ya kuanza kufanyiwa majaribio katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro; na kuandaliwa kwa miongozo ya uuzaji wanyama hai na ngozi;

(vii) Zao la Mahindi na Mpunga: Maandalizi ya kuanza kuuza mahindi na mpunga yanaendelea kwa kushirikiana na wadau kwenye sekta ndogo ya nafaka;

(viii) Mazao ya Vitunguu, Viazi na Pilipili Manga: kukamilika kwa miongozo ya mauzo; na kuanza kwa mafunzo kwa wadau katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Njombe, Arusha na Kilimanjaro; na

(ix) Kutolewa kwa mafunzo ya matumizi ya mfumo wa TMX kwa wadau 10,754 ikijumuisha kamati mbalimbali za wabunge katika mikoa ya Tanzania Bara.

### 3.3.4 Kukuza Biashara na Uwekezaji

#### 3.3.4.1 Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji

**A. Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi**

**(a) Huduma za Uwekezaji Mahala Pamoja (One Stop Facilitation Centre -OSC) - TIC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupatiwa huduma kwa jumla ya wateja 9,037 katika kituo cha OSC ambapo jumla ya miradi 121 (48 wageni, 38 Watanzania 35 ubia kati ya wageni na Watanzania) ilisajiliwa yenye thamani ya dola za Marekani milioni 982.6 na inatarajiwa kutoa ajira kwa watanzania wapatao 25,260; kutolewa kwa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na OSC kwa njia ya “Documentary” na vyombo vya habari; kuboreshwa kwa mfumo wa kupokea maombi na kusajili miradi ya uwekezaji kwa njia ya mtandao; na kuunganishwa kwa mifumo ya TEHAMA ya Taasisi zinazotoa huduma kwa wawekezaji ili kuwa na dirisha moja la uwekezaji (*Tanzania Electronic Investment Window – TeIW)*.

**(b) Mifumo ya Kisheria ya Kusimamia Uwekezaji**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilisha hatua za kutungwa kwa Sheria Mpya ya Uwekezaji nchini; kufanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji; kuendelea na maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Uwekezaji (National Investment Development Strategy-NIDS) pamoja na kuandaliwa kwa mapendekezo ya maboresho ya sheria na kanuni zenye muingiliano ikiwemo maeneo ya tozo kero, adhabu, leseni na vibali kwenye sekta mbalimbali za biashara.

**(c) Uhamasishaji wa Uwekezaji Ndani na Nje ya Nchi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kushiriki katika mikutano tisa (9) ya ndani ikiwemo Maonesho ya Utalii ya Kanda ya Afrika Mashariki (EA Regional Tourism Expo), Jukwaa la Viwanda lililofanyika Zanzibar na maonyesho ya viwanda vidogo (SIDO Trade Fair) yaliyofanyika Kigoma; kushiriki katika mikutano mitano (5) kwa njia ya mtandao (Visual meetings) na mikutano ya ana kwa ana nane (8) kwa lengo la kuhamasisha na kuvutia uwekezaji kutoka nje ikiwemo Afrika Kusini, Algeria, Burundi, China, Italia, Kenya, Oman, Qatar, Ubelgiji na Uturuki.

**B. Kuimarisha Ushiriki wa Sekta Binafsi**

**(a) Kuimarisha Majadiliano kati Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa Mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 26 Juni, 2021 Jijini Dar es Salaam; na kuendelea na uratibu wa utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa 12 wa Taifa wa Baraza la Biashara ikiwemo kuandaliwa kwa Mpango kazi wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao yaliyohandisiwa *(Engineered Wood Products Development* - EWP) wa mwaka 2021 – 2031.

**(b) Kutatua Changamoto za Biashara na Uwekezaji**

Hatua iliyofikiwa ni: kuainishwa kwa sababu zinazopelekea kudorora kwa matumizi ya Ushoroba wa Uchukuzi wa Dar Es Salaam na miundombinu mingine ya Tanzania inayotumiwa na nchi za SADC na EAC zikiwemo miundombinu hafifu ya reli, Bomba la mafuta na barabara, ukosefu wa muunganiko wa miundombinu ya msingi na Bandari ya Dar es Salaam, miundombinu iliyopo kutotoa huduma kwa ufanisi, mazingira hafifu ya ufanyaji Biashara, kukinzana kwa sheria na usimamizi hafifu wa ushoroba na miundombinu mingine.

**(c) Kujengea Uwezo Mabaraza ya Mikoa na Wilaya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa mafunzo kwa Katibu Tawala wa Mkoa, Katibu Tawala Msaidizi (Uchumi na Uzalishaji) na Afisa Biashara wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakuu wa Idara za Mipango, Maafisa Biashara na Maafisa Kilimo na wajumbe wa mabaraza ya mikoa na wilaya kupitia Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) katika mikoa saba (7) ya Manyara, Singida, Dodoma, Rukwa, Ruvuma, Njombe na Iringa.

**C. Kukuza Ushiriki wa Wananchi kwenye Shughuli za Kiuchumi**

**(a) Mifuko na Programu za Uwezeshaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo kwa kampuni 31 zinazozalisha na kuchakata bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo na kilimo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kutumia Mpango wa SANVN (SIDO, AZANIA Bank, NEEC, VETA na NSSF); kuanzishwa kwa mpango wa kuendeleza viwanda vidogo na vya kati kupitia *SANVN Viwanda Scheme* ambapo mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 imetolewa katika mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Geita, Simiyu, Dodoma, Kilimanjaro, Shinyanga, Mwanza na Mbeya; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 44.5 katika mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Geita, Dodoma, Simiyu na Singida kupitia Vituo 17 vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na kufanyika kwa tathmini ya mifuko 30 inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa na inayotoa dhamana ya mikopo ili kuboresha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji.

**(b) Kukuza Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuwezesha elimu ya ujasiriamali kwa wajasiriamali 8,799 kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika mkoa wa Geita ili waweze kushiriki zabuni zinazotolewa na Kampuni ya Dhahabu ya Geita (Geita Gold Mine Limited); kujenga uwezo kwa wananchi 3,245 katika mkoa wa Geita kuhusu kuanzisha Kongano; kutolewa mafunzo kwa vijana 118 kutoka mkoani Dar es Salaam kuhusu ujasirimali, upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi, kujiamini katika kufanya biashara, mazingira ya biashara, ushindani, fursa zilizopo katika maeneo yao na uwezo wa kujenga mitandao na kupanua wigo; kutolewa kwa mafunzo kuhusu umuhimu wa Bima ya Vikundi kwa vikundi 1,034 vyenye wanachama 25,898 katika Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Tanga, Mbeya, Rukwa na Morogoro; na kukamilika kwa kanzidata ya uwezeshaji ili kuwaunganisha watoa huduma wa kitanzania na wawekezaji pamoja na taasisi mbalimbali za uwezeshaji.

### 3.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 3.3.5.1 Afya

**(a) Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Sewa Haji (wodi namba 18) kwa ajili ya wodi za kulaza wagonjwa binafsi; kuendelea na ujenzi wa jengo la wodi za wagonjwa binafsi na watu mashuhuri ambapo utekelezaji umefikia asilimia 15; kuendelea kutoa huduma za kibingwa za kupandikiza uloto (*bone marrow transplant* ambapo wagonjwa sita (11) wamehudumiwa, huduma ya kupandikiza vifaa vya usikivu ambapo jumla ya wagonjwa 41 wamepatiwa huduma hiyo, huduma ya upandikizaji wa figo (wagonjwa 68) na huduma za tiba radiolojia (wagonjwa 1,625); kuboresha kitengo cha ushonaji kwa kununua mitambo ya kisasa ya kuzalisha barakoa; kufungwa kwa mashine mbili (2) za *apheresis* kwa ajili kuvuna chembe kuu na kuanza kutoa huduma za kubadilisha chembechembe nyekundu za damu (Red Cell Exchange Transfusion); kukarabatiwa kwa jengo la kutolea huduma za kupandikiza ujauzito (IVF); kuanza kwa hatua ya ununuzi wa mashine na vifaa kwa ajili ya huduma kupandikiza ujauzito (IVF);

kukarabatiwa kwa jengo la kutoa huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya damu kuganda (haemophilia) pamoja na kununuliwa kwa vifaa kwa ajili ya huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya damu kuganda; ukarabati wa vyumba vitano (5) vya wagonjwa mahututi (ICU) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; na ukarabati wa vyumba vya radiolojia (MRI 1, CT-SCAN 1 na X-ray 2). Jumla ya shilingi bilioni 5.09 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6364: Hospitali Taifa Muhimbili - Mloganzila**

Hatua iliyofikiwa ni: Kudhaminiwa kwa watumishi 55 katika fani mbalimbali za kibingwa katika masomo ya uzamili ndani na nje ya nchi; upandikizaji wa vifaa vya usikivu (cochlear implants) kwa wagonjwa watatu (3) na hivyo kupunguza rufaa za nje ya nchi; kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo huduma za kuhifadhi maiti; kukamilisha ujenzi na usimikaji wa mtambo wa kuzalisha tiba hewa (Oxygen generating plant) wenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 yenye ujazo wa 8.5 $M^3$ kwa siku; ukarabati wa wodi za watoto wachanga mahututi (NICU), wodi ya kawaida ya watoto, wodi ya mama wajawazito mahututi, wodi ya uangalizi maalumu wa wamama wajawazito (HDU) na chumba maalumu kwa ajili ya kufanya matengenezo ya vifaa tiba (biomedical workshop).

**(c) Mradi Na. 5491: Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa maabara maalumu na usimikaji wa mtambo wa kisasa (Angio-Suite) kwa ajili ya kufanya uchunguzi na upasuaji bila kufungua fuvu kwa matatizo ya mishipa ya damu kwenye ubongo; kununuliwa kwa mashine moja ya *Angio Suite* ikiwa na *Mobile C-ARM System* tatu (3), *Patient Monitors nane (8), Craniotomy Basic Kit* moja (1), *Minimal Invasive Spine Set* moja (1) *Orthopaedic Basic Kit* moja (1) na *Sign nail basic Sets* moja (1).

**(d) Mradi Na. 5419: Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufungwa kwa mtambo wa kisasa (cathlab) wenye uwezo wa kufanya uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo, kufunga vifaa visaidizi vya moyo, kuzibua mishipa ya damu ya moyo na kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo (Catheterization Laboratory) uliounganishwa na mtambo wa *Caro 3D & mapping electrophysiology System*; kununuliwa kwa mashine za *X-ray* moja (1) *, X-ray mobile* moja (1)*, CR* moja (1) na *Ultrasound* mbili (2); kukamilika kwa wodi ya watoto; kutoa huduma za kibingwa kwa kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua kwa wagonjwa 365, kufanyiwa upasuaji kwa watu wazima 161 wenye matatizo ya mishipa ya damu; wagonjwa 1,402 walipatiwa matibabu kwa kufanyiwa upasuaji wa moyo kupitia tundu dogo kwa kutumia mtambo maalumu wa *Catheterization laboratory*; kuanzishwa kwa programu mpya za mafunzo ya kibingwa ya udaktari katika maeneo ya upasuaji wa moyo (*Cardiothoracic & Vascular Surgery*), dawa za usingizi kwa wagonjwa wa moyo (*Cardiothoracic Anaesthesia*), wagonjwa mahututi na wanaohitaji uangalizi maalumu (*Critical Care*) na *Perfusion* (*Cardiothoracic Perfusion*).

**(e) Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa jengo, ununuzi na ufungaji wa mashine ya *Positron Emmission Tomography Computerized Tomography scan* (PET/CT Scan) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; kununuliwa kwa samani na kufanyika kwa ukarabati wa sehemu ya radiolojia ikijumuisha marekebisho ya kuongeza chumba cha *Ultrasound*, upakaji rangi na ukarabati wa mfumo wa maji; kukamilika kwa ukarabati wa miundombinu ikiwemo majengo na maeneo ya kutolea huduma katika jengo la utawala, jengo la famasia, ofisi ya *Quality Improvement Team*, chumba cha *mammography*, chumba cha radiolojia, jengo la kuhifadhia maiti na vyoo vya wagonjwa; ukarabati wa jengo wa wagonjwa mahututi (asilimia 20) na chumba cha kufunga mashine ya MRI ambao utekelezaji umefikia asilimia 30; kujengwa kwa kituo cha habari kwa magonjwa ya saratani (Patient Information Centre); kununuliwa kwa dawa za kutibu saratani ambazo zimesaidia kupunguza rufaa nje ya nchi; kununuliwa kwa mashine za kuchunguza matokeo ya tiba saratani kwa njia ya damu (tumor markers), majokofu manne (4) kwa ajili ya maabara na mashine za *Oxygen Concentrators* tisa (9) kwa ajili ya wagonjwa wanaolazwa wenye uhitaji maalumu wa hewa ya *oxygen*; kufungwa kwa mashine yenye uwezo mkubwa wa vipimo vya kikemia na *X-ray* ya upimaji wa matiti (Mammography); uchunguzi wa saratani kwa huduma za mkoba katika mikoa ya Dar es Salaam, Simiyu, Tanga, Geita, Lindi na Mtwara; jumla ya wanawake 37,237 wamefanyiwa uchunguzi wa saratani ya matiti na saratani ya mlango wa kizazi; jumla ya wanaume 3,981 wamefanyiwa uchunguzi wa saratani ya tezi dume; kugharamia mafunzo ya wanafunzi 70 wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology) na wanafunzi 33 wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology) na wanafunzi 10 wa shahada ya uzamili katika uuguzi katika onkolojia (Masters in Nursing and Oncology); kununuliwa kwa mashine ya kupima virusi mbalimbali hususan vinavyosababisha saratani (PCR Machine); kununuliwa kwa jokofu la kuhifadhia maiti lenye uwezo wa kuhifadhi miili sita (6); kupokelewa kwa mashine moja (1) ya kisasa ya *ultrasound*; kununuliwa na kufungwa kwa mashine tatu (3) ambazo ni *Digital X-ray*, mashine ya *mammography* na *tissue processor*; na kufanyika kwa matengenezo kinga madogo na makubwa ya mashine za tiba mionzi za *LINACS* 2, *Cobalt*-60 (E-100), mionzi ya ndani (Gynesource), mashine 3 za *haematology*, mashine mbili (2) za *electrolyte*, mashine mbili (2) za *chemistry analyzer*, mashine za *mammography* na x-ray. Jumla ya shilingi milioni 994.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 5424: Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto (Kilimanjaro)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Maabara ya Afya ya Jamii ngazi ya tatu (BSL3) la ghorofa tatu ambapo ujenzi umefikia asilimia 90; kununuliwa kwa mashine za *Digital X-Ray* na *Ultrasound*, vifaa vya maabara na mashine za uchunguzi wa kifua kikuu kwa kuotesha vimelea *BACTEC 960* (Mycobacteria Growth Indicator Tube - MGIT) na *Blood Culture Machine;* kuendelea na ujenzi wa maabara ya kisasa kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa ya kuambukiza; na ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20. Jumla ya shilingi bilioni 2.90 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na 5425: Hopitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

Hatua iliyofikiwa ni: Ukarabati wa chumba cha X-ray na Utra-sound (asilimia 20), wodi za wagonjwa na majengo mengine (asilimia 5); na kuendelea na ujenzi wa jengo la dharura (EMD) na wagonjwa mahututi (ICU) ambao utekelezaji umefikia asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 4.2 zimetolewa hadi Januari 2022.

**(h) Mradi Na 5411: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Mashariki CCBRT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa huduma za kibingwa kama ifuatavyo: upasuaji wa wagonjwa 3,120 wenye matatizo ya macho, wagonjwa 777 wenye matatizo ya mifupa, watoto 33 wenye miguu kifundo (Clubfoot), wanawake 258 wenye fistula itokanayo na uzazi na wagonjwa 235 wenye midomo wazi (Cleft lip/Cleft palate); kutolewa kwa huduma kwa watoto 358 wenye miguu kifundo (Clubfoot) kwa njia ya Ponseti; kutolewa kwa huduma ya kusafisha figo (dialysis) kwa wagonjwa 208 wenye matatizo ya figo; kutolewa kwa viungo saidizi kwa wagonjwa 906 (Orthosis 592 na Prosthesis 51s); kujengewa uwezo kwa watumishi wa vituo 22 vya afya vya umma katika Mkoa wa Dar es Salaam katika nyanja ya afya ya mama na mtoto; kujengwa kwa majengo ya kutolea huduma za afya ya Mama na Mtoto (Maternal and Newborn Wing) yanayojumuisha vyumba vya kujifungulia (*delivery suites)* nane (8), vyumba vya upasuaji sita (6) na maabara; kununuliwa kwa vifaa tiba na samani kwa ajili ya huduma za afya ya Mama na Mtoto; na kuwekwa kwa mitambo ya hewa tiba ya oksijeni.

**(i) Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda**

**(i) Mradi Na. 5426: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa wodi za wagonjwa wa saratani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 57; kukamilika kwa ukarabati wa chumba cha mashine ya MRI na kufungwa kwa mashine husika; (iii) kununuliwa CT – Scan, *Ultrasound* 12, mashine za Radiotherapy, *Digital X-ray*, *ventilators* 5 za ICU, mashine ya kufua *Oxygen*, mashine za ECHO (Portable), *ECG*, *plasma apheresis;* kununuliwa kwa vitanda, magodoro na *bed side lockers, advanced ambulances* na *blood collecting van;* kuendelea na ujenzi wa kliniki ya wagonjwa wa macho ambapo ujenzi umefikia asilimia 65; ukarabati na upanuzi wa ICU (asilimia 4) na upanuzi wa cumba cha X-ray (asilimia 5); ununuzi wa vifaa vya idara ya dharura na ICU na kujengea uwezo watumishi; kuendelea kutoa huduma za tiba, upasuaji wa kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo upasuaji wa moyo na kifua (wagonjwa 67), ubongo na mishipa ya fahamu (wagonjwa 106), mifupa (wagonjwa 977), *Vesico Viginal Festula* (VVF) (wagonjwa 188), mdomo sungura (wagonjwa 278), kusafisha damu (wagonjwa 5,546) na upasuaji kwa kutumia matundu madogo (Laparoscopi surgery). Jumla ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi Na. 5427: Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa jengo la wodi ya wagonjwa wa saratani; upanuzi wa jengo kwa ajili ya kusafisha damu na figo (Hemodialysis) na kitengo cha *Endoscopy* ambao umefikia asilimia 90; kuendelea na ujenzi wa jengo la mionzi katika Idara ya saratani (KCMC Radiation Centre); kukamilika kwa ujenzi wa jengo

la mbele (front building) lenye sehemu ya ofisi, *CT-Scan* na *Flouroscpy*; kuendelea na ujenzi wa mabweni (hostel) ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40; kuendelea na ujenzi wa vyumba nane (8) vya upasuaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80; kuendelea na ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30; kununuliwa kwa *Ventilator* mbili (2) na *Patient's monitor* 15 katika idara ya *ICU*; kununuliwa kwa mashine mbili (2) za *Autoclave* zenye uwezo wa lita 150 katika idara ya famasia; na kufungwa kwa transfoma mbili (2) zenye uwezo wa KVA 500 kila moja. Jumla shilingi bilioni 2.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Mradi Na. 5422: Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini - Mbeya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93; na kuanzishwa kwa kiwanda cha kuzalisha maji tiba (infusion) ambacho kina uwezo wa kuzalisha lita 120 za maji tiba kwa siku. Jumla ya shilingi bilioni 9.39 zimetumika hadi kufikia Januari 2022

**(iv) Mradi Na. 5408**: **Hospitali ya Kanda Burigi (Chato)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la huduma za uchunguzi kwa njia ya mionzi (Radiolojia) ambapo ujenzi umefikia asilimia 90, jengo la ghorofa mbili (2) la wodi ya wagonjwa (asilimia 45), uzio na njia za kuunganisha majengo (asilimia 98), nyumba 20 za watumishi (asilimia 96), njia za kutembelea (walk ways) (asilimia 80), jengo la nyumba ya mashine ya kufua umeme (power house) (asilimia 95), kisima cha maji (asilimia 30) na jengo la nyumba ya walinzi (asilimia 80). Jumla ya shilingi bilioni 4.63 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Mradi Na. 5423: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini – Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo maalumu la hospitali (OPD Complex) kwa ajili ya wagonjwa wa nje, uchunguzi (Maabara na Radiolojia), upasuaji, huduma za kufua, mochwari na wagonjwa wa ndani (wodi za wagonjwa) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98. Jumla shilingi bilioni 14.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(j) Mradi Na. 5428: Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutoa huduma za ubingwa wa juu ikiwemo kutumia maabara maalumu (CathLab) kuchunguza na kutibu magonjwa ya moyo ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021 jumla ya wagonjwa 80 walinufaika na huduma hii, hivyo kufanya idadi ya wagonjwa 521 waliohudumiwa tangu ilipoanza kutolewa; kufanyika kwa matibabu ya moyo kwa kufungua kifua (Open Heart Surgery) kwa watoto wanne (4); upandikizwaji wa figo (Kidney Transplant) kwa wagonjwa wawili (2); na uvunjaji wa mawe kwenye figo kwa kutumia mawimbi (Extra Corporeal Shock Wave Lithotripsy) na kutumia miale (laser lithotripsy) ambapo jumla ya wagonjwa 55 wamehudumiwa; upasuaji wa Ubongo na uti wa mgongo kwa wagonjwa 204; matibabu ya saratani kwa kutumia dawa (chemotherapy) kwa wagonjwa 466; upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 12; uchunguzi na matibabu ya maradhi ya magoti kwa kutumia matundu madogo

(Arthroscopy) kwa wagonjwa 17; kukamilika kwa hatua za mwisho za kuanzisha huduma ya upandikizaji wa uloto (bone marrow transplant) kwa kushirikiana na Hospitali ya St. Gerrado ya nchini Italia; kuanza kwa utoaji wa huduma za maabara ya *Histopathology* ambapo jumla ya wagonjwa 1,576 walihudumiwa; na ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20. Jumla ya shilingi milioni 100 zimetumika hadi Januari 2022.

**(k) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**

**(i) Hospitali ya Rufaa Mwananyamala – Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la mama na mtoto na ukamilishaji wa jengo la kutolea huduma za mama na mtoto (maternity block) kwa kuweka zege la njia ya kuunganisha jengo na maeneo mengine, kuweka mifumo ya huduma za ndani ya jengo ikiwa ni pamoja na maji safi, maji taka, maji ya mvua, umeme, gesi tiba, ung'amuzi wa moto na kuzima moto pamoja na TEHAMA ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98; kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) na jengo la huduma ya dharura (EMD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; na kuendelea na ukarabati wa chumba X-Ray. Jumla ya shilingi bilioni 4.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Hospitali ya Rufaa Sekou Toure – Mwanza**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) la huduma za afya ya uzazi na mtoto ambapo kazi zilizofanyika ni ujenzi wa jengo lote lenye ghorofa sita hadi kufikia hatua za umaliziaji, ufungwaji wa awali wa mifumo mbalimbali ndani ya jengo ikijumuisha mifumo ya umeme, maji, tehama, viyoyozi; kazi ya rangi na uwekaji wa marumaru / terazo; na ufungaji wa milango na wa nyumba ya mtumishi na ukarabati wa chumba cha X-Ray.

**(iii) Hospitali ya Rufaa Njombe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali inayojumuisha jengo la chini la maabara, jengo la ghorofa tatu (3) la huduma za afya ya uzazi, jengo la ghorofa tatu (3) la wodi ya upasuaji, magonjwa ya ndani na mifupa, jengo la ghorofa mbili (2) la huduma za dharura na uangalizi maalumu, jengo la chini la Damu Salama, jengo la kufulia nguo, kichomea taka na nyumba tano (5) za watumishi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96; na ukarabati wa chumba cha X-Ray. Jumla ya shilingi bilioni 2.97 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iv) Hospitali ya Rufaa Songwe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la maabara; kuendelea na ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.9, jengo la Afya ya uzazi (asilimia 14) na ufungaji wa mifumo mbalimbali ndani ya jengo la OPD; jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi (asilimia 7); na kuendelea na ukarabati wa chumba cha *X - Ray*. Jumla ya shilingi bilioni 6.21 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Hospitali ya Rufaa Simiyu**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa jengo la maabara limejengwa na kukamilika, jengo la huduma za upasuaji na radiolojia pia limekamilika, mwagaji wa zege “roof beam” kushikilia paa kwenye jengo la afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 55; kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 7; na kuendelea na ukarabati wa chumba cha CT Scan. Jumla ya shilingi bilioni 1.21 zimetumika hadi Januari 2022.

**(vi) Hospitali ya Rufaa Geita**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la wagojwa wa nje na jengo la maabara; kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa moja (1) la huduma za upasuaji na radiolojia, mghahawa na jengo la kufulia ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na kuanza kwa ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) la huduma za afya ya uzazi; kukamilika kwa asilimia 99 ya ujenzi wa jengo la maabara na jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi (asilimia 7). Jumla ya shilingi bilioni 1.87 zimetumika hadi Januari 2022.

**(vii) Hospitali ya Rufaa Katavi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Maabara na kukabidhiwa; kukamilika kwa ujenzi wa kuta za boma za “Kitalu A”; kukamilika kwa ujenzi wa kuta za boma kwa sehemu ya sakafu ya chini “Kitalu B”; kuendelea na ukamilishaji wa Kitalu A kwa Kupiga lipu “Plastering” na ufungaji wa mifumo ya Umeme, maji na TEHAMA (First Fix). Kwa jumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95. Aidha, ujenzi wa jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi umefikia asilimia 7. Jumla ya shilingi bilioni 4.76 zimetumika hadi Januari 2022.

**(viii) Hospitali ya Rufaa Mara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi na kuanza kutoa huduma kwa Kitalu C cha jengo la hospitali lenye vitalu vitatu (A, B na C) vilivyoungana; kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha dharura cha kuzalisha umeme (power house), kichomea taka, karakana, jengo la kufulia na jengo la kuhifadhi maiti. Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 94. Jumla ya shilingi bilioni 2.68 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ix) Hospitali ya Rufaa Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni:Kukamilika kwa usimikaji wa lift mbili katika jengo la afya ya Uzazi; ujenzi wa Framed Structure hadi sakafu ya tatu pamoja na kupauwa umekamilika, na kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya jengo la *Methadone* lenye ghorofa tatu (3) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.

**(x) Hospitali ya Rufaa Kigoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za upasuaji kwa kufungaji wa mifumo mbalimbali ndani ya jengo; frame za milango na madirisha; dari (ceiling); kupigaji rangi; kuchimba mashimo ya maji taka (septic tank na soakway) na kuweka marumaru. Kwa jumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 99. Aidha, ujenzi wa jengo la

Damu Salama umefikia asilimia 40 na jengo la wagonjwa Mahututi (ICU) na Huduma ya dharura (EMD) (asilimia 15). Jumla ya shilingi bilioni 1.64 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xi) Hospitali ya Rufaa Iringa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura kwa kuanzaa kuta kwa ajili ya kupaka rangi na kufunga fremu za milango ambapo utekelezaji umefikia asilimia 99.9; na kuendelea na ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20. Jumla ya shilingi milioni 150.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xii) Hospitali ya Rufaa Tabora**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za dharura kwa kufunga milango ya jengo na kuweka mifumo ya umeme na maji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5. Jumla ya shilingi bilioni 1.22 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xiii) Hospitali ya Rufaa Shinyanga**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la wagojwa wa nje (OPD); kuendelea na kazi za ufungaji wa mifumo mbalimbali kama umeme, maji, viyoyozi na gesi tiba ndani ya jengo la afya ya mama na mtoto ambapo utekelezaji umefikia asilimia 93; kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa UVIKO (Covid 19) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95 na jengo huduma ya dharura na wagonjwa mahututi (asilimia 10). Jumla ya shilingi bilioni 5.22 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xiv) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutoa huduma kwa majengo ya msingi yakiwemo jengo la afya ya uzazi, jengo la kufua, maabara na jengo la mochwari; na kuendelea na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, jengo la Damu Salama (asilimia 30) na jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi (asilimia 10). Jumla ya shilingi bilioni 1.86 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xv) Hospitali ya Rufaa Singida**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika na kuanza kutumika kwa jengo la huduma za afya ya uzazi, huduma za uchunguzi kwa njia ya mionzi na jengo la nyumba ya madaktari wa zamu; na kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tatu la wodi za kulaza wagonjwa, vyumba vya upasuaji, huduma za famasia, huduma za maabara na wagonjwa mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70 na jengo la huduma ya dharura na wagonjwa mahututi (asilimia 7). Jumla ya shilingi bilioni 5.13 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xvi) Hospitali ya Rufaa Mbeya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi ya wagonjwa wa upasuaji ambapo utekelezaji umefikia asilimia 82, wodi ya wagonjwa walio chini ya uangalizi maalum (ICU) (asilimia 99.9), jengo la huduma za dharura (EMD) (asilimia 99) na ukarabati wa jengo la ICU (asilimia 20). Jumla ya shilingi bilioni 1.02 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xvii) Hospitali ya Rufaa Kilimanjaro - Mawenzi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma ya afya ya uzazi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70; na ujenzi wa jengo la huduma za dharura umefikia asilimia 98 na jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 30). Jumla ya shilingi bilioni 3.15 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xviii) Hospitali ya Rufaa Rukwa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati na upanuzi wa jengo la huduma za dharura; na ujenzi wa jengo la Damu Salama ambao umefikia asilimia 20; kuendelea na ukarabati wa jengo la watu mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 5 na ujenzi wa jengo la Damu Salama umefikia asilimia 20. Jumla ya shilingi milioni 247.14 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xix) Hospitali ya Rufaa Ruvuma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea huduma za dharura (EMD) kwa kufanya ufungaji wa awali (1st Fix) wa mifumo ya maji na umeme, fremu za milango na madirisha na ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa kazi zinazoendelea na zinazofuata ambapo ujenzi umefikia asilimia 99.9. Jumla ya shilingi milioni 630.34 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xx) Hospitali ya Mkoa wa Pwani – Tumbi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo la huduma za dharura ambapo utekelezaji umefikia asilimia 10 na jengo la wagonjwa mahututi (asilimia 30). Jumla ya shilingi milioni 628.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xxi) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za Wagonjwa Mahututi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60, jengo la *Paediatric ICU* (asilimia 10); kuendelea na ukarabati wa jengo la huduma za dharura ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20. Jumla ya shilingi milioni 660 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xxii) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera - Bukoba**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa mahututi (ICU) na jengo la huduma za dharura (EMD). Jumla ya shilingi bilioni 1.22 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xxiii) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Temeke**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa mahututi (ICU) na jengo la huduma za dharura (EMD). Jumla ya shilingi milioni 310 zimetumika hadi Januari 2022.

**(xxiv) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Ligula - Mtwara**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la huduma za kuhifadhi maiti; kuendelea na ukamilishaji wa jengo la upasuaji, kutakasa vifaa, Wodi ya uzazi, ukarabati wa wodi 1, 2 na Wodi ya afya ya akili. Jumla ya shilingi milioni 334 zimetumika hadi

Januari 2022.

**(l) Mradi Na 2208: Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR) Kuimarisha Utengenezaji wa Dawa za Asili na Kuimarisha Mafunzo kwa Watoa Huduma za Tiba Asili**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na usimikaji wa mashine na mitambo ya kisasa ya kutengenezea dawa za asili; kuboresha kituo (centre) ya NIMR-Mabibo kwa kununua vifaa, mashine na mitambo ya kisasa ya kufanyia tafiti za dawa za asili; na kuendelea kutoa mafunzo ya kujiendeleza kwa watoa huduma wa tiba asili katika vyuo vya afya nchini vya DIHAS, MCOHAS, ITM-MUHAS, COTC-Sumbawanga, TNC - Kahama ambapo jumla ya waganga 50 wamepewa mafunzo. Jumla ya shilingi milioni 736.45 zimetumika hadi Januari 2022.

**(m) Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa na kusambazwa kwa chanjo zifuatazo: chanjo ya polio ya sindano(IPV) dozi 612,900, chanjo ya kichomi (PCV) dozi 3,167,400, Rota dozi 20,550, chanjo ya Saratani ya Mlango wa Kizazi (HPV) dozi 552,200, chanjo ya kuzuia surua na rubella (MR) dozi 2,000,000, chanjo ya polio ya matone (BOPV) dozi 6,000,000, na chanjo ya kukinga magongwa ya kifaduro, pepopunda, homa ia ini, homa ya uti wa mgongo na kichomi (DTP-HepB/Pentavalent) dozi 4,800,500; na kupatikana kwa chanjo dhidi ya UVIKO - 19 aina ya *Janssen* dozi 1,058,400 na *Sinopharm* dozi 2,578,200. Hadi kufikia mwisho wa Januari 2022 jumla ya watu 2,074,507 wamechanjwa. Jumla ya shilingi bilioni 24.06 zimetumika hadi Januari 2022.

**(n) Mradi Na. 5492: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

Hatua iliyofikiwa: Kutambuliwa kwa asilimia 89 ya Watu Wenye Virusi vya Ukimwi ambapo kati ya hao, asilimia 98 wanatumia dawa za kufubaza VVU na asilimia 96.1 ya wanaotumia dawa wamefanikiwa kufubaza VVU; na kuongezeka kwa vituo vya vinavyotoa huduma ya Tiba ya UKIMWI hadi vituo 6,759 kutoka vituo 5,555 mwaka 2015.

**(o) Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Watumishi wa Sekta ya Afya 2020 – 2025; kuandaliwa kwa mfumo wa mafunzo kwa njia ya masafa (e-Learning Platform); na kuhuishwa kwa mitaala ya stashahada ya juu ya *operating theatre management*, afya ya kinywa na meno, Matibabu kwa Vitendo (Occupational Therapy) na utabibu. Jumla ya shilingi bilioni 6.47 zimetumika hadi Januari 2022.

**(p) Mradi Na. 5441: Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati, upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia Chanjo - IVD Mabibo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52; kununuliwa kwa vifaa na vifaa tiba pamoja na mitambo sita (6) ya kufua hewa ya oksijeni; kuendelea na ujenzi wa majengo ya dharura 80 (Emergency Medical Departments - EMD); kuendelea na ujenzi wa majengo ya wagonjwa mahututi (ICU) 26 na nyumba 150 za watumishi (3 in

1) kwa ajili ya familia 450 katika maeneo ya pembezoni; ununuzi wa magari 407 yakijumuisha magari ya kubeba wagonjwa (Ambulance) 195, magari ya usimamizi katika Halmashauri na Mikoa 210 na magari mawili (2) Ofisi ya Rais-TAMISEMI; ununuzi wa pikipiki 368 kwa ajili ya kuwezesha huduma ya mkoba na uhamasishaji; na kuratibu Huduma Tembezi ya Mkoba ya Chanjo ya UVIKO-19, mafunzo ya huduma ngazi ya jamii na uhamasishaji. Jumla ya shilingi bilioni 355.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(q) Mradi Na. 5401: Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 127 ambapo jumla ya shilingi bilioni 38.4 zimetumika hadi Januari 2022 na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba ambapo kiasi cha shilingi bilioni 3.94 zimetumika.

**(r) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya 70; na kuendelea na ukamilishaji wa zahanati 564, ikiwa ni wastani wa maboma matatu (3) kwa kila Halmashauri. Jumla ya shilingi bilioni 27.4 zimetumika hadi Januari 2022 ikiwa shilingi bilioni 13.7 kwa ajili ya vituo vya afya na shilingi bilioni 15.31 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati 564.

**(s) Mradi Na. 5440: Miradi ya Maendeleo ya Tozo za Mawasiliano**

Hatua iliyofikia ni: Kuendelea na ujenzi wa vituo vya afya 233 katika Tarafa 207 zikiwemo Kata za Kimkakati vyenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji ambapo majengo yanayojengwa ni Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Jengo la Maabara na kichomea taka. Jumla ya shilingi bilioni 65.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(t) Mradi Na. 2204: Ujenzi na Upanuzi wa Majengo mbalimbali ya kutolea huduma za Mafunzo katika Vyuo vya Afya**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Wodi Maalum (Private wards) katika chuo cha Tabora *Clinical Officers Training* Centre ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75; kuendelea na ukarabati mkubwa wa majengo mbalimbali ndani ya chuo cha Ngudu Environmental Health School ambapo utekelezaji umefikia asilimia 65, Kilosa Clinical Officers Training Centre (asilimia 55) na Kagemu Environmental Health School (asilimia 70). Jumla ya shilingi bilioni 1.95 zimetumika hadi Januari 2022.

**(u) Ujenzi na Upanuzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na ujenzi wa Jengo la ofisi za Wizara Mtumba ambao umefikia asilimia 15. Jumla ya shilingi bilioni 3.45 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.5.2 Ustawi na Maendeleo ya Jamii

**(a) Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa karakana ya useremala, choo cha watumishi na cha wanafunzi, ukumbi wa mihadhara, jengo la maabara ya udongo, karakana ya ujenzi na ujenzi wa geti na uzio katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii

Misungwi (Mwanza); kukamilika kwa ujenzi wa madarasa matatu (3) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200 kila moja na ukarabati wa bweni lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 56 na darasa lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 250 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai (Tanga); na kuendelea na ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 568 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 50 na kumbi pacha za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,008 (asilimia 70) katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Jumla ya shilingi bilioni 2.1 zimetumika hadi kufikia Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa Kampeni ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto ya "Twende Pamoja: Ukatili Tanzania Sasa Basi" katika mkoa wa Kigoma; kutolewa kwa mikopo yenye masharti nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni 9.8 kupitia dirisha la wanawake katika Benki ya Posta; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.91 kwa wajasiriamali kupitia asilimia 4 ya pato la halmashauri; kuwezeshwa kwa wanawake wajasiriamali 500 kushiriki katika maonesho ya biashara ikiwemo Maonesho ya Sabasaba ili kukuza masoko ya bidhaa zao; kufanyika kwa uelimishaji wa masuala ya jinsia (Educational-Gender Caravan) katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Iringa, Taasisi ya Mafunzo ya Afya na Sayansi Shirikishi - Njombe, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia – Mbeya na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo jumla ya wananchi 43,678 walifikiwa.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa kwa Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000) na Rasimu ya Sera ya Taifa ya Jinsia (2021) na Mkakati wa Utekelezaji, Rasimu ya Mwongozo wa Dawati la Jinsia katika taasisi za elimu ya juu, rejista kwa ajili ya kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia katika vyuo vya elimu ya juu na kati na kanzidata ya Wanawake Katika Uongozi ambayo itakuwa ikipatikana mtandaoni ambapo wanawake wenye ujuzi mbalimbali wataweka wasifu wao (Curriculum Vitae) ili waajiri na mamlaka za uteuzi ziwapate kwa urahisi; kuadhimishwa kwa Siku ya Mwanamke wa Kijijini (tarehe 15 Oktoba) kwa lengo la kuielimisha jamii juu ya changamoto za mwanamke wa kijijini ambapo jumla ya washiriki 2,000 walishiriki (wanawake 1,300 na wanaume 700); kuadhimishwa kwa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambapo jumla ya washiriki 1,238 walishiriki (wanawake 820 na wanaume 418); kuzinduliwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Kuwezesha Utekelezaji wa Ahadi za Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum); na kuendelea kuratibu jitihada za kuimarisha ulinzi wa Wanawake na Watoto kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22). Jitihada hizi zimewezesha kuanzishwa kwa Kamati 1,843 na kufanya idadi ya Kamati za ulinzi wa Wanawake na Watoto Kufikia 18,186 kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Jumla ya shilingi milioni 58.2 zimetumika hadi kufikia Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto**

Hatua iliyofikiwa ni: kuandaliwa kwa Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na

Maendeleo ya Awali ya Mtoto; kutolewa kwa mafunzo kwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto; kutolewa kwa mafunzo katika ngazi ya mkoa kwa mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa washiriki 156 wakiwemo Waganga, Maafisa Elimu, Maafisa Lishe, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii na Waandishi wa Habari kuhusu Programu Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto; kuhudumiwa kwa watoto 2,122 kupitia taarifa za simu bure (116) dhidi ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa watoto; kuwezesha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike (tarehe 11 Oktoba) kwa lengo la kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kumlinda na kumuendeleza mtoto wa kike.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kijamii 30 vya kulelea watoto wadogo wakati wa mchana katika Mikoa ya Dar es Salaam (10) na Dodoma (20) kwa ajili ya majaribio ili kuimarisha utoaji wa huduma za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto; kuandaliwa kwa Ajenda ya Kitaifa ya Uwajibikaji wa Wazazi wote wawili katika malezi ya watoto na kutolewa kwa elimu kwa wazazi 300 kuhusu ajenda katika Halmashauri (tisa) 9 za mikoa ya Songwe (Ileje, Tunduma na Mbozi), Mbeya (Rungwe, Chunya na Mbeya) na Kigoma (Kibondo, Kasulu na Ujiji); wanawake, vijana na wasichana balehe 130 walifundishwa malezi chanya kwa ajili ya kuwalinda watoto wao dhidi ya vitendo vya ukatili katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Singida, Geita na Dodoma: kuandaliwa kwa Taarifa ya 6 ya Nchi ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto; kufanyika kwa tathmini ya hali ya vikundi vya kijamii vya malezi vilivyoanzishwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Iringa, Mwanza, Njombe na Dar es Salaam kwa lengo la kutafuta namna bora ya kuendesha vikundi hivyo nchini; kutolewa kwa mafunzo kuhusu ulinzi na haki za watoto kwa walimu 2,333 katika mikoa ya Morogoro (1,176), Singida (487) na Geita (670) ili watumie elimu hiyo kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili wakiwa shuleni pamoja na kuwafundisha mbinu za kujilinda na ukatili shuleni na katika jamii; kuandaliwa kwa rasimu ya kitini cha kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi kuhusu athari za ukatili dhidi ya watoto mtandaoni kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la vitendo vya ukatili kwa watoto katika mitandao mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi milioni 285.1 zimetumika hadi kufikia Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 5451: Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii**

Hatua iliyofikiwa ni: kusajiliwa kwa vituo 303 vya kulelea watoto wadogo mchana ambapo watoto 6,772 (wavulana 3,194 na wasichana 3,578) wameandikishwa; kusajiliwa kwa makao 24 ya watoto yenye jumla ya watoto 707 (Wavulana 412 na Wasichana 295); kutolewa kwa mafunzo ya malezi kwa walezi wa watoto 1,156 (wanaume 199 na wanawake 957) katika mikoa ya Dar es salaam (545), Mbeya (381) na Pwani (230); kutolewa kwa malezi ya kambo kwa watoto 22 (wavulana 9 na wasichana 13) na kuasiliwa kwa watoto 25 (wavulana 9 na wasichana 16); kuchepushwa kwa watoto 49 (wasichana 7 na wavulana 42) walio katika mkinzano na sheria kutoka mfumo rasmi wa haki jinai na kutengamanishwa na familia zao; kufanyika kwa tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003 na kuandaliwa kwa rasimu mpya ya sera.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Kutolewa kwa Huduma ya mahitaji ya msingi (chakula, mavazi, malazi na huduma za afya) kwa watoto 195 (wasichana 22 na wavulana 173) walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu tano (5) za watoto; kutolewa kwa huduma ya mahitaji ya msingi kwa watoto 76 (wavulana 45 na wasichana 31) katika Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo; kutolewa kwa huduma ya mahitaji ya msingi kwa watoto 37 (wavulana 35 na wasichana 2) waliobainika kufanya makosa ya jinai waliopo katika Shule ya Maadilisho Irambo, Mbeya; kutolewa kwa huduma ya mahitaji ya msingi kwa wazee 537 wasiojiweza (wanaume 295 na wanawake 242) katika makazi 20 yanayomilikiwa na taasisi binafsi na wazee wasiojiweza 275 (wanaume 164 na wanawake 111) katika makazi 14 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali; kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee (tarehe 01 Oktoba) kwa lengo la kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kuwajali na kuwatunza wazee. Jumla ya shilingi bilioni 1.39 zimetumika hadi kufikia Januari 2022.

#### 3.3.5.3 Elimu

**(a) Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa bwalo la chakula, mfumo wa maji taka na uwekaji wa samani katika hosteli ya Chuo Kikuu cha Mzumbe; na kuendelea na ujenzi wa shule ya mfano Iyumbu – Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 55; kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa ya shule za msingi 1,970, sekondari 1,249, matundu ya vyoo shule za msingi 5,303, na sekondari matundu 80, mabweni ya shule za msingi 6 na sekondari 106, mabwalo ya shule za sekondari 6, nyumba za walimu wa msingi 17 na sekondari 14, majengo ya utawala 4 na maabara za shule za sekondari 11; na ujenzi wa shule mpya za msingi 9 na sekondari 15. Jumla ya shilingi bilioni 21.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 4321: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MMEM) LANES II**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa uchapaji na usambazaji wa jumla ya machapisho 6,498,965 yakijumuisha vitabu vya kiada 5,898,995 na kiongozi cha mwalimu 599,970 kwa masomo yote ya Darasa la VI na VII ili kuimarisha uwiano kati ya mwanafunzi na kitabu; uchapaji wa vitabu vya kiada 1,544,177 na kiongozi cha mwalimu 154,500 ili kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa wanafunzi waliopo kwenye Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA); kuendelea na mafunzo kwa wawezeshaji kitaifa 195 wanaotarajiwa kutoa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa ngazi ya shule na vituo vya walimu (TRC); kufanyika kwa mafunzo ya kuimarisha uthibiti ubora wa shule wa ndani kwa Walimu Wakuu 7,612 na Waratibu Elimu Kata 3,860; kukamilika kwa michoro kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya awali 150 ya mfano na mabweni 10 ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu; na kuendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 304, matundu ya vyoo 548, mabweni nane (8), nyumba za walimu 21 na majengo ya utawala manne (4) katika Shule za msingi. Jumla ya shilingi bilioni 24.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 6,096, vifaa vya kunawia mikono 1,655 na ununuzi wa matenki 238 ya kuhifadhi maji katika shule 235 za msingi; kutolewa kwa mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (School WASH Guideline) kwa waratibu wa SWASH wa mikoa 17 na halmashauri 86; na kuwezesha Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ujenzi wa vyoo, miundombinu ya maji na vifaa vya kunawia mikono katika Shule za Msingi. Jumla ya shilingi bilioni 7.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa shule mpya 231 za Sekondari za kata katika kata ambazo hazina shule za Sekondari; na ujenzi wa shule 10 kati ya lengo la shule 26 maalum za bweni za wasichana kwa masomo ya Sayansi. Jumla ya shilingi bilioni 139.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa katika shule 34 (msingi 26 na sekondari 8) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30; kuendelea na ujenzi wa ofisi za walimu za shule mbili (2) za sekondari zenye uhitaji mkubwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; kuendelea na ujenzi wa maabara tatu (3) za sayansi katika shule tatu (3) za sekondari zenye uhitaji mkubwa ambapo ujenzi umefikia asilimia 30; kuendelea na ujenzi wa matundu 1,920 ya vyoo katika shule 58 za msingi na 22 za sekondari zilizo na uhitaji mkubwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kuboresha miundombinu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule 8 za msingi na shule moja (1) ya sekondari ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20; na kutolewa kwa mafunzo ya ufundi stadi kwa vijana 1,627 wanaotoka katika kaya maskini na wenye ulemavu chini ya mradi wa kukuza ujuzi (Bursary Scheme – SDF). Jumla ya shilingi bilioni 8.24 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 6363: Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha - ATC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 420 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 35; kuendelea na ujenzi wa kliniki yenye hadhi sawa na hospitali ya wilaya itakayohudumia wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo jirani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53; na kuendelea na usanifu wa mfumo wa ndani wa mtandao (local area network installation) kwa lengo la kuwezesha kutoa mafunzo kwa kutumia TEHAMA. Jumla ya shilingi milioni 772.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa wanagenzi 2,164 kutoka kwenye sekta isiyo rasmi; kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera ambapo umefikia asilimia 92; na kukamilika kwa ujenzi wa Chuo Cha

VETA cha Wilaya ya Kasulu. Jumla ya shilingi bilioni 30.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Mradi Na. 4371: Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu - UTC**

**(i) Chuo cha Ualimu Ndala - Tabora:** Kukamilika kwa ujenzi na uwekaji wa samani katika mabweni mawili (2) ya ghorofa moja (1), madarasa mawili (2) ya ghorofa moja (1), jengo la maktaba, jengo la maabara, ukumbi wa mikutano; kukamilika kwa ujenzi wa matanki mawili (2) ya kuhifadhi maji, nyumba tano (5), majengo mawili (2) ya ghorofa moja, majengo mawili (2) ya vyoo na ukarabati wa mabweni mawili (2) ya wanafunzi;

**(ii) Chuo cha Ualimu Kitangali - Mtwara:** Kukamilika kwa ujenzi na uwekaji wa samani katika nyumba 11 za wafanyakazi, ukumbi wa mikutano, majengo mawili (2) ya ghorofa moja (1) kwa ajili ya madarasa, majengo mawili (2) ya ghorofa moja (1) kwa ajili ya mabweni, jengo la maktaba, jengo la maabara, jengo la ukumbi wa mihadhara na majengo matatu (3) ya vyoo;

**(iii) Chuo cha Ualimu Shinyanga:** Kukamilika kwa ujenzi na uwekaji wa samani katika majengo yafuatayo: mabweni mawili (2), jengo moja (1) la ghorofa moja kwa nyumba za wafanyakazi; kukamilika kwa ujenzi wa majengo mawili (2) ya ghorofa moja (1) kwa ajili ya madarasa, jengo la maktaba, majengo mawili (2) ya vyoo; kukamilika kwa ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la Chuo; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba tatu (3), mabweni mawili (2), ukumbi wa chakula, jiko, jengo la utawala, kisima cha kuhifadhi maji na uwekaji wa mifumo ya gesi ya kupikia; na

**(iv) Chuo cha Ualimu Mpuguso - Mbeya:** Kukamilika kwa ujenzi na uwekaji wa samani katika mabweni mawili (2), nyumba tatu (3) za ghorofa za watumishi; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba nne (4) za watumishi, majengo mawili (2) ya ghorofa kwa ajili ya madarasa, jengo la maktaba, jengo la maabara, jengo la ukumbi wa mihadhara na ukumbi wa mikutano.

Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(i) Mradi Na. 4392: Kuendeleza Elimu ya Ualimu - TESP**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa maabara za sayansi, maktaba na vyumba vya TEHAMA katika Vyuo 7 vya Butimba (asilimia 100), Morogoro (asilimia 80), Tukuyu (asilimia 80), Kasulu (asilimia 65), Patandi (asilimia 50), Mpwapwa (asilimia 70) na Dakawa (asilimia 20); kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga ambapo umefikia asilimia 98; kukamilika kwa ujenzi wa maktaba ya Chuo cha Ualimu Korogwe; kukamilika kwa ukarabati wa Kituo cha Hisabati Morogoro; kununuliwa kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo vya ualimu 35 ambapo ununuzi umefikia asilimia 75; kukamilika kwa ununuzi wa vifaa na madawa ya maabara katika vyuo 10 vya ualimu vya sayansi; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA ambapo umefikia

asilimia 45 na kuendelea na uunganishaji wa vyuo 35 vya ualimu katika Mkongo wa Taifa ambapo umefikia asilimia 35; kuendelea na ukamilishaji wa uundaji wa mfumo wa usahihishaji wa kielektroniki ambapo umefikia asilimia 55; kutolewa kwa mafunzo ya TEHAMA kwa wakufunzi 1,203, mafunzo kazini katika masomo ya kufundishia kwa wakufunzi 1,042, mafunzo kuhusu mtaala wa umahiri kwa walimu shule za msingi na sekondari, maafisa elimu kata na wilaya, wathibiti ubora na wakufunzi 797, na mafunzo ya uongozi kwa menejimenti ya vyuo vya ualimu kwa viongozi 306 wa vyuo 35 vya ualimu vya Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 15.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(j) Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukusanyaji wa mikopo iliyoiva ambapo kiasi cha shilingi bilioni 97.97 kilikusanywa sawa na asilimia 49 ya lengo la mwaka; kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 210.95 kwa wanafunzi 176,617 kati ya hao wanafunzi 69,274 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 107,343 ni wanaoendelea na masomo; kuanzishwa kwa Kituo Mahsusi cha Wateja; na kufanyika kwa ukaguzi kwa waajiri 1,521 na kubaini wanufaika wapya 17,997. Jumla ya shilingi bilioni 215.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(k) Mradi Na. 4392: Mradi wa Elimu wa Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi ya ESPJ**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 35; kununuliwa kwa vifaa na samani katika vyuo vya ufundi stadi vya Kongwa, Kasulu, Nyasa na Ruangwa; kuendelea na utekelezaji wa mfuko wa kuendeleza ujuzi ambapo tathmini ya mahitaji imefanyika; kuwezesha utekelezaji wa Program ya Mafunzo ya Utarajali (Internship) na Uanagenzi (Apprentiship) kupitia SIDO, TEA, NCT (National College of Tourism), VETA na ERB; kutolewa kwa mafunzo kwa watumishi 2,400 wa VETA na FDCs kwa lengo la kuimarisha stadi za ujuzi; kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa vyuo 14 vya maendeleo ya wananchi (FDCs) ambapo ujenzi umefikia asilimia 95 na ujenzi wa vyuo 25 vya ufundi stadi vya wilaya umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(l) Mradi Na. 4322 na 4393: Elimumsingi Bila Ada**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea kutolewa kwa ruzuku ya uendeshaji wa shule za msingi na sekondari; kugharamiwa kwa chakula cha wanafunzi 47,714 wa bweni na kutwa kwa shule za msingi; kulipwa kwa fidia ya ada kwa wanafunzi 2,261,095 wa bweni na wa kutwa kwa shule za sekondari; na kulipwa kwa posho ya madaraka kwa walimu wakuu 16,602 na maafisa elimu kata 3,921. Jumla ya shilingi bilioni 166.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(m) Mradi Na. 4314: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maabara ya baiolojia ambapo umefikia asilimia 75; kuendelea na ukarabati wa hosteli, jengo la maabara ya Kemia namba 3, jengo la utawala, jengo la maabara za kompyuta na majengo ya mihadhara ambapo ujenzi umefikia asilimia 85; na kununuliwa kwa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kumbi tano

(5) za mihadhara na semina. Jumla ya shilingi milioni 129.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(n) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maabara kuu ya kemikali ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na utoaji wa huduma za upimaji wa sampuli za Viwandani; kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Viumbe Maji Baridi Chato, mkoani Geita; kuendelea na ukamilishaji wa Kituo cha Wanafunzi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na kuendelea na ujenzi wa jengo la jengo la Shule Kuu ya Uchumi katika kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(o) Mradi Na. 4385: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa upanuzi wa jengo la utawala awamu ya pili (Hatua ya Tatu); na kukamilika kwa usanifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maabara za sayansi katika shule ya sekondari ya mazoezi ya Chang'ombe. Jumla ya shilingi milioni 455.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(p) Mradi Na. 6353: Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uwekaji wa samani katika hosteli za wanafunzi katika kampasi kuu; kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala lenye uwezo wa kuchukua watu 143; kuendelea na taratibu za ununuzi wa vifaa vya jengo la kumbi za mihadhara, madarasa na mabwalo ya chakula yenye uwezo wa kuhudumia watu 900 na ukarabati wa bwalo la chakula katika Ndaki ya Mbeya. Jumla ya shilingi milioni 172.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(q) Mradi Na. 6354: Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 592; kukamilika kwa uwekaji wa samani katika sehemu ya Wing B ya jengo la ardhi kwa ajili ya wanafunzi 32 wa shahada ya uzamivu na wafanyakazi 67; kuendelea na ukarabati wa karakana, madarasa, maabara, mabweni ya wanafunzi na miundombinu ya barabara na TEHAMA ambapo umefikia asilimia 60; na kuendelea na usanifu na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa mihadhara. Jumla ya shilingi bilioni 2.8 zimetumika hadi Januari 2022.

**(r) Mradi Na. 6365: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; kuendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara; kuendelea na ukarabati wa ofisi za Kampasi Kuu Moshi, vyuo vya mikoani, nyumba tatu (3) za makazi ambapo mbili (2) zipo katika Kampasi ya Moshi na moja (1) ipo ofisi ya Chuo Mbeya ambapo utekelezaji umefikia asilimia 80. Jumla ya shilingi bilioni 1.1 zimetumika hadi Januari 2022.

**(s) Mradi Na. 6364: Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Mloganzila**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Umahiri wa Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu – Mloganzila; kuendelea na uimarishaji wa miundombinu ya TEHAMA ambapo ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuboresha jukwaa la kujifunzia kwa njia ya mtandao umefikia asilimia 99; kukamilika kwa ujenzi wa tanki la maji na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya majitaka, katika eneo la Hosteli ya Chole; na kuendelea na ukarabati wa awamu ya pili ya kituo cha kufundishia cha Bagamoyo. Jumla ya shilingi milioni 110.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(t) Mradi Na. 4384: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaaam – DIT**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa matano (5) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200 na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 160 ambapo ujenzi umefikia asilimia 50; kuendelea na taratibu za ununuzi wa samani na vifaa vya TEHAMA katika maktaba ya DIT na vifaa vya karakana; kukamilika kwa uwekaji wa miundombinu ya mtandao na ununuzi wa samani za madarasa na mabweni katika Kampasi ya Myunga. Jumla ya shilingi milioni 23.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(u) Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki - TAEC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara na ofisi zilizopo Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza ambapo utekelezaji umefikia asilimia 92, asilimia 18, asilimia 48 na asilimia 58 mtawalia; kuendelea na upembuzi yakinifu kwa mradi wa kinu cha tafiti za kinyuklia (Research Reactor) kwa ajili ya uchunguzi ikiwemo magonjwa na matibabu ya saratani; kuendelea na ujenzi wa jengo maalumu Dar es salaam kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi kwa kutumia teknolojia ya mionzi (Multipurpose Irradiator Facility). Jumla ya shilingi bilioni 1.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Mradi Na. 6333: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa maktaba awamu ya pili ambapo ujenzi umefikia asilimia 99, mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 (asilimia 42), maabara za kufundishia (asilimia 21), karakana (asilimia 33); na kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia vya maabara. Jumla ya shilingi milioni 426.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(w) Mradi Na. 6361: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara na mahema; kuendelea na utekelezaji wa miradi 13 ya tafiti zinazohusu uzalishaji na afya za wanyama na samaki; kuendelea na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na mimea ya asili, kilimo endelevu cha mazao mbalimbali, mabadiliko ya tabia nchi, maliasili, misitu na rasilimali maji; kuendelea na ujenzi wa jengo la maabara mtambuka ambapo ujenzi umefikia asilimia 98; kuendelea na ukarabati wa madarasa, mabweni ya wanafunzi, viwanja vya michezo na ujenzi wa daharia ya muda katika kampasi ya Mizengo Pinda; kuendelea na

uanzishaji wa shamba la mbegu za mazao ya mpunga na maharage; kuendelea na uboreshaji wa uendelezaji wa shamba la mafunzo ikiwa ni pamoja na kupanda miche 500 ya michikichi, malisho ya ng'ombe - Magadu, kufunga mfumo wa umwagiliaji wa matone kwenye hekari tatu (3) bustani ya mboga; na kuendelea na ukarabati wa mabwawa matano (5) ya samaki na mabwawa 12 madogo kwa ajili ya vifaranga vya samaki.

**(x) Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kujenga na kufunga mifumo ya nishati mbadala katika vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi.

**(y) Mradi Na. 4381:Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa mabweni mawili (2) yanayohudumia wanafunzi 768 kila moja katika kampasi ya Karume – Zanzibar ambapo utekelezaji umefikia asilimia 17; kuendelea na ujenzi wa nyumba tatu (3) za wafanyakazi kwa ajili ya watumishi 30 katika Kampasi ya Karume; na kuendelea na ujenzi wa madarasa na bweni la wanafunzi katika tawi la Pemba. Jumla ya shilingi milioni 800.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(z) Mradi Na. 4306: Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuanza kwa ujenzi wa ghorofa moja (1) lenye kumbi nne (4) za mihadhara na ofisi kumi (10) katika Kampasi ya Mbeya; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba moja (1) pamoja na uunganishaji wa maji safi ya bomba kwa nyumba zote 14 za wafanyakazi, kumbi nne (4) za mihadhara na ofisi nne (4) za watumishi katika Kampasi ya Bagamoyo. Jumla ya shilingi milioni 408.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(aa) Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ugharamiaji wa miradi 12 ya utafiti na ubunifu inayoendelea ambapo miradi nane (8) ni ya utafiti, mitatu (3) ni ya ubunifu na mmoja (1) ni wa miundombinu ya utafiti; kukamilika kwa ufadhili wa jumla ya miradi mipya 20 (3 ya uboreshaji wa matokeo ya utafiti, miwili (2) ya miundombinu, 13 ya ubunifu wa wabunifu MAKISATU na wabunifu wengine na miwili (2) ya SAIS Boost-Up Start-Ups); kuendelea na uchambuzi wa maandiko matano (5) ya miradi ya ubunifu inayoendelea iliyokidhi vigezo kwa ajili ya kupata mradi mmoja wa ubiasharishwaji; kuendelea na uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu na mfumo wa TEHAMA wa Menejimenti ya Utafiti na Ubunifu ili kuongeza ufanisi na upatikanaji wa taarifa za watafiti na wabunifu; kuendelea na uratibu wa vigoda vya utafiti nchini ambapo taasisi tano (5) za utafiti ziliwezeshwa kuandaa miongozo ya namna ya kuanzisha na kuendeleza vigoda vya utafiti kwa lengo la kutengeneza mtandao wa watafiti bobezi katika sekta za kipaumbele za afya, kilimo, mifugo na madini; kujengea uwezo watafiti katika kufanya tafiti ambazo zitachangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini na Afrika; kuanzishwa kwa kumbi bunifu 10 katika vyuo vya maendeleo ya Wananchi 10 (Chiswalu - Dodoma, Kiswangwa - Mara, Sengerema - Mwanza, Kasulu -Kigoma, Katumba - Mbeya, Kilwa Masoko, Mto wa Mbu - Arusha, Newalla - Mtwara, Kiwanda– Tanga na Njombe); na kukamilika kwa mapitio ya rasimu ya mwongozo wa Kitaifa wa kusimamia vituo vya umahiri vya utafiti (National

Framework for Research Centers of Excellence). Jumla ya shilingi bilioni 1.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(bb) Mradi Na. 4386: Ujenzi na Ukarabati Chuo Kikuu cha Dodoma**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ya jengo la Chimwaga, kumbi mbili (2) za mihadhara na kumbi mbili (2) za semina na ununuzi wa samani; na kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa usakinishaji wa *fiber* awamu ya pili, upangaji na usanifu wa mtandao. Jumla ya shilingi bilioni 17.9 zimetumika hadi Januari 2022.

**(cc) Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ununuzi wa msanifu wa kuandaa Mpango Kabambe wa kampasi ya Oswald Mango'mbe, Butiama; kukamilika kwa ununuzi wa msanifu majengo, uainishwaji wa vifaa vya ujenzi, makadirio ya gharama na ukarabati wa majengo katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe; na kuendelea na utunzaji wa shamba la miti ya matunda mbalimbali (Orchard) lenye ukubwa wa ekari mbili (2) Butiama.

**(dd) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa maboma ya vyumba 1,853 ya madarasa katika Shule za Msingi, maboma 1,840 ya vyumba vya madarasa ya Shule za Sekondari na vyumba 869 vya maabara za sayansi katika Shule za Sekondari. Jumla ya shilingi bilioni 59.73 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.5.4 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**(a) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kupanga na kupimwa kwa viwanja 32,775 katika halmashauri 29 za Buhigwe DC (1,767), Kigoma DC (711), Songea Manispaa (400), Dodoma Jiji (4,191), Geita TC (320), Moshi DC (157), Busega DC (351), Mbeya Jiji (2,400), Iringa DC (1,006), Iringa Manispaa (1,060), Misungwi DC (312), Sengerema DC (2,481), Kaliua DC (1,035), Mpanda Manispaa (170), Rufiji DC (1,568), Mafia DC (460), Kinondoni Manispaa (383), Jiji la Dar es Salaam (5,845), Temeke Manispaa (1,112), Kigamboni Manispaa (456), Biharamulo DC (321), Mtwara Manispaa (1,385), Njombe TC (324), Wanging'ombe DC (538), Makete DC (236), Ludewa DC (990), Iramba DC (712), Manyoni DC (2,312), Singida Manispaa (141) na Ikungi (342); kuandaliwa kwa hati ya hakimiliki ya kimila 1,011 katika Halmashauri za Kigoma DC (711) na Mwanga DC (300); kutambuliwa kwa vipande vya ardhi 18,686 katika Halmashauri za Misungwi DC (3,719), Meru DC (3,537), Tabora Manispaa (715), Arusha DC (1,133), Longido DC (3,359), Monduli DC (5,612) na Kilwa DC (611); na kutolewa kwa leseni za makazi 17,847 katika Halmashauri 29. Jumla ya shilingi bilioni 1.95 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuimarishwa kwa kilometa 83 za mpaka kati ya Tanzania na Kenya hivyo kufanya jumla ya eneo la mpaka lililoimarishwa kuwa kilometa 255 kati ya kilometa 758 za mpaka wa nchi kavu wa Tanzania na Kenya. Jumla ya shilingi bilioni 3.7

zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na 2329: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa andiko la mradi na makubaliano ya awali ya mradi (loan lending agreement) baina ya Serikali na Benki ya Exim ya Korea kwa ajili ya kuwezesha kuanza utekelezaji wa mradi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 65.

**(d) Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa maandalizi ya upatikanaji wa mkopo ikiwa ni pamoja na kuandaa nyaraka muhimu za mradi na ushirikishwaji wa wadau; na kukamilika kwa majadiliano na Benki ya Dunia ambapo Benki hiyo imeidhinisha mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya dola za Marekani milioni 150.

**(e) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika wilaya tano (5) za Mbalali, Kinondoni, Kigamboni, Kongwa na Sengerema; na ununuzi wa samani katika Mabaraza ya Ardhi matatu (3) ya wilaya za Kongwa, Kigamboni na Ubungo. Jumla ya shilingi milioni 26 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa Wilaya za Uvinza na Tanganyika; kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 22 vilivyopo katika mkuza wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa wilaya za Kibaha, Chamwino na Mpwapwa; kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 69 vilivyopo kwenye maeneo ya vyanzo vya maji yanayoingiza katika bonde la mto Rufiji kwa wilaya za Wanging'ombe, Mufindi, Kilolo na Mbarali; kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 127 vilivyopo katika wilaya 21; kujengea uwezo timu 224 (*Participatory Land Use Management – PLUM*) kutoka halmashauri za wilaya 28 na Kamati za uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi vijijini (VLUM) kuhusu kupanga, kutekeleza na kusimamia masuala ya matumizi ya ardhi. Jumla ya shilingi milioni 884.6 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.5.5 Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

Katika mwaka 2021/22, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maji nchini ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini na mijini. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imeongezeka kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwezi Juni 2020 hadi wastani wa asilimia 72.3 Januari 2022. Aidha, kwa upande wa mijini katika kipindi kama hicho hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi imeongezeka kutoka asilimia 84 hadi asilimia 86.

**(a) Mradi Na. 3436: Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP - II)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kununuliwa kwa magari manne (4) na vitendea kazi kama vile kompyuta na *scanner* kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji wa miradi ya maji; na kufuatiliwa

kwa utekelezaji wa miradi 107 ya maji na usafi wa mazingira katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro, Singida, Shinyanga, Kagera, Geita, Mbeya, Rukwa, Songwe, Pwani na Tanga. Jumla ya Shilingi bilioni 7.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vituo 101 vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji; kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa; kukamilika kwa zoezi la kuhamisha makaburi kutoka katika Vijiji vya Bubutole na Mombose kwenda katika eneo la Sankwaleto Halmashauri ya Wilaya ya Chemba; na kukamilika kwa usanifu wa ukarabati wa mabwawa 20 ya ukubwa wa kati katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 5.04 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 3435: Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Shughuli zilizotekelezwa ni: kununuliwa kwa vifaa na vitendea kazi vya maabara; kufuatilia ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali vya maji na katika mifumo ya kusambaza maji; kutengenezwa na kusambazwa teknolojia ya kuondoa/kupunguza madini ya *Floride* katika maji kwenye mikoa ya Arusha na Singida; na kutoa mafunzo kwa wataalamu 16 wa maabara kuhusu uaandaaji wa Mpango wa Usalama wa Maji. Jumla ya shilingi milioni 560.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

Shughuli iliyotekelezwa ni kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 249 na imeanza kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wapatao 1,115,056 waishio vijijini. Jumla ya shilingi bilioni 214.68 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 3306: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira Arusha ambapo utekelezaji umefikia asilimia 73; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji na usafi wa mazingira mji wa Kigoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95. Jumla ya shilingi bilioni 9.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Longido; kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Maji Orkesumet ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 98.5; na kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mugango – Kiabakari - Butiama ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 31. Jumla ya shilingi bilioni 6.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa chanzo cha maji ambapo utekelezaji

umefikia asilimia 65; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika miji ya Same na Mwanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 92. Jumla ya shilingi milioni 132.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(h) Mradi Na. 3342: Mradi wa Maji wa Tabora – Igunga - Nzega**

Shughuli iliyotekelezwa ni kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka maji katika miji ya Tinde na Shelui ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 13.

**(i) Mradi Na. 3437: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji eneo la DAWASA**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi katika eneo linalohudumiwa na DAWASA linalohusisha maeneo ya Kibamba hadi Kisarawe, Mlandizi hadi Chalinze/Mboga, Kisarawe – Pugu - Ukonga - Kisukulu, Mbezi Luis, Kiluvya, Tegeta, Wazo, Madale, Mivumoni, Mabwepande na Bagamoyo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 95; na kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi wa mabwawa ya majitaka eneo la Kurasini (Temeke). Jumla ya shilingi bilioni 11.5 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.5.6 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

**(a) Programu Na. 5301: Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**(i) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia Vijijini**

Hatua iliyofikiwa ni: Ujenzi wa viwanda vidogo viwili (2) vya kutengeneza bidhaa za ngozi katika Halmashauri za Simanjiro na Kishapu; majosho mawili (2) katika Halmashauri za Mpwapwa na Simanjiro; mabirika mawili (2) ya kunyweshea mifugo katika Halmashauri za Simanjiro na Mpwapwa; vitalu vya Mkonge (Ekari 20) katika Halmashauri ya Kishapu; ujenzi wa nyumba za nyuki (Manzuki) 16 katika halmashauri ya Kishapu; kutengeneza na kusambaza mizinga 400 ya ufugaji nyuki katika Halmashauri za Kishapu (200) na Simanjiro (200); kuanza ujenzi wa mfereji wa Skimu ya Umwagiliaji ya Lukenge katika halmashauri ya Mvomero na uchimbaji wa visima virefu vitatu (3) katika Halmashauri ya Mpwapwa. Aidha, katika Wilaya ya Kaskazini A Unguja kazi zifuatazo zimetekelezwa: utengenezaji wa majiko banifu kwa kaya 90; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika Shehia tatu (3) za Matemwe Kijini, Matemwe Jugakuu na Matemwe Mbuyutende; utafiti wa maji chini ya ardhi ya kubaini maeneo ya kuchimba visima; na mafunzo ya utengenezaji wa sabuni na vipodozi kwa washiriki 45 kutoka Shehia tatu za Matemwe. Jumla ya shilingi bilioni 1.88 zimetumika hadi Januari 2022.

**(ii) Mradi wa Kujengea Uwezo wa Taasisi ili Kupunguza Hewa Ukaa Inayosababishwa na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu**

Hatua iliyofikiwa ni: Ununuzi wa vitendea kazi ikijumuisha kompyuta mpakato 14, mashine ya kudurufu, skana na projekta; kushiriki vikao vya majadiliano katika mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Glasgow, Uskoch; na kuwezesha uratibu na ushiriki katika vikao mbalimbali vya masuala ya REDD+. Jumla ya shilingi milioni 219.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iii) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 15 vya Tanzania bara na shehia nane (8) katika wilaya ya Micheweni (Pemba); kuandaliwa kwa hati miliki za kimila 1,750 ambapo kati ya hizo hati 1,350 zimekabidhiwa kwa Wilaya za Magu na Nzega; kutolewa mafunzo ya matumizi ya ardhi na usimamizi wa maliasili kwa washiriki 3,472; kuanzishwa kwa mashamba darasa 92 yenye wajumbe 1,475; kutolewa kwa mafunzo ya shamba darasa kwa maafisa ugani na wakulima 603; kutolewa kwa mafunzo ya jinsia kwa washiriki 575; kuandaliwa kwa Mkakati wa jinsia na vijana *(Gender and Youth Strategy)*; kutolewa mafunzo kwa watalaam wa misitu 12 kuhusu tathmini shirikishi ya misitu kwa ajili ya kuandaa mpango wa usimamizi wa misitu kutoka; kutolewa kwa mizinga ya nyuki 1,264 kwa vikundi vya uzalishaji mali katika wilaya ya katika wilaya zote za mradi; kukamilika kwa ukarabati wa tuta lenye urefu wa meta 850 na kujenga *spill ways* mbili na kurabati *spill way* moja katika shehia ya Ukele, Micheweni, Pemba kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari yasiingie kwenye mashamba ya mpunga; kufanyika kwa ziara za mafunzo kwa ajili ya kujifunza kilimo hifadhi na kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabia nchi kwa wakulima 292 kutoka katika wilaya tano za mradi; kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali na ubora wa ardhi (biophysical assessment) kwa kutumia *Land Degradation Surveillance Framework* (LDSF) katika maeneo ya mradi; na kuendelea na zoezi la ufuatiliaji wa kaboni kwa kutumia Ex-Ante Carbon-balance Tool (EX-ACT) katika maeno ya mradi. Jumla ya shilingi milioni 652.99 zimetumika hadi Januari 2022.

**(iv) Mradi wa majaribio wa Kikanda wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria (Adapting to Climate Change in Lake Victoria Basin):**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uchimbaji wa visima viwili katika kitongoji cha Mbiti vyenye urefu wa mita 110 na mita 80; kukamilika kwa uchimbaji wa kisima kimoja (1) katika kitongoji cha Busalanga chenye urefu mita 100 na ukarabati wa kisima kimoja (1) katika kitongoji cha Sekouture chenye urefu wa mita 64; kununuliwa na kutundikwa kwa mizinga ya nyuki 149 katika kitongoji cha Bugando na Busalanga; kukamilika kwa uwekaji wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye baadhi ya majengo ya shule ya Sekondari Ng'haya, upandaji wa miti zaidi 400; na kuandaliwa kwa maandiko 14 ya miradi midogo ya jamii ya kuhimili mabadiliko ya tabia nchi na kuongeza kipato cha jamii katika maeneo ya ufugaji wa kondoo, kilimo cha bustani, kilimo cha matunda, ufugaji kuku, kuongeza thamani mazao yatokanayo na ufugaji nyuki na kuyawasilisha UNEP ili kupata ufadhili. Jumla ya shilingi milioni 287.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(v) Mradi wa Kupunguza Hewa Ukaa inayosababishwa na Ukataji na Uharibifu wa Misitu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa mapitio ya utekelezaji wa mradi kati ya Serikali na Ubalozi wa Norway; na kufanyika kwa vikao vitatu (3) vya utambulisho wa mradi kwa timu ya uratibu, maandalizi na kamati ya wataalamu. Jumla ya shilingi milioni 64.6 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

**(i) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa vikundi 15 vya wavuvi kuhusu uvuvi endelevu; kutolewa kwa mafunzo kwa wakulima 50 kuhusu upandaji miti kibiashara; kutolewa kwa mafunzo kwa wachimbaji wadogo 150 kuhusu uchimbaji endelevu wa madini; kuwezesha vikundi 10 vya wakulima kufanya ziara za mafunzo kuhusu kilimo endelevu; kuandaliwa kwa programu za uelimishaji jamii kuhusu usimamizi endelevu wa Bonde la Ziwa Nyasa; kujengwa kwa majiko banifu 96 ya kupikia katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga majiko (63) na Nyasa (33); na kutolewa kwa elimu ya hifadhi ya mazingira kwa wananchi wanaoishi katika eneo la Bonde la Ziwa.

Aidha, kwa upande wa halmashauri za wilaya tano (5) za Kyela, Ludewa, Makete, Nyasa na Mbinga hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo kwa vikundi 15 vya wakulima na wadau mbalimbali kuhusu matumizi bora ya ardhi; kukamilika kwa tathmini ya kubaini shughuli mbadala za kuongeza kipato cha kaya; kutolewa kwa mafunzo ya uzalishaji wa mkaa mbadala na matumizi ya majiko banifu na usimamizi endelevu wa vyanzo vya maji; kutolewa kwa mafunzo kwa vikundi 15 vya wanawake na 15 vya vijana kuhusu uwekezaji mdogo wa kilimo biashara; kutolewa kwa mafunzo ya usimamizi shirikishi wa misitu kwa wakulima 325; kutolewa kwa mafunzo ya shamba darasa kwa wakulima 50 kwa ajili ya kilimo biashara; na kufanyika kwa tathmini na utambuzi wa jamii zinazotumia maji katika halmashauri za Wilaya ya Mbinga na Nyasa zinazoishi maeneo ya karibu na Mto Luhekei ambapo jumla ya vijiji 26 vilifanyiwa tathmini (Mbinga Vijiji 16) na Nyasa (vijiji 10).

**(ii) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo ya Ikolojia, Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai Tanzania**

Hatua iliyofikiwa ni: Kusainiwa kwa Mkataba wa Mashirikiano ya utekelezaji wa mradi " Project Cooperation Agreement" kati ya Serikali na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *"United Nations Environmental Programme – UNEP";* kukamilisha uanzishwaji wa Ofisi ya uratibu wa Mradi ikujumuisha Mshauri Mkuu wa Mradi (Chief Technical Advisor), Mratibu wa Mradi, Afisa Ufuatiliaji na Tathmini na Afisa Usimamizi wa Fedha na Afisa manunuzi; kuanzishwa kwa kamati mbalimbali za mradi katika ngazi ya kitaifa na Halmashauri ambazo ni pamoja na Kamati ya Kitaalamu ya Ushauri, Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mradi na Kamati saba (7) za Utekelezaji wa Mradi za Halmashauri; kutolewa kwa mafunzo kwa wataalamu 35 kutoka halmashauri saba (7) zinazotekeleza mradi huu kuhusu Ukusanyaji wa Taarifa za Tathmini ya Fursa na Mikakati ya Urejeshaji wa Mifumo-ikolojia (Resource and Opportunity Assessment Methodology -ROAM); kukamilisha maandalizi ya nyaraka muhimu na kutangaza tenda ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Jamii na Mazingira (Environmental and Social Safeguard Assessment). Jumla ya shilingi milioni 511.2 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukusanywa kwa sampuli za mafuta yaliyopo kwenye transfoma yenye kemikali aina ya PCB katika vituo vya kupozea umeme vya Same, Mlandizi, Chalinze, Mwanza, Mbeya, Mufindi, Bukoba, Tabora na Musoma; kukamilika kwa rasimu ya Kanuni za Usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu (POPs); na kutolewa kwa elimu juu ya madhara yatokanayo na kemikali aina ya PCB katika Mikoa na Wilaya za Mwanza, Mbeya, Tabora, Same, Mlandizi, Chalinze, Mufindi, Bukoba na Musoma na Kupitia, kutoa maoni na kuwasilisha African Institute jina na andiko la Mtaalam Elekezi *(Consultant)* ambaye atatekeleza shughuli za mradi hususan kukusanya; kuhifadhi; na kuondosha mafuta yaliyobainika kuwa na kemikali aina ya PCB's na vifaa ambavyo vilitumika kuhifadhia mafuta hayo kwa ajili ya kwenda kuteketezwa. Jumla ya shilingi milioni 25.3 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni**

Hatua iliyofikiwa ni: Kufanyika kwa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni; kufanyika kwa Warsha ya mafunzo kwa maafisa forodha na Mamlaka za Udhibiti kuhusu utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozone; kufanyika kwa warsha ya kukuza uelewa kwa Wataalam wa Mazingira wa Mikoa yote nchini na Wataalam kutoka Mamlaka za Usimamizi wa Sheria kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Montreal; kuendelea na maandalizi ya Kanzidata ya masuala mbalimbali yanayohusina na ozoni (National Ozone Unit Database) na Kufanya kikao cha kupitia rasimu ya marekebisho ya kanuni za usimamizi wa kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni za mwaka 2007. Jumla ya shilingi milioni 77.4 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

Shughuli zilizotekelezwa ni: Kuandaliwa kwa hadidu za rejea nne (4) kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; kuandaliwa kwa mfumo mtandao wa utoaji wa vibali vya Tathmini ya Kimkakati wa Mazingira; kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka; na kuandaliwa kwa mpango-kazi wa Usimamizi wa Mazingira wa jiji la Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 641.9 zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.5.7 Usimamizi wa Maafa Nchini

Hatua iliyofikiwa ni: Kuandaa Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa ya Mwaka 2022; kuzijengea uwezo Kamati saba (7) za Usimamizi wa Maafa na kuwajengea uwezo waratibu wa maafa wa mikoa; kuratibu vikao vya Kamati ya Mawaziri na Kamati ya Makatibu Wakuu zinazoshughulika na udhibiti wa UVIKO – 19; maandalizi ya Mpango wa Dharura wa Kukabiliana na Ukame; kuratibu hatua za kumaliza tatizo la mafuriko katika Kata ya Nkuhungu; kutoa elimu kwa umma kuhusu usimamizi wa maafa kupitia vipindi sita (6) vya luninga na viwili (2) vya redio; kuratibu shughuli za Kimataifa na Kikanda za usimamizi wa maafa; kuandaa Mikakati na Mipango ya aina nne (4) kwa ajili ya kutoa

mwongozo na vipaumbele vya usimamizi wa maafa nchini; kuongeza vifaa vya huduma za kibinadamu katika maghala manne (4) ikiwemo magodoro 1,500, mablanketi 5,000 na mabegi maalumu ya kulalia 2,000; kufanyika kwa kikao kimoja (1) cha Baraza la Usimamizi wa Maafa Tanzania; kufanyika kwa kikao kimoja cha Jukwaa la Taifa la Wadau wa Usimamizi wa Maafa. Jumla ya shillingi milioni 98.49 fedha za ndani zimetumika hadi Januari 2022.

### 3.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu

#### 3.3.6.1 Ujuzi na Uwezeshaji

**(a) Mradi Na. 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa mafunzo ya ujenzi wa vitalu nyumba (Green House) kwa ijana 720 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani, Tabora na Singida; kuendelea na mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kwa njia ya Uanagenzi kwa vijana 14,440; kutolewa kwa mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa Wahitimu 2,215 wa elimu ya juu na ya kati kupitia waajiri wa sekta binafsi na umma; na kupatiwa mafunzo ya kurasimisha ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kwa Watanzania 2,644 ambapo kati yao 2,537 wamefaulu na kupata vyeti vya VETA. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi 43,000,000 kwa vikundi 4 katika Mikoa ya Dar es Salaam (Maniaspaa ya Kinondoni na Kigamboni), Geita (Halmashauri ya Wilaya ya Geita) na Katavi (Halmashauri ya Mlele); Kutolewa mafunzo ya ujuzi tepe na mikopo kwa vijana 1,000 kupitia vikundi 100; na kuendelea na mandaalizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Mfuko. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 zimetumika hadi Januari 2022.

**(c) Mradi Na. 6205: Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha**

Hatua iliyofikiwa ni: Kutolewa kwa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa vijana 286 wakiwemo Wenye Ulemavu, wanaoishi na VVU, Mama Wadogo na vijana kutoka Jamii ya Wafugaji katika Halmashauri za Sengerema - Mwanza, Missenyi - Kagera na Kiteto - Manyara; kusajiliwa kwa vikundi 48 vya vijana wazalishaji mali katika katika Halmashauri za Sengerema, Missenyi na Kiteto ambapo, vikundi 37 vimepatiwa mitaji anzishi katika Wilaya za Misenyi na Sengerema; kutolewa kwa mafunzo ya stadi za maisha kwa waelimishaji rika 120 katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Halmashauri ya Mji Handeni na Halmashauri ya Lushoto Mkoani Tanga; kutambua na kuendeleza bunifu 15 za vijana na Watu wenye Ulemavu; kutolewa kwa mtaji wa vitendea kazi kwa vijana 690 waliohitimu katika fani mbalimbali; kutolewa kwa mafunzo kwa vitendo kwa vijana 100 Wenye Ulemavu waliosomea fani ya ualimu; na kuendelea na mapitio ya Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha. Jumla ya shilingi milioni 802.03 zimetumika hadi Januari 2022.

#### 3.3.7 Maeneo Mengine Yaliyopewa Kipaumbele

##### 3.3.7.1 Utamaduni, Sanaa na Michezo

**(a) Mradi Na. 6504: Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi**
Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mshauri Elekezi (Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi) atakayesimamia ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Geita; na kusainiwa na kuidhinishwa kwa mkataba wa Mshauri Elekezi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**(b) Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania**
Hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Ofisi za muda za Mfuko katika jengo la Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dar es Salaam; kuzinduliwa kwa Bodi ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania pamoja na Sekretariati ya uendeshaji wa Mfuko; na kuandaliwa kwa taratibu za kuendesha Mfuko ikiwemo Mwongozo wa uendeshaji na Katiba ya Mfuko.

**(c) Mradi Na. 6385 – Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa maandalizi ya eneo la ujenzi wa hosteli (bweni) pamoja na nyaraka za kitaalamu (*structural drawings* na *architectual drawings*); kununuliwa kwa vifaa vya ujenzi na kukamilika kwa ujenzi wa msingi na nguzo (*beam*) za ghorofa la hosteli.

Aidha, shughuli nyingine zilizotekelezwa ni: Utambuzi wa eneo la ujenzi wa Kituo cha Kukuza Vipaji (*Centre of Sports Exellence*) katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya pamoja na uhakiki wa mipaka yote ya eneo kwa ajili ya urasimishwaji wa eneo hilo; kurekebishwa ramani ya eneo husika na kukamilika kwa zabuni ya ujenzi wa kituo hicho. Jumla ya shilingi milioni 300 zimetumika hadi Januari 2022.

**(d) Mradi Na. 6523: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam**
Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa marekebisho ya mifumo ya umeme ikijumuisha uunganishaji wa kangavuke (Generator) kubwa kuingia katika mfumo wa umeme wa TANESCO; kuendelea na ukarabati wa uwanja wa ndani (indoor stadium) na chumba cha mazoezi (Gym); kununuliwa kwa vifaa vya *gym* na samani kwa ajili ya matumizi ya ofisi, kumbi na ofisi za viongozi; na kupaka rangi katika maeneo ya uwanja wa ndani, *call room, gym* na *corridor*. Jumla ya shilingi milioni 447 zimetumika hadi Januari 2022.

**(e) Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**
Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi wa Afrika kwa ajili ya kuanzisha Kituo cha Kitaifa na Makumbusho ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; Kufanyika utafiti wa kukusanya taarifa za maeneo 15 yenye historia ya Ukombozi pamoja na kufanya mahojiano na mashuhuda tisa (9) wa Harakati za Ukombozi wa Afrika; kufanyika kwa utambuzi na ukusanyaji wa nyaraka za picha na magazeti yenye taarifa za harakati za ukombozi wa Afrika; na kufanyika kwa maonesho

ya historia ya Ukombozi wa Afrika. Jumla ya shilingi milioni 340 zimetumika hadi Januari 2022.

**(f) Mradi Na. 4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa)**

Hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ukarabati wa madarasa ya zamani, ofisi, ukumbi wa Mwembeni, maktaba, jengo la TEHAMA, jengo la muziki na Ofisi ya Utawala na Sanaa ya Uchoraji (Fine Arts); na kununuliwa kwa vifaa mbalimbali vya kujifunzia na kufundishia (Picha Jongefu na Teknologia ya Sauti). Jumla shilingi milioni 250 zimetumika hadi hadi Januari 2022.

**(g) Mradi Na. 6260: Mfumo wa Leseni na Usajili wa Hakimiliki**

Hatua iliyofikiwa ni: kusanifu mfumo wa usajili wa wabunifu na kazi za wasanii; utoaji wa uthibitisho wa umiliki wa kazi (copyright Clearance); uwekaji wa miundombinu na mifumo ya mawasiliano ya TEHAMA na kuunganisha na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Jumla shilingi milioni 340 zimetumika hadi Januari 2022.

**3.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

**(a) Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini**

Hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa ukarabati wa majengo matano (5) katika ubalozi wa Tanzania, Lusaka (Zambia); kukamilika kwa ukarabati wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden); kuendelea na ukarabati wa Makazi ya Balozi na nyumba ya Mkuu wa Utawala Ubalozi wa Tanzania Stockholm (Sweden); kuendelea na ukarabati wa majengo matatu (3) ya Ubalozi wa Tanzania Kampala (Uganda); kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi na Makazi ya Balozi wa Tanzania Brussels (Ubelgiji); kuendelea na ukarabati wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi Ubalozi wa Tanzania Khartoum (Sudan); na kukamilika kwa usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania, Nairobi (Kenya), jengo la ofisi na kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania, Kinshasa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), jengo la ofisi na kitega uchumi katika Ubalozi wa Tanzania, Moroni (Comoro); jengo la ofisi na makazi ya balozi katika Ubalozi wa Tanzania, Muscat (Oman) na majengo kwenye viwanja vya Serikali vilivyopo Kigali (Rwanda), Maputo (Msumbiji), Bujumbura (Burundi) na Lilongwe (Malawi).

Shughuli nyingine zilizofanyika ni: usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa jengo la zamani katika Ubalozi wa Tanzania, Washington D.C (Marekani); usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya balozi na watumishi katika Ubalozi wa Tanzania, Harare (Zimbabwe); na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania, Kigali (Rwanda). Jumla ya shilingi bilioni 4.7 zimetumika hadi Januari 2022.

**(b) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

**Upanuzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia**

Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa msingi wa vyumba vya mihadhara tisa (9) katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini Dar es Salaam.

### 3.3.7.3 Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

Katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya shilingi bilioni 637.66 zilikusanywa kama Mapato yasiyo ya Kodi kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma ikiwa ni punguzo la asilimia 15.42 ikilinganishwa na shilingi bilioni 753.95 mwaka 2019/20. Kupungua kwa mapato hayo kumetokana na kuathirika kwa makusanyo ya Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyopo kwenye sekta za Utalii, Uchukuzi na Biashara za Kimataifa sababu ya Mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO-19. Aidha, Shilingi Bilioni 223.56 zimekusanywa kama Mapato yasiyo ya Kodi kutoka kwenye Taasisi na Mashirika ya Umma hadi kufikia robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/22. Vile vile, uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kutoka shilingi trilioni 64.45 mwaka wa fedha 2019/20 hadi kufikia shilingi trilioni 67.06 mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 4.

### 3.3.7.4 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya PPP ni:

(a) Kuendelea na taratibu za ununuzi wa mbia wa miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa chini ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya;

(b) Kuendelea na hatua za mwisho za ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu kwenye mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza;

(c) Kuendelea na ununuzi wa Mbia wa miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Jengo la Biashara *"Commercial Complex"* katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

(d) Kuendelea na ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi (Mwanza) chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

(e) Kuanza hatua ya kuandaa upembuzi yakinifu wa mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara baada ya kumpata Mshauri Elekezi;

(f) Kuendelea na taratibu za ununuzi wa Mshauri Elekezi atakayetayarisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi wa ujenzi wa reli ya standard gauge ya Tanga – Arusha – Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu kwa utaratibu wa PPP;

(g) Kuendelea na ununuzi wa Mshauri Elekezi atakayetayarisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi wa ujenzi wa reli ya standard gauge ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa utaratibu wa PPP;

(h) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam;

(i) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Tanzania Kampasi ya Dar es Salaam na Mbeya;

(j) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa Mradi wa Kituo cha Tiba ya Ugonjwa wa Saratani chini ya Taasisi ya Tiba ya Ocean Road - (Mloganzila); na
(k) Kuendelea na upembuzi yakinifu wa Mradi wa Kusimika Boya la Kuegeshea meli za mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Tanga.

## 3.4 Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

### 3.4.1 Ufuatiliaji wa Miradi katika kipindi cha Mwaka 2021/22

Katika mwaka 2021/22, Wizara ya Fedha na Mipango iliendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22. Miradi iliyofuatiliwa inajumuisha miradi yote ya maendeleo iliyogharamiwa kwa fedha za Serikali na Sekta Binafsi.

Hadi kufikia Desemba 2021, jumla ya miradi 105 ilifuatiliwa katika sekta za kukuza uchumi, huduma za jamii na utawala bora, uwajibikaji na utoaji haki. Kwa upande wa sekta za kukuza uchumi, miradi iliyofuatiliwa ni ya viwanda, biashara, maliasili na utalii, ujenzi, uchukuzi, kilimo, mifugo, uvuvi, madini na nishati. Aidha, sekta za Huduma ya Jamii zilizofuatiliwa ni afya, elimu, maji na ardhi. Kwa upande wa utawala bora, uwajibikaji na utoaji haki, sekta zilizofuatiliwa ni sheria, mambo ya ndani, habari na mawasiliano, utawala na utumishi. Miradi yote iliyofuatiliwa inatekelezwa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Aidha, katika kipindi hicho ulifanyika ufuatiliaji maalumu wa ujenzi wa vyumba vya madarasa vilivyojengwa kwa kutumia fedha zilizotolewa na IMF za Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (Tanzania Covid Relief Plan - TCRP). Orodha ya miradi iliyofuatiliwa imeainishwa katika ***Kiambatisho I*.**

### 3.4.2 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2021/22

(i) Kuchelewa kukamilika kwa miradi kutokana na changamoto zinazotokana na ugonjwa wa UVIKO-19 uliopelekea kutokufika kwa wakati kwa wataalamu na vifaa mbalimbali kutoka nje ya nchi;
(ii) Kutoandaliwa kwa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi;
(iii) Upungufu wa rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalamu wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa;
(iv) Rasilimali fedha kutotosheleza mahitaji halisi ya utekelezaji wa Mpango;
(v) Mmomonyoko wa wigo wa kodi kutokana na biashara nyingi kufanyika kwa njia ya mtandao;
(vi) Baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kukwepa kodi, hususan kupitia njia za magendo, kutokutoa stakabadhi za kielektroniki (EFD receipt) wakati wa mauzo na uhamishaji wa faida (transfer pricing) kwa kampuni zenye mtandao wa kimataifa; na
(vii) Upungufu wa vifaa vya ujenzi nchini ikiwemo saruji na nondo uliosababishwa na uzalishaji wa viwanda vya ndani kutokidhi ongezeko la mahitaji ya vifaa vya ujenzi kufuatia Serikali kutumia vifaa vinanvyoazlishwa nchini katika miradi yake.

### 3.4.3 Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto

(i) Kuchukua hatua za kisera na kiutawala ili kuendelea kupambana na athari za UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na kuendelea kutumia malighafi, vifaa na wataalamu wa ndani kwa maeneo yote ambayo hakuna ulazima wa huduma hizo kutoka nje ya nchi;

(ii) Kuendelea kujenga uwezo wa Mafungu ili kuyawezesha kuandaa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP ili ijumuishwe katika Mpango;

(iii) Kuendelea kuajiri wahandisi na wataalamu watakaosimamia utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo;

(iv) Kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya ndani, kubuni vyanzo vipya vya mapato na kutafuta masoko ya bidhaa nje ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia Mpango na Bajeti. Aidha, Serikali inaendelea na kufuatilia mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwa Taasisi mbalimbali ili kuweza kutekeleza miradi ya kipaumbele;

(v) Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi pamoja na kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki; na

(vi) Kuhamasisha viwanda vya vya ndani kuongeza uzalishaji wa vifaa vya ujenzi ili kukidhi mahitaji ya soko yaliyoongezeka.

# SURA YA NNE

# MIRADI YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2022/23

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa ufupi miradi ya kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23. Miradi hiyo inazingatia Mpango Kazi wa kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26 ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya maendeleo 2025.

## 4.2 Misingi ya Mpango na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

### 4.2.1 Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

(i) Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.0 mwaka 2021, kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2022 na kuendelea kukua kwa wastani wa asilimia 5.4 ifikapo mwaka 2024;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 16.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2022/23 na 2023/24;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.5 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23 kutoka matarajio ya asilimia 11.2 mwaka 2021/22;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(vi) Kuhakikisha kuwa viashiria vya ustawi wa jamii vinaimarika.

### 4.2.2 Misingi *(Assumptions)* ya Mpango kwa Mwaka 2022/23

Misingi itakayozingatiwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo;

(ii) Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili kama vile ukame, vita na magonjwa ya mlipuko;

(iii) Kuwepo kwa athari ndogo za kiuchumi zinazotokana na vita ya Urusi na Ukraine;

(iv) Kuendelea kuwa na utoshelevu wa chakula nchini; na

(v) Uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na katika nchi jirani.

## 4.3 Miradi ya Kipaumbele kwa Mwaka 2022/23

### 4.3.1 Miradi ya Kielelezo

**(a) Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa reli ya Standard Gauge kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa

kipande cha Morogoro - Makutupora (km 422); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Makutopora – Tabora (km 368); kuanza ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Tabora - Isaka (Km 165); kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa na mitambo kwa ajili ya matengezo ya njia wakati itakapoanza kufanya kazi; kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli kwa sehemu za Tabora - Kigoma (km 411), Kaliua – Mpanda - Karema (km 320), Uvinza – Musongati – Gitega (km 282), na Isaka - Rusumo (km 371); kugharamia uendeshaji wa reli ya *Standard Gauge*; na kuendelea kugharamia mafunzo ya wataalamu wa uendeshaji na usimamizi wa treni ya *Standard Gauge*. Jumla ya shilingi bilioni 1,263 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa bwawa (main dam); ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels); ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (Power House); ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard); na ujenzi wa nyumba za makazi na ofisi. Jumla ya shilingi bilioni 1,365 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege tano (5) mpya ambapo ndege moja (1) ni aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner*, ndege mbili (2) aina ya *Boeing 737-9*, ndege moja (1) ya mizigo aina ya *Boeing 767-300F* na ndege moja (1) aina ya Dash 8 Q400; kuendelea na ukarabati wa karakana za matengenezo ya ndege (Hangar) za JNIA na KIMAFA (KIA); kugharamia mahitaji ya awali ya uendeshaji wa ndege tano (5) ambazo ni boeing 787 – 8, Boeing 737- 9 mbili (2), Boeing 767 - 300F na Dash 8 Q400 (1); kununua vifaa vya kuhudumia ndege na abiria viwanjani; ukarabati wa jengo la ATCL makao makuu na kiwanja cha ndege cha JNIA Terminal I; kuendelea na ukarabati wa nyumba 38 zilizopo Kilimanjaro, kuendelea kulipa madeni ya Shirika na kujenga majengo ya kuhifadhia mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Songwe. Jumla ya shilingi bilioni 562.88 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuratibu ujenzi wa mradi pamoja na uwekezaji mwingine; na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa mradi na fursa zilizopo. Jumla ya shilingi bilioni 465.96 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kulipia gharama za hisa za serikali (asilimia 15) katika ushiriki na umiliki wa mradi.

**(e) Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha majadiliano ya kimkataba (Host Government Agreement negotiations) na wawekezaji; na kukamilisha mapitio ya mikataba ya ugawanaji mapato (Production Sharing Agreements – PSAs). Aidha, mshauri elekezi ataendelea kuzijengea uwezo wa masuala ya kiufundi, kifedha, kiuchumi, kisheria na kimkataba Timu ya Majadiliano ya Serikali (GNT) na Kamati Kuu ya Usimamizi na

Uongozi wa Mradi (Steering Committee) ili kufanikisha majadiliano kati ya serikali na wawekezaji katika mradi wa LNG. Jumla ya shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi wa Magadi Soda Engaruka**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kuendelea na hatua za kutafuta mwekezaji wa mradi; kuanza ujenzi wa miundombinu muhimu hususan ya barabara ili kuwezesha kufika kwa urahisi katika eneo la mradi; kulipa leseni za uchimbaji; na kufanya uratibu na usimamizi. Jumla ya shilingi bilioni 15.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na majadiliano na Mwekezaji na kukamilisha masuala ya kimkataba; kuendelea na taratibu za ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; ukaguzi na ufuatiliaji wa hali ya vitalu; kulipa leseni za vitalu vya makaa ya mawe; na usimamizi na ulinzi wa eneo. Jumla ya shilingi bilioni 12.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 3165: Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) – Njombe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha uhuishaji wa upembuzi yakinifu; kuweka mipaka ya njia ya umeme*;* kukamilisha usanifu wa mradi (Conceptual Design)*;* kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kujenga miundombinu wezeshi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 45.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.6 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 3167: Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222) - Njombe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha uhuishaji wa upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi (Conceptual Design); kuweka mipaka ya njia ya umeme; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 10.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.0 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4015: Daraja la JPM - Kigongo – Busisi (Mwanza)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara unganishi (km 1.66). Jumla ya shilingi bilioni 20.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 4191: Daraja Jipya la Selander - Tanzanite (Dar es Salaam)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja jipya na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa km 5.2. Jumla ya shilingi milioni 55.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.9 fedha za nje zimetengwa.

**(l) Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha matayarisho ya shamba na kupanda miwa katika eneo lililobaki lenye ukubwa wa hekta 845 ili kukamilisha hekta 3,600 zinazotakiwa kulimwa; kuweka mfumo wa umwagiliaji katika shamba lenye ukubwa wa hekta 845;

ujenzi wa bwawa la umwagiliaji lenye ukubwa wa mita za ujazo 2,500; kukamilisha ujenzi wa kiwanda kipya cha sukari; na ununuzi wa vifaa vya kupakia na kusafirisha miwa kwenda kiwandani. Jumla ya shilingi bilioni 85.64 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 3115: Uendelezaji wa Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia**

**Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Vitalu vya Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi – Wembere**

**Eyasi – Wembere:** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuchakata na kutafsiri taarifa za mfumo wa 2D umbali wa kilomita 260; kuandaa moduli ya mfumo wa 3D kwa kutumia taarifa za kijiofizikia; na kukusanya taarifa na kufanya tathmini ya kijiokemia juu ya uwepo wa viashiria vya miamba inayozalisha mafuta (hydrocarbon seep detection). Jumla ya shilingi bilioni 3.1 fedha za ndani zimetengwa.

**Mnazi Bay Kaskazini:** Shughuli zitakazotekelezwa ni: kutafsiri taarifa za kijiolojia; kusanifu na kuandaa mpango wa kina wa uchorongaji wa kisima cha utafutaji na kisima cha uhakiki; na kuanza uchorongaji wa visima vya utafutaji na uhakiki. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

**Mradi Na. 4920: Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa na kukamilisha nyaraka za kisheria kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa na timu ya majadiliano ya Serikali pamoja na uamuzi wa serikali; kuendelea na zoezi la kuweka mipaka na kukamilisha taratibu zote za umilikishaji ardhi katika eneo lililolipiwa fidia; na kuendelea na tafiti, ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji uliofanywa katika eneo hilo. Jumla ya shilingi bilioni 7.8 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.2 Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi

#### 4.3.2.1 Kuimarisha Mazingira Wezeshi ya Uwekezaji

##### 4.3.2.1.1 Uendelezaji wa Miundombinu na Huduma

**A. Reli**

**(a) Mradi Na. 4216: Ukarabati wa Njia Kuu za Reli**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ukarabati wa njia ya reli kwa maeneo yaliyobaki kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Isaka (km 970); kuboresha vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka; na kufanya stadi kwa ajili ya ukarabati wa njia za reli kwa maeneo ya Kilosa - Gulwe, Tabora - Kigoma, Isaka - Mwanza na Tanga – Moshi - Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 175.68 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ukarabati wa njia ya reli iliyopo; kufufua njia za reli zilizofungwa; kukarabati mabehewa; kununua vichwa vya treni na mabehewa; kuboresha mfumo wa ishara na mawasiliano katika njia ya reli iliyopo; kuboresha mfumo wa TEHAMA; kukarabati karakana, majengo na stesheni; kupima na kuweka alama katika maeneo ya reli ili kuzuia uvamizi wa maeneo; na kukamilisha stadi mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli. Jumla ya shilingi bilioni 835.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Uboreshaji wa Reli ya TAZARA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kununua mataruma 20,000 ya mbao kwa ajili ya kuwekwa katika maeneo ya madaraja; malipo ya awali ya ununuzi wa mashine ya kushindilia kokoto; kununua mitambo kwa ajili ya kiwanda cha kokoto - Kongolo; kulipa malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa *excavators* mbili (2); na kufanya ukarabati wa mabehewa 14 kwa ajili ya treni ya jiji la Dar es Salaam na mabehewa 7 kwa ajili treni ya Udzungwa. Jumla ya shilingi bilioni 12.5 fedha za ndani zimetengwa.

**B. Barabara na Madaraja**

**Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi**

**(a) Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499*)***

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.0) na kuanza ujenzi wa barabara za Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396.0), Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50) na Dakawa Jct – Mbigiri (km 7.00). Jumla ya shilingi bilioni 23.46 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4113: Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke – Kibena (km 220)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya Kihansi – Mlimba – Taweta – Madeke – Kibena (km 220) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Aidha, mradi huu utahusisha kuanza ujenzi wa barabara za Ifakara – Kihansi (km 50) na Kibena – Lupembe – Madeke (km 130) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 15.56 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.65 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4148: Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (km 365.36)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8), Kasinde – Mpanda (km 111.7) na Tabora – Sikonge (km 30). Jumla ya shilingi milioni 40.00 fedha za ndani na shilingi milioni 8,869.42 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na.4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Makutano – Sanzate (km 50.0) na Waso – Sale Jct (km 49.0), kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40.0) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara za Natta – Mugumu (km 35.0) na Tarime – Mugumu (km 86.0). Jumla ya shilingi bilioni 20.08 zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4130: Barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora (km 259.75)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Nyahua – Chaya (km 85.4) na Tabora – Nyahua (km 85). Jumla ya shilingi milioni 30.00 fedha za ndani na shilingi bilioni 1.0 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50) kwa kiwango cha zege; na kuanza ujenzi wa barabara ya Itoni – Lusitu (km 50) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 14.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4193: Handeni – Kibaya – Singida (Km 460)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Handeni – Kiberashi (km 50.0), Arusha – Kibaya – Kongwa na maandalizi ya ujenzi wa Sabasaba – Sepuka – Ndago - Kizaga kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4195: Barabara ya Dodoma – Iringa (km 273.3)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass - km 7.3) kwa kiwango cha lami; na kuendelea kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma. Jumla ya shilingi milioni 8.96 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4196: Barabara ya Dodoma – Babati (km 243.8)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35) na Mela – Bonga (km 88.80); na kuendelea na usanifu wa kina wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass - km 15.5) pamoja na Maporomoko ya Magara (Magara Escarpment) (km 3.00). Jumla ya shilingi bilioni 2.53 fedha za ndani zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni (Mkiwa) Road (km 528)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa madai ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mbeya – Lwanjilo (km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 39); kuanza ujenzi wa barabara za Noranga – Itigi - Mkiwa (km 56.9), Mbalizi – Makongolosi (km 56), Makongolosi – Rungwa – Noranga: sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50) na ujenzi wa barabara za Mji wa Itigi kwa kiwango cha

lami za Jumla ya shilingi milioni 12.72 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 4112: Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 36); kuendelea na ujenzi wa barabara ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Makandarasi wa barabara ya Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56) na Urambo – Kaliua (km 28). Jumla ya shilingi bilioni 3.14 fedha za ndani na shilingi bilioni 17.52 fedha za nje zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 4002: Barabara ya Mtwara – Newala - Masasi (km 210)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara ya Mnivata – Tandahimba - Masasi (km 160); na kulipa madai ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi, sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 23.46 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 4003: Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

Shughuli itakayotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 10) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 4107: Barabara za Kuelekea kwenye Mradi wa Kufua Umeme wa Maji katika Mto Rufiji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78), kipande cha Bigwa – Matombo (km 40) kwa kiwango cha lami; ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Striggler’s Gorge; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178), sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4). Jumla ya shilingi bilioni 10.73 fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (Km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2). Jumla ya shilingi bilioni 10.73 fedha za ndani zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4004: Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)**

Jumla ya shilingi milioni 880.00 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mhandisi Mshauri aliyefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130).

**(q) Mradi Na. 4005: Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Ubena Zomozi –

Ngerengere Jeshini – Ngerengere SGR Station (km 19.00), Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10.00), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3.00), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2.00), Igandu – Igandu SGR Station (km 27.00), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.50), Kizota – Zuzu SGR Station (km 14.00), Bahi – Bahi SGR Station (km 4.00), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22.00) na barabara za ndani ya kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station ) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 33.54 zimetengwa.

**(r) Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45.0); na barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100), sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.20) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 15. 80 fedha za ndani zimetengwa.

**(s) Mradi Na. 4197: Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) na daraja la Mnywamaji; na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi washauri wa ujenzi wa barabara ya Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66). Jumla ya Shilingi bilioni 9.04 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.0 fedha za nje zimetengwa.

**(t) Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani (km 50) kwa kiwango cha lami; na kuanza ujenzi wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami pamoja na daraja la Pangani. Shilingi bilioni 7.92 fedha za ndani na shilingi bilioni 35.05 fedha za nje zimetengwa.

**(u) Mradi Na. 4152: Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110) kwa kiwango cha lami; kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65) kwa kiwango cha lami na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi kwa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1). Jumla ya shilingi bilioni 1.78 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 4186: Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni - Mafinga (km 234.8)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152), Mafinga – Mgololo (km 78) na Nyololo – Mtwango); kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa, sehemu za Tumbaku Jctn – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi; na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ukarabati wa sehemu za Mafinga – Nyigo (km 74.1) na Nyigo – Igawa (km 63.8). Jumla ya shilingi bilioni 14.61 fedha za ndani zimetegwa.

**(w) Mradi Na. 4199: Barabara ya Igawa – Songwe –Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (Mbeya Bypass) (km 273.5)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ukarabati wa barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) na ujenzi wa mchepuo wa Mbeya (Uyole – Songwe - km 49); na kukamilisha usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa barabara ya Iwambi – Mbalizi (km 6.5) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 6.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje, kipande cha Njombe – Moronga (km 53.9), . Njombe – Makete – Isyonje, kipande cha Njombe – Moronga (km 53.9 na kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 11.87 fedha za ndani zimetengwa.

**(y) Mradi Na. 4194: Barabara ya Makambako – Songea (Songea Bypass) (km 295)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea na kuanza ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Songea (Songea Bypass). Jumla ya shilingi bilioni 10.98 fedha za ndani zimetengwa.

**(z) Mradi Na. 4123: Barabara ya Dumila – Kilosa (km 141)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi kwa sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24) kwa kiwango cha lami; kuanza ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Dumila – Rudewa (km 45). Jumla ya shilingi bilioni 15.61 fedha za ndani zimetengwa.

**(aa) Mradi Na. 4023: Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha malipo ya fidia na kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(bb) Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga na Barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200) sehemu ya Ntendo – Muze (km 37) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 7.15 fedha za ndani zimetengwa.

**(cc) Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 133), sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60) na Murushaka – Nkwenda – Murongo (km 125), sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1). Jumla ya shilingi bilioni 6.61 fedha za ndani zimetengwa.

**(dd) Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (km 172)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi barabara ya Ipole – Rungwa (km 172) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 5.5 fedha za ndani zimetengwa.

**Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani**

**(a) Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107). Jumla ya shilingi bilioni 3.86 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 84.8)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kwa Sadala – Masama – Machame *Junction* (km 16) na Kiboroloni – Kiraracha – Tsuduni – Kidia (km 10.8); kuanza ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25); kuanza ujenzi wa barabara ya Tarakea – Holili (km 53); na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Sanya Juu – Kamwanga, sehemu za Sanya Juu – Elerai (km 32) na KIA – Mirerani (km 26). Jumla ya shilingi bilioni 17.02 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4129: Barabara ya Isaka - Lusahunga (km 242.2)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi; kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92); na kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110). Jumla ya Shilingi bilioni 2.66 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.19 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4111: Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel – Murugarama (km 141)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi milioni 10.16 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza, sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159), Kibaoni – Sitalike (km 71) na Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.3) na Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112.00) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65) Jumla ya shilingi bilioni 19.81 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4155: Barabara ya Nyanguge – Musoma/Kisesa Bypass (Km 202.25)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4); kuanza maandalizi ya upanuzi wa barabara iendayo Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kuweka taa za barabarani; na kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5) na Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass km 16.35). Jumla ya shilingi milioni 580.00 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4141: Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51). Jumla ya shilingi bilioni 4.96 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4162: Barabara ya Mwigumbi - Maswa - Bariadi - Lamadi (km 121)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mchepuo wa barabara ya Maswa (Maswa Bypass - km 11) na kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula – Magu – Kwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Makandarasi wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na Maswa – Bariadi (km 49.7). Jumla ya shilingi bilioni 3.17 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25**)
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (59.35), Nduta Junction – Kabingo (62.5), na Nduta Junction – Kibondo (25.9); kuanza ujenzi wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 48) kwa kiwango cha lami; na kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kabingo (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 17.79 fedha za ndani na shilingi bilioni 62.33 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4025: Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa daraja katika barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21) na Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.1) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 1.66 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 4103: Barabara ya Geita - Bulyanhulu - Kahama (km 174)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7) na Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54) kwa kiwango cha lami. Jumla ya shilingi bilioni 24.85 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 4138: Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kulipa madai ya Makandarasi wa barabara za Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Mbezi Mwisho – Goba (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7), Ardhi – Makongo – Goba; Sehemu ya Goba – Makongo (km 4), Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Madale – Goba (km 5) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Wazo Hill – Madale (km 6.0).

Aidha, kazi nyingine ni: Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo (km 5.0) na kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4.0), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry Road (One Lane Widening: km 25.1), Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27.0) na Goba – Matosa – Temboni (km 6.0) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1). Jumla ya shilingi bilioni 13.74 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu.

**(m) Mradi Na. 4132: Barabara za Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukarabati km 672.77 kwa kiwango cha changarawe; kujenga kilometa 61.82 kwa kiwango cha lami; na kujenga madaraja 31 katika Mikoa mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 58.69 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 4285: Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka**

**Awamu ya Kwanza**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuboresha miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika awamu ya kwanza katika eneo la Jangwani. Jumla ya shilingi bilioni 5.94 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kazi hizi.

**Awamu ya Pili**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Lot 1 inayohusisha barabara yenye urefu wa km 20.3 (Mbagala - Mzunguko wa Bandari - Bendera Tatu), Bendera Tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Kawawa Road – Morogoro Road (Magomeni), Chang'ombe Road – Kilwa Road) na Lot 2 inayohusisha ujenzi wa majengo (vituo viwili (2), yadi moja (1) na vituo mlisho vinne (4). Jumla ya shilingi milioni 55.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 44.0 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Tatu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu inayohusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi, Uhuru na Nyerere hadi Gongo la Mboto zenye jumla ya km 23.6 na kituo kikuu cha mabasi Kariakoo, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA. Jumla ya shilingi milioni 330.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 13.2 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Nne**

Awamu ya Nne itahusisha barabara za Ali Hassan Mwinyi, Bagamoyo - Tegeta na barabara ya Sam Nujoma (Ubungo - Mwenge) zenye jumla ya km 25.9. Jumla ya shilingi milioni 220.00 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.3 fedha za nje zimetengwa.

**Awamu ya Tano**

Awamu ya Tano itahusisha barabara za Mandela, Kigogo – Tabata na barabara za Mbagala zenye jumla ya km 25.6. Jumla ya shilingi bilioni 2.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Mradi Na. 4161: Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover) Jijini Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct); na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza. Jumla ya shilingi bilioni 1.61 fedha za ndani na shilingi bilioni 5.5 fedha za nje zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4146: Barabara za Mzunguko Katika Jiji la Dodoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa *Dry Port* (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60) na kulipa fidia kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Bahi R/About - Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3); kuanza ujenzi wa barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Junction (km 76.1) kwa kiwango cha lami; kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa barabara za kati za mzunguko wa Jiji la Dodoma: Nanenane (Nzuguni) – Miyuji - Mnadani Sekondari - Mkonze, Ntyuka - Nanenane (Km 47.2); kuanza ujenzi wa barabara ya Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) Road (km 18); na kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 220) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50) na Dodoma – Arusha (km 50). Jumla ya shilingi bilioni 13.06 fedha za ndani na shilingi bilioni 31.9 fedha za nje zimetengwa.

**Barabara za Vijijini na Mijini**

**Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Matengenezo ya kawaida (routine maintenance) km 33,615.68, matengenezo maalumu na sehemu korofi (periodic maintenance and spots) (km 4,516.77) na madaraja 3,350 kwa barabara za kuu na za mikoa zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Aidha, kwa upande wa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) shughuli zitakazotekelezwa ni: matengenezo ya barabara za vijijini na mijini zenye urefu wa km 24,630.42 ambapo km 17.930.24 ni matengenezo ya kawaida,

km 5,876.01 ni matengenezo ya maeneo korofi na km 3,287.22 ni matengenezo ya muda maalum; ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa km 232.47, barabara za changarawe zenye urefu wa km 13,060.73, madaraja madogo 12 na madaraja makubwa yenye urefu wa km 744.16; na ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zenye urefu wa km 80 katika mikoa mitano (5) ya Iringa, Mbeya, Songwe, Ruvuma na Njombe. Jumla ya shilingi bilioni 828.8 fedha za ndani na nje zimetengwa.

**Ujenzi wa Madaraja**

**(a) Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa Madaraja ya Magufuli (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Mara (Mara), Magara (Manyara), Lukuledi (Lindi), Msingi (Singida) na Kiegeya (Morogoro). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara), ujenzi wa barabara unganishi za Daraja la Sibiti (Singida) na ujenzi wa Daraja la Sukuma (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kuanza Usanifu na Ujenzi wa Daraja la Mirumba (Katavi), ujenzi wa Madaraja ya Simiyu (Mwanza), Sanza (Singida), Mkenda (Ruvuma) na Mpiji Chini (Dar es Salaam). Vilevile mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Madaraja ya Mtera (Dodoma), Godegode (Dodoma) na Mitomoni (Ruvuma); kuanza upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) na kununua madaraja ya Dharura (Emergency Mabey Parts). Jumla ya shilingi bilioni 22.61 zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4020: Daraja Jipya la Wami (Pwani)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa daraja na barabara unganishi. Jumla ya shilingi bilioni 4.46 fedha za ndani zimetengwa.

**Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa nyumba 20 za viongozi na nyumba 100 za watumishi Jijini Dodoma; ujenzi wa nyumba za makazi za watumishi katika eneo la Temeke Kota Dar Es Salaam; ujenzi wa nyumba za makazi za watumishi katika eneo la Magomeni Kota; na kuendelea na ukarabati wa nyumba za Viongozi pamoja na watumishi wa umma maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 75.06 fedha za ndani zimetengwa.

**C. Usafiri Majini**

**(a) Meli**

**(i) Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika ziwa Victoria; kujenga meli mpya (Wagon ferry) yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria; kujenga meli mpya (Barge/Cargo ship) ya kubeba shehena ya mizigo katika Ziwa Tanganyika yenye uwezo wa kubeba tani 2,800; ujenzi wa meli mpya

ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo tani 2,700 katika Bahari ya Hindi; kukarabati meli za MV Liemba, MV Umoja, MT. Ukerewe, MT. Nyangumi na MT. Sangara; kufanya ukaguzi wa kina (Comprehansive) kuhusu Meli ya MV Mwongozo katika Ziwa Tanganyika, kujenga matishari mbili (2) zenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja; na kufanya ukarabati wa boti moja (1) ya mwendokasi (Sea Warrios) kwa ajili ya kusaidia kazi za uokozi sambamba na usafirishaji wa watalii wanaotembelea kisiwa cha Gombe yenye uwezo wa kubeba abiria 10 katika Ziwa Tanganyika; na kuendelea na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA katika vituo vya Maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa). Jumla ya shilingi bilioni 274.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua boti moja (1) kwa ajili ya utafutaji na uokoaji; kujenga kituo cha utafutaji na uokoaji; kununua vifaa na vitendea kazi katika ofisi ya utafutaji na uokoaji iliyopo Mwanza; kuwezesha uendeshaji wa ofisi ya utafutaji na uokoaji; ujenzi wa banda la kukaushia samaki kwa ajili ya wanawake wajasiriamali; kuwezesha ushiriki wa mikutano ya kitaifa na kikanda inayohusu usalama majini na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu afya kwa jamii, usalama na mazingira. Jumla ya shilingi bilioni 4.2 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Vivuko**

**(i) Mradi Na. 4125: Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na upanuzi wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni (maegesho na barabara za magari), kufunga mifumo ya tiketi za Kieletroniki kwenye vituo vitano (5) vya (Magogoni – Kigamboni, Kigongo - Busisi, Kisorya - Rugezi, Pangani - Bweni na Ilagala - Kajeje); kujenga na kukarabati maegesho sita (6) ya (Magogoni - Kigamboni, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo, Iramba - Majita, Nyakarilo - Kome na Kasharu - Buganguzi); kujenga miundombinu mipya kwenye vituo vitatu (3) vya Kisorya - Rugezi, Nyakarilo - Kome na Bugolora – Ukara; kujenga maegesho mapya ya vivuko vya Kayenze – Kanyinya na Muleba – Ikuza; na kujenga maegesho mapya manne (4) ya Ijinga - Kahangala (Magu) na Bwiro – Bukondo (Ukerewe) mkoani Mwanza. Jumla ya shilingi bilioni 3.05 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia na Magogoni – Kigamboni. Jumla ya shilingi bilioni 8.88 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 4144: Ukarabati wa Vivuko**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa vivuko vya MV Musoma, MV Mara, MV Ujenzi, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kyanyabasa, MV Tanga, MV Kitunda, MV Kazi, MV Magogoni MV Kilombero II na kukihamishia Malinyi – Mlimba. Jumla ya Shilingi bilioni 16.84 fedha za ndani zimetengwa.

## D. Bandari

### (a) Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam

**(i) Bandari ya Dar es Salaam.**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea kuongeza kina na kupanua lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli (entrance channel and turning basin); kuboresha wa Gati Na. 8 - 11 na Gati Na. 12-15 ; kuendelea na ujenzi wa bandari ya Kwala; kuendelea na ujenzi wa miundombinu saidizi kwa ajili ya uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; kufunga na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya TEHAMA; na kuimarisha miundombinu ya reli kwa ajili ya kusafirisha mizigo kwa njia ya reli. Jumla ya shilingi bilioni 70.249 fedha za ndani na shilingi bilioni 150.078 fedha za nje zimetengwa.

**(ii) Bandari ya Tanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Tanga awamu ya pili (II) kwa kuboresha na kuimarisha Gati Na. 1 - 2; kujenga uzio wa kuzunguka eneo la Bandari ya Chongoleani; kukarabati zahanati ya Bandari; kuimarisha miundombinu ya bandari; kuendeleza eneo la Raskazone na Chongoleani kwa ajili ya kupokea na kuhifadhi mafuta katika Bandari ya Tanga. Jumla ya shilingi bilioni 157.03 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Bandari ya Mtwara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia makasha; ujenzi wa barabara ya gati jipya; kuboresha sehemu ya majahazi shangani (Shangani Dhow Wharf) kwa kufanya ukarabati wa ghala, ofisi, barabara na sehemu ya maegesho; kuendelea na ujenzi wa uzio kwa ajili ya kuimarisha usalama katika eneo la Bandari ya Kilwa Masoko na Bandari ya Mtwara; kuendelea na ujenzi wa minara ya taa katika Bandari za Lindi na Kilwa Masoko; kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa awali wa kihandisi, usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya uendelezaji wa eneo jipya la kuhifadhi mafuta na matanki; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya uendelezaji wa Bandari za Kilwa, Rushungi, Lindi na Kisiwa Mgao katika Bahari ya Hindi. Jumla ya shilingi bilioni 27.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Bandari ya Ziwa Victoria**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na maboresho na upanuzi wa miundombinu ikiwemo ujenzi wa Bandari za Bukoba na Kemondo; kuboresha bandari ya Mwanza Kaskazini na kukamilisha usanifu wa kina katika bandari za Mwanza Kusini, Nansio na Musoma; na kuendelea na ununuzi wa vifaa katika bandari hizo. Jumla ya shilingi bilioni 20.61 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Bandari ya Ziwa Tanganyika**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa gati katika Bandari za Kibirizi na Ujiji; kukamilisha ujenzi wa Gati la Kasanga na Lagosa; kukamilisha ujenzi wa bandari mpya ya Karema; na kuanza usanifu wa kina katika kitengo cha abiria katika Bandari ya

Kigoma. Jumla ya shilingi bilioni 24.229 fedha za ndani na shilingi bilioni 13.00 fedha za nje zimetengwa.

**(vi) Bandari ya Ziwa Nyasa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya Bandari za Kiwira, Itungi, Matema, Mbambabay, Manda na Liuli katika Ziwa Nyasa; na kukamilisha ujenzi wa Gati katika Bandari ya Ndumbi. Jumla ya shilingi bilioni 2.68 fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Ununuzi wa Mitambo**

Shughuli itakayotekelezwa ni ununuzi wa mitambo, vyombo na vifaa mbalimbali ikiwemo *"tug boats",* winchi na magari ambapo jumla ya shilingi bilioni 148.419 zimetengwa.

**E. Usafiri wa Anga**

**(a) Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha ujenzi na upanuzi wa maegesho ya ndege pamoja na ujenzi wa jengo jipya la abiria. Jumla ya shilingi bilioni 6.96 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4220: Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio na maegesho ya ndege; kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege; ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari; na ujenzi wa uzio wa usalama. Jumla ya shilingi bilioni 6.49 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga jengo la abiria na ukarabati wa miundombinu ikiwemo maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani; kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege; kujenga uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Jumla ya shilingi bilioni 6.05 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.3 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari; kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege na kulipa fidia kwa waathirika wa maeneo yatakayotwaliwa. Jumla ya shilingi bilioni 1.7 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.3 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa

hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari; kufunga taa na mitambo ya kuongozea ndege; na ujenzi wa uzio wa usalama. Jumla ya shilingi milioni 650.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.3 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Songwe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria na mifumo ya ulinzi; kufunga taa za kuongozea ndege; kukarabati tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio; na kujenga uzio wa uwanja. Jumla ya shilingi bilioni 11.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Geita, Iringa, Ruvuma (Songea), Simiyu, *Lake* Manyara, Tanga, Moshi na Mara (Musoma); kujenga uzio wa usalama na barabara ya ukaguzi katika kiwanja cha ndege cha Dodoma; kujenga barabara ya kuruka na kutua ndege kwa kiwango cha lami katika kiwanja cha ndege cha Nachingwea; na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Manyara. Jumla ya shilingi bilioni 31.58 fedha za ndani na shilingi milioni 544.5 fedha za nje zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Msalato**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha Ndege cha Msalato Jijini Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 5.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 20.37 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 4158: Kiwanja cha Ndege Mpanda**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa jengo la abiria. Jumla ya shilingi milioni 12.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 4159: Kiwanja cha Ndege Tabora**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa uwanja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa. Jumla ya shilingi milioni 662.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.34 fedha za nje zimetengwa.

**(k) Kiwanja cha Ndege cha Lindi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni ukarabati na upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, ujenzi wa maegesho ya ndege na magari, ujenzi wa jengo la abiria, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, ujenzi wa jengo la abiria, ujenzi wa jengo pamoja na kufunga taa na mitambo ya kuongozea, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa na kituo cha kuzalisha umeme wa dharura (Power House). Jumla ya shilingi bilioni 2.62 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 4210: Kiwanja cha Ndege Arusha**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kujenga uzio wa usalama na kufanya maandalizi ya ujenzi

wa jengo la abiria. Jumla ya shilingi milioni 242.02 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na.6267 : *Institutional Support***

**(i) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA-TB III) na Kuboresha Huduma katika Viwanja Vingine vya Ndege**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na uendeshaji na uwekaji wa miundombinu katika jengo la tatu la abiria (JNIA TB III) unaohusisha matengenezo (preventive maintanance) ya mitambo na mifumo mbalimbali (switchgears 33 kV, lift 14, eskaleta saba (7), travelators mbili (2) za abiria, mashine 20 za ukaguzi wa abiria na mizigo, mifumo ya tiketi za abiria na mifumo ya TEHAMA); kufunga taa za kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Arusha; kukarabati taa za kuongozea ndege katika viwanja vya ndege vya Mwanza na Dodoma; kukarabati jengo na miundombinu ya jengo la kwanza la abiria (JNIA TB I); ufungaji wa mifumo ya kuhudumia abiria katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Arusha, Songwe, Bukoba na Dodoma; ununuzi wa magari ya zimamoto katika viwanja vya ndege vya JNIA (2), Dodoma (1) na Arusha (1); kuhuisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Manyara na kulipa fidia katika maeneo ya viwanja vya ndege vya JNIA (Kipunguni), Nachingwea, Kilwa masoko na Simiyu; na kununua *Scanner* kwa ajili ya uwanja wa ndege wa KIA. Jumla ya shilingi bilioni 117.78 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Kuboresha Mawasiliano katika Viwanja vya Ndege**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya rubani na waongoza ndege (VHF Area Cover Radios) katika viwanja vya Dar es salaam, Arusha, Tanga, Seronera, Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Kigoma, Mtwara, Songea, Gairo, Songwe, Mbeya, Iringa na Tabora; kuwajengea uwezo wataalamu wa kutumia mfumo mpya wa mawasiliano kati ya rubani na waongoza Ndege; maandalizi ya awali ya ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Usafiri wa Anga; kununua na kufunga vifaa vya kuongozea ndege (flight calibration) katika viwanja vya Ndege vya JNIA, AAKIA, KIA, Mwanza, Tabora, Songwe, Dodoma na Pemba; na kukarabati jengo la TCAA makao makuu - Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 7.43 bilioni fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Ununuzi wa Rada**

**Mradi Na. 4290: Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa**

Sughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha malipo ya ununuzi wa rada mbili (2) zitakazofungwa katika viwanja vya ndege vya KIA na Dodoma; kununua rada sita (6) kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa taarifa ya hali ya hewa katika Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi; kuendelea na ujenzi wa maabara ya hali ya hewa na ufungaji wa mifumo husika; kuendelea na ujenzi wa ofisi ya hali ya hewa katika kanda ya mashariki; kufunga vifaa saidizi katika vituo vya hali ya hewa; na kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala na hosteli katika Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa. Jumla ya shilingi bilioni 31.5 ya fedha za ndani zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4309: Mradi wa Afrika Mashariki wa Ujuzi wa Mabadiliko na Ujumuishaji wa Kikanda (EASTRIP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo (Mabibo) – Dar es Salaam; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kuhusu taaluma za usafiri wa anga; kujenga uwezo kwa watumishi kupitia ziara za kitaaluma, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya vitendo na kubadilishana wakufunzi na vyuo vya nje ya nchi; na kuandaa na kuboresha mitaala ya mafunzo inayokidhi mahitaji ya soko la kimataifa kwenye taaluma za usafiri wa anga. Jumla ya shilingi bilioni 6.2 fedha za nje zimetengwa.

**(q) Mradi Na.6377 Ujenzi wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia**

**(i) Chuo cha Taifa cha Usafirishaji – NIT**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kununua ndege moja (1) ya kufundishia marubani; kuwezesha uendeshaji wa vifaa vya kufundishia; kulipa fidia ya ardhi katika eneo la Kitelela - Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kufundishia watalaamu wa reli; kujenga kampasi kwa ajili ya kufundisha watalaamu wa bahari na mafuta/gesi katika Mkoa wa Lindi; na kukamilisha ujenzi wa jengo la maktaba - NIT Mabibo. Jumla ya shilingi bilioni 24.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Chuo cha Bahari Dar es Salaam - DMI**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) kwa ajili ya madarasa, ofisi za utawala, maabara na maktaba; na kununua vifaa vya kufundishia ikiwemo *crane simulator na live radar*. Jumla ya shilingi bilioni 10.9 fedha za ndani zimetengwa.

**F. Nishati**

**Miradi ya Kufua Umeme**

**(i) Mradi Na. 3164: Kinyerezi I *Extension* (MW 185)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme; na kufunga mitambo ya kuzalisha umeme. Jumla ya shilingi bilioni 88.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 3169: Kufua Umeme wa Maji Rusumo (MW 80)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa bwawa na kituo cha kufua umeme. Jumla ya shilingi bilioni 3.85 fedha za nje zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 3168: Kufua Umeme wa Maji Kikonge (MW 300)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha upembuzi yakinifu; kufanya tathmini ya athari kwa mazingira na jamii, uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi na ulipaji wa fidia; kukamilisha usanifu wa mradi; na ununuzi wa Mtaalamu Mshauri wa kusimamia mradi na mkandarasi. Jumla ya shilingi bilioni 1.04 fedha za nje zimetengwa.

**Miradi ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme**

**(i) Mradi Na. 3179: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi**.

**Kinyerezi - Chalinze kV 400:** Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na utekelezaji wa mradi na kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya shilingi bilioni 40.0 fedha za ndani zimetengwa.

**Rufiji - Chalinze - Dodoma kV 400:** Shughuli zitakazotekelezwa ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 180.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 – North – West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi)**

**Awamu ya Kwanza: Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga:** Shughuli zitakazotekelezwa ni ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha tathmini ya athari kwa mazingira; ununuzi wa Mtaalamu Mshauri wa kusimamia ujenzi wa mradi na mkandarasi; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vinne (4) vya kupoza umeme vya Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**Awamu ya Pili: Kigoma – Nyakanazi:** Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa mradi na kuanza usambazaji wa umeme katika vijiji vinavyopitiwa na mradi. Jumla ya shilingi bilioni 13.77 fedha za nje zimetengwa.

**(iii) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220, Geita – Nyakanazi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi, kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kusambaza umeme katika vijiji/mitaa 32 vitakavyopitiwa na mradi. Jumla ya shilingi bilioni 20.3 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 220 (Rusumo – Nyakanazi)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rusumo hadi Nyakanazi. Jumla ya shilingi bilioni 32.7 fedha za nje zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme vya Singida, Arusha na Manyara; na kusambaza umeme katika vijiji vitakavyopitiwa na mradi. Jumla ya shilingi bilioni 10.2 fedha za nje zimetengwa.

**(vi) Mradi Na. 3113: Usambazaji wa Umeme Vijijini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza

umeme vijijini kupitia mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya III Mzunguko wa II unaohusisha kufikisha umeme katika vijiji vyote vilivyobakia; kuendelea kutekeleza miradi ya kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji; kuendelea kuteleza miradi ya kusambaza umeme kwenye vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati (Densifiction); kuendelea kuunganisha wateja na ufungaji wa mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa. Jumla ya shilingi bilioni 363.11 fedha za ndani na shilingi bilioni 63.76 fedha za nje zimetengwa.

**(vii) Uimarishaji wa Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization)**
Serikali kupitia TANESCO na REA imefanya tathmini ya ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini na kubainisha miradi mbalimbali itakayohusisha ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme 57 kwa ajili ya kuimarisha gridi ya Taifa, kununua na kufunga mashine umba (transformer) 114, kununua na kufunga nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa kwenye gridi ya Taifa zenye urefu wa kilomita 3,698 ili kuweza kuhudumia idadi kubwa ya wateja inayoongezeka. Gharama za miradi hii kwa pamoja ni dola za Marekani bilioni 1.9 sawa na takriban shilingi trilioni 4.4. Miradi hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu. Katika mwaka 2022/23, shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga vituo vipya vya kupoza umeme kwa ajili ya kuimarisha gridi ya Taifa; kununua na kufunga mashine umba (Transformer); na kununua na kufunga nyaya zenye uwezo wa kusafirisha umeme mkubwa kwenye gridi ya Taifa. Jumla ya shilingi bilioni 400.0 fedha za ndani zimetengwa.

**Miradi ya Gesi Asilia na Mafuta**

**(i) Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)**
Shughuli itakayotekelezwa ni ununuzi wa Mtaalam Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu wa mradi pamoja na kufanya tathmini ya athari za mazingira na Jamii. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 3162: Usambazaji wa Gesi Asilia kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani**

**Dar es Salaam na Pwani**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia katika jiji la Dar es Salaam; na kuanza ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Tegeta hadi Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 51.53 fedha za ndani zimetengwa.

**Mtwara na Lindi**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuunganisha gesi asilia katika nyumba 500 katika mkoa wa Mtwara; kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia yenye urefu wa kilomita 10 kutoka BVS-3 hadi Mnazi Mmoja pamoja na kujenga miundombinu; na kujenga miundombinu ya usambazaji gesi asilia majumbani yenye urefu wa kilomita 16.2 itakayounganisha nyumba 200 za awali eneo la Mnazi Mmoja katika Mkoa wa Lindi.

Jumla ya shilingi bilioni 10.74 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.2.2 Mapinduzi ya TEHAMA

**(i) Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na upanuzi wa mkongo wa taifa km 2,884 za njia kuu ya mkongo wa taifa (Backbone Infrastructure), ujenzi wa km 6,294 za mkongo wa kuunganisha wilaya 83 (Regional Networks) na ujenzi wa km 160 za mkongo wa majini kuunganisha mkongo wa taifa wa mawasiliano na nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kupitia Ziwa Tanganyika; ujenzi wa miundombinu ya uunganishaji wa mkongo kwa watumiaji wa mwisho (lastmile connectivity) kwenye halmashauri 10 nchini kwa kuunganisha vituo vya afya, ofisi za Serikali na shule; kuhuisha na kuboresha miundombinu iliyopo; usanifu wa mfumo wa taarifa za miundombinu ya TEHAMA nchini utakaounganisha mifumo yote ya Serikali ili kurahisisha utumaji wa *data* na taarifa kutoka mfumo mmoja kwenda mwingine; ujenzi wa miundombinu muhimu ya kudhibiti mawasiliano ya mitandao; kuhuisha sheria za masuala ya usalama wa mitandao; na kuandaa mwongozo wa kitaifa wa bunifu za kidigitali. Jumla ya shilingi bilioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 4234: Anuani za Makazi na Postikodi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga uelewa kwa viongozi na watendaji sambamba na kujenga uwezo kwa wataalamu kuanzia ngazi ya Taifa hadi Vijiji/Mitaa katika halmashauri 179 nchini kuhusu mfumo wa anwani za makazi; kuboresha wavuti na programu ikiwa ni pamoja na ununuzi wa *backup servers* mbili (2); na kuboresha sera, sheria, kanuni na miongozo ili kuimarisha utekelezaji na matumizi ya Mfumo wa Anuani za Makazi.

Aidha, shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: kuainisha namba ya kila nyumba/jengo kwa kuandika namba husika sambamba na jina la mtaa/barabara kwenye ukuta/geti katika halmashauri 179; na kukusanya taarifa na kutoa anuani za makazi kwa wananchi katika halmashauri 179 nchini; na ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya kurahisiha utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 83.27 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Kidijitali (Digital Tanzania Institute – DTI) na vituo vya ubunifu vitano (5) vya kikanda; uendelezaji wa mfumo wa anuani za makazi na postikodi; ununuzi wa vifaa kwa ajili ya Mfumo wa Taifa wa Takwimu za TEHAMA; kuboresha na kuendeleza Mfumo wa Kidijitali wa Biashara Mtandao (e-commerce); kupanua na kuongeza uwezo wa mtandao wa mawasiliano wa Serikali (GovNet); kujenga minara ya mawasiliano 150 ili kuboresha upatikanji wa intaneti yenye kasi (broadband) maeneo ya vijijini; ununuzi wa vifaa vya uhifadhi na mtandao ili kuongeza uwezo wa vituo mahiri vya *data*; kufanya ukarabati wa vituo kumi (10) vya Huduma Pamoja; kuwajengea uwezo watumishi wa serikali 150 wa kada ya TEHAMA; na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kitengo cha utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 58.4 za fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 4279: Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufunga mitambo ya masafa ya FM katika wilaya 29; kuimarisha Chaneli ya Tanzania Safari kwa kununua mitambo na vifaa vya uandaaji na utangazaji mahsusi kwa ajili ya vipindi vya utalii; kutoa mafunzo kwa watendaji kuhusu uandaaji bunifu wa vipindi; ununuzi wa mitambo, magari na vifaa kwa ajili ya matangazo mubashara ya redio na televisheni; kukarabati majengo na studio za redio na televisheni makao makuu na ofisi za kanda; kukarabati studio za ukombozi wa Nchi Kusini mwa Afrika katika jengo la utangazaji barabara ya Nyerere; ujenzi wa makao makuu ya TBC jijini Dodoma sambamba na kufunga mifumo ya uhariri, upokeaji wa matangazo kupitia mifumo ya TEHAMA; kuendelea na ufungaji wa mitambo ya redio na TEHAMA katika studio za redio barabara ya Nyerere pamoja na jengo la TBC2 awamu ya pili; na ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kupokea na kuchanganya picha studio na matukio ya nje (Tricaster System, CG & monitoring). Jumla ya shilingi bilioni 52.1 za fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukusanya na kusambaza habari na taarifa kwa wananchi kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Serikali katika mikoa, wilaya na halmashauri zote nchini; kuandaa vibango, video fupi na makala za video na redio zenye kuonesha utekelezaji wa Serikali kwa ajili ya matangazo ya televisheni, redio na mitandao ya kijamii; kuwezesha ununuzi wa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya ukusanyaji, uchakataji na uandaaji wa taarifa vikiwemo kamera na visaidizi vyake, LIVE U na kompyuta; kujenga kituo cha habari (*press centre*) na studio ya kisasa jijini Dodoma; kuanzisha Chaneli ya Televisheni ya Serikali itakayokuwa inaonesha habari za Serikali ikijumuisha shughuli zinazotekelezwa na Wizara, Mikoa, Halmashauri na Taasisi nyingine zilizopo chini ya Serikali; na kuandaa makala maalumu ya utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 11.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na taratibu za ununuzi wa mzabuni wa kutengeneza mitambo ya uchapaji; kuanza ujenzi kiwanda cha uchapaji baada ya kukamilisha michoro (drawings) na makisio ya gharama (bill of quantities); na kupokea na kusimika (installation) mitambo ya uchapaji. Jumla ya shilingi bilioni 29.0 za fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Mradi Na. 6226: Kujenga Kituo Kuu cha Kuendeleza Ubunifu wa TEHAMA na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Sekta ya TEHAMA Nchini**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Uanzishaji wa vituo vya ubunifu na atamizi katika wilaya zote; kukiendeleza kituo cha kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT startups) cha Dar es Salaam (Soft center) na kutenga fedha za mitaji (revolving ICT innovation challenge fund) kwa ajili ya wajasiriamali wa TEHAMA katika vituo vidogo vya kuendeleza sekta ya TEHAMA nchini; ujenzi wa vituo vya kanda vya watengeneza bidhaa za TEHAMA; kuanzisha/kuendeleza program ya mafunzo ya kuendeleza wataalamu wa

TEHAMA waliosajiliwa (Continuing Professional Development - CPD); kutengeneza *Portal* ya wataalamu wa TEHAMA; kujenga kituo cha kitaifa cha kuendeleza wataalam, tafiti zinazotoa fursa za uwekezaji na ubunifu katika sekta ya TEHAMA, vifaa na makao makuu ya Tume ya TEHAMA Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 68.7 fedha za ndani zimetengwa.

**4.3.2.3 Kuimarisha Miundombinu na Mifumo ya Kitaasisi**

**A. Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge**

**(i) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Bunge**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukarabati wa Majengo ya Bunge na Makazi ya Kiongozi wa Bunge; na ununuzi na ufungaji wa viti 118 kwa ajili ya ukumbi wa Bunge. Jumla ya shilingi bilioni 2.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa nyumba mbili (2) za makazi ya viongozi; na ujenzi wa jumba la makumbusho ya Bunge. Jumla ya shilingi bilioni 2.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulijengea uwezo Bunge katika maeneo ya kutunga sheria na usimamizi wa fedha za umma; na kutoa mafunzo kwa Wabunge na Watumishi kwenye masuala ya uchambuzi wa miswada, masuala ya bajeti pamoja na ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge. Jumla ya shilingi milioni 700 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 6216: Kulijengea Bunge Uwezo Awamu ya Pili (LSP II)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi katika maeneo ya usimamizi wa bajeti, utungaji wa sheria na ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika shughuli za Bunge; na kuendelea kuboresha miongozo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za Bunge. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za nje zimetengwa.

**B. Maboresho ya Mahakama**

**(a) Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi Kigoma; kukamilisha ujenzi wa majengo ya Mahakama za wilaya nne (4) za Liwale, Manyoni, Kwimba, Ulanga; na kujenga majengo ya Mahakama za wilaya 17 za Mbulu, Tunduru, Kahama, Kilosa, Nachingwea, Chamwino, Rufiji, Kibiti, Nyasa, Mkalama, Ikungi, Momba, Nkasi, Ubungo, Serengeti, Tarime na Masasi. Jumla ya shilingi bilioni 14.25 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo sita (6) za Newala Mjini (Newala), Kinesi (Rorya), Madale (Dar es Salaam), Luilo (Ludewa), Mahenge (Kilolo), Usevya (Mlele); na kujenga majengo ya Mahakama za Mwanzo 10 katika mikoa mbalimbali. Jumla ya shilingi bilioni 4.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

**Nyumba za Majaji na Mahakimu**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi na ujenzi wa jengo la ghorofa sita kwa ajili ya makazi ya Majaji jijini Dodoma. Jumla ya shilingi billion 20.0 za fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi**

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama Dodoma**
Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania jijini Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 39.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6215: Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Mahakama (Citizen Centic Judiciary Modernisation Project)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 60 katika mikoa yote ya Tanzania Bara na kuendelea na ujenzi wa Vituo Jumuishi tisa (9) katika Mikoa ya Geita, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Njombe, Pwani, Simiyu na Singida. Jumla ya shilingi bilioni 59.0 fedha za nje zimetengwa.

**C. Serikali Kuhamia Dodoma**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba kwa kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu. Jumla ya shilingi bilioni 7.0 fedha za ndani zimetengwa.

**D. Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa cha Serikali**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kupiga chapa cha Serikali eneo la Kisasa; na ununuzi wa mitambo mipya ya uchapaji. Jumla ya shilingi bilioni 2.5 fedha za ndani zimetengwa.

**E. Utawala Bora na Utawala wa Sheria**

**(a) Mradi Na. 5501: Kuimarisha Upatikanaji wa Haki za Binadamu**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mafunzo na uhamasishaji kuhusu upatikanaji wa Haki za Msingi kwa wanawake na watu wenye mahitaji maalum; kukamilisha na kuanza kutekeleza programu ya kuratibu utekelezaji wa Sheria za Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, Sura ya 449 na Sheria ya Mapitio na

Majadiliano Kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri asili na Maliasilia za Nchi, Sura 450 kwa manufaa ya watanzania; kuwezesha mashirika ya kitaifa na Asasi za Kiraia kulinda na kutetea haki za binadamu na haki za wanawake; kuandaa semina za kuongeza uelewa kuhusu uvunjifu wa haki za binadamu, msaada wa kisheria na vita dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia kwa maafisa 45 kutoka taasisi zinazojihusisha na haki za binadamu; kukamilisha na kuanza kutekeleza mpango kazi wa pili wa kitaifa wa kulinda haki za binadamu nchini; na kujenga uwezo wa kusimamia, kuratibu na kutoa taarifa za haki za binadamu na utekelezaji wake. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 5502: Mpango Kazi Endelevu wa Kupambana na Rushwa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa utekelezaji wa programu ya maboresho ya mfumo wa Haki Jinai kwa kufanya mikutano na wadau wa haki jinai; kukamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Mashtaka na mkakati wa utekelezaji; kufanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri, kuandaa Kanuni za Sheria ya kuwalinda mashahidi na watoa taarifa za uhalifu na kufanya marekebisho ya Sheria ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi; kuratibu vikao vya jukwaa la haki jinai kwa ngazi ya Mawaziri; kuratibu vikao vya wadau kuhusu kufanya marekebisho ya Sheria zitakazotokana na Sera ya Taifa ya Mashtaka; kuandaa mfumo wa Kielektroniki wa kupata maoni ya Wadau kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa; na kuandaa kanuni za kufifilisha makosa ya jinai. Jumla ya shilingi milioni 630 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6201: Haki Mtandao**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mafunzo ya mifumo ya utoaji haki pamoja na elimu kwa umma; kujenga mifumo ya ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini; kununua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya mawasiliano ya kielektroniki kwenye taasisi za sheria; na kuandaa mfumo wa kuratibu uoanishaji wa mifumo ya TEHAMA baina ya Wizara na Taasisi za Haki Jinai. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 6207: Kuboresha Uwajibikaji na Kuongeza Upatikanaji wa Haki**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya msaada wa sheria hususan kwa wanawake na watoto na watu wa makundi maalum kwa kufungua madawati ya msaada wa kisheria katika mahakama kwenye mikoa sita (6) ya Arusha, Temeke, Kinondoni, Mwanza, Morogoro na Dodoma; kuwajengea uwezo wa kulinda haki za ardhi na mali kwa wanawake na watoto nchini kwa njia ya kuwafanyia mafunzo ili kutambua haki zao na kufanya uwakilishi wa kisheria kwenye mashauri yanayowahusu wanawake na watoto; kujenga uwezo wa taasisi rasmi na zisizo rasmi ikiwemo kutoa mafunzo kwa Kamati za Mikoa za msaada wa kisheria kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria na kulinda haki za binadamu nchini; kutoa mafunzo mbalimbali kwa watoa huduma ya msaada wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria ya msaada wa kisheria; kuwezesha vikao vya wadau wa sekta ya sheria kujadili kuhusu mwenendo wa utoaji haki nchini; kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za

msaada wa kisheria nchini. Jumla ya shilingi bilioni 1.05 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6517: Kuimarisha Haki za Mtoto**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendeleza programu ya kuandikisha taarifa za vizazi na utoaji wa vyeti kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Dar es Salaam; kuwezesha upatikanaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa watoto katika Chuo cha Uanasheria kwa vitendo Tanzania; na kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Haki ya Mtoto wa mwaka 2020/21-2024/25. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu**

Shughuli itakayotekelezwa ni ujenzi wa ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika mikoa mitatu (3) ya Tabora, Arusha na Mbeya. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka**

Shughuli itakayotekelezwa ni ujenzi wa majengo ya ofisi ya Taifa ya mashtaka katika mikoa sita (6) ya Rukwa, Mwanza, Tanga, Dodoma, Shinyanga na Geita. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na usajili na utambuzi wa watu 804,738 katika mikoa na wilaya zote Tanzania Bara na Zanzibar; ununuzi wa kadighafi milioni 10 kwa ajili ya kuzalisha vitambulisho vya Taifa kwa raia wa Tanzania, wageni wakaazi na wakimbizi; kuzalisha na kusambaza vitambulisho milioni 10, ununuzi wa vifaa na mifumo ya kiusalama ya TEHAMA kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi; kuunganisha na kuboresha miundombinu ya mtandao wa mawasiliano kati ya Ofisi za Usajili za Wilaya 10 na Makao Makuu; kuboresha mifumo kumi na moja (11) ya usajili na utambuzi; kuunganisha taasisi za Serikali na binafsi katika Kanzidata ya Mamlaka; ununuzi wa magari sita (6) kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi; na kuanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma pamoja na ofisi 31 za Usajili za Wilaya. Jumla ya shilingi bilioni 74.11 fedha za ndani na shilingi bilioni 6.78 fedha za nje zimetengwa.

**(i) Usalama wa Raia**

**(i) Mradi Na. 6302 - Ujenzi wa Ofisi, Vituo na Nyumba za Makazi Tanzania Bara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa jengo la Kamanda wa Mkoa wa Songwe; ujenzi wa jengo la Kamanda wa Mkoa wa Mtwara; ujenzi wa Jengo la Kamanda wa Mkoa wa Simiyu; ukarabati wa ukumbi wa mikutano - Polisi Jamii Dodoma; kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa ofisi ya TEHAMA depot – Dodoma; kukamilisha ujenzi wa jengo la Maji Makao Makuu ya Polisi Dodoma; kumalizia ujenzi wa jengo la Kituo cha Polisi Daraja "C" Isoko Ileje - Songwe; kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa kituo cha Polisi Daraja A Namtumbo – Songea; na kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Polisi Daraja "A" Mkalama Singida.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Polisi Daraja "A" Ikungi Singida; kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Polisi Daraja "B" Bariadi Simiyu; kuanza kwa ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja "A" Sikonge Tabora; kuanza kwa ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi familia tatu (3) za Askari Buyekera Mkoa wa Kagera; ukarabati wa nyumba 14 za kuishi Maofisa na Askari wa kikosi cha wanamaji Itungi *Port* Mbeya; kuanza kwa ujenzi wa jengo la *Rest House* – Mbeya; ukarabati wa *Rest House* Mkoa wa Shinyanga; na kuanza ujenzi wa majengo mawili (2) ya Ghorofa kwa ajili ya makazi ya kuishi Askari wa Kikosi cha kutuliza ghasia (FFU - Dodoma). Jumla ya shilingi bilioni 20.59 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Mradi Na. 6303 - Ujenzi wa Ofisi, Vituo na Nyumba za Makazi Zanzibar**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa awamu ya pili ya ujenzi wa majengo saba (7) ya familia 14 za Makazi ya Askari Mfikiwa Kusini Pemba Zanzibar; na kuanza kwa awamu ya pili ya ujenzi wa majengo matatu (3) ya Familia 12 za makazi ya askari Finya Kaskazini Pemba Zanzibar. Jumla ya shilingi milioni 550 fedha za ndani zimetengwa.

**(j) Magereza**

**(iii) Mradi Na. 1201 - Uimarishaji wa Viwanda vya Magereza**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa jengo la Kiwanda cha Mawese katika Gereza la Kwitanga (Kigoma) na ununuzi wa mitambo ya uchakataji wa mawese; na ununuzi wa mashine mpya kwa ajili ya uchakataji wa chumvi katika Gereza la Machole (Lindi). Jumla ya shilingi bilioni 4.65 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi Na. 2301: Upimaji wa Maeneo na Ulipaji Fidia**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa upimaji wa maeneo na ulipaji wa fidia katika magereza ya Bukombe, Kyerwa, Liwale, Rorya na Kishapu. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 6308: Ujenzi na Ukarabati wa Magereza Makuu**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa magereza mapya katika wilaya za Kakonko - Kigoma, Kaliua - Tabora, Msalato - Dodoma pamoja na Kilosa na Gairo - Morogoro; na ukarabati wa magereza ya Ruanda (Mbeya), Butimba (Mwanza), Kwitanga (Kigoma), Mbigiri (Morogoro), Ukonga (Dar es Salaam), Njombe, Kitete (Tabora), Isanga (Dodoma), Isupilo (Iringa), Nachingwea (Mtwara), Mwanga (Kilimanjaro), Geita (Geita), Kahama (Shinyanga), Nzega (Tabora) na Masasi (Mtwara). Jumla ya shilingi bilioni 43.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi Na. 4428 - Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na maghala ya kuhifadhia mazao ya kilimo katika mashamba ya gereza Kalilankulukulu (Katavi), Kiabakali (Mara) na Ilagala (Kigoma). Jumla ya shilingi bilioni 4.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: ununuzi wa magari matano (5) ya kuzimia moto na mawili (2) ya kubebea wagonjwa (ambulance); ujenzi wa vituo 10 vya zimamoto na uokoaji vya wilaya; ujenzi wa nyumba mbili (2) za walimu na vyumba viwili (2) vya madarasa katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo wilayani Handeni Mkoani Tanga; na ununuzi wa vifaa vya zimamoto na uokoaji. Jumla ya shilingi bilioni 17.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Geita, Lindi na Mtwara; ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Njombe na Katavi; ujenzi wa ofisi za Wilaya za Simanjiro, Mufindi, Rorya, Kyerwa na Mlele; kuendelea na ujenzi wa Kambi ya Mafunzo ya Kichakamiba kwa kujenga *Mess* - 2, bwalo moja (1), Tanki la maji (reservoir tank), nyumba za wakufunzi 10, *Rest house 1*, kuongeza mabweni 6 na uwanja wa paredi; ujenzi wa nyumba za makazi za Makamishna saba (7) na nyumba za makazi ya maafisa na askari 100 mkoani Dodoma; ukarabati wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Mara, Morogoro na Dar es Salaam (Kurasini) pamoja na nyumba za makazi ya maafisa na askari katika mikoa ya Tabora na Pwani; na ununuzi wa nyumba 12 za maafisa na askari katika eneo la Msamala Mkoani Ruvuma. Jumla ya shilingi bilioni 16.81 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuchochea maendeleo ya wananchi kupitia fedha za maendeleo ya Jimbo. Jumla ya shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani zimetengwa.

**F. Utumishi wa Umma**

**(a) Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa**
Shughuli itakayotekelezwa ni kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Jumla ya shilingi bilioni 3 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6284: Programu ya Maboresho ya Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza kwa ujenzi wa Klabu ya Viongozi (Leaders club Dodoma); kuwajengea uwezo watumiaji wa mfumo mpya wa HCMIS katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Serikali na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili waweze kusimamia masuala ya kiutawala na rasilimaliwatu pamoja na kuwa na taarifa sahihi za watumishi katika Taasisi zao kupitia mfumo huo; kukamilisha Mwongozo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini na kuwajengea uwezo watumiaji; kuanza utekelezaji wa mfumo wa e-Malalamiko na e-HRP pamoja na kuwajengea uwezo watumiaji.

Aidha, shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: kuimarisha upatikanaji wa taarifa za viongozi (Kanzidata) ili kubaini viongozi wenye sifa stahiki pamoja na kuwezesha zoezi la

upekuzi, uteuzi na uhamisho wa viongozi; kuratibu uendelezaji wa watumishi wa umma wenye vipaji vya uongozi pamoja na kuwajengea uwezo viongozi waliopo katika usimamizi na utoaji wa maamuzi ya kimkakati; kupitia miundo ya maendeleo ya utumishi ili kuwianisha na kuoanisha viwango vya mishahara kwa lengo la kupunguza tofauti ya mishahara; kuboresha na kuongeza miundombinu na mifumo shirikishi; kuimarisha miundombinu na vifaa vya kiusalama kwa mifumo na taarifa; upanuzi wa miundombinu ya mtandao wa mawasiliano Serikalini ili kufikisha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kuanza utekelezaji wa awali wa mfumo mkuu wa kubadilishana taarifa baina ya mifumo ya Serikali na Taasisi zake. Jumla ya shilingi bilioni 19.03 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6282: Ujenzi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara Serikalini (HCMIS)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuboresha mifumo ya kielektroniki ya utoaji huduma za kiutumishi (HCMIS, e-HRP, PEPMIS[2], e-OPRAS, e- Malalamiko, e-Service Portal); na kutoa usaidizi wa kitaalamu kwenye eneo la TEHAMA. Jumla ya shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.3 Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma

#### 4.3.3.1 Uzalishaji Viwandani

**(a) Mradi Na. 6103: Kuboresha Kituo cha Kuendeleza Teknolojia ya Magari Tanzania - TATC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua mashine na mitambo pamoja na kukarabati mashine, mitambo na majengo kwa ajili ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia; kuanzisha Karakana Kuu ya Kukalibu Chuma (Heavy Duty Foundry); kuanzisha kiwanda cha kuunda magari (Nyumbu Brand) na magari ya kuzima moto (Fire Fighting Vehicles) sita (6) hadi kumi kwa mwaka; kuendeleza wataalamu 45 katika fani za utafiti, ubunifu na utengenezaji wa magari na mitambo; na kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia wa zana na vifaa mbalimbali, magari na mitambo. Jumla ya shilingi bilioni 38.58 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 1214: Kuendeleza Programu ya Maendeleo ya Viwanda - PCP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha nyaraka za Programu ya PCP; kuratibu utekelezaji wa programu ya PCP chini ya UNIDO; kuratibu ujenzi wa Kongano 2 za viwanda katika eneo la viwanda Kigamboni (Pembamnazi) na Kahama - Shinyanga; kufanya tathmini ya kisekta ya mnyororo wa thamani kwa ajili ya ushindani wa viwanda katika chuma na bidhaa za chuma, mbao na bidhaa za mbao na sharubati (juice) za matunda; na kufanya tathmini ya uzalishaji viwandani. Jumla ya shilingi bilioni 4.8 fedha za ndani zimetengwa.

---

[2] Mfumo wa e-OPRAS utafanyiwa maboresho na kubadilishwa jina kuwa Public Employee Performance Management System (PEPMIS) yaani Mfumo wa Kupima Utendaji Kazi wa Mtumishi (katika Utumishi wa Umma)

**(c) Mradi Na. 6260: Miradi ya Kusaidia Taasisi**

**(i) Kiwanda cha Mashine na Vipuri KMTC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa kiwanda kwa kujenga tanuru la kuyeyushia chuma (Foundry), kubadilisha baadhi ya mashine chakavu na kujenga karakana ya kuchomelea vyuma (Fabrication workshop); na kununua malighafi kwa ajili ya kuzalisha mashine na vipuri. Jumla ya shilingi bilioni 7.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta ya URSUS – TAMCO, Kibaha**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha majadiliano kati ya Serikali na mwekezaji kutoka Poland; na kukamilisha ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta. Jumla ya shilingi bilioni 2.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Eneo la Kongano ya Viwanda – TAMCO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa km 3.8, kituo cha kupoozea umeme na mfumo wa maji taka; na kuendelea kuhamasisha wawekezaji. Jumla ya Shilingi bilioni 20.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Mradi wa Mashamba na Viwanda vya Mazao ya Mafuta ya kupikia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ununuzi wa eneo na ukamilishaji wa umiliki wa ardhi kwa ajili ya kilimo cha chikichi na kiwanda. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi wa Makaa ya Mawe Katewaka**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuthamini mali za wananchi watakaopisha mradi; na kulipia leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi milioni 357 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Mradi wa Maganga Matitu *Sponge Iron***

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuthamini mali za wananchi watakaopisha mradi; na kulipia leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi milioni 232 fedha za ndani zimetengwa.

**(vii) Mradi wa Maka ya Mawe Mhukuru**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya upembuzi yakinifu wa kubaini kiwango cha makaa ya mawe; na kulipia leseni za uchimbaji. Jumla ya shilingi milioni 648 fedha za ndani zimetengwa.

**(viii) Mradi wa Kongano za Viwanda za Nyanza, KMTC na Kange**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya usanifu wa miundombinu ya msingi; na kuendelea kutafuta wawekezaji. Jumla ya shilingi milioni 378 zimetengwa.

**(ix) Kuboresha Maktaba**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya ukarabati; kununua vifaa na samani; na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo wa kidijidali. Jumla ya shilingi milioni 346 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi wa Kiwanda cha Viuadudu (TBPL)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya majaribio ya pili ya viwatilifu; kukamilisha usajili na kupata vibali vya uzalishaji pamoja na kufanya majaribio ya mbolea zisizo na kemikali (*Bio-fertilizer)*. Jumla ya shilingi milioni 350 fedha za ndani zimetengwa.

**(xi) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini - CAMARTEC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanzisha kiwanda darasa cha uchakataji wa mafuta ya chikichi na ubanguaji wa korosho wilaya za Kigoma na Manyoni; kuanzisha shamba darasa la matumizi ya zana za kilimo kwenye uzalishaji wa alizeti kwa wakulima wadogo na wakati katika wilaya ya Chemba, mkoa wa Dodoma; kuanzisha kitovu cha teknolojia za kihandisi (Engineering Technology Hubs-ETH) katika wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe; kufanya utafiti wa kubaini mahitaji ya zana za kilimo, mifugo, uvuvi na teknolojia za vijijini kwa wakulima nchini; kutoa mafunzo ya ujasiriamali katika ukaushaji wa dagaa, mbogamboga na matunda, ubanguaji korosho, uundaji wa Mashine za kupura alizeti, matumizi ya matrekta, zana za kilimo na teknolojia za vijijini kwa vijana na wanawake kwa lengo la kukuza ujuzi, ajira na kipato; kujenga ufahamu wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini kwa wadau; kuimarisha shughuli za ukaguzi wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini kwenye maeneo ya mipakani; kujenga maabara ya majaribio ya zana za kilimo; kununua vifaa vya majaribio ya teknolojia za vijijini; kukarabati majengo ya kituo na mashine za karakana; kununua mashine na mitambo ya karakana; kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA; na kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Jumla ya shilingi bilioni 9.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(xii) Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania - TIRDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhawilisha teknolojia ya *hybrid solar-biomass drying steam* kwa wakulima/wasindikaji wadogo na wa kati kupitia maonesho na mafunzo; kuhawilisha teknolojia ya uzalishaji wa *Bio-ethanol* kwa kuzalisha *ethanol* kutokana na taka mbalimbali za kilimo na viwandani zikiwemo mabibo, kokwa za matunda, taka wanga za muhogo, na molasi kwa kutumia mfumo mdogo wa kutakasa (Micro distillery system); kujenga uwezo wa kuchakata zao la mwani ili kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kutokana na mwani na upatikanaji wa masoko; kutoa ushauri na usimamizi wa ujenzi wa viwanda ikiwa ni pamoja na kiwanda cha kusindika ngozi, kiwanda cha mafuta ya chikichi Kigoma, kiwanda cha kukoboa mpunga Mkuyuni Mwanza; kujenga uwezo kwa wachomeleaji na mafundi mchundo kwa kuwafundisha na kuwahakiki ili waweze kushiriki katika mradi wa bomba la mafuta Tanga mpaka Hoima- Uganda; kuendelea na mradi wa uibuaji fursa za uwekezaji na uandaaji wa ramani za viwanda (industrial mapping); kukamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya kemia na mazingira; kufanya tathmini ya viwanda na kuanisha fursa za uwekezaji; kuongeza vigezo vya uhakiki wa maabara ya bidhaa za chakula kutoka vitano (5) hadi 20; na kukamilisha ujenzi wa jengo la utawala. Jumla ya shilingi bilioni 6.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(xiii) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo – TEMDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kubuni na kuendeleza mtambo mkubwa wa kuchakata mkonge ili kupata nyuzi bora (export quality sisal fibres) na kuwezesha ukuaji wa viwanda

na ongezeko la ajira; kubuni na kuendeleza teknolojia ya kutengeneza matofali ya kuzuia joto kali (refractory bricks) kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa; kuendeleza na kuhawilisha teknolojia ya mtambo mdogo wa kuchakata miwa na kutengeneza sukari (sugar processing mini-plant); kusanifu na kuendeleza teknolojia ya kuhifadhi maziwa wakati wa kukusanya na kusafirisha ili yasiharibike mapema (kwa kiwango cha mjasiriamali mdogo, wa kati na mkubwa); ujenzi wa Karakana ya useremala na ununuzi wa mashine za kisasa kwa ajili ya kuendeleza mradi wa vifaa tiba; kuendeleza teknolojia ya kichomea taka (heavy duty biomedical waste incinerator); kuboresha karakana kwa kusimika mashine na vifaa vya kisasa (Heavy duty 6-axes CNC Machines) pamoja na miundombinu; na ujenzi wa karakana Subu na karakana ya kufua vyuma (Foundry and Forging Workshop). Jumla ya Shilingi  billioni 7.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(xiv) Uendelezaji wa Viwanda Vidogo - SIDO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga majengo ya viwanda (industrial buildings) kwa ajili ya viwanda vya kusindika mafuta ya kupikia na nafaka katika mikoa ya Simiyu, Dar es Salaam, Iringa, Tabora, Shinyanga na Dodoma; kuendelea kuimarisha vituo vya Kuendeleza Teknolojia (TDCs) katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro na Vituo vya Mafunzo na Uzalishaji (TPCs) katika mikoa ya Morogoro (Chanzulu) na Kilimanjaro (Usangi) kwa kuweka mitambo ya kisasa ya uzalishaji; na kuendelea kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF). Jumla ya Shilingi billioni 34.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(xv) Kuendeleza Biashara Kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa jengo jipya la Vipimo na Mizani katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na jengo jipya la ukumbi wa mihadhara, madarasa na ofisi katika Kampasi ya Dodoma; kumalizia ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (lecture theatre) katika Kampasi ya Mwanza; kuendelea na ujenzi wa majengo awamu ya pili eneo la Iganzo Kampasi ya Mbeya hatua itakayopelekea kuachana na kutumia majengo ya kukodi; kuanza ujenzi wa majengo Kampasi mpya ya Zanzibar eneo la Chwaka; na kuendeleza rasirimali watu kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu hasa katika ngazi za shahada ya uzamivu (PhD) na shahada ya uzamili (Masters' Degree). Jumla ya Shilingi 6.98 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Maeneo Mengine Maalum ya Uwekezaji (SEZ/EPZ)**

**(i) Mradi Na. 4933: Uendelezaji wa Kanda Maalumu za Kiuchumi**

**Eneo Maalum la Uwekezaji Tanga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupata hati miliki; kuanza maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Kina wa uendelezaji (Master plan/layout plan); na kufanya Tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA).

**Eneo la Maalum la Uwekezaji Kigoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kufanya usanifu wa miundombinu, kuanza ujenzi wa miundombinu ya msingi na kuendelea na programu za uhamasishaji wa kuvutia

wawekezaji.

**Eneo Maalum la Uwekezaji Kahama**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupata hati miliki na kukamilisha ulipwaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na mradi; kuanza maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Kina wa uendelezaji (Master plan/layout plan); kufanya Tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA), usanifu wa miundombinu na hatimaye kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya msingi; na kufanya uhamasishaji kwa ajili ya kuvutia uwekezaji.

**Eneo Maalum la Uwekezaji Bunda**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupata hati miliki; kuanza maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Kina wa uendelezaji (Master plan/layout plan); na kufanya Tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA) na Usanifu wa Kina wa miundombinu ya msingi.

**Eneo Maalum la Uwekezaji Songwe**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kupata hati miliki na kukamilisha ulipwaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na mradi.

**Eneo Maalum la Uwekezaji Manyara**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupata hati miliki; kuanza maandalizi ya Upembuzi Yakinifu na Mpango wa Kina wa uendelezaji (Master plan/layout plan); na kufanya Tathmini ya kimkakati ya mazingira (SEA) na Usanifu wa Kina wa miundombinu ya msingi.

**Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara Free Port Zone**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika eneo la Bandari huru (Free Port Zone) hususani kwa makampuni ya Mafuta na Gesi.

**(e) Mradi Na. 4486: Uzalishaji Viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa kongano la viwanda vya ngozi katika Jiji la Dodoma; kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya masoko ya kimkakati ya mpakani ya Murongo na Kabanga; kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wasindikaji wa bidhaa za kilimo kuhusu ubora,vipimo, matumizi ya taarifa za Mfumo wa Trade Portal na mahitaji ya kufikia soko la ndani na nje ya nchi; kufanya mapitio ya Mikakati ya Sekta ndogo za Pamba, Ngozi, Korosho, Mafuta ya kupikia pamoja na kusimamia na kuendeleza viwanda vya sekta hizo; kufanya tafiti kwenye mazao ya Pamba, Ngozi, Chai, Kahawa, Sukari, Korosho pamoja na viwanda vya vifungashio; kufanya tathmini ya teknolojia katika sekta ya uzalishaji viwandani; na kufanya upembuzi yakinifu ili kuwezesha uanzishwaji wa kongano la mafuta yatokanayo na mbegu za pamba katika Manispaa ya Kahama – Shinyanga; na kufanya tafiti na tathmini ya utekelezaji wa sera ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mchango wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Katika Uchumi wa Viwanda**

**Kilimanjaro International Leather Industries *Co Ltd* (KLICL)**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha ngozi na miundombinu wezeshi ikiwemo maji taka, barabara za ndani na uzio kuzunguka eneo la kiwanda.

**Kiwanda cha Nyama cha Nguru - Morogoro**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha maboresho ya maeneo ya kiwanda pamoja na taratibu za ununuzi wa mifugo na upatikanaji wa vibali vya kusafirisha na kuuza nyama katika soko la ndani na nje ya nchi.

**Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi cha Mamba**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ukarabati wa jengo la utawala na eneo la kupokea tangawizi; na uchimbaji wa kisima ili kuhakikisha upatikanaji wa maji wa uhakika kipindi chote cha mwaka.

**Kiwanda cha Chai cha Mponde – Tanga**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya matengenezo ya kifaa cha kufua mvuke (boiler) na mifumo ya umeme; na ununuzi wa mtambo mpya wa kuchakata chai. Jumla ya shilingi billioni 4 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.3.2 Ubiasharishaji wa Mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia ASDP II

**A. Kilimo**
**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II**

**(a) Kuimarisha miundombinu ya utafiti na kufanya tafiti zitakazozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha uwezo wa vituo vya TARI kwa kuzalisha mbegu tani 862.5 za alizeti kwa mwaka; kufanya utafiti wa zao la chikichi na kuwezesha uzalishaji wa miche milioni 5; kujenga ofisi na nyumba 3 za watumishi kituo cha utafiti Kihinga - Kigoma; ujenzi wa miundombinu na kupanua mashamba kufikia uzalishaji wa tani 2,141.7 za mbegu za ngano (mbegu mama tani 9.4, mbegu za awali tani 163, mbegu za msingi tani 177.9 na mbegu zilizothibitishwa tani 1,791.4); kufanya utafiti wa zao la katani na kuimarisha uzalishaji wa miche milioni 5 ya mkonge; kuimarisha maabara ya udongo ya TARI Mlingano, maabara za *tissue culture* na bayoteknolojia ya TARI Mikocheni; kujenga miundombinu ya umwagiliaji TARI Ifakara kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na utafiti wa zao la Mpunga; kuzalisha na kutafiti mbegu za mazao ya mboga, pareto, minazi, mtama na zabibu; na kuzalisha na kusambaza mbegu za awali kwa mazao ya maharagwe, mahindi na alizeti. Jumla ya shilingi bilioni 20.03 fedha ndani na shilingi bilioni 5.0 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Kuongeza tija kwa kuongeza upatikanaji na usambazaji wa pembejeo**

**(i) Kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuzalisha tani 6,355 za mbegu bora kwa mazao ya kipaumbele (alizeti, ngano, soya, mahindi, mikunde na mbomboga); kuzalisha miche ya michikichi 800,000; kuzalisha mbegu za daraja la kuazimia (Quality Decleared Seeds-QDS) kwa kutumia vikundi vya wakulima wadogo; na kujenga na kukarabati maghala ya kuhifadhia mbegu. Jumla ya shilingi bilioni 10 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Upatikanaji wa mbolea**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukaguzi wa wafanyabiashara 3,340 wa mbolea nchini; kutoa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea kwa maafisa kilimo 30 wa Halmashauri za wilaya; ununuzi wa vifaa vya maabara ya uchunguzi wa ubora wa mbolea; kuanzisha ofisi za kanda (kanda ya kati na Magharibi) na kuimarisha ofisi za Kanda ya ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) na kanda ya Kaskazini (Arusha); kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbolea; kusajili mbolea mpya na visaidizi vyake 80; kusajili maeneo ya biashara mapya 1,000 na kutoa leseni 2,000; kusimamia uingizwaji wa mbolea tani 650,000; na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya taarifa za mbolea. Jumla ya shilingi bilioni 2.3 fedha ndani zimetengwa.

**(iii) Upatikanaji wa Viuatilifu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kununua viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya milipuko; kufanya tafiti za kuainisha maeneo ya mazalia ya visumbufu na kuwaangamiza; kuimarisha usimamizi wa matumizi bora na sahihi ya viuatilifu; kuimarisha upatikanaji wa viuatilifu bora; kuimarisha uchambuzi wa kina wa visumbufu vya kikalantini; kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi za kuhifadhi mazao ya nafaka katika kanda nne (4) zenye uwezo mkubwa wa uzalishaji nafaka; kuhamasisha uhifadhi wa asili wa mazao ya nafaka kwa kutumia mimea dawa; kupima masalia ya sumu katika sampuli 3,000 katika mazao ya kimkakati ili yaendane na sheria za masalia ya sumu za kimataifa na kuwezesha upatikanaji wa masoko nje; kufanya kaguzi ya usafi wa afya ya mimea ili kuzingatia ubora wa mazao wa kikanda na kimataifa; kutoa elimu juu ya usafi wa afya ya mimea katika mazao ya bustani; kutambua na kdhibiti visumbufu katika mazao ya bustani; kukagua viuautilifu 6,600 na kuainisha ubora wa viuatilifu vinavyo ingia inchini na kusajili viuwatilifu 300; kukagua shehena 1,800 za mimea zinazotarajiwa kuingizwa nchini; na kuchambua aina 3,500 za viuatililifu ili kubaini ubora na athari zake kupitia masalia kwenye mazao. Jumla ya shilingi bilioni 14.2 fedha ndani zimetengwa

**(iv) Kuongeza Matumizi ya Teknolojia Bora katika Uzalishaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa zana za kilimo kwa vyama viwili (2) vya ushirika katika mikoa ya Singida na Dodoma ambazo ni matrekta manne (4), mashine nne (4) za kupandia, mashine nne (4) za kunyunyuzia dawa na mashine nne (4) za kuvunia mazao; kuandaa Mkakati wa Zana za Kilimo wa Kitaifa (TAMS) ili kusimamia matumizi bora ya zana za kilimo nchini; kutoa mafunzo kwa wamiliki na waendeshaji mashine za zana za kilimo katika mikoa saba (7); na kutambua na kuendeleza matumizi ya zana za kilimo kwa ajili ya kupanda na kuvuna katika mazao mizizi katika kanda tatu (3). Jumla ya shilingi

bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Kuimarisha huduma za ugani katika sekta ya Kilimo**

**(i) Kuimarisha Vyuo vya Mafunzo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kudahili wanafunzi 2,500 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada; kukarabati miundombinu ya Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo Uyole, KATRIN, Inyala, Ukiriguru, Igurusi, Mtwara, Mlingano na HORTI - Tengeru; kuvipatia vifaa vya kufundishia na usafiri vyuo vya kilimo vya Mlingano, HORTI - Tengeru, Inyala, Maruku, KATC, Mubondo na Mtwara. Jumla ya shilingi bilioni 15.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Huduma za Ugani**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha mafunzo rejea kwa maafisa Ugani 2,000 kuhusu uzalishaji bora wa mazao na mfumo wa M-Kilimo; kuandaa Mpango Kabambe wa Usimamizi wa huduma za Ugani na Kilimo; kuandaa na kusambaza mwongozo wa usimamizi huduma za ugani kwa sekretarieti za mikoa na halmashauri; kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya mfano 2,000, mashamba darasa 4,000 kwa mazao ya kimkakati na kipaumbele; kuwapatia maafisa ugani vitendea kazi ambavyo ni pikipiki 2,000, simu janja 2,000, vifaa vya kupimia afya ya udongo, na visanduku vya ugani 2,000 (Ext. Ki) katika halmashauri 46; kujenga uwezo kwa vituo vya rasilimali kilimo vya kata (WRCs) katika halmashauri 38; na kuimarisha viwanja vya maonesho ya kilimo katika Kanda nane (8). Jumla ya shilingi bilioni 17.1 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Kuimarisha Miundombinu ya Umwagiliaji na Matumizi Bora ya Ardhi**

**(i) Kuimarisha Miundombinu ya Umwagiliaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu sita (6) na mabwawa tisa (9) ambazo ni skimu za Ukwavila (Busekelo); Masimavalafu (Ludewa), Mangola (Karatu), Nindo (Nzega), Maleza (Sumbawanga), Kiru Six (Babati) na mabwawa ya Malagarasi (Uvinza), Kalabe (Bukoba), Simiyu (Magu), Mgungira (Ikungi), Saguti Valley (Bund na Musoma), Kisese (Kondoa), Iyendwe (Momba), Kisegese (Mlimba) na Katuma (Tanganyika); kukamilisha ujenzi na ukarabati wa skimu 14 za Kirya (Mwanga), Endagaw (Hanang'), Usense (Nsimbo), Msufini (Morogoro), Ilemba (Sumbawanga), Mgambalenga (Kilolo), Katunguru (Sengerema), Mahiga (Kwimba), Ikindwa (Nzega), Kasoli (Bariadi), Singiwe na Katuka (Kalambo) Ng'ongo (Sumbawanga) na Idudumo (Nzega); ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya ya Mkombozi hekta 6,000 (Iringa) na Luiche hekta 3,000 (Ujiji - Kigoma); na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu sita (6) ambazo ni Lwanyo (Mbarali), Ibanda (Geita), Msange (Singida), Masimba (Iramba), Udagaji - Mgugwe (Morogoro) na Mwamapuli (Igunga). Jumla ya shilingi bilioni 143.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 51.0 fedha za nje zimetengwa.

**(ii) Matumizi bora ya Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhakiki mashamba 150 yenye hati miliki na ukubwa

kuanzia hekta 20; kushiriki katika utatuzi wa migogoro inayohusu matumizi ya ardhi ya kilimo; kuandaa Mpango Mkakati wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo; kuendelea kutoa elimu kwa maafisa ugani juu ya teknolojia za uhifadhi wa udongo na maji maeneo ya kilimo; kurudisha afya ya udongo katika mashamba 60 yalioathirika na tindikali; kuanzisha kanzi data ya ardhi ya kilimo; kufanya tathmini ya udongo katika mashamba 40 yaliotambuliwa kwa ajili uwekezaji wa kibiashara; kuandaa Mwongozo ili kulinda mabonde yanayozunguka maeneo ya umwagiliaji kwa kuzuia mmomonyoko wa udongo; kutambua maeneo yanayofaa kwa kilimo, kufanya tathmini ya udongo na kuwezesha upatikanaji wa CCRO katika mashamba ya vijana na watu wenye mahitaji maalum. Jumla ya shilingi milioni 571.6 fedha ya ndani zimetengwa.

**(e) Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko ya Mazao ya Kilimo;**

Shughuli zitakazotekelezwa: Kuwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kuboresha soko la mazao ya mahindi, mpunga, alizeti, ngano na maharage; kutoa mafunzo kwa wadau 300 na kuanzisha modeli nne (4) za kuchakata muhogo katika mikoa ya Tanga, Pwani na Lindi; kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo 4,000 kuhusu mazao ya bustani kupitia mfumo wa SHEP; kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 2,000 katika mikoa 26 ya Tanzania Bara kuhusu kilimo biashara na mifumo ya masoko; kuwezesha Bodi za Mazao kuongeza uzalishaji wa mbegu, miche, mazao na upatikanaji wa bei na masoko ya mazao makuu ya biashara ndani na nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 7.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Kuimarisha Kilimo Anga kwa ajili ya Kudhibiti Visumbufu**

Shughuli zitakazotekelezwa: ununuzi wa ndege mbili (2) ili kujenga uwezo wa kituo cha Kilimo Anga ili kudhibiti milipuko ya wadudu; na ununuzi wa viuatilifu vya kudhibiti milipuko ya visumbufu. Jumla ya shilingi bilioni 11.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Kuimarisha Mifumo ya Upatikanaji wa Mitaji katika Sekta ya Kilimo**

Shughuli zitakazotekelezwa: Kamati ya Viongozi kuendelea na mazungumzo ili kupunguza riba ya mikopo kwa wakulima; kuendelea kusimamia utekelezaji wa ukopeshaji wa bilioni 100 toka NMB kwenda katika sekta ya kilimo; kukamilisha mapitio ya sera ya mikopo katika mfuko wa pembejeo; na kukamilisha utafiti utakaobainisha changamoto zinazokwamisha sekta ya fedha zinazozuia kutokopesha wawekezaji katika sekta ya Kilimo.

**(h) Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe**

Shughuli zitakazotekelezwa: Kukarabati ghala 15 katika halmashauri za Songea, Madaba na Njombe; kujenga vihenge vya kisasa 13 vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 97,000; kukarabati vihenge 18 vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 41,850 katika mikoa ya Arusha na Iringa; kukarabati jumla ya ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 59,000 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa na Mwanza; kuhamasisha Taasisi za Serikali na sekta binafsi kujenga ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 300,000; kuimarisha vituo vya kukusanyia mazao ya bustani, nyumba za kuchakatia na kuhifadhi katika maeneo ya uzalishaji, masoko, viwanja vya ndege na bandari ili kupunguza upotevu, kudumisha ubora na

kuboresha usafirishaji wa mazao nje ya nchi. Jumla ya shilingi bilioni 7.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika Huduma za Ugani, Kilimo Biashara na Masoko ya Mazao**

Shughuli zitakazotekelezwa: Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kutoa huduma za ugani na masoko kwa kutumia mfumo wa M-Kilimo na kutoa huduma za biashara ya mazao kwa kutumia mfumo wa *Agriculture Trade Management Information System* (ATMIS); kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 2000 kuhusu kutumia mfumo; kusajili wakulima na wanunuzi 1,375 wa mazao kwenye mfumo; kutoa ushauri kwa wakulima 20,000 juu ya kilimo bora kulingana na maswali waliyouliza kwa kutumia mfumo; kuimarisha mawasiliano ya huduma ya *Internet* inapatikana kwa vituo vyote vya PHS vilivyopo mipakani; na kutoa elimu kwa watumiaji wa mfumo. Jumla ya shilingi milioni 320.0 fedha za ndani zimetengwa.

**Mradi Na. 4499 Kudhibiti Sumukuvu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa ghala 14 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 21,500; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Kibaiolojia – Kibaha; kujenga Kituo Mahili Baada Mavuno (Post Harvest Centre of Excellence) Wilayani Kongwa Mkoani Dodoma; kujenga maabara kuu ya kilimo (Dodoma). Jumla ya shilingi bilioni 41.6 fedha za ndani zimetengwa.

**Mradi Na. 4497 Kuongeza Uhifadhi wa Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi vihenge vya kisasa 56 na maghala nane (8) vyote vikiwa na uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 250,000. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 23 fedha za nje zimetengwa.

**Mradi Na. 4427 Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - AFDP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utafiti ili kugundua aina nne (4) zenye ubora na teknolojia tano (5) zenye ukinzani dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi kwa mazao ya alizeti, mahindi, na maharagwe; kuzalisha tani 53.2 za mbegu za awali na tani 5.6 za mbegu mama za alizeti, mahindi na maharagwe; kuhamasisha matumizi ya teknolojia 10 za kisasa ikiwemo mbegu za kisasa kwa mikoa ya Dodoma, Manyara, Singida, Tabora, Geita na Morogoro; kuchimba visima 2, kununua pampu 2 za maji, na kusimika mitambo ya umwagiliaji; na kuendeleza hekta 25 za mashamaba ya TARI ili kuzalisha mbegu za mahindi, alizeti na maharage.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: kuongeza miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 600 hadi kufikia hekta 850; kufungua mashamba pori hekta 900; kununua mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu; kununua trekta nne (4) na zana zake; kujenga maabara yenye uwezo wa kuchambua kemikali na lishe katika mazao kwenye mikoa ya Morogoro na Mwanza; kukarabati na kununua vifaa vya maabara ya mbegu Arusha; kutoa mafunzo kwa wakaguzi 50 wa mbegu wa Wilaya (Authorized Seed Inspectors); kuimarisha matumizi ya lebo za kielektroniki na ukaguzi ili kudhibiti uuzaji wa mbegu feki; na

majaribio ya kuhakiki ubora wa mbegu zilizoko kwenye uzalishaji (Control Plot Test) katika skimu za mbegu za Shirika la Ushirikiano Maendeleo na Uchumi (OECD) na Shirika la Kupima Ubora wa Mbegu (ISTA). Jumla ya shilingi bilioni 18.9 fedha za nje zimetengwa.

**Kuimarisha Ushirika**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupitia miongozo na kuandaa Mpango Kabambe wa usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika; kutoa mafunzo kwa wakaguzi 437 wa ushirika; kuhamasisha uanzishwaji na usajili wa vyama vya ushirika katika vikundi vidogo vya wakulima 120 wa mazao ya mboga na matunda; kuendeleza kibiashara mashamba 52 yanayomilikiwa na vyama vya ushirika; kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vikubwa vya uongezaji thamani wa mazao yanayozalishwa na wanachama wa vyama vya ushirika; kuunganisha vyama vya ushirika wazalishaji na masoko ya ndani na nje ya nchi; kujenga miundombinu ya masoko ya korosho katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa; kutoa elimu kwa wakulima 5,075 wa korosho kuhusu ubora na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi; kutoa mafunzo kwa wakulima 5,317 kuhusu kilimo bora cha mpunga; na kukabarabati wa ofisi za Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Jumla ya shilingi bilioni 16.1 fedha za ndani zimetengwa.

## B. Mifugo

**Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)**

**(a) Kuimarisha Afya ya Mifugo**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga majosho 2,000 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kununua dawa za kuogesha mifugo lita 17,739; kujenga na kuweka vifaa jengo la uzalishaji chanjo ya FMD; kununua genereta, kuchimba kisima na kuweka vifaa vya kibaiolojia vya kudhibiti maji taka; na kununua magari 6 yenye mfumo baridi ya kusambazia chanjo na kuweka miundombinu ya baridi katika vituo vya kusambazia chanjo. Jumla ya shilingi bilioni 56.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 10.0 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Huduma za Ugani**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua pikipiki 1,978 kwa ajili ya maafisa ugani wa Kata na vituo vya ukusanyaji maduhuli; kununua magari 184 kwa ajili ya huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ufuatiliaji na uratibu wa shughuli za maendeleo ya mifugo; kununua Zana za Uhimilishaji (Artificial Insemination Kit) kwa Maafisa Ugani wa Mifugo katika Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa; kutengeneza Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Mifugo; Utoaji na Usimamizi wa Huduma za Ugani na kununua vifaa vya kimfumo (*computer facilities and accessories*) katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri; kuwezesha upatikanaji wa Vifaa vya kimfumo (computer facilities and accessorires) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuwajengea uwezo wafugaji na wadau wa sekta ya mifugo kuhusu kutumia mfumo wa kielektroniki; na kuimarisha Vituo vya

Mafunzo kwa Wafugaji (FTC) 3 katika maeneo ya Lugoba, ZVC Sumbawanga na ZVC Iringa na kuanzisha Mashamba Darasa (FFS) 830 ya ufugaji. Jumla ya shilingi bilioni 16.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 10 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Huduma za Utafiti**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utafiti wa vimelea *(brucella strain)* ili kuzalisha chanjo sahihi ya ugonjwa wa kutupa mimba katika mazingira ya Tanzania, kuzalisha mbuzi bora wa nyama na maziwa; kuzalisha nguruwe wenye kutoa nyama nyingi; utafiti wa mbari za ng'ombe wa nyama; utafiti wa teknolojia rahisi za uzalishaji wa vyakula vya mifugo; uboreshaji mbari za ng'ombe wa maziwa kulingana na ikolojia za Tanzania; uhifadhi wa rasilimali za kijenetiki za mifugo ya asili (mbuzi, kondoo na ng'ombe) na kufanya utafiti wa malisho; kufanya uchambuzi na uchaguzi wa kuku aina ya Horasi kwa ajili ya nyama na mayai; na kufanya uchambuzi wa vinasaba na muonekano wa punda waliopo Tanzania ili kubaini kosaafu na mbari za punda hao kwa ajili ya kuwatambua na kuwasajili kimataifa ili watumike kikamilifu kibiashara kama wanyama kazi na lishe. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Uboreshaji wa Mbari kwa ajili ya Uzalishaji wa Maziwa na Nyama**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhimilisha ng'ombe 1,000,000 kwa kutumia homoni na kutumia madume bora ya mbegu; kununua magari 37 kwa ajili ya Mikoa na Wizara kuratibu shughuli za maendeleo; kuimarisha miundombinu (nyumba, mazizi na kuondoa vichaka) ya Mashamba 5 ya Serikali ya Kuzalisha Mitamba (LMUs); na kununua ng'ombe wazazi 1,000 kwa ajili ya LMUs. Jumla ya shilingi bilioni 18 fedha za ndani na shilingi bilioni 10.5 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Mifugo na Mazao Yake**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa minada mipya saba (7) ya upili kulingana na michoro mfanano *(Standard Designs)*; kujenga kituo cha Taifa cha ukaguzi na upumzishaji mifugo inayokwenda kuchakatwa kwa ajili ya soko la nje *(National Quaratine Station)* katika eneo la Kwala, mkoa wa Pwani; kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa usajili, ukaguzi, vibali, utoaji leseni na udhibiti wa ubora wa maziwa na bidhaa zake; na kujenga Vituo vitano (5) vya kukusanyia maziwa katika maeneo ya kimkakati. Jumla ya shilingi bilioni 4.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.0 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Kuimarisha Huduma za Maji, Malisho na Vyakula vya Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga malambo 30 ya maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame na mikoa 11 yenye mifugo mingi; kuchimba visima virefu 100 kwa ajili ya mifugo katika maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame; kutenga na kupima maeneo ya kupumzishia mifugo na malisho; kuzalisha mbegu za malisho katika mashamba ya Serikali; na kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uendelezaji wa maeneo ya malisho na kuanzisha mashamba darasa ya malisho. Jumla ya shilingi bilioni 18.0 fedha za ndani na bilioni 10.0 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Kuboresha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga vyumba vipya sita (6) vya mihadhara; kujenga hosteli mpya saba (7); kujenga maabara mpya nane (8); kujenga maktaba mpya nane (8); na kujenga nyumba 120 za watumishi wa LITA; na kununua mabasi 8 katika kampasi 8 za LITA. Jumla ya shilingi bilioni 7.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha uzalishaji wa mifugo bora (ng'ombe wazazi 5,000, mbuzi 1,733, kondoo 1,733, farasi 40 na kuhimilisha ng'ombe 10,000) ili kuongeza biashara ya nyama na maziwa; kujenga na kukarabati miundombinu ya ranchi 8 ili kuongeza uzalishajiwa nyama na maziwa; kununua mitambo, zana na mashine za shambani katika ranchi 8 za NARCO; na kujenga miundombinu ya unenepeshaji katika ranchi nane (8) za NARCO. Jumla ya shilingi bilioni 9.0 fedha za ndani zimetengwa.

**C. Uvuvi**

**(a) Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga soko la samaki Kipumbwi (Pangani); ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari; kununua vifaa vya kuvutia samaki (Fish Aggregate Device – FADs) na kuziweka katika maeneo yaliyotambuliwa; kujenga vichanja 10 vya kuanikia dagaa; kujenga vibanda vinne (4) vya kukaushia mazao ya uvuvi kwa kutumia mionzi ya jua; na kusimika mitambo minne (4) ya umeme ya kukaushia dagaa katika mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara na Geita. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za ndani na shilingi bilioni 10.6 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II)**

**(i) Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania – TAFICO**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu ya TAFICO; kuendelea na ukarabati wa gati la kuegeshea Meli na karakana ya uhandisi wa mitambo ya baharini, kujenga na kuendesha mtambo wa kuzalisha barafu na ghala la ubaridi la kuhifadhia mazao katika eneo la Uvuvi la Ras Mkwavi - Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 5.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(ii) Kuwajengea uwezo wataalamu wa Uvuvi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mafunzo rejea kwa wadau wa uvuvi 25,000; kutoa mafunzo kwa maraghabishi 16 na wavuvi 400 katika mialo minne (4) kuhusu kuzuia upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvunwa; kununua pikipiki 80 kwa ajili ya wataalam wa uvuvi ili kuimarisha huduma ya ugani na kuwawezesha wataalam watano (5) kushiriki mafunzo ya uzamili na uzamivu kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Jumla ya shilingi milioni 920.67 fedha za ndani zimetengwa.

**(iii) Kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa maktaba katika Kampasi ya Gabimori - Mara; ujenzi wa hosteli ya ghorofa tatu (3) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 katika Kampasi ya Nyegezi - Mwanza; kununua magari matatu (3) kwa ajili ya kampasi mpya za Gabimori – Mara, Mikindani - Mtwara na Kibirizi – Kigoma mtawalia; kujenga jengo la zahanati katika Kampasi ya Nyegezi – Mwanza; kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya Kampasi mpya za Gabimori - Mara na Mikindani – Mtwara na kununua vifaa tiba kwa ajili ya zahanati na samani za madarasa. Jumla ya shilingi bilioni 3.8 fedha za ndani zimetengwa.

**(iv) Kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utafiti wa wingi, bioanuwai na mtawanyo wa samaki kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari - EEZ na maji ya ndani ili kuwezesha upatikanaji wa takwimu zitakazosaidia uwekezaji kwenye uchumi wa buluu; kuwezesha kituo cha utafiti cha Mwanza kuwa kitovu cha utafiti wa kuzalisha mbegu bora za samaki na kufanya utafiti wa vyakula bora vya samaki kwa ajili ya kuendeleza ufugaji wa samaki nchini; kununua vifaa vya maabara ya utafiti katika kituo cha TAFIRI Dar es Salaam; kununua magari nane (8) kwa ajili ya utafiti na kuendesha shughuli za utawala na usimamizi; na kununua meli ya utafiti wa baharini inayoweza kufika na kufanya utafiti katika EEZ. Jumla ya shilingi bilioni 22.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Kukabiliana na Vitendo vya Kihalifu katika Maziwa na Bahari Kuu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga miundombinu ya kukaushia samaki; kununua boti ya doria; na kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Kuratibu Mapambano dhidi ya Vitendo vya Kihalifu katika Maziwa na Bahari Kuu. Jumla ya shilingi bilioni 2.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(vi) Kuimarisha Usimamizi na Ulinzi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi**

Shughuli zitakazotelezwa ni: Kujenga vituo saba (7) vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi vya Sengerema, Busega, Mtera, Kasanga, Ikola, Bukoba, Kilwa Kivinje na Kigoma pamoja na kukarabati kituo kimoja (1) cha Mtwara; na ununuzi wa boti 15 za doria zenye injini na injini 15 za kupachika; kuandaa mpango mkakati wa kuimarisha mnyororo wa thamani wa zao la dagaa katika maziwa makuu na bahari nchini; na ununuzi wa magari nane (8) na pikipiki 15 katika vituo vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Jumla ya shilingi bilioni 4.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4702: Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko-Lindi. Jumla ya shilingi bilioni 176.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4486: Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II) na Mradi Na. 4429: Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi - Kujenga na Kukarabati Vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya ukuzaji

viumbe maji vya Kingolwira, Mwamapuli na Rubambagwe; kukamilisha ukarabati na upanuzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Ruhila - Ruvuma, Nyengedi - Lindi na Ruvula - Mtwara; kujenga mashamba darasa 40 katika halmashauri 40; kujenga kituo cha ukuzaji viumbe maji ukanda wa Ziwa Tanganyika; kujenga kituo cha ukuzaji viumbe maji ukanda wa Ziwa Nyasa; na kuanzisha kanda mbili (2) za ukuzaji viumbe maji katika ukanda wa Ziwa Victoria. Jumla ya shilingi bilioni 8.4 fedha za ndani na shilingi bilioni 9.3 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Kujenga na Kuimarisha Miundombinu ya Mazao ya Uvuvi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga soko la samaki Tunduma na mialo mitatu (3) ya kupokelea samaki ya Katonga (Kigoma), Chato *Beach* (Geita) na Mchinga (Lindi). Jumla ya shilingi bilioni 4.6 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.3.3 Uchimbaji wa Madini, Vito vya Thamani na Gesi Asilia

**(a) Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini - SMMRP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuboresha Sheria ya Madini Sura 123 na kanuni zake pamoja na kufanya mapitio ya Sera ya Madini ya Mwaka 2009 ili kukidhi matakwa ya Sheria ya Madini Sura 123; kukamilisha ujenzi wa Jengo la ofisi ya makao makuu ya Tume ya Madini - Dodoma; kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Afisa Madini Mkazi (RMO) Geita; kuendelea kuimarisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini vilivyopo kwa kuviwekea huduma wezeshi na kufungua masoko na vituo vya uuzaji madini hususan ya dhahabu nchini kadri mahitaji yatakavyojitokeza; kuendelea kuboresha mazingira ya kibiashara kwa kuingia mikataba ya ubia kati ya Serikali na wawekezaji; kuwajengea uwezo wa uwekezaji wachimbaji wadogo hasa wanawake wakihamasishwa kwa kuwadhamini na kuwaunganisha na taasisi za kifedha kwa ajili ya mikopo nafuu hususan kupitia STAMICO; kufanya ununuzi wa mashine mbalimbali kwa ajili ya kuboresha kazi za uchorongaji kwa wachimbaji wadogo na mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira – Kabulo; kufanya utafiti kuhusu njia mbalimbali za uongezaji thamani madini; kukijengea uwezo Kituo cha Jimolojia cha Arusha (TGC) kwa kukiongezea miundombinu mbalimbali pamoja na kuongeza udahiri wa wanafunzi kwenye fani za uongezaji thamani madini; na kuendelea kuimarisha udhibiti wa biashara ya madini ya vito. Jumla ya shilingi bilioni 15.0 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.3.4 Huduma

##### 4.3.3.4.1 Maliasili na Utalii

**(a) Mradi Na. 5203: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa kilometa 2,051 za barabara, kilometa 132.5 za njia za utalii wa miguu, majengo 80, madaraja na viwanja vya ndege 14 katika

hifadhi za Taifa Mikumi, Ruaha, Nyerere, Udzungwa na Hifadhi Asili ya Kilombero; kukamilisha ununuzi wa boti za upepo (airboat) mbili (2), magari matatu (3) ya kuoneshea sinema, malori 41, matrekta 8 pamoja na viambata vyake 22; kutangaza utalii kwenye maeneo ya kipaumbele ya mradi katika nyanda za juu kusini; kufanya tafiti zinazohusiana na wanyamapori na kutoa ushauri wa kisera ili kuboresha usimamizi na kuongeza idadi ya watalii; kutambulisha mradi kwa wadau na Mamlaka za Serikali za mikoa miwili (2) na wilaya tatu (3); kutambua vikundi vilivyopo katika vijiji 46 vya mradi; kuteua wawezeshaji jamii katika vijiji 46; kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa wawezeshaji jamii na maafisa watendaji wa vijiji husika; kupanda miti, ujenzi wa malambo 10 ya mifugo, kuimarisha kingo za mto Kioga na Mbarali; kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 10 na ujenzi wa ofisi na mafunzo kwa Jumuiya 10 za Watumia Maji (Water User Association).

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: kutoa mafunzo ya Benki ya Hifadhi za Jamii (*Community Conservation Bank* - COCOBA) kwa vikundi kwenye vijiji 46; kufanya tathmini ya masoko kwenye vijiji 46; kuwezesha ufadhili wa masomo kwa wananchi; kufadhili miradi ya kuzalisha mali; kuboresha miundombinu ya skimu za umwagiliaji na matumizi ya maji na utunzaji wa vyanzo vya maji vya Mto Ruaha Mkuu ili kuwezesha shughuli za kilimo endelevu na utunzaji wa ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha; kuwezesha usimamizi na uratibu wa mradi kwa kufanya tathmini na kuratibu ufuatiliaji wa shughuli za mradi; kuwezesha usimamizi wa fedha, manunuzi, kusimamia usalama wa jamii na mazingira kwenye maeneo ya mradi, mafunzo pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi kwa watekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi milioni 300.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 189.3 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4812: Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuandaa mpango wa kitaifa wa kukusanya rasilimali za kutekeleza Mpango Mkakati wa Kupambana na Ujangili na Biashara haramu ya Nyara; kuwezesha doria za ki-intelijensia na za ushirikiano na nchi jirani na kwenye vikundi 10 vya Kikanda vya kupambana na ujangili (*Tasking and Coordination Groups* – TCG 10); ununuzi wa vifaa vya doria; kuandaa kanzidata kwa ajili ya kutunza taarifa na kumbukumbu mbalimbali za ujangili na biashara haramu ya nyara; kufundisha watumishi wa TCG kuhusu namna ya kutumia kanzidata; kufanya mapitio ya kanuni mbalimbali za matumizi ya wanyamapori; kutoa mafunzo kwa watumishi wanaohudumu katika *National Taskforce Anti-poaching* – NTAP na TCGs; kuandaa mwongozo kwa ajili ya usimamizi wa doria shirikishi; kuwezesha mapitio ya Mpango Mkakati wa Uendelezaji wa Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori; kuwezesha hatua za awali za kuanzisha Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori Chamwino; kuanza kwa utekelezaji wa mbinu mbadala za kupambana na wanyamapori wakali na waharibifu; na kuwajengea uwezo kwa watumishi 250 wanaosimamia utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 2.86 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 4647: Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)**

Shughuli zitakazotelezwa ni: Kujenga uwezo wa usimamizi wa misitu kwa wakulima wadogo wa miti na vikundi vyao, wajasiliamari wadogo na wa kati na vikundi vyao katika vijiji 80 ambapo vijiji 27 vipo katika kongano ya Njombe, vijiji 20 vipo kongano ya Mafinga na vijiji 33 vipo kongano ya Makete; kutoa mafunzo kwa wilaya saba (7) zenye jumla ya vijiji 80 na huduma za ugani, ikiwa ni utekelezaji wa mwongozo wa uanzishaji na utunzaji misitu pamoja na uzalishaji wa mazao ya miti katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya misitu; na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 40 (Train of Trainers) wanaohudumia maeneo ya mradi katika vijiji 80 kwa watoa huduma wa mradi na maafisa wa Serikali; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 18 na kutoa mafunzo kuhusu masuala ya kijinsia, haki za binadamu, usalama kazini, mabadiliko ya tabianchi na kupunguza umasikini ili kuchochea maendeleo endelevu katika sekta. Jumla ya shilingi bilioni 3.36 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4650: Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme – FORVAC)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanzisha hifadhi tano (5) za Nyuki za vijiji katika Kongano ya Tanga (Kilindi, Mpwapwa, Handeni); kufanya majaribio ya modeli ya uzalishaji wa mkaa kwa jamii katika misitu ya vijiji viwili (2) katika Kongani ya Tanga; kuwajengea uwezo wakulima, wajasiriamali na wazalishaji wa mazao ya misitu kuhusu mikataba baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP); ununuzi na usimikaji wa mashine katika viwanda vinne (4) vya kuzalisha mbao na ununuzi wa mitambo miwili (2) ya kukaushia mbao; kutoa mafunzo ya uvunaji endelevu wa mazao ya misitu; kufanya majaribio ya uzalishaji wa mianzi na utengenezaji wa bidhaa za mianzi; kuwezesha vikundi vinne (4) vya wakulima wa mbao katika vijiji vinne (4) vya wilaya ya Nyasa kwa kupanda ziada ya hekta 100 za Miti ya mitiki katika maeneo yaliyochaguliwa; kutoa mafunzo kwa Kamati za Maliasili 131 za Vijiji katika Halmashauri 12 za vijiji kuhusu sheria na kanuni zinazohusu misitu ya hifadhi inayosimamiwa na vijiji; kutoa mafunzo kwa Kamati za Halmashauri na Serikali za vijiji kuhusu Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii, upangaji wa matumizi bora ya ardhi (LUP) na sheria na kanuni zinazohusu maendeleo ya mnyororo wa thamani; kutoa mafunzo kwa watumishi wa wilaya 12 kuhusu maendeleo ya mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu; na kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wawili (2) wa shahada ya uzamili kuhusu minyororo ya thamani ya mazao ya misitu na mfumo wa soko na maendeleo ya biashara.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: Kuandaa mikakati ya utekelezaji na miongozo ya ugani ya sera za misitu na ufugaji nyuki; kukamilisha kazi ya Takwimu za misitu ya jamii kwa mwaka 2020 na kuchapisha vijitabu na kuvisambaza; kuendelea na kuandaa Miongozo ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu Asilia, na kuichapisha; kufanya mapitio ya Sheria ya Kitaifa ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2021; kuchapisha na kusambaza Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Misitu na Nyuki na Miongozo ya Ugani; na kuwezesha uandaaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mkaa na usambazaji wake. Jumla ya shilingi bilioni 5.6 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4651: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki - BEVAC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kuanza kwa ujenzi wa bweni la wanachuo wa kike lenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 200 katika Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI) – Tabora; ununuzi wa vifaa vya kitafiti kwa ajili ya maabara ya Utafiti wa Nyuki katika Kituo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki Njiro – Arusha; kuanzisha hifadhi za nyuki na manzuki katika mikoa ya Kusini Pemba, Kaskazini Pemba, Tabora, Katavi na Kigoma; kutoa mafunzo kwa wafugaji nyuki na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki waliopo katika mikoa sita (6), taasisi sita (6) za kiserikali na taasisi binafsi nane (8). Jumla ya shilingi bilioni 4.2 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4816: Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio – MICE**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Utalii wa Mikutano na Matukio katika halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 1.98 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 4648: Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kusimamia Rasilimali za Misitu na Nyuki**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga maabara ya mafunzo kwenye Chuo cha Viwanda vya Ufugaji Nyuki – Tabora (BTI); kuhamisha shughuli za Chuo cha Viwanda vya mazao ya Misitu (FITI) kutoka Moshi kwenda Mufindi. Jumla ya shilingi milioni 700 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na.4810: Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha miundominu na utoaji wa hudumu katika maeneo ya Hifadhi; kupima eneo na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ghala la nyara Jijini Dodoma; kununua vitendea kazi kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi; kuperemba na kufanya tathmini ya pamoja ya shughuli za mradi; na kuwezesha uratibu na usimamizi wa shughuli za mradi.

#### 4.3.3.4.2 Sekta ya Fedha

**(a) Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi 26 inayoendelea. Jumla ya shilingi bilioni 112.3 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.4 Kukuza Biashara na Uwekezaji

#### 4.3.4.1 Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji

**(a) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Kukuza Uwekezaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Uwekezaji

na Sheria mpya ya uwekezaji; kukamilisha na kusambaza Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Uwekezaji nchini; kuboresha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji nchini; na kuratibu maandalizi na usambazaji wa Mwongozo wa uwekezaji wa mikoa. Jumla ya shilingi milioni 800 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Programu za Kuboresha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi/*Blueprint* pamoja na kuimarisha hatua za kitaifa na kikanda zinazosaidia uwekezaji na kupunguza gharama za kufanya biashara; na kuhamasisha uelewa wa pamoja na kuzingatia sheria za kimataifa na viwango vya kitaalamu. Jumla ya shilingi milioni 600 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Kuimarisha Mifumo ya Uratibu na Usimamizi wa Masuala ya Uwekezaji Kitaifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuboreshwa kwa Huduma za Mahala Pamoja (OSC) na kuimarishwa kwa mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha kutoa vibali vya wawekezaji kwa muda mfupi kwa kuunganisha mifumo ya Taasisi zilizopo ziweze kusomana (system interface); kuanzisha kituo cha pamoja cha TEHAMA (Tanzania Electronic Investment Window-TEIW); Kuanzisha tovuti ya mtandao wa ardhi ya wawekezaji ambayo itakuwa na taarifa jumuishi za masuala ya uwekezaji ikiwemo maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji; kuanzisha kanzidata ya maoni/malalamiko kwa wawekezaji; kufanya utafiti ambayo matokeo yake yataboresha kanzidata ya uwekezaji nchini; kuwezesha Halmashauri kuandaa mpango na kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji; kuendelea kuratibu programu za uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje ya nchi; kuratibu ufanikishaji wa uwekezaji ikiwemo kuongeza ufanisi wa miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC); kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa; na kuboresha mifumo ya kushughulikia changamoto za uwekezaji. Jumla ya shilingi bilioni 5.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Kukuza Ushiriki wa Watanzania kwenye Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya tathmini ya ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati; kuandaa Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania katika miradi ya kimkakati pamoja na mkakati wake wa utekelezaji; na ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi jijini Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.4.2 Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji kwa kuwaunganisha wajasiriamali na fursa za kiuchumi pamoja na kuwawezesha kupata mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu; kukuza ujuzi na maarifa kwa wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa ili kukuza biashara zao na kuzalisha kwa tija na ubora; na kuimarisha vituo vya uwezeshaji ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa wananchi. Jumla ya shilingi milioni 900 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.4.3 Kukuza Sekta Binafsi

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika miradi na programu za maendeleo nchini; kufanya tathmini ya mchango wa sekta binafsi katika

kukuza uchumi; kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi pamoja na Mkakati wake wa utekelezaji; kuimarisha majadiliano na mashirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi; na kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa Taifa wa Baraza la Biashara nchini. Jumla ya shilingi milioni 600 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.4.4 Huduma za Biashara na Masoko

**(a) Mradi Na. 4933: Kituo cha Biashara na Ugavi Kurasini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutafuta wawekezaji; kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya msingi ya maji, umeme na barabara za ndani ya eneo; na kujenga majengo ya viwanda (Industrial Shades). Jumla ya shilingi milioni 500 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Uendelezaji wa Masoko ya Bidhaa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha Mfumo wa taarifa za masoko na biashara na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mazao ya kilimo na bidhaa; kuimarisha ulinzi kwa kufunga kamera na vifaa vya TEHAMA katika miundombinu ya ghala; ununuzi wa magari mawili (2) ya Taasisi ya WRRB; na kuimarisha utafiti wa masoko, ukusanyaji wa taarifa, uchambuzi na usambazaji wa matokeo yake. Jumla ya shilingi bilioni 1.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DTIF) - TANTRADE**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuratibu maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Dar es Salaam International Trade Fair - DITF); kuendeleza miundombinu ya uwanja wa Maonesho wa Mwl. J. K. Nyerere; kuandaa na kuratibu maonesho ya kimkakati ya biashara ya nje ya nchi, B2Bs, Misafara ya Biashara, Jukwaa na kongamano ili kutangaza bidhaa za Tanzania katika masoko ya Nje; kuanzisha na kuendeleza Rajamu ya Taifa "National Brand Mark (NBM)"; na kutengeneza na kusimamia Mfumo Mama wa Usimamizi wa Taarifa za Biashara Jumuishi wa TanTrade "Integrated Trade Information management System (iTIMS)". Jumla ya shilingi bilioni 3.6 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Udhibiti wa Ubora wa Bidhaa - TBS**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Maabara; kununua vifaa, vitendea kazi na kujenga uwezo wa wataalamu wa maabara za udhibiti viwango vya ubora wa bidhaa; kuboresha mfumo wa usimamizi wa masoko kwa kusimamia Mkakati wa Maendeleo ya Biashara ya Nje; kuhamasisha wafanyabiashara kuzingatia viwango vya ubora katika uzalishaji na uagizaji wa bidhaa; na kuendelea kuimarisha matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika uzalishaji wa bidhaa ili kukidhi viwango vya ubora vinavyohitajika katika soko la ndani na nje. Jumla ya shilingi bilioni 15 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.5 Kuchochea Maendeleo ya Watu

#### 4.3.5.1 Afya

**(a) Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la kutoa huduma kwa wagonjwa binafsi na wagonjwa mashuhuri (Private Wing); ukarabati wa vyumba vitano (5) vya wagonjwa mahututi (ICU) na vyumba vya radiolojia (MRI 1, CT-SCAN 1 na X-ray 2); kufunga mtambo wa kuzalisha dawa maji (compound and infusion); kufunga mtambo wa kuzalisha hewa tiba (medical oxygen plant); kununua mashine ya *fluoroscopy*, *operating towers* tatu (3), *laparascopic instruments*, *towers for video assisted thoracoscopic surgery* mbili (2) na *pharacoscopic instruments;* kuanza kwa maandalizi ya utenegenezaji wa mfumo mpya wa TEHAMA (HIMS) pamoja na kununua kompyuta 1,000; ukarabati wa Hospitali ya Watoto; ukarabati na upanuzi wa jengo la OPD; na kujenga majengo mawili (2) ya kuegesha magari.

**(b) Mradi Na. 6364: Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kuimarisha huduma za tiba za rufaa, kutoa huduma za vikoba, kusomesha wataalamu pamoja na ununuzi wa vifaa tiba; na ujenzi wa kituo cha upandikizaji viungo *(Transplant Center)* na sehemu ya kufulia nguo (Laundry).

**(c) Mradi Na. 5491: Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kulipa mkopo wa ujenzi kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; kununua vifaa tiba (vipandikizi); Kujenga kituo cha tiba mazoezi *(rehabilitation centre )* katika kiwanja cha Taasisi kilichopo Mbweni Mpiji; Upanuzi wa vyumba vya kuonea wagonjwa wa nje (OPD) na vyumba vya mazoezi tiba *(physiotherapy)*.

**(d) Mradi Na. 5419: Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Upanuzi wa chumba cha kutakasia vifaa ili kuimarisha huduma za upasuaji wa moyo; na kukarabati wodi namba moja na tatu.

**(e) Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ufungaji wa mashine nyingine ya PET/CT SCAN ya kufanya uchunguzi wa saratani; kuanza ujenzi wa jengo la kutolea huduma za dawa na *bunkers* nne (4) na kununua na kusimika mashine mbili (2) za LINAC kwa ajili ya tiba mionzi na kununua mashine za *cobalt*; na kuanza ujenzi wa vituo vya saratani vitakavyotekelezwa kwa ubia (PPP).

**(f) Mradi Na. 5424: Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto (Kilimanjaro)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ikiwemo maabara ya ngazi ya tatu (3) ili kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ya kuambukiza, ujenzi wa jengo la mionzi la ghorofa mbili (2), ujenzi wa jengo la OPD *Complex* na ujenzi wa jengo la utawala; kukarabati wodi na kununua mashine za uchunguzi; na uejnzi wa jengo la wagonjwa mahututi na vifaa vya maabara.

**(g) Mradi Na 5425: Hopitali ya rufaa ya Afya ya Akili Mirembe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ukarabati wa wadi za wagonjwa na majengo mengine.

**(h) Hospitali za Rufaa za Kanda**

**(i) Mradi Na. 5426: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Ziwa, Bugando**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa jengo la mama na mtoto lenye ghorofa tano (5); kuanza ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje lenye ghorofa tano (Out patient one stop centre); kuanza ujenzi wa taasisi ya moyo yenye ghorofa tano (BMC Heart Institute); kumalizia ujenzi wa wodi za wagonjwa wa saratani na clinic ya wagonjwa wa macho; na ujenzi wa hosteli ya wagonjwa.

**(ii) Mradi Na. 5427: Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC)**

Shughuli zitakazoendelezwa ni: kuendelea kuimarisha huduma za kibingwa na kuimarisha miundombinu kwa kuendelea kujenga jengo la tiba mionzi; eneo la kusubiria ndugu wa wagonjwa (Patients' waiting area); ukarabati wa wodi za wagonjwa mahututi na vyumba nane (8) vya upasuaji, kuanza ujenzi wa kituo cha magonjwa ya moyo (CardiovascularCentre), na kuanza ujenzi wa maabara kuu (Centralized Labaratory) na ukarabati wa jengo la wagonjwa mahututi (ICU).

**(iii) Mradi Na. 5422: Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za tiba za kibingwa na ununuzi wa vifaa tiba; kuendelea na uejnzi wa jengo la wazazi – Meta.

**(iv) Mradi Na. 5428: Hospitali ya Benjamini Mkapa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: huduma za tiba za kibingwa; kuendelea na ujenzi wa jengo la kutolea huduma ya tiba mionzi; kufanya ukarabati wa vyumba vitatu vya upasuaji; kufanya ukarabati (renovation ) eneo ambalo litatumika kwa ajili ya kutoa huduma ya upandikizaji figo ambalo linatakiwa kuwa na vyumba vya upasuaji, maabara, famasi na ICU kwa ajili ya wagonjwa watakaokuwa wanafanyiwa upandikizaji wa figo; kufanya ukarabati (renovation) wa chumba kilichotengwa kwa ajili ya 'skills lab; kuanza ujenzi wa Hosteli kwa ajili ya wanafunzi na kukamilisha uanzishaji wa wa kitengo cha kuzalisha maji tiba (infusion unit); na kuanzisha mradi wa Uzalishaji Gas (Medical Oxygen) ambao utakuwa unazalisha mitungi 384 ya Medical Oxygen kwa siku.

**(v) Hospitali ya Rufaa Kanda ya Mashariki CCBRT**

Shughuli zitakayotekelezwa ni: Kuendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa ya macho, watoto wanaozaliwa na hitilafu ya viungo kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania ili kuepusha ulemavu unaoweza kuzuilika, watu wazima wenye matatizo ya mifupa; wanawake wenye matatizo ya fistula itokanayo na uzazi, watoto na watu wazima wenye midomo wazi (Cleft lip/Cleft Palate) pamoja na huduma ya utengemao (health related rehabilitation); kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya huduma za afya ya macho, upasuaji wa mifupa kama vile C-arm X-ray, mashine ya mionzi ya macho (PASCAL Laser machine-TOPCON), *Ultrasound machine, auto edging machine* kwa ajili ya huduma za

miwani na kuimarisha mfumo wa kukusanya taarifa za afya (Information System development: HMIS).

**(vi) Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Burigi**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya hospitali ikiwemo jengo la upasuaji, wodi za kulaza wagonjwa, jengo la kufulia, chumba cha kuhifadhia maiti, nyumba za watumishi, uzio pamoja na nyumba za walinzi, kisima na jengo la huduma ya mionzi.

**(vii) Mradi Na. 5423 Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Kusini - Mtwara**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya hospitali ikiwemo jengo la upasuaji na wodi za kulaza wagonjwa.

**(viii) Hospital ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi – Kigoma**
Shughuli zitakazotekelezwa ni kuanza ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi katika mkoa wa Kigoma.

**(i) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Mikoa ya Katavi, Songwe, Njombe, Singida, Shinyanga, Simiyu, Geita na Mrara; na kuendelea kuboresha miundombinu ya hospitali za rufaa za mikoa za Mount Meru (Arusha), Sekou Toure (Mwanza), Mwananyamala (Dar es Salaam), Temeke (Dar es Salaam), Tumbi (Pwani), Morogoro, Maweni (Kigoma),Amana, Temeke (Manyara), Mawenzi (Kilimanjaro); Rukwa, Mbeya, Mtwara, Dodoma, Mtwara, Tanga, Kigoma na Kagera.

**(j) Mradi wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga Hospitali ya Taifa (Dodoma) ya Afya ya Mama na Mtoto; kuanza kwa ujenzi wa hospitali kibingwa na ubingwa bobezi ya Afya ya Mama na Mtoto katika mkoa wa Dodoma; kuimarisha upatikanaji wa damu salama; kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba; na kuimarisha na kuongeza watalaamu wa afya wenye ujuzi.

**(k) Mradi Na 2208: Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMRI) Kuimarisha Tafiti za Afya, Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kugharamia tafiti za magonjwa ya binadamu, tiba asili na tiba mbadala ili kuwezesha kufanyika maamuzi sahihi katika kutekeleza afua za kupambana na magonjwa ya binadamu; kuimarisha utengenezaji wa dawa za asili katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Kuimarisha mafunzo kwa watoa huduma za tiba asili katika Taasisi za Mafunzo (Afya).

**(l) Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kununua vifaa kwa vituo 318 vinavyojengwa ambapo kati ya hivyo, vituo 233 ni vya tozo; na ununuzi wa Vifaa Tiba kwa zahanati za Halmashauri

558. Jumla ya shilingi bilioni 123.3 fedha za ndani zimetengwa.

Aidha, shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: Kununua na kusambaza wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa vituo vyote vya umma na binafsi vya kutolea huduma za afya nchini na ugomboaji wa dawa za msaada; na kugharamia huduma za uchunguzi.

**(m) Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo**

Shughuli itakayotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kupitia huduma za chanjo. Jumla ya shilingi bilioni 30 fedha za ndani na shilingi bilioni 21.5 fedha za nje zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 5492: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP)**

Shughuli itakayotekelezwa ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma kwa watu wenye VVU na UKIMWI ili kufikia malengo ya asilimia 95 – 95– 95 (kutambua - kutumia dawa - kujikinga). Jumla ya shilingi bilioni 20.0 fedha za nje zimetengwa.

**(o) Mradi Na.5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuongeza huduma za kinga na kinga ya kifua kikuu kwa vituo vya msingi vya huduma ya afya; kutoa mafunzo kazini ya kuwajengea wafanyakazi uwezo wa kuongeza ufanisi wa uibuaji wa wahisiwa na utoaji wa huduma wa Kifua Kikuu *(QI Mentorship)*; kutekeleza mradi wa Tambua TB na elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari; na kutoa huduma za ufuatiliaji na upimaji wa wahisiwa wa Kifua Kikuu magerezani *(Prison screening)*.

**(p) Mradi Na. 5406: Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha huduma za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza, ya mlipuko na yale yasiyo ya kuambukiza . Jumla ya shilingi bilioni 30.18 fedha za nje zimetengwa ikiwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa mradi Kisopwa.

**(q) Mradi wa Huduma za Damu Salama**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Vituo vya Damu Salama vya Mkoa kwenye Mikoa ya Katavi, Songwe, Ruvuma, Geita, Morogoro itakayoongeza uwezo wa ukusanyaji na uchakataji wa mazao ya damu kwa ajili ya kuongeza tija na ufanisi kwenye tiba na kupunguza vifo vya akina mama na watoto; utengenezaji wa mfumo wa taarifa wa mnyororo wa huduma za Damu Salama (Blood Safety Information System) kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa pamoja na takwimu sahihi za huduma za damu salama nchini; na ununuzi wa mashine tano (5) za kuchakata mazao ya damu “Apheresis” ili kurahisisha utoaji wa huduma za kibingwa na kibobezi.

**(r) Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa hosteli ya wsataalamu (Intern), hosteli ya wanafunzi, jengo la madarasa  na utawala, ukarabati wa hostel ya MTC na upanuzi wa karakana ya ufundi  katika Chuo cha Sayansi ya Afya cha Muhimbili; Ujenzi wa Jengo la

Wodi Maalum (Private wards) katika chuo cha *Tabora Clinical Officers Training Centre*; ukarabati wa majengo mbalimbali ndani ya chuo cha *Ngudu Environmental Health School*; *Kilosa Clinical Officers Training Centre*; na *Kagemu Environmental Health School*; kufanya tathmini ya uendelezaji ubora (continuous quality improvement) wa vyuo, utekelezaji wa mafunzo endelevu (Continuous Professional Development-CPD) kwa watumishi wa Sekta ya Afya; kuongeza watahiniwa na kugharamia mafunzo ya uzamili kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea; na kufanya upanuzi na ujenzi wa majengo na ukarabati kwenye vyuo vya mafunzo ya afya vya uuguzi nchini.

**(s) Mradi Na. 5416: Kuimarisha Matumizi ya TEHAMA katika Utoaji wa Huduma za Afya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao, mafunzo, utawala, usimamizi wa fedha, dawa na bidhaa zote za dawa pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika ngazi zote za hospitali, vituo vya afya na zahanati.

**(t) Bima ya Afya kwa Wote**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kutoa elimu ya Waraka wa Bima ya afya kwa wote na kuweka mifumo ya utekelezaji wa mpango wa Bima kwa wote.

**(u) Mradi Na. 5401: Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hospitali 28 za Halmashauri kwa awamu ya 2 ambazo zimeanza kujengwa katika mwaka 2021-2022 ikijumuisha ujenzi wa jengo la Utawala, *incinerator,* mama na mtoto na wodi ya wanaume na wanawake; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa hospitali 31 za Halmashauri awamu ya 3 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya wodi ya magonjwa ya kuambukiza, jengo la kuhifadhi maiti, jengo la kufulia na wodi ya watoto; kukarabati hospitali kongwe 21 za Halmashauri; na kujenga nyumba 200 (3 in 1) za watumishi wa Afya katika Halmashauri za wilaya zenye maeneo yasiyofikika kirahisi. Jumla ya shilingi bilioni 116.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 5429: Huduma ya Afya ya Msingi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa zahanati 642 katika Halmashauri 184. Jumla ya shilingi bilioni 32.1 fedha za ndani zimetengwa.

**4.3.5.2 Ustawi na Maendeleo ya Jamii**

**(a) Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**

Shughuli zitakazotekezwa ni:

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Misungwi:** Kujenga hosteli ya ghorofa 1 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600; Ujenzi wa karakana ya *automobile* pamoja na vifaa vyake; Kuboresha Maabara ya udongo na Karakana za Chuo (Useremala na Ujenzi) kwa kuweka vifaa; Kujenga Hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja; Kujenga jengo la utawala lenye ghorofa mbili (2); na Kufanya ukarabati wa

nyumba mbili (2) za watumishi.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mabughai:** Kukarabati kafteria na nyumba za watumishi yenye kuhudumia familia nne (4); Kukarabati mfumo wa maji safi na miundombinu ya umeme katika mabweni; kujenga hosteli ya wanawake yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 250 kwa wakati mmoja; kujenga jengo la utawala lenye ghorofa moja (1) lenye ofisi 10 na ukumbi wa mikutano; kujenga Karakana yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 75 kwa wakati mmoja; na Ununuzi wa samani katika madarasa matatu (3) yenye kuchukua wanafunzi 750 na kuweke mtandao wa *Internet.*

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba:** kujenga hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 pamoja na ukumbi wenye uwezo wa kuhudumia watu 600; kujenga kumbi za mihadhara *(two in one)* zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 kwa wakati mmoja; kujenga jengo la maktaba na maabara ya kompyuta yenye uwezo wa kuhudumia wanachuo 400 kwa wakati mmoja; na kujenga zahanati yenye vyumba 10.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Ruaha:** kujenga ukumbi wa kisasa *(3 in 1)* wenye uwezo wa kuhudumia watu 900; kujenga hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500; kujenga kantini ya wanafunzi *(2 in 1)* yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; kujenga jengo la utawala lenye ofisi 25; kujenga uzio wenye mzingo wa kilomita mbili (2); kujenga hosteli yenye ghorofa 3 yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kwa wakati mmoja; na kujenga maabara ya kompyuta yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 150 kwa wakati mmoja.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Mlale:** Kujenga bweni lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 kwa wakati mmoja; kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja; na kukarabati nyumba 15 za watumishi.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tengeru:** kujenga *multipurpose hall*; kujenga bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 684; kujenga jengo la utawala lenye ofisi 25 na kumbi mbili (2) za mikutano; kununua vifaa vya TEHAMA katika kumbi pacha za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,008 kwa wakati mmoja; na kununua samani katika bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 568 kwa wakati mmoja.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Buhare:** Kujenga kumbi Pacha za Mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000 kila moja; na kujenga hosteli zenye uwezo wa kiuhudumia wanafunzi 1,000.

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Monduli:** Kujenga hosteli tatu (3) zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 450 kila moja; Kujenga bweni lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 600 kwa wakati mmoja.

Jumla ya shilingi bilioni 41.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo**

Shughuli zitakazotekezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa Kampeni ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto "Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi" katika mkoa wa Geita na Mwanza; kujenga uwezo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii na Wanasheria kuhusu utoaji wa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia; kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Kamati za Ulinzi za Wanawake na Watoto; kukamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); kuwezesha utekelezaji wa Ahadi za Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum); kutekeleza afua za kuzuia ukeketaji wa wanawake; utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali kupitia dirisha la wanawake katika Benki ya Posta na asilimia 4 ya mapato ya halmashauri; kuwezesha uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika vyuo vya elimu ya juu na vya kati; na kufanya tathmini ya programu za kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni: Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na Kuandaa Awamu ya Pili ya MTAKUWWA; kufanya mapitio ya Mkakati wa Kukabiliana na Ajira Mbaya kwa Mtoto; kufanya upembuzi yakinifu kuhusu Mikataba na Miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya usaidizi wa kisaikolojia na kijamii (Psychosocial supports) kwa Vijana na Watu Wenye Ulemavu hususan wanaoishi na VVU/UKIMWI na waraibu wa madawa ya kulevya kwa kuzingatia mazingira ya kitaifa; na kufanya mapitio ya miongozo ya kitaifa ya udhibiti wa VVU/UKIMWI na Magonjwa Yasiyoambukiza. Jumla ya shilingi bilioni 1.4 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto**

Shughuli zitakazotekezwa ni: kuwezesha uanzishwaji wa Dawati la Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya watoto ndani na nje ya shule za msingi na sekondari; kuendelea kujenga uelewa wa jamii kuhusu malezi chanya kwa watoto; kuwezesha uanzishwaji wa vikundi vya kijamii vya malezi; kutekeleza afua za kuzuia ukatili wa watoto mitandaoni (online child abuse); kuwezesha uanzishwaji wa vituo vya kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Watoto; kuendelea kuimarisha mabaraza ya watoto; na kutekeleza afua za kuzuia ukeketaji wa watoto wa kike. Jumla ya shilingi milioni 617 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 5451: Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii**

Shughuli zitakazotekezwa ni:

(i) Shule ya Maadilisho Irambo: Kulima mahindi, maharage na ngano katika shamba lenye ukubwa wa hekari 473;

(ii) Makazi ya Wazee cha Chazi: Kulima mpunga na mahindi katika mashamba yenye ukubwa wa hekari 3000;

(iii) Mahabusu ya Watoto Upanga: Kujenga jengo la ghorofa kwa ajili ya ofisi kubwa za

biashara, kumbi za mikutano na eneo la maegesho ya magari;

(iv) Makazi ya Wazee Nunge: Kujenga Mahabusu ya Watoto katika eneo la Makazi ya Wazee;

(v) Mahabusu ya Watoto Mbeya: Kujenga uzio kuzunguka Mahabusu;

(vi) Taasisi ya Ustawi wa Jamii: Ukarabati wa Makazi matano (5) ya wazee; Ujenzi wa mabweni ya wanafunzi katika taasisi ya Usatwi wa Jamii; na Ukarabati wa mahabusu tano (5) za watoto.

Jumla ya shilingi bilioni 9.15 fedha za ndani na shilingi bilioni 7.95 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6290: Ufuatiliaji na Tathmini**

Shughuli zitakazotekezwa ni: Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wizara, taasisi, vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vituo vya Ustawi wa Jamii. Jumla ya shilingi milioni 400 fedha za ndani zimetengwa.

**4.3.5.3 Elimu**

**(a) Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukusanyaji wa mikopo ya shilingi bilioni 190 kutoka kwa wanufaika wa mikopo iliyoiva; kuendelea na ugharamiaji wa mikopo ya wanafunzi 205,893 ambapo wanafunzi 70,000 ni wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 135,893 ni wanaoendelea na masomo; na kufanya ukaguzi kwa waajiri 8,000 pamoja na kuwabaini wanufaika wapya 30,000. Jumla ya shilingi bilioni 558.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6363: Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha - ATC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja; kuendelea na ujenzi na ununuzi wa samani katika bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 420 kwa wakati mmoja; kuendelea na ufungaji wa mtandao wa ndani (LAN) katika majengo ya Chuo; kuendelea na uboreshaji wa miundombinu katika Kituo cha Mafunzo Kikuletwa ikiwemo ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji (turbine), karakana tatu (3), jengo la utawala na ukumbi wa mihadhara na mikutano; na kuendelea na ujenzi wa kliniki itakayohudumia wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo jirani. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki - TAEC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa maabara changamano, Arusha; kuendelea na ujenzi wa maabara za kanda katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Zanzibar; kuendelea na awamu ya pili ya upembuzi yakinifu kwa mradi wa kinu cha tafiti za kinyuklia; na kuendelea na ujenzi wa jengo maalumu kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi kwa kutumia teknolojia ya mionzi (Multipurpose Irradiator Facility). Jumla ya

shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R II)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarishwa kwa Mfumo wa Takwimu wa Wizara (Education Management Information System - EMIS) kwa kuhuisha zana za ukusanyaji takwimu na viashiria vya mfumo; kuendelea na uchapaji na usambazaji wa vitabu na vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wa shule za awali na msingi zenye uhitaji mkubwa; kutolewa kwa mafunzo kwa wakuu wa shule na walimu 3,000 wa shule za msingi za Serikali kuhusu Programu ya Shule Salama (Safe School Programme); na kuboresha ofisi 195 za uthibiti ubora wa shule. Jumla ya shilingi bilioni 27.2 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa sekondari wa masomo ya hisabati na sayansi; kuendelea kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa shule 500 za sekondari nchini; na kukarabati vituo sita (6) (Tabora, Kilimanjaro, Mbeya, Mtwara, Dodoma na Mwanza) na kujenga vituo vinne (4) (Lindi, Songwe, Kagera na Manyara) vya watu wazima ili kuongeza udahili katika elimu ya watu wazima; na Ujenzi wa miundombinu katika shule mpya 234 za sekondari za kata; kuendelea na ukamilishaji wa shule 10 za wasichana za mikoa; na ujenzi wa shule mpya za Sekondari za kata 100 na shule tano (5) za sekondari za wasichana za mikoa. Jumla ya shilingi bilioni 159.7 fedha za nje zimetengwa

**(f) Mradi Na. 4321: Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya Msingi (MMEM) LANES II**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo endelevu kazini (CPD) kwa ngazi ya shule na Vituo vya Walimu (TRC), walimu wa elimu ya awali, msingi, wawezeshaji wa COBET na walimu wa elimu maalumu; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuimarisha utoaji wa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) katika ngazi ya shule na vituo vya walimu (TRC); kufanya tathmini ya jumla ya ubora wa elimu "Whole School Visits" kwa Shule za Msingi kupitia wathibiti ubora wa shule; na kuendelea na uchunguzi wa mapema wa mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wote wenye umri wa miaka 4 hadi 6 (kwa tofauti ya jinsia, umri na aina ya uhitaji/ulemavu) ili kuongeza idadi ya watoto wanaoandikishwa katika shule za msingi kulingana na mahitaji yao stahiki ya kielimu. Jumla ya shilingi bilioni 40.0 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea kutoa mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa maafisa elimu 17 wa mikoa na 86 wa halmashauri; kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya vyoo na maji, matanki ya maji na sehemu za kunawia mikono katika shule za msingi 800; na kununua magari matano (5) kwa ajili ya uthibiti ubora wa shule. Jumla ya shilingi bilioni 29.3 fedha za nje zimetengwa.

**(h) Mradi 4315: Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu Kwa ajili ya Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali (mabweni, vyumba vya madarasa, maabara, kumbi za mikutano, ofisi, samani na vituo atamizi) katika vyuo Vikuu na taasisi vilivyo chini ya Wizara ya Elimu pamoja na taasisi vitano (5) zilizochini ya Wizara ya Fedha na Mipango; kuendela na uboreshaji wa miundombinu na matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na kujifunzia na mifumo ya uendeshaji wa taasisi katika vyuo na taasisi 17; kusomesha Wahadhiri 700 na watumishi wa Wizara ya Elimu na Wizara ya Fedha na Mipango 128; kuendesha mafunzo ya muda mfupi na ya viwandani kwa wahadhiri 3,500; na kufadhili masomo kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu Binafsi 12. Jumla ya shilingi bilioni 117.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi 4309: Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (EASTRIP)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga miundombinu ikiwemo karakana, maabara, madarasa, hosteli katika taasisi zote zinazotekeleza mradi huu (Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya teknolojia Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji); kununua na kufunga mitambo na vifaa katika karakana na maabara; na kujengea uwezo wakufunzi 100 wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi katika ufundishaji na upimaji wa wanafunzi. Jumla ya shilingi bilioni 34.6 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na.6350: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na upanuzi wa hosteli ya Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuongeza ghorofa mbili (2); kuendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000; kuendelea na ujenzi wa maabara kuu ya kemikali itakayotumika kwa ajili ya utafiti na utoaji wa huduma za kupima sampuli za viwandani; kuendelea na ujenzi wa kituo cha wanafunzi na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Shule Kuu ya Uchumi; kuendelea kwa ujenzi wa jengo jipya katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SJMC); na kuendelea na ujenzi wa *Buyu Project* katika eneo la Buyu (IMS) Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 29.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 6365: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la maktaba na kitaaluma (lecture theatre); kuendelea na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya Chuo iliyopo Kampasi kuu ya Moshi, Taasisi ya Elimu ya Ushirika na Biashara Kizumbi na ofisi za Chuo za mikoani; na kununua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na magari mawili (2). Jumla ya shilingi bilioni 13.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na tafiti mbili (2) zenye lengo la kutatua changamoto za wananchi katika afya, kilimo na mifugo zilizopo katika vipaumbele vya tafiti vya Taifa MTUSATE; kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya ubunifu, uendelezaji wa wabunifu na kubiasharisha matokeo ya tafiti nchini; kufungasha (package) na kusambaza matokeo ya utafiti kwa ajili ya watumiaji wakiwemo wananchi, watunga sera na viongozi

mbalimbali; kuandaa mfumo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia (Inventory of emerging technologies); na kuimarisha uwezo wa kusimamia na kuendesha Kongano nchini. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(m) Mradi Na. 6333: Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya - MUST**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala katika Kampasi Kuu; na kuendelea na ujenzi wa hosteli za wanafunzi, ununuzi wa samani na vifaa vya kisasa vya maabara pamoja na karakana kwa ajili ya kufundishia. Jumla ya shilingi bilioni 13.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(n) Mradi Na. 6354: Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na tafiti 25 zinazolenga kutatua changamoto za jamii hususan katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na majenzi; kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa midahalo, madarasa, maabara, studio, karakana, jengo la shahada za juu na utafiti pamoja na mabweni; kuendelea na ujenzi wa jengo la Ardhi (Lands Building) 'Wing A' na ukarabati wa madarasa, maabara, mabweni ya wanafunzi, ofisi na nyumba za wafanyakazi. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(o) Mradi Na. 6361: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine – SUA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa tafiti mpya 45 na kuendelea na tafiti zilizopo (120) kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo, misitu na uvuvi ili kuhuisha elimu na uwezo wa wananchi katika kuzalisha mali na malighafi za mazao ya kilimo kwa ajili ya viwanda; kuendelea na ujenzi wa ofisi na majengo ya taaluma katika hosteli ya Kihonda kwa ajili ya Ndaki ya Sayansi ya Jamii na Jinsia; kuendelea na ujenzi wa majengo mawili (2) ya taaluma yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,500, hosteli mbili (2) za wanafunzi, vibanda vya biashara na maktaba awamu ya kwanza katika kampasi ya Edward Moringe na Solomoni Mahlangu; kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya Ndaki ya Uchumi na Mafunzo ya Biashara; kuendelea na ujenzi wa maabara ya mafunzo ya anatomi ya mifugo na teknolojia ya wanyama; kuendelea na ujenzi wa vitalu nyumba 100 vya kupangisha kwa wahitimu; kuendelea na ujenzi wa maabara katika kampasi ya Mizengo Pinda; na kuendelea na upandaji wa miti katika kituo cha mafunzo Madaba. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(p) Mradi Na. 4392: Kuendeleza Elimu ya Ualimu - TESP**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 35 vya ualimu vya Serikali; kuendelea na uunganishwaji wa vyuo vya ualimu 15 katika Mkongo wa Taifa; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maabara, maktaba za sayansi na TEHAMA katika vyuo saba (7) ambavyo ni Mpwapwa, Dakawa, Patandi, Kasulu, Morogoro, Tukuyu na Butimba; kuendelea na uandaaji wa mfumo wa usahihishaji kwa njia ya kielektroniki (E-marking system) na ununuzi wa vifaa vya TEHAMA. Jumla ya shilingi bilioni 12.6 fedha

za nje zimetengwa.

**(q) Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi - FDC**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa majiko kwa ajili ya vyuo 20 vya maendeleo ya wananchi; kuanza kwa ufungaji wa mfumo wa gesi katika majiko kwa vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya karakana katika vyuo 20 vya maendeleo ya wananchi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo 30 vya maendeleo ya Wananchi. Jumla ya shilingi bilioni 17.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(r) Mradi Na. 4384: Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam – DIT**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukarabati wa hosteli za wanafunzi katika Kampasi Kuu ya DIT; kuendelea na ujenzi wa kituo cha RAFIC na hosteli ili kuhudumia wanafunzi wa kimataifa na kumbi za mihadhara katika Chuo Kikuu cha DIT; na kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa sita (6) Kampasi Kuu ya DIT. Jumla ya shilingi bilioni 40.7 fedha za ndani zimetengwa.

**(s) Mradi Na. 6364: Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Mloganzila**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa mpango wa ujenzi wa Kliniki ya Uporoto; kuendelea na ujenzi wa miundombinu (mihadhara, madarasa, ofisi za utawala na walimu) ya kufundishia Mloganzila; kuendelea na ujenzi wa tanki kubwa la maji katika hosteli za Chole na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili; na kuendelea na ukarabati wa miundombinu (nyumba ya wahadhiri na mifumo ya maji na umeme) ya kituo cha kufundishia cha Bagamoyo cha kampasi ya Muhimbili. Jumla ya shilingi bilioni 2.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(t) Mradi Na. 4322 & 4393: Elimumsingi Bila Ada**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea kutoa elimumsingi bila ada ikijumuisha ruzuku ya uendeshaji wa shule, ruzuku ya ununuzi wa vitabu, posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na maafisa elimu kata, fidia ya ada kwa shule za bweni na kutwa na kugharamia chakula kwa shule za bweni na kutwa. Jumla ya shilingi bilioni 393.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(u) Mradi Na. 4314: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa kununua vifaa vya TEHAMA, vitabu na vifaa vya maabara; na kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya kisasa na hosteli. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(v) Mradi Na. 4341: Chuo Kikuu cha Mwl. Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza kwa uandaaji wa Mpango Kabambe kwa maeneo ya chuo yaliyopata hati miliki ikiwemo Oswald Mang’ombe Butiama (Ekari 86), Kinesi-

Rorya (Ekari 95) na Kisangura- Serengeti (Ekari 136); kuendelea na ukarabati na ujenzi wa majengo ikiwemo bweni moja (1) lenye kuhudumia wanafuzi 400 katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe; na kuendelea na ujenzi wa Ndaki moja (1) ya Kilimo na Shule kuu tatu (3) za Biashara, Uchumi na Mafunzo ya Ujasiriamali, Uhandisi, Teknolojia ya Kilimo na Usindikaji, Uhandisi na Teknolojia ya Nishati katika Kampasi Kuu ya Chuo eneo la BAIC- Butiama. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(w) Mradi Na. 4385: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa kununua vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi 55 na vifaa vya utafiti kwa wanataaluma; kuendelea na ukarabati wa miundombinu ikiwemo mabweni, kumbi za mihadhara na miundombinu ya TEHAMA; kuendelea na ujenzi wa mfumo wa ukusanyaji wa maji taka; kununua samani kwa ajili ya hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi) kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi 500; kununua eneo eneo Msata – Bagamoyo kwa ajili ya upanuzi wa Chuo; kuendelea na ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi 450 katika shule ya Msingi Mazoezi Chang'ombe na madarasa kwa ajili ya wanafunzi 920 na maabara 4 za sayansi katika shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe; na kuendelea na ununuzi wa vifaa vya nishati mbadala na vifaa vya ulinzi katika maktaba ya Chuo. Jumla ya shilingi bilioni 5.3 fedha za ndani zimetengwa.

**(x) Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa 90 katika Shule za Msingi 40 na Sekondari 30, ofisi za walimu katika shule 10, maabara za sayansi katika shule 10 za Sekondari na nyumba za walimu katika shule 20 zenye mahitaji makubwa; kuendelea na ujenzi wa matundu ya vyoo 1,200 katika shule 50 zenye upungufu mkubwa; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule 20 zenye uhitaji mkubwa; kuendelea na ukarabati wa shule kongwe tano (5) za kitaifa na shule za kata zenye mahitaji makubwa; na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa Ofisi ya TEA - Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 20.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(y) Mradi Na. 4306: Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi na ununuzi wa samani katika jengo la ghorofa moja (1) lenye kumbi (4) za mihadhara zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 564 na ofisi (10) katika Kampasi ya Mbeya; na kuendelea na ukarabati wa ofisi (4) na kumbi za mihadhara (3), nyumba (3) za watumishi, mnara na tenki kuu la maji katika Kampasi ya Bagamoyo. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(z) Mradi Na. 4386: Ujenzi na Ukarabati Chuo Kikuu cha Dodoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa hosteli (1) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 152 mkoani Iringa; kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya maabara; kuendelea na ukarabati wa majengo (34); na kuendelea na ujenzi wa visima (3) vya maji. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(aa) Mradi Na. 6353: Upanuzi wa Chuo Kikuu Mzumbe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala na jengo la madarasa (6) lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 3,129 Kampasi Kuu; kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za mihadhara na madarasa mawili (2) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,000, jengo la maktaba (wanafunzi 3,000), jengo la taaluma (ofisi pamoja na madarasa mawili (2) lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 1,000 na walimu 100), jengo la TEHAMA na Kituo Cha Kuatamia Ubunifu, bwalo la chakula lenye uwezo wa kuhudumia watu 900, mabweni manne (4) yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 250 kwa wakati mmoja, mitambo ya kutibu maji na usafi wa majitaka, tanki la kuhifadhi maji na bweni la wanafunzi eneo la Tegeta Ndaki ya Dar es Salaam lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 100; kuendelea na ukarabati wa mfumo wa maji na mabweni nane (8) ya wanafunzi, Kampasi Kuu na Ndaki ya Mbeya; kuendelea na ununuzi wa samani za madarasa na ofisi; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo, jengo la Lumumba Complex, zahanati ya Ndaki ya Mbeya na madarasa (4) ya kompyuta. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(bb) Mradi Na. 4381: Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa mabweni mawili (2) ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,536 (Wanaume 768 na Wanawake 768) pamoja na nyumba tatu (3) za wafanyakazi zenye uwezo wa kuhudumia watumishi 30 katika Kampasi ya Karume Zanzibar; kuendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara wa wanafunzi 1,000 kwa mara moja Kampasi ya Kivukoni; na kuendelea na ujenzi wa madarasa na bweni la wanafunzi katika Tawi la Pemba. Jumla ya shilingi bilioni 4.2 fedha za ndani zimetengwa.

**(cc) Mradi Na. 4397: Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na uboreshaji wa mfumo wa uchunguzi wa soko la ajira kwa kukamilisha uandaaji wa mfumo wa VETdataMIS; kuendelea na upanuzi wa miundombinu ya VETA ikiwemo ujenzi wa ofisi za Makao makuu ya VETA Mjini Dodoma, karakana nne (4) katika Chuo Cha Kihonda, chuo cha VETA Kanadi - Itilima (nyumba ya Mkuu wa chuo, nyumba pacha moja (1) ya watumishi, bwalo la chakula na mabweni mawili (2)), Chuo cha VETA Nyamidaho (bweni la wavulana, nyumba 2 pacha za watumishi), Chuo cha VETA wilaya ya Ileje (mabweni mawili (2), nyumba ya mkuu wa chuo, nyumba moja (1) ya mtumishi, bwalo la chakula na jiko), Chuo cha VETA Urambo (bwalo la chakula na jiko), Chuo cha VETA cha Simanjiro (bweni la wasichana) na Chuo cha Wilaya Namtumbo (mabweni mawili (2), bwalo la chakula, nyumba pacha moja (1) ya watumishi na uwekaji wa vifaa vya kujifunzia); kuanza kwa ujenzi wa vyuo 29 vya Wilaya vya VETA na chuo kimoja (1) cha mafunzo ya ufundi stadi na huduma cha Mkoa wa Kagera; kuendelea na ujenzi wa Chuo cha VETA cha Dar es Salaam Kampasi ya Kigamboni; kuendelea na ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Songwe; kuendelea na ukarabati wa vyuo 5 vya VETA ngazi ya mkoa katika mikoa ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Dar es salaam na Dodoma; na kuendelea na ununuzi na ukarabati wa vifaa na zana za mafunzo (1,175), mitambo, magari (20) na nyumba 15 za watumishi (Moshi, Singida na Kigoma) na nyumba 10 katika eneo la Tabata. Jumla ya shilingi bilioni 87.8 fedha za

ndani zimetengwa.

**(dd) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukamilishaji wa maboma ya madarasa ya shule za msingi 3,800 na sekondari 1,200, maboma wa vyumba vya maabara za Sayansi 291 katika Shule za sekondari, maboma ya mabwalo ya chakula 6 katika shule za msingi, maboma ya mabweni 28 katika shule za msingi zenye mahitaji maalum na 387 kwa shule za sekondari, maboma ya mabwalo ya chakula 75 katika shule za sekondari; na ujenzi wa nyumba za walimu (three in one) 338 katika shule za msingi na 200 kwa shule za sekondari, uzio katika mabweni 99 ya watoto wenye mahitaji maalum, na madarasa 3,400 ya shule kongwe za msingi. Jumla ya shilingi bilioni 213.8 fedha za ndani zimetengwa.

### 4.3.5.4 Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**(a) Mradi Na. 2326: Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi kwa ajili ya uwekezaji na makazi kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji ambapo hati za kumiliki ardhi 300,000 na hatimiliki za kimila 520,000 zitatolewa; kuandaa mipango minne (4) ya uendelezaji upya wa maeneo kongwe katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza na Arusha, kuandaa Mipango kina mitano (5) ya uendelezaji wa visiwa na fukwe kwa kushirikiana na wadau mbalimbali; kuandaa mipango ya uendelezaji miji katika miradi ya kimkakati ya EACOP, SGR na JNHPP kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji na kuimarisha Mfuko wa Fidia. Jumla ya shilingi bilioni 39.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha mipaka miwili (2) ya kimataifa kati ya Tanzania na Kenya (km 110) na Tanzania na Burundi (km 100) pamoja na mipaka kati ya Tanzania na nchi za DRC Congo, Zambia na Burundi katika Ziwa Tanganyika; kuandaa kanzidata ya taarifa ya mipaka ya kimataifa (ndani ya maji na nchi kavu); kufanya tafiti na kukusanya takwimu za upimaji ndani ya maji; na kuhuisha andiko la maombi ya eneo la nyongeza lenye ukubwa wa kilometa za mraba 60,000 nje ya ukanda wa bahari ya Hindi lililowasilishwa Umoja wa Mataifa. Jumla ya shilingi bilioni 5.4 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na 2329: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani**
Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga vituo 30 vya kielektroniki vya upimaji ardhi (Continuously Operating Reference Station- CORS) katika makao makuu ya mikoa yote na kuongeza alama 357 za upimaji nchini zitakazoongeza kasi na kupunguza gharama za upimaji ardhi; kuandaa ramani za msingi zenye uwiano mdogo kwa nchi nzima (Tanzania bara) na ramani za uwiano mkubwa katika miji mikuu ya mikoa yote nchini; kununua ndege moja inayoendeshwa na rubani pamoja na Kamera kwa ajili ya kupiga picha za anga za kutayarisha ramani za msingi za uwiano mkubwa; kununua *Satellite image* kwa ajili ya kutayarisha ramani za msingi za uwiano mdogo; kujenga kanzidata ya

kitaifa ya taarifa za kijiografia katika kituo cha *National Land Information Centre* - NLIC; na kuwajengea uwezo wataalamu 30 katika maeneo ya upimaji na ramani. Jumla ya shilingi bilioni 45 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ujenzi wa Ofisi za ardhi za mikoa 25 nchini; kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi 200,000; kununua vifaa vya upimaji ardhi (RTK na Total Station); kupima mipaka ya vijiji 50; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya sita (6); kuandaa mipango ya matumizi ardhi ya vijiji 50; kujenga miundombinu wezeshi na vifaa vya TEHAMA vya mfumo Unganishi wa taarifa za ardhi (ILMIS); kubadilisha taarifa za Ardhi kutoka Analogia kwenda Digitali katika Halmashauri 100; kufunga vifaa vya kudhibiti majanga na vihatarishi (Disaster recovery site) kwa ajili ya mifumo ya taarifa za ardhi; kuwajengea uwezo watumishi wanaoshiriki katika kazi ya kuboresha mfumo wa ILMIS na miundombinu; kujenga alama za msingi 22 (continous reference operations – CORS) nchini kwa ajili ya kurahisisha upimaji wa ardhi na kupiga picha za anga; na kuhuisha viwango vya thamani ya ardhi nchini. Jumla ya shilingi bilioni 109.0 fedha za nje na shilingi bilioni 18.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa maktaba na ujenzi wa madarasa mawili (2) katika Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA); ujenzi wa madarasa mawili (2) ya Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO); ujenzi na ukarabati wa majengo 15 ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; na kukarabati miundombinu ya ofisi za Wizara na Mikoa. Jumla ya shilingi bilioni 4.35 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya 11; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 826 na mipango kina 175; kuandaa mipango ya uendelezaji wa shoroba katika maeneo ya miradi ya Kimkakati (EACOP, SGR, JNHPP) na Wilaya za mipakani; kuzijengea uwezo mamlaka za upangaji 11 katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, sheria na taratibu; kutatua migogoro ya ardhi; kutoa elimu ya kupanga, kutekeleza, kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vitavyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi; kuandaa sheria ndogo ndogo za usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 1,000 vitakavyoandaliwa mipango; na kupima mipaka ya vijiji pamoja na kuandaa vyeti vya ardhi ya vijiji. Jumla ya shilingi bilioni 15.63 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.5.5 Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

**(a) Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

Shughuli itakayotekelezwa ni kukamilisha miradi ya maji 924 inayoendelea kutekelezwa vijijini. Jumla ya shilingi bilioni 248.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 324.0 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 3306: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Dodoma, Morogoro, Arusha, Shinyanga na Kigoma; na kujenga miundombinu ya majitaka katika miji ya Musoma, Bukoba na Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 123.93 fedha za ndani na shilingi bilioni 113.63 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha utekelezaji wa mradi wa maji *Orkesumet* (Simanjiro), Wanging'ombe (Njombe), Mgango – Kiabakari – Butiama (Mara); na kuanza utekelezaji wa miradi ya kuboresha huduma za maji katika miji 28. Jumla ya shilingi bilioni 46.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 21.3 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi inayohusisha ujenzi wa chanzo na mitambo ya kusafisha maji; na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji katika miji ya Mwanga na Same. Jumla ya shilingi bilioni 9.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 3.0 fedha za nje zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 3342: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria – Tabora - Nzega - Igunga**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji itakayowanufaisha wananchi wapatao 117,300 katika miji ya Tinde (vijiji 15) na Shelui (vijiji 9): na kukamilisha miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Nzega, Igunga, Uyui na Tabora pamoja na vijiji vilivyopo kando kando ya bomba kuu umbali wa kilometa 12 kila upande. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 6.6 fedha za nje zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya karibu na bomba kuu la maji kwenda miji ya Malampaka, Sumve na Malya; kuanza utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wa Simiyu; na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kupeleka maji katika mikoa ya Singida na Dodoma kutoka Ziwa Victoria. Jumla ya shilingi bilioni 5.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 22.0 fedha za nje zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 3437: Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya Dar es Salaam na Pwani; na kujenga mitambo ya kutibu maji, mabomba ya kutolea majitaka kutoka maeneo ya makazi na kupelekwa kwenye mitambo ya usafishaji. Jumla ya shilingi bilioni 6.0 fedha za ndani na shilingi bilioni 45.0 fedha za nje zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 3439: Mradi wa Maji wa Mpera na Kimbiji**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji eneo la Kisarawe II lenye uwezo wa mita za ujazo 15,000; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza huduma za maji kwa wananchi wa Kigamboni kutoka katika visima vya Kimbiji na Mpera. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani na zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na utekelezaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na utumiaji wa rasilimali za maji nchini kwa kujenga vituo vya kufuatilia mwenendo wa maji katika mito; kutoa leseni mpya za uchimbaji visima na vibali vya kuchimba visima vya maji; kutoa vibali vya matumizi mbalimbali ya maji; kuanzisha jumuiya za watumia maji; kufanya utafiti wa maeneo ya kuchimba visima; kuweka mipaka na kutangaza vyanzo vya maji katika Gazeti la Serikali; kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Maji ya Bonde la Wami – Ruvu; na kuanza ujenzi wa majengo ya maabara za maji katika mikoa ya Geita, Manyara, Tabora, Lindi, Simiyu, Songwe, Katavi, Dodoma, Tanga na Arusha. Jumla ya shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 27.0 fedha za nje zimetengwa.

**(j) Mradi Na. 3435: Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufuatilia ubora wa maji kwa kukusanya na kuhakiki usalama wa sampuli za maji kutoka katika vyanzo mbalimbali vya maji; kuunda na kusambaza mitambo ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji; na ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya maabara za maji. Jumla ya shilingi bilioni 2.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 2.5 fedha za nje zimetengwa.

**(k) Mradi Na. 3436: Ufuatiliaji na Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kugharamia ulipaji kwa kampuni ya wataalamu wanaotoa huduma katika usimamizi wa mradi; kukamilisha maandalizi ya Awamu ya Tatu ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Maji (WSDP III); na kuratibu utekelezaji wa programu ya maji (WSDP III). Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani na shilingi bilioni 6.2 fedha za nje zimetengwa.

**(l) Mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa Bwawa la Kidunda kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa matumizi ya wakazi wanaohudumiwa na Mamlaka ya Maji Dar es Salaam. Jumla ya shilingi bilioni 100.0 fedha za ndani zimetengwa.

**4.3.5.6 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

**(a) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

**(i) Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia Vijijini**

Shughuli zitakazotekelezwa: Ujenzi wa Visima virefu katika Wilaya za Simanjiro, Mvomero, Mpwapwa na Kaskazini A; Ujenzi wa Skimu ya Umwailiaji ya Lukenge (Mvomero); Ujenzi wa Kituo cha huduma za Mifugo (Veterinary Centre) katika Wilaya ya Mpwapwa; Ujenzi wa Majosho (livestock diptanks) Kishapu (2), Mpwapwa (1), Simanjiro (1) and Mvomero (2); Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Nafaka (12x25x6m Grain Storage Facility/godown) katika Wilaya ya Simanjiro; Ujenzi wa Mabwawa (charcodams) Mpwapwa (1), Kishapu (1) and Simanjiro; Ununuzi wa ng'ombe, mbuzi, kuku, kuwezesha vikundi vya ufugaji katika Wilaya za Kishapu, Mpwapwa, Mvomero na Kaskazini A; Kutoa mafunzo na vifaa kwa vikundi vya Ususi/Ushonaji/Ufumaji; kuanzisha mashamba darasa (Farmer Field Schools - FFS) na kujenga vitalu nyumba (greenhouse/screenhouse) 12 kwa kilimo cha mbogamboga Kaskazini A (2), Mvomero (3), Mpwapwa (4) and Simanjiro (3); Kutoa mafunzo na vifaa vya ufugaji nyuki kwa vikundi vya vilivyoanzishwa; na kuongoa maeneo ya mito, vyanzo vya maji na nyanda za malisho yayoharibiwa kwa kupanda miti. Jumla ya shilingi bilioni 6.87 fedha za nje zimetengwa.

**(ii) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo wa Ikolojia, Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai Tanzania.**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya tathnimi ya Athari kwa Jamii na Mazingira; kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa moduli za mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa kisekta na mamlaka za Serikali za mitaa katika kutekeleza program za urejeshaji wa mifumo ikolojia; kufanya warsha na mafunzo kwa maafisa wa ngazi mbalimbali kuhusu shughuli za mradi; kufanya mapitio ya sera, mikakati na mipango kwa ajili ya uhuishaji wa masuala ya urejeshwaji; kuanzisha program za uhamasishaji wa jamii nchini kuhusu masuala ya urejeshwaji na hifadhi ya bioanuai; kuandaa mkakati wa ushirikiano kuwezesha ushirikishwaji wa taasisi mbalimbali washirika katika kupanga na kutekeleza urejeshwaji endelevu wa mifumo ikolojia na bioanuai katika ngazi ya kata; Ukusanyaji wa Taarifa za Tathmini ya Fursa na Mikakati ya Urejeshaji wa Mifumo-ikolojia (Resource and Opportunity Assessment Methodology -ROAM) katika eneo la mradi; kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 27 katika halmashauri zinazotekeleza mradi; kuwezesha vikundi vya jamii kuanzisha shughuli mbadala na rafiki kwa mazingira katika halmashauri saba (7); kuhamasisha na kuziwesha taasisi na jamii kutumia majiko banifu na nishati mbadala hususani zenye matumizi makubwa ya kuni na mkaa katika maeneo ya mradi; na kuwezesha makundi yenye mahitaji maalum kushiriki katika shughuli za Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira (SLR). Jumla ya shilingi bilioni 5.75 fedha za nje zimetengwa.

**(iii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi ili Kupunguza Hewa Ukaa Inayosababishwa na Ukataji Miti na Uharibifu wa Misitu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kupitia na kuandaa Nyenzo za Kisera (Policy Instrument)

kwa ajili ya utekelezaji wa Biashara ya Hewa Ukaa; kuwezesha wataala kushiriki Mkutano wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabinchi (COP 27); na kuwezesha Usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi. Jumla ya shilingi milioni 965 fedha za nje zimetengwa.

**(iv) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuwezesha wakulima na wafugaji kuanzisha na kuendesha mashamba darasa ya kilimo hifadhi na kinachohimili mabadiliko ya tabianchi; kuboresha nyanda za malisho na kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali; utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na mipango kazi ya jamii (community action plans) iliyoandaliwa chini ya mradi pamoja na uandaji na utoaji wa hatimiliki za kimila; uchimbaji na uendeshaji malambo saba (7) na mabwawa madogo sita (6); ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua, mabirika ya kunyweshea mifungo na majosho kwa ajili ya mifugo; kujenga uwezo kwa kamati za kijamii za watumia maji (Community-based Water Supply Organizations) ili kuifanya miradi ya maji kuwa endelevu baada ya mradi kumaliza muda wake; kukamilisha kazi ya tathmini ya hali ya afya ya udongo na mimea, uzalishaji wa hewa ukaa na kupunguza hewa ukaa kupitia utekelezaji wa shughuli za mradi; kuwezesha jamii kuwa na usimamizi endelevu wa rasilimali za maliasili kwa upandaji wa miti na hifadhi ya misitu ya asili yenye kunufaisha jamii kwa mazao timbao (kama vile mbao, nguzo na kuni) na mazao yasiyo timbao (kama vile ufugaji wa nyuki, matundapori na wanyamapori) katika maeneo ya mradi; na kutoa vitendea kazi kwa vikundi vya uzalishaji vya kilimo cha mwani, ufugaji nyuki, ufugaji wa kuku na usindikaji wa mazao. Jumla ya shilingi bilioni 2.75 fedha za nje zimetengwa.

**(v) Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kujenga uelewa wa jamii inayoishi kwenye Bonde la ziwa Nyasa juu ya usimamizi endelevu wa rasilimali za ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa; kutoa mafunzo kwa watumishi 60 wa Halmashauri za Wilaya za Mbinga, Ludewa, Nyasa, Makete na Kyela kuhusu upangaji shirikishi wa matumizi ya ardhi na usimamizi wa vyanzo vya maji kwenye maeneo yao; kutoa mafunzo kwa wakulima wa halmashauri za Mbinga, Ludewa, Nyasa, Makete na Kyela kuhusu kilimo cha misitu ki-biashara kwa lengo la kuwapatia shughuli za kuongeza kipato; kutoa mafunzo kwa jamii inayoishi kwenye bonde la ziwa Nyasa kuhusu uzalishaji wa mkaa wa kupikia kwa njia endelevu na jinsi ya kutengeneza majiko banifu ambayo hutumia kuni na mkaa kidogo katika kupikia kwa lengo la kupunguza kasi ya ukataji miti kwa ajili ya kupata nishati ya kuni na mkaa; kuwezesha jamii ya bonde la ziwa nyasa kuanzisha vikundi vya usimamizi endelevu wa rasilimali za maji, ili kuzuia uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa misitu kwenye eneo la bonde; kusaidia vikundi vya wanawake na vijana kufanya shughuli za ujasiriamali wa mazao ya kilimo kwa lengo la kuongeza kipato binafsi na kuboresha ustawi wa jamii kwa ujumla. Jumla ya shilingi milioni 736.97 fedha za nje zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kubaini transfoma zinazosadikiwa kuwa na kemikali aina ya PCBs kwa upande wa Zanzibari; kukamilisha Kanuni za udhibiti na usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu zitakazotumika kudhibiti na kusimamia kemikali hizo; kufanya ukarabati wa sehemu za muda za kuhifadhi mafuta (*temporary storage facility*) yatakayokusanywa ambayo yamebainika kuwa na kemikali aina ya PCBs kabla ya kusafirishwa kwa ajili ya kuteketezwa; kukusanya kuhifadhi na kuondosha mafuta yaliyobainika kuwa na kemikali aina ya PCB's kwa ajili ya kuteketezwa nchini Afrika ya Kusini; na kuandaa Mpango wa Kitaifa wa uondoshaji wa kemikali aina ya PCBs. Jumla ya shilingi milioni 369.28 fedha za nje zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomomonyoa Tabaka la Ozoni**

**Shughuli zitakazotekelezwani:**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuandaa warsha za kujenga uelewa kwa Jumuiya ya Mafundi Mchundo wa Viyoyozi na Majokofu wa Zanzibar (*Zanzibar Association for Refrigeration and Air Conditioning Technicians and Engineering (ZERATE)*; ukusanyaji wa takwimu za matumizi ya kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni; uandaaji na usambazi wa nyenzo za kuelemisha umma kuhusu kemikeli zinazomong'onyoa tabaka la ozoni; na kuandaa warsha ya mafunzo kwa vitendo kwa mafundi mchundo wanaohudumia majokofu na viyoyozi kuhusu njia bora za kuhudumia vifaa hivyo. Jumla ya shilingi milioni 94.77 fedha za nje zimetengwa.

**(d) Programu Na. 6571: Programu ya Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004**

Shughuli zitakazotekeleza ni: Kufanya Tathmini ya Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; Kuandaa mfumo mtandao wa utoaji wa vibali vya Tathmini ya Kimkakati wa Mazingira; Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka; Kuandaa Mpango Kazi wa Usimamizi wa Mazingira wa jiji la Dodoma; na ununuzi wa vifaa. Jumla ya shilingi milioni 826.74 fedha za nje zimetengwa.

### 4.3.5.7 Hifadhi ya Jamii

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii (2019/20 - 2022/23); kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Isiyo Rasmi; kuratibu maandalzi ya Kanzidata ya Walengwa wa Kinga Jamii *(Unified Social Register)*; na kukamilisha ya Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii. Jumla ya shilingi milioni 110.0 fedha za ndani na shilingi milioni 122.0 fedha za nje zimetengwa.

### 4.3.5.8 Usimamizi wa Maafa Nchini

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Maafa Waratibu wa Maafa katika Mikoa tisa; kufanya tathmini za vihatarishi vya majanga katika Mikoa minne ikiwemo maeneo yaliyo katika hatari kubwa ya kuathirika na Maafa; kufanya

tafiti na tathmini za majanga na kuandaa mipango ya kisekta ya usimamizi wa maafa; Kuandaa na kutekeleza mkakati wa utafutaji wa rasilimali kwa ajili kukabiliana na dharura za Maafa; Kuandaa mipango ya kuzuia na kujiandaa na maafa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati; Kutekeleza mpango wa kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya Maafa; kuandaa mipango ya kujiandaa na kukabiliana na maafa pamoja na mikakati ya kupunguza madhara katika Halmashauri 10 na kurejea mipango 20 ya Wilaya iliyopo; kuratibu maandalizi na kushiriki shughuli za usimamizi wa maafa Kikanda na Kimataifa; na Kuratibu shughuli za kuzuia, kujiandaa, kukabili na kurejesha hali baada ya maafa (Mfuko wa Maafa). Jumla ya shilingi bilioni 6.48 zimetengwa.

### 4.3.6 Kuendeleza Rasilimali Watu

**(a) Mradi Na. 6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi Nchini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya Utafiti wa Hali ya Rasilimaliwatu nchini (Manpower Survey) ili kupata takwimu za hali na mahitaji ya ujuzi nchini; kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi kwa vijana 14,784; kutoa mafunzo ya utarajali kwa wahitimu 9,000 wa vyuo vya elimu ya juu na kati ili kuwawezesha kupata uzoefu wa kazi na hatimaye kujiari au kuajirika; kutoa mafunzo ya kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kwa vijana 6,400; kuwezesha mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi 2,000 walio makazini katika sekta binafsi na ya umma kwa lengo la kuongeza tija na ubunifu; kutoa mafunzo kwa vijana 7,000 kuhusu kilimo cha kisasa kupitia teknolojia ya vitalu nyumba katika mikoa tisa (9); kutoa mafunzo ya ujuzi katika uchumi wa kijani kupitia kilimo cha vizimba (block farming) kwa vijana 2,000; kutoa mafunzo ya ujuzi wa teknolojia ya uchumi wa buluu katika sekta ya uvuvi kwa vijana 1,000; kutoa mafunzo ya ujuzi katika fani mbalimbali kupitia Vyuo vya Mafunzo na ufundi Stadi na Huduma za Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu kwa vijana 800; kukamilisha Mfumo wa Taarifa za Soko la ajira nchini ili kuwezesha kupatikana kwa taarifa sahihi na kwa wakati; na kuendelea kuratibu upatikanaji wa fursa za ajira nchini. Jumla ya shilingi bilioni 9.94 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mikopo kwa vikundi 100 vya vijana vya uzalishaji mali; kujenga uwezo wakopaji na wasimamizi wa Mfuko katika mikoa ya mitano (5) ya Dodoma, Kigoma, Shinyanga, Lindi na Kilimanjaro ili kuimarisha usimamizi wa Mfuko; na kukamilisha mandaalizi ya Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Jumla ya shilingi bilioni 1.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6205: Programu ya Taifa ya Kukuza Kazi za Staha**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: na Kukamilisha Mapitio ya Programu ya Kukuza Kazi za Staha; kufanya upembuzi wa Asasi na Mitandao inayojihusisha na masuala ya maendeleo ya vijana katika mikoa 26; kukamilisha Mfumo wa Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa vijana walio nje ya shule (Life Skills Framework); kutoa mafunzo ya stadi za maisha kwa waelimishaji rika 150 katika Halmashauri saba (7) Kasulu, Kahama, Chamwino, Ruhangwa, Tarime, Kisarawe na Makete wakiwemo Watu wenye Ulemavu, wanaoishi na VVU, Mama Wadogo na vijana kutoka Jamii ya Wafugaji ili kuwawezesha

kushiriki katika miradi ya kimkakati. Jumla ya shilingi bilioni 1.8 fedha za nje zimetengwa

### 4.3.7 Maeneo Mengine ya Kipaumbele

#### 4.3.7.1 Utamaduni, Sanaa na Michezo

**(a) Mradi Na. 6504: Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzika Wananchi**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza ujenzi wa vituo vya mazoezi na kupumzikia wananchi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Geita; kuanza hatua za awali za utambuzi wa maeneo ya michezo na mazoezi katika mji wa Serikali Dodoma; na kuratibu ujenzi wa *Arts na Sports Arena* katika Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. Jumla ya shilingi bilioni 10.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo wadau wa utamaduni na sanaa nchini; kuwaimarisha kimtaji wasaniii na kuwajengea utaalamu wa kuzalisha kazi bora za sanaa zinazomudu ushindani wa kitaifa na kimataifa; na kuuhabarisha umma kuhusu shughuli za Mfuko kupitia matukio mbalimbali. Jumla ya shilingi bilioni 3.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(c) Mradi Na. 6385: Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa madarasa matano (5), ujenzi wa hosteli ya wanafunzi, bwalo, bwawa la kuogelea, jengo la utawala pamoja na *gym*; ukarabati wa nyumba tatu (3); ujenzi wa kituo cha ukuzaji vipaji vya michezo (Centre of Sports Exellence) na miundombinu ya maji na mfumo wa umeme; na kuimarisha mipaka ya chuo kwa kuweka uzio katika maeneo yanayozunguka Chuo. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(d) Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kufanya utambuzi, ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa, masimulizi na nyaraka zinazohusu historia ya Ukombozi wa Afrika; kuendelea na ukarabati majengo yaliyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika ili yatumike kwa utalii na utafiti; kukamilisha ukarabati wa jengo lililotumiwa na Kamati ya Ukombozi ya O.A.U na kuanzisha Makumbusho ya kisasa kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika katika jengo hilo; kuandaa filamu kuhusu mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Afrika; na kuandaa Makongamano na maonesho kuhusu historia yaharakati za ukombozi wa Afrika. Jumla ya shilingi bilioni 7.3 zimetengwa.

**(e) Mradi Na. 4353: Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Ukarabati wa madarasa, maktaba, kumbi ikiwemo *Flexible Hall*, studio, miundombinu ya maji safi na taka Mabwenini, jengo la utawala; kununua vifaa vya studio ikijumuisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika teknolojia ya sauti, muziki, redio na televisheni, ubunifu na uzalishaji wa picha jongefu; kuimarisha mafunzo ya redio na televisheni; ujenzi wa uzio wa Chuo na jukwaa/eneo la maonyesho la nje na

vifaa vyake (*mobile/ outdoor stage)* pamoja na magari mawili ya kubebea vifaa. Jumla ya shilingi bilioni 5.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(f) Mradi Na. 6523: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukarabati vyumba viwili (2) vya mikutano; kukamilisha ukarabati wa uwanja wa ndani, kuweka taa za kuwezesha michezo na matukio kufanyika usiku katika Uwanja wa Uhuru; kuweka ubao mkubwa wa matokeo *(big screen score board*) na kamera za usalama katika Uwanja wa Uhuru; ukarabati wa mifumo ya zimamoto, usalama, umeme na maji na kuweka zulia jipya (*tatan*) la eneo la michezo wa riadha katika uwanja wa Benjamin Mkapa. Jumla ya shilingi bilioni 6.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(g) Mradi Na. 6503: Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuweka miundombinu na maandalizi ya eneo la kujenga uwanja; kukamilisha mikataba ya mkandarasi pamoja na mshauri elekezi, marejeo na uhakiki wa nyaraka za kitaalamu na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa uwanja huo. Jumla ya shilingi bilioni 4.5 fedha za ndani zimetengwa.

**(h) Mradi Na. 6260: Mfumo wa Leseni na Usajili wa Hakimiliki**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na usanifu wa mfumo wa usajili wa wabunifu na kazi za wabunifu; kuimarisha usimamizi wa hakimiliki; utoaji wa uthibitisho wa umiliki wa kazi *(copyright Clearance)*; kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ya uuzaji wa kazi za ubunifu hususan muziki, filamu na sanaa za ufundi, uwekaji wa miundombinu na mifumo ya mawasiliano ya TEHAMA na kuunganisha na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kupata taarifa za watumiaji wa kazi za Sanaa, kama BRELA, LATRA, TCRA, TRA kwa ajili ya kukusanya na kugawa mirabaha. Jumla ya shilingi bilioni 4.9 za ndani zimetengwa.

**(i) Mradi Na. 6355: Ujenzi wa Ukumbi wa Wazi (BASATA)**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuanza maandalizi ya ujenzi kituo cha utamaduni na sanaa katika eneo la Ilala Sharif Shamba Dar es Salaam ambalo ndani yake kutakuwa na *Culture and Arts Galleries*, studio na kumbi za kuendeshea shughuli za sanaa na utamaduni; kuanzisha maeneo maalumu ya kufanyia maonyesho na mazoezi ya sanaa na utamaduni kwa wasanii. Jumla ya shilingi bilioni 1.5 za ndani zimetengwa.

**(j) Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukiendeleza, kukikuza na kubidhaisha (kukiuza) Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni nje ya nchi katika Balozi 10 za Tanzana; kuwapata walimu wenye ujuzi; kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia; kusaidia ufundishaji wa Kiswahili katika nchi nyingine kupitia *diaspora*; kuzamisha wataalamu katika Jamii-Lugha ili kubobea katika lugha wanazohudumu; kuandaa na kuwezesha upatikanaji wa wafasiri na wakalimani wenye weledi katika mikutano ya Jumuiya za kimataifa pamoja na walimu wa Kiswahili kwa wageni; kuwezesha ukalimani wa lugha ya alama kwa kuwapa mafunzo pamoja na kuandaa machapisho mahususi ya lugha ya alama; kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa

ajili ya usajili wa wataalamu wa Kiswahili ndani na nje ya nchi; kufanya ukarabati katika majengo mawili (2) na kukarabati miundombinu ya kuendeshea mafunzo ya kuimarisha stadi za ukalimani, tafsiri, kiswahili kwa wageni na mafunzo ya wadau mbalimbali wa Kiswahili. Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

**(k) Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalum 56 za Michezo**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuimarisha miundombinu ya mazoezi, kujifunza, mafunzo na mashindano katika shule maalum 56 za michezo nchini ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya viwanja vya michezo na mazoezi katika mikoa mbalimbali ikiwemo viwanja maalumu (multi-purpose) vitakavyotumika kwa ajili ya mpira wa kikapu, wavu na pete; kuwapata walimu na wakufunzi wa michezo katika shule hizo; kuwaongezea uwezo wa kitaaluma katika michezo; kununua vifaa na nyenzo za kujifunzia, kufundishia na mafunzo na kufanya ufuatiliaji na tathmini. Jumla ya shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.7.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**(a) Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Balozini**

Shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi na kitega uchumi katika kiwanja cha Ubalozi za Tanzania, Kinshasa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo); kuendelea na ujenzi wa jengo la ofisi na makazi ya Balozi katika kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania, Muscat (Oman); kuendelea na ujenzi wa makazi ya Balozi katika kiwanja cha Ubalozi wa Tanzania, Addis Ababa (Ethiopia); kuendelea na ujenzi wa ofisi na kitega uchumi katika kiwanja cha ubalozi wa Tanzania, Nairobi (Kenya); kuendelea na ujenzi wa jengo la makazi ya Balozi wa Tanzania, Moroni (Comoro); kuanza ujenzi wa jengo la ofisi na makazi katika kiwanja cha Ubalozi za Tanzania, Abuja (Nigeria); ukarabati wa ofisi na makazi ya Balozi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, New York (Marekani); ukarabati wa makazi ya Balozi, Geneva (Switzerland); ukarabati wa ofisi na makazi ya Balozi Rome (Italy); ukarabati wa jengo la ghorofa 3 kwa ajili ya ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania, Beijing (China); ujenzi wa ofisi na makazi ya Balozi wa Tanzania, Riyadh (Saudi Arabia); ukarabati wa ofisi, nyumba za watumishi na makazi ya balozi wa Tanzania na ujenzi wa kitega uchumi Ubalozi wa Tanzania, London (Uingereza); Ukarabati wa Makazi ya Balozi wa Tanzania, Harare (Zimbabwe), Ukarabati wa jengo la Ofisi, Makazi ya Balozi na Makazi ya Mkuu wa Utawala Ubalozi wa Tanzania, Pretoria (Afrika ya Kusini); usanifu wa jengo la ofisi na kitega uchumi, Kampala (Uganda); na kuanza ujenzi wa jengo la kudumu la mahakama ya haki za binadamu, Arusha (Tanzania). Jumla ya shilingi bilioni 56.9 fedha za ndani zimetengwa.

**(b) Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi**

**Upanuzi na Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia**

Shughuli zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa vyumba tisa (9) vya mihadhara

katika Chuo cha Diplomasia, Kurasini Dar es Salaam.  Jumla ya shilingi bilioni 4.0 fedha za ndani zimetengwa.

#### 4.3.7.3 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

(i) Ununuzi wa Mbia wa Miradi ya Ujenzi wa Viwanda vya Dawa Muhimu na Vifaa Tiba itakayotekelezwa chini ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) katika Mikoa ya Pwani, Mwanza na Mbeya;

(ii) Ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu kwenye mradi wa Usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza;

(iii) Ununuzi wa Mbia wa miradi ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Nne na Jengo la Biashara" Biashara "Commercial complex katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

(iv) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa mradi wa Kusambaza Gesi Asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara;

(v) Kukamilisha ununuzi wa Mshauri Elekezi atakayetayarisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi wa ujenzi wa reli ya standard gauge ya Tanga – Arusha – Musoma pamoja na matawi ya Engaruka na Minjingu kwa utaratibu wa PPP;

(vi) Kukamilisha ununuzi wa Mshauri Elekezi atakayetayarisha taarifa ya upembuzi yakinifu ya mradi wa ujenzi wa reli ya *standard gauge* ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa utaratibu wa PPP;

(vii) Kukamilisha upembuzi yakinifu na kuingia katika hatua ya ununuzi wa mbia wa Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi za Dodoma na Dar es Salaam;

(viii) Kuendelea na hatua ya maandalizi ya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Kampasi za Dar es Salaam na Mbeya; na

(ix) Ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza simu za mkononi chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

# SURA YA TANO

## UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2022/23

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 kama vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Aidha, sura hii imeainisha mikakati ambayo Serikali itachukua ili kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vilivyoainishwa vinafikia malengo yanayotarajiwa.

### 5.2 Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2022/23

Katika mwaka 2022/23 jumla ya shilingi bilioni 15,521.3 zinatarajiwa kugharamia shughuli za maendeleo, sawa na asilimia 37.8 ya bajeti yote. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12,122.1 sawa na asilimia 78.1 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,399.2 sawa na asilimia 21.9 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje.

### 5.3 Mikakati ya Vyanzo vya Mapato ya Kugharamia Mpango kwa Mwaka 2022/23

Mikakati ya vyanzo vitakavyotumika kugharamia miradi ya maendeleo ni pamoja na mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, mikopo na misaada pamoja na vyanzo mbadala na bunifu.

#### 5.3.1 Mapato ya Ndani

##### 5.3.1.1 Mapato ya Kodi na Yasiyo Kodi

Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali vya ndani ili kuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wanunuzi kuchukua risiti wanaponunua bidhaa;

(ii) Kuendelea na kampeni mbalimbali za kutoa elimu kwa mlipakodi kupitia runinga, redio, mitandao ya kijamii na semina;

(iii) Kupanua wigo wa kodi kwa kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi kupitia kampeni ya Mlango kwa Mlango;

(iv) Kuendelea kutumia Mpango wa Usimamizi wa Viashiria Hatarishi (Compliance Risk Management Plan) ili kubaini na kutambua wakwepaji wa kodi;

(v) Kuendelea kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa mipaka yote kwa kuongeza ushirikiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na vyombo vya ulinzi na usalama nchini ili kudhibiti bidhaa za magendo na kupunguza tatizo la ukwepaji wa kodi;

(vi) Kuimarisha mazingira rafiki ya ulipaji kodi kwa hiari kwa kuboresha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mifumo

itakayosaidia na kurahisisha ulipaji kodi;

(vii) Kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kuijumuisha kwenye mfumo rasmi wa ulipaji kodi;

(viii) Kurasimisha shughuli zisizo rasmi, zikiwemo shughuli za wajasiriamali wadogo kwa kuwatengea maeneo maalum na kuwapatia vitambulisho vilivyoboreshwa kwa kuwekewa taarifa sahihi ili kutambua shughuli zao za kiuchumi;

(ix) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wapya, kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi utakaowezesha kuongeza wigo wa kodi;

(x) Kufanya tafiti katika maeneo mapya ambayo yanaweza kutozwa kodi;

(xi) Kuimarisha usimamizi wa tozo na ada mbalimbali ili kuhakikisha zinakusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali;

(xii) Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kufuatilia Mizigo inayokwenda nchi jirani (Eletronic Cargo Tracking System) ili kuimarisha uwezo wa usimamizi wa mizigo inayopita kwenda nchi jirani;

(xiii) Kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway- GePG) ili kurahisisha ulipaji na kudhibiti upotevu wa mapato;

(xiv) Kuimarisha mfumo wa Dirisha Moja la Kielekroniki la Uondoshaji wa Mizigo Bandarini (e-Single Window System) ili kurahisisha uondoshwaji wa mizigo katika vituo vya mipakani pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;

(xv) Kuimarisha na kufungamanisha mfumo mkubwa wa kodi za ndani wa Domestic Revenue Administration System (IDRAS) utakaounganisha mifumo yote ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Serikali ili kuimarisha usimamizi wa mapato yatokanayo na kodi za ndani nchini; na

(xvi) Kuboresha Mfumo wa mawasiliano kati ya NIDA na TRA kwa kuhahikisha kuwa kila raia mwenye namba ya NIDA anaunganishwa na mfumo wa utambulisho wa mlipa kodi (TIN).

### 5.3.2 Mikopo na Misaada ya Nje

#### 5.3.2.1 Misaada ya Nje

Serikali inaendelea kuimarisha mahusiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework - DCF) ili kuhakikisha fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinaendelea kupatikana kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali. Katika hatua nyingine, Serikali imeanza maandalizi ya kufanya tathmini na mapitio ya Mwongozo wa Ushirikiano ili uweze kuendana na hali ya sasa ya dunia katika masuala ya diplomasia ya uchumi na maendeleo. Mapitio hayo, yatazingatia mwenendo na vipaumbele vya Washirika wa Maendeleo pamoja na fursa nyingine zinazoibuka kutokana na mabadiliko mbalimbali duniani.

Tathmini na mapitio ya Mwongozo wa Ushirikiano, itasaidia kuliweka Taifa katika nafasi ya kimkakati ili kunufaika zaidi na fursa zilizopo kwa makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali, Sekta binafsi pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali katika masuala ya

ushirikiano wa kimataifa. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika utekelezaji wa miradi hiyo na hatimae kupata matokeo yaliyokusudiwa.

#### 5.3.2.2 Mikopo ya Nje

Kupitia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (DCF), Serikali itahakikisha mikopo nafuu inapatikana kama ilivyopangwa. Aidha, Serikali itaendelea kuzingatia Mkakati wa Usimamizi wa Madeni katika Muda wa Kati wa mwaka 2021/22-2023/24 (Medium Term Debt Management Strategy – MTDS) kwa kukopa zaidi kwenye mikopo yenye masharti ya kati kwa utaratibu wa *Export Credit Agency* (ECA), kwa lengo la kuziba pengo litokanalo na kupungua kwa mikopo ya masharti nafuu. Vile vile, Serikali itaendelea kukopa katika vyanzo vya mikopo ya masharti ya kibiashara. Mikopo hii itaelekezwa katika miradi ya kipaumbele yenye kuchochea ukuaji wa uchumi na mauzo ya nje. Hatua nyingine inayochukuliwa na Serikali ni kukamilisha zoezi la Tathmini na Ukadiriaji wa Kukopesheka kwa Nchi (Sovereign Credit Rating) ili kuongeza wigo wa wakopeshaji hususan katika masoko ya mitaji ya kimataifa (International Capital Market).

### 5.3.3 Mikopo ya Ndani

Ili kugharamia miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani kupitia hatifungani za Serikali kwa kuzingatia Mkakati wa Muda wa kati wa Usimamizi wa Madeni wa mwaka 2021/22 - 2023/24 ambao pamoja na masuala mengine, unasaidia maendeleo ya soko la fedha la ndani. Hatifungani zitakazotumika katika ugharamiaji wa kutekeleza miradi ya maendeleo ni miaka miwili (2), mitano (5), saba (7), kumi (10), kumi na tano (15), ishirini (20) na ishirini na tano (25). Aidha, Serikali itaendelea kutoa elimu na uhamasishaji kwa umma juu ya ushiriki katika soko la awali na upili la dhamana za Serikali.

## 5.4 Vyanzo Mbadala na Bunifu vya Kugharamia Miradi ya Maendeleo

Kwa kutambua uwepo wa pengo la rasilimali fedha zinazohitajika katika kufikia shabaha ya maendeleo tuliyojiwekea, Serikali imeainisha vyanzo mbadala na bunifu katika Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano sanjari na Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa mwaka 2020/21-2029/30. Katika kufikia azma hiyo, Serikali itafanya maboresho ya sheria mbalimbali pamoja na kuweka miongozo itakayowezesha kunufaika na vyanzo mbadala na bunifu katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Baadhi ya vyanzo vitakavyopewa kipaumbele ni pamoja na Hatifungani za Halmashauri (Municipal Bond) kwa ajili ya kugharamia miradi ya kimkakati katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; Hatifungani ya Miundombinu (Infrastructure Bond); Hatifungani ya Buluu (Blue Bond); Hatifungani za Makampuni (Corporate Bond); Dhamana za Muda wa Kati; Hatifungani ya Mazingira (Green Bond); Hatifungani ya Kiislam (SUKUK); *Micro-Saving Bond* na *Lease Financing*; matumizi ya fedha kupata mitaji ya muda mrefu kupitia utaratibu wa *syndication*; bima na ugharamiaji hatarishi (risk financing) na ushiriki wa sekta binafsi kwa kugharamia maendeleo kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na utaratibu wa miradi ya pamoja (JV).

Serikali itaendelea kuchukua hatua mahsusi kwa kuwekeza kwenye rasilimali watu na kuwaongezea ujuzi watumishi katika taasisi mbalimbali zinazotekeleza miradi ya maendeleo. Programu za kuwajengea uwezo watumishi zitakuwa katika maeneo ya uibuaji, uandaaji na usimamizi wa miradi. Hatua hizi zinatarajia kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa miradi mipya na inayoendelea.

# SURA YA SITA

## UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

### 6.1 Utangulizi

Katika kuhakikisha kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/23 unafikia malengo yaliyoainishwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali, Wizara ya Fedha na Mipango itaratibu na kusimamia ufuatiliaji na tathmini (U&T). Ufuatiliaji na Tathmini ni nyenzo muhimu katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati kwa ajili ya uandaaji wa mipango, bajeti, mikakati na sera. Taarifa za U&T pia zitawawezesha wafanya maamuzi na wadau mbalimbali kupata taarifa sahihi kwa ajili ya kufanya maamuzi. Aidha, taarifa za U&T zitatoa mrejesho wa utekelezaji unaowezesha kufanya maboresho wakati wa utekelezaji wa miradi, kubaini miradi yenye tija na mafanikio makubwa na kuwezesha kufanya maamuzi ya kuongeza wigo wa utekelezaji wake. Msingi mkuu wa U&T ni kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa miradi kwa thamani halisi ya fedha kwa ajili ya matokeo makubwa ya kukuza uchumi na kuwa nchi ya uchumi wa kati wa juu, kuondoa umaskini na kuleta ustawi bora wa maisha kwa wote.

Katika mwaka 2022/23, miongozo itakayozingatiwa katika U&T ni pamoja na: Sheria ya Bajeti, Sura 439, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo *(National Monitoring and Evaluation Framework)*; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23; Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha; na Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti.

### 6.2 Misingi ya Ufuatiliaji na Tathmini

Ili kufikia malengo yaliyobainishwa katika utekelezaji wa miradi na uratibu wa ufuatiliaji na tathmini, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zina wajibu wa kuzingatia misingi ifuatayo katika upangaji na utekelezaji wa ufuatiliaji na tathmini wa mipango, miradi na programu za maendeleo.

(i) **Uwezo wa Rasilimali Watu katika Ufuatiliaji na Tathmini:** Kila taasisi itabainisha mahitaji ya idadi ya rasilimali watu, uwezo wa kutekeleza ufuatiliaji, tathmini, uchambuzi na utoaji taarifa. Aidha, katika maeneo yenye upungufu, Serikali itaajiri wataalamu stahiki na kuendelea kujenga uwezo wa wataalamu.

(ii) **Upatikanaji wa Rasilimali Fedha na Vitendea Kazi:** Wakati wa uandaaji wa miradi, taasisi zitatenga bajeti inayoakisi mahitaji ya kifedha na vitendea kazi kama vile magari, vifaa vya TEHAMA n.k, katika eneo la ufuatiliaji na tathmini ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa bora na kwa wakati hivyo kuleta ufanisi na tija katika utekelezaji wa miradi.

(iii) **Ushirikishwaji wa Wadau wote Muhimu:** Taasisi zitabainisha wadau wote muhimu katika ufuatiliaji na tathmini na kuwashirikisha katika hatua zote za upangaji, uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini na uandaaji wa taarifa kwa lengo la kuoanisha utekelezaji wa miradi.

(iv) **Uwajibikaji:** Baada ya taarifa za U&T kubainisha changamoto na kasoro mbalimbali, taasisi zitachukua hatua stahiki kwa wakati za kurekebisha kasoro.

(v) **Kuoanisha na Kuunganisha Mifumo na Nyenzo za Kukusanya Taarifa:** Ili kuwa na takwimu na taarifa zinazowiana, taasisi zitahakikisha kuwa mifumo na nyenzo zinaoana ili kutoa taarifa bora na kwa wakati. Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kutoa mafunzo ya kuhakikisha kuwa mifumo ya U&T katika Wizara na Taasisi za Umma ina uwezo wa kubadilishana taarifa na Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS).

### 6.3 Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23

Kwa mwaka 2022/23, mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo zitajikita katika:

(i) **Udhibiti:** Hii itajumuisha usimamizi wa matumizi ya rasilimali, mifumo ya udhibiti wa kifedha, ununuzi na rasilimali watu. Mbinu hii itatumia mifumo iliyopo ya udhibiti fedha na taarifa za ukaguzi wa ndani;
(ii) **Ufuatiliaji:** Ufuatiliaji utafanyika kwa kuzingatia mpangokazi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mtiririko wa mahitaji ya fedha;
(iii) **Matumizi ya Viashiria:** mbinu hii itajikita katika uchambuzi wa viashiria (viashiria tendeshi na viashiria vya matokeo) kwa kulinganisha mipangokazi, taarifa za utekelezaji na hali halisi ya utekelezaji wa miradi;
(iv) **Uratibu:** Kuhimiza uratibu na ushirikishaji wa wadau katika nyanja zote za utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
(v) **Kuimarisha Taasisi za U&T**: Kujenga uwezo wa wataalamu wa U&T, vitengo na ofisi zinazohusika na U&T kwa kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi na fedha kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika ngazi zote; na
(vi) **Tathmini:** kufanya tathmini ya miradi ili kubaini iwapo matokeo ya miradi yamekidhi malengo ya miradi husika.

### 6.4 Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini ni pamoja na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitakazobainisha mafanikio, changamoto na fursa katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mpango. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitaandaliwa na kuwasilishwa kwa wapangaji, watekelezaji na Wafanya Maamuzi katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kutatua kwa wakati changamoto zitakazobainishwa. Aidha, vikao vya mrejesho vitafanyika katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyoabainishwa.

## 6.5 Muundo wa Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Taarifa za Ufuatiliaji na tathmini zitazingatia miundo ya taarifa iliyoainishwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini. Aidha, Taarifa za utekelezaji zitaandaliwa katika kipindi cha kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima.

## 6.6 Mgawanyo wa Majukumu

Wadau muhimu watashirikishwa katika kufanikisha zoezi la ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla. Mgawanyo wa majukumu ya wadau utakuwa kama ifuatavyo:

### 6.6.1 Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu (IMTC)

Kamati hii inaundwa na Makatibu Wakuu na ni chombo cha juu cha kupokea taarifa za utekekelezaji wa mipango na miradi ya maendeleo. Taarifa za U&T zinazowasilishwa katika Kamati hii maalumu katika kipindi cha nusu mwaka na mwaka zitajadiliwa na kufanyiwa maamuzi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kwa taasisi zinazotekeleza na kusimamia miradi.

### 6.6.2 Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango ina majukumu yafuatayo: kufanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ya kielelezo na kimkakati inayotekelezwa na Serikali au Sekta Binafsi; kupokea taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji wa miradi kutoka katika Sekta na Taasisi mbalimbali; kupokea na kuchambua taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kupitia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (National Projects Management Information System – NPMIS); kubainisha maeneo ya kuboresha ya utekelezaji wa miradi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa; na kuandaa na kutoa taarifa ya nusu mwaka na ya mwaka ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuiwasilisha katika Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu.

### 6.6.3 Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kuandaa na kutoa miongozo mbalimbali ya ukusanyaji, uchambuzi na uchakataji wa takwimu za viashiria vinavyosaidia katika ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Mpango. Miongozo hiyo itapaswa kuzingatiwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi wakati wa kuandaa taarifa za kitakwimu za mwenendo na matokeo ya utekelezaji wa Mpango. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itajenga uwezo kwa wadau katika kukusanya, kuchambua, kuchakata, kuandaa na kutoa taarifa za kitakwimu za utekelezaji wa Mpango na miradi ya maendeleo.

### 6.6.4 Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma

Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma

zitawajibika kuaandaa Mpango Kazi wa U&T, kufanya U&T pamoja na kuandaa taarifa za U&T kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima. Mpango Kazi na taarifa za utekelezaji zitawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kupitia mfumo wa NPMIS kwa ajili ya uchambuzi na ushauri. Aidha, kila Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma inapaswa kutenga rasilimali fedha na kuvijengea uwezo Vitengo vya Ufuatiliaji na Tathmini ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

### 6.6.5 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM)

Ofisi ya Rais – TAMISEMI itaratibu na kutoa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawajibika kuandaa Mpango Kazi wa ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo Ofisi ya Rais- TAMISEMI katika kipindi cha kila robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima. Aidha, Mamlaka za Serikali ya Mitaa zitakusanya taarifa za ufuatiliaji kutoka katika Kamati za Maendeleo za Kata ambazo zitachambua taarifa mbalimbali kutoka katika Kamati za Maendeleo za Vijiji na Mitaa na kuziwasilisha katika Sekretarieti za Mikoa. Ofisi ya Rais - TAMISEMI itachambua na kuandaa taarifa jumuishi na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mfumo wa NPMIS.

### 6.6.6 Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia

Wizara ya Fedha na Mipango kama mratibu wa U&T itaendelea kushirikiana na Taasisi za sekta binafsi kupitia uratibu wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) na Asasi za Kiraia kupitia Baraza la Taifa la Asasi Zisizo za Serikali (NaCoNGO). Aidha, TNBC kupitia miamvuli ya taasisi zake ikiwemo TPSF, CTI na TCCIA itawasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa muhimu za uwekezaji wa Sekta Binafsi ikibainisha thamani ya uwekezaji uliofanywa na kuwasilisha utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Maendeleo. Taarifa hizo zitajielekeza katika kufanya mapitio ya mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji hivyo kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa Mpango. Vile vile, Asasi za kiraia zitawasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zao Baraza la Taifa la Asasi Zisizo za Serikali (NaCoNGO) kwa ajili ya majumuisho. Wizara ya Fedha na Mipango itapokea na kuchambua taarifa zilizowasilishwa kutoka TNBC na NaCoNGO ili kuweza kubaini mchango wa sekta hizi katika utekeleza wa miradi ya maendeleo.

## SURA YA SABA

## VIHATARISHI NA HATUA ZA KUKABILIANA NAVYO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 pamoja na kupendekeza mikakati ya kukabiliana navyo. Vihatarishi hivyo vinaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama na kutokalimika kwa wakati kwa utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika Mpango. Katika kuhakikisha Mpango unatekelezwa kwa mafanikio, Serikali kwa kuzingatia Mwongozo wa Kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma wa mwaka 2012 itachukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na vihatarishi hivyo vilivyogawanyika katika makundi makuu mawili (2) ambayo ni vihatarishi vya ndani na nje.

### 7.2 Vihatarishi vya Ndani na Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

**Vihatarishi vya Ndani** vilivyoainishwa ni pamoja na: Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika mipango ya maendeleo; upotevu wa mapato ya Serikali kupitia biashara mtandao; mabadiliko ya Viwango vya Riba; uharibifu wa Mazingira; rushwa; na uhalifu wa kimtandao. Udhibiti wa vihatarishi hivi upo ndani ya uwezo wa Serikali.

**Vihatarishi vya Nje** vilivyoainishwa ni pamoja na: Majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko; mitikisiko ya Kiuchumi duniani; mabadiliko ya kisiasa ya ndani na nje; mabadiliko ya Tabianchi; kubadilika kwa teknolojia; na Kutopatikana kwa Misaada na Mikopo kwa wakati. Udhibiti wa vihatarishi hivi upo nje ya uwezo wa Serikali katika utekelezaji wa Mpango.

Maelezo ya kina ya vihatarishi vya ndani na nje na hatua za kukabiliana navyo yameainishwa katika **Jedwali Na. 7.2 (a)** na **Jedwali Na. 7.2 (b)**

**Jedwali 7.2 (a): Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| 1. | Ufinyu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | (i) Kasi ndogo katika utekelezaji wa miradi na hivyo kutokamilika kwa wakati<br>(ii) Kuongezeka kwa gharama za miradi<br>(iii) Kuchelewa kwa upatikanaji wa huduma zilizotarajiwa | (i) Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa kodi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti za kielektroniki wanapouza bidhaa na wanunuzi kuchukua risiti wanaponunua bidhaa<br>(ii) Kuhamasisha ulipaji kodi katika sekta isiyo rasmi kwa kuijumuisha kwenye |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | | mfumo rasmi wa ulipaji kodi<br>(iii) Kuendelea kusimamia Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway-GePG) ili kurahisisha ulipaji na kudhibiti upotevu wa mapato<br>(iv) Kuweka msisitizo wa kipekee kwa sekta binafsi kushiriki kwenye maeneo yanayovutia uwekezaji wa sekta hiyo kupitia miradi ya pamoja (JV) na miradi ya ubia (PPP)<br>(v) Kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati yenye kuongeza mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa<br>(vi) Kuimarisha sekta ya fedha na Kuendeleza soko la fedha la ndani (domestic debt market) ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo<br>(vii) Kupata fedha kupitia mikopo yenye masharti nafuu na mikopo ya kibiashara<br>(viii) Matumizi ya Vyanzo Mbadala na Bunifu. |
| 2. | Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika mipango ya maendeleo | (i) Uwekezaji mdogo wa Sekta binafsi katika miradi ya kimkakati<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi kutokana na uhaba wa mitaji teknolojia na mazingira duni ya | (i) Kufanya majadiliano na Sekta binafsi ili kuweka mikakati ya kutatua changaamoto zinazowakabili<br>(ii) Kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ya |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | kufanya biashara | biashara ili kuvutia uwekezaji katika maeneo yanayofaa kwa Sekta binafsi<br>(iii) Kutenga fedha katika Mfuko wa Uwezeshaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuwezesha taasisi za Serikali kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi ya PPP na kuiuza kwa Sekta Binafsi kwa ajili ya uwekezaji |
| 3. | Kupotea kwa mapato ya Serikali kupitia biashara mtandao | (i) Kupungua kwa mapato ya Serikali<br>(ii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo | (i) Serikali kuandaa Mkakati wa kuwezesha utozaji kodi katika uchumi wa Kidigitali<br>(ii) Kupitia mifumo ya kisheria iliyopo ili kudhibiti upotevu wa mapato yatokanayo na biashara mtandao<br>(iii) Kuongeza na kuimarisha uwekezaji katika TEHAMA. |
| 4. | Mabadiliko ya Viwango vya Riba | (i) Kuongezeka kwa matumizi ya malipo ya riba na nakisi ya bajeti;<br>(ii) Serikali kutumia fedha kutoka kwenye vifungu vingine vya bajeti kugharamia malipo ya riba; na<br>(iii) Sekta binafsi kutofikia malengo ya mikopo na hivyo kupungua kwa shughuli za kiuchumi na kusababisha Serikali kukosa mapato. | (i) Kuendelea kutekeleza Sera zitakazowezesha viwango vya riba kuwa himilivu;<br>(ii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kudhibiti matumizi ili kupunguza utegemezi katika misaada na mikopo kutoka nje; na<br>(iii) Kuendeleza soko la fedha la ndani. |
| 5. | Uharibifu wa Mazingira. | (i) Kubadilika kwa hali hewa na kusababisha uharibifu wa miundombinu kutokana | (i) Kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira ili |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | na mvua nyingi;<br>(ii) Kutoweka kwa bioanuai;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za utoaji wa huduma za afya kutokana na kuongezeka kwa magonjwa yanayotokana na uharibifu wa mazingira;<br>(iv) Kuongezeka kwa gharama za kurejesha mazingira katika hali ya awali na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa; na<br>(v) Kupungua kwa uzalishaji wa mazao na bidhaa viwandani. | kuthibiti uharibifu wa miundombinu unaotokana na uharibifu wa mazingira;<br>(ii) Kutunza na kurejesha uoto wa asili na bioanuai;<br>(iii) Kuendelea kuimarisha kamati za usimamizi wa mazingira katika maeneo ya vyanzo vya maji na misitu ili kudhibiti athari za uchafuzi wa mazingira<br>(iv) Kusimamia miongozo na kanuni za usimamizi wa mazingira; na<br>(v) Kuhamasisha wananchi kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. |
| 6. | Rushwa | (i) Upotevu wa fedha za umma;<br>(ii) Miradi kutekelezwa bila kuzingatia ubora;<br>(iii) Kuongezeka kwa muda na gharama za utekelezaji wa miradi; na<br>(iv) Kasi ndogo ya ukuaji wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya Maendeleo. | (i) Kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa;<br>(ii) Kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya miradi;<br>(iii) Kuendelea kuchukua hatua za kisheria kwa wanaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa;<br>(iv) Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na yenye uwazi ili kuruhusu sekta binafsi kushamiri na kurasimisha sekta isiyo rasmi; na<br>(v) Kuimarisha mfumo wa utoaji motisha kwa watoaji taarifa zinazohusiana na rushwa. |
| 7. | Uhalifu wa kimtandao | (i) Kuharibiwa kwa mifumo ya kielektroniki ya Serikali; na<br>(ii) Upotevu wa mapato. | (i) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya taarifa ya kielektroniki ya |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | | Serikali;<br>(ii) Serikali kuendelea kuimarisha maeneo ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali (Data recovery sites); na<br>(iii) Kusimamia utekelezaji wa sera ya udhibiti wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha za umma. |

**Jedwali 7.2 (b): Vihatarishi vya Nje na Hatua za Kukabiliana Navyo**

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| 1. | Majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko | (i) Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi;<br>(ii) Kuathiri mapato ikiwemo mapato ya kodi yatokanayo na kipato; na<br>(iii) Kuelekezwa raslimali fedha katika kukabiliana na majanga na magonjwa ya mlipuko badala ya kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo kama ilivyokusudiwa. | (i) Kuboresha mifumo ya kuzuia na kukabiliana na majanga; na<br>(ii) Kufanya mapitio ya utekelezaji wa miradi ili kukabiliana na athari zilizojitokeza. |
| 2. | Mitikisiko ya Kiuchumi duniani | (i) Kupungua kwa mikopo kutoka nje na fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;<br>(ii) Kupungua kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi;<br>(iii) Kupungua kwa akiba ya fedha za kigeni;<br>(iv) Kupungua kwa uwekezaji kutoka nje ya nchi; na<br>(v) Kuongezeka kwa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia zikiwemo bidhaa za petroli, malighafi za viwandani, pembejeo na | (i) Serikali kuandaa mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi yanayoweza kutokea duniani;<br>(ii) Serikali kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana ndani ya nchi na kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini;<br>(iii) Kuongeza akiba ya bidhaa za petrol, na<br>(iv) Kuimarisha ubora wa |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | vifaa vya ujenzi | bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuhimili ushindani katika masoko ya kimataifa. |
| 3. | Migogoro na hali ya siasa isiyo imara katika maeneo mbalimbali ikiwemo nchi jirani, kikanda na kimataifa. | (i) Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi hususan inayotumia vifaa kutoka nje;<br>(ii) Kupungua kwa uwekezaji wa mitaji ya kigeni ya moja kwa moja;<br>(iii) Kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu katika soko la dunia kama mafuta, mashine na mitambo;<br>(iv) Kupungua kwa mikopo na misaada kutoka nje; na<br>(v) Kukosekana kwa masoko nje ya nchi kwa ajili ya kuuza bidhaa zinazozalishwa nchini. | (i) Kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje;<br>(ii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano kupitia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ili kuzuia matukio yanayoweza kuhatarisha amani kikanda na kimataifa;<br>(iii) Kujenga uwezo wa nchi kushiriki katika majadiliano ya kikanda na kimataifa kwa lengo la kupunguza athari za migogoro itokanayo na kuyumba kwa ushirikiano kati ya nchi na nchi; na<br>(iv) Kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi jirani na kikanda ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani. |
| 4. | Mabadiliko ya Tabia nchi | (i) Kupungua kwa uzalishaji wa mazao na bidhaa viwandani;<br>(ii) Kuongezeka kwa gharama za uzalishaji;<br>(iii) Kuongezeka kwa mfumuko wa bei; na | (i) Kuimarisha mbinu za kukabiliana na kuendana na mabadiliko ya tabianchi;<br>(ii) Kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa kuhusu utunzaji wa |

| NA. | KIHATARISHI | ATHARI | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|---|---|
| | | (iv) Kuathiri ikolojia | mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; na<br>(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021. |
| 5. | Kubadilika kwa teknolojia | (i) Mifumo ya kisheria, kisera, na kitaasisi iliyopo kutoendana na mabadiliko ya teknolojia;<br>(ii) Uhitaji wa zana zinazoendana na teknolojia mpya na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi;<br>(iii) Kuongezeka kwa gharama za uwekezaji katika mifumo ya teknolojia mpya; na<br>(iv) Kupungua kwa uwezo wa kiushindani katika soko la kikanda na kimataifa. | (i) Kuendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya teknolojia; na<br>(ii) Kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani. |

**Kiambatisho I: Miradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2021/22**

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Kilimo | Kudhibiti Sumukuvu – Halmashauri ya Wilaya ya Nzega | Tabora |
| 2. | Elimu | Ukarabati wa Jengo la Maktaba ya Mkoa wa Tabora | Tabora |
| 3. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Ipole - Koga - Mpanda (Km 365.98) | Tabora |
| 4. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Nyahua – Chaya (Km 170), Kipande cha Nyahua - Chaya (Km 85.4) | Tabora |
| 5. | Uchukuzi | Ukarabati Wa Majengo ya Mamlaka ya Hali ya Hewa, Tabora | Tabora |
| 6. | Viwanda | Ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata na Kufungasha Mazao ya Nyuki – Sikonge | Tabora |
| 7. | Ujenzi | Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Tabora | Tabora |
| 8. | Maji | Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Mkoa Wa Kigoma | Kigoma |
| 9. | Uchukuzi | Uboreshaji wa Bandari-Ziwa Tanganyika (Kigoma) | Kigoma |
| 10. | Afya | Ujenzi wa Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Wa Kigoma | Kigoma |
| 11. | Utawala Bora | Uimarishaji wa Mashamba ya Magereza | Kigoma |
| 12. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Kabingo - Kasulu - Manyovu (Km 260.6) | Kigoma |
| 13. | Ujenzi | Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kigoma | Kigoma |
| 14. | Nishati | Kuzalisha Nishati Jadidifu Kigoma | Kigoma |
| 15. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza -Kaliua – Tabora (Km 389.7) | Kigoma |
| 16. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma – Kagera | Kagera |
| 17. | Viwanda | Uendelezaji wa Miundombinu ya SIDO – Bukoba | Kagera |
| 18. | Afya | Ujenzi wa Jengo la Mionzi Katika Kituo cha Afya cha Zamzam | Kagera |
| 19. | Ujenzi | Ujenzi wa Daraja la Kitengule | Kagera |
| 20. | Afya | Ukarabati wa Chuo cha Afya Kagemu | Kagera |
| 21. | Elimu | Ukarabati wa Maktaba Kuu ya Mkoa Wa Kagera | Kagera |
| 22. | Uvuvi | Kujenga Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Rubambagwe – Chato | Geita |
| 23. | Ujenzi | Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Geita – Chato | Geita |
| 24. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) – Chato | Geita |
| 25. | Viwanda | Uendelezaji wa Miundombinu ya SIDO – Geita | Geita |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 26. | Utawala Bora | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa – Geita | Geita |
| 27. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkoa ya Uhamiaji – Geita | Geita |
| 28. | Afya | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita | Geita |
| 29. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Askari Tanzania | Geita |
| 30. | Madini | Kituo cha Mfano cha Uchenjuaji Madini ya Dhahabu kwa ajili ya Wachimbaji Wadogo – Lwamgasa. | Geita |
| 31. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya – Nansio (km 121.9) | Mara |
| 32. | Afya | Mradi wa kuboresha Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara – Kwangwa | Mara |
| 33. | Elimu | Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (EP4R) | Mara |
| 34. | Elimu | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) cha Wilaya ya Butiama kupitia programu ya ESPJ | Mara |
| 35. | Usatwi wa Jamii | Ujenzi na upanuzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) | Mara |
| 36. | Maji | Usambazaji maji katika Manispaa ya Musoma na vijiji 21 vya Wilaya ya Butiama | Mara |
| 37. | Maji | Usambazaji maji wa Mugango - Kiabakari – Butiama | Mara |
| 38. | Utawala Bora | Ujenzi wa majengo mawili ya ghorofa tatu kwa ajili ya makazi ya askari polisi Manispaa ya Musoma | Mara |
| 39. | Viwanda | Kiwanda cha kuchakata kahawa cha Northern Highlands Coffee Company Limited - Tarime | Mara |
| 40. | Viwanda | Kiwanda cha Kusindika Alizeti – Rorya | Mara |
| 41. | Viwanda | Kiwanda cha Kuchakata Samaki Manispaa ya Musoma | Mara |
| 42. | Utawala Bora | Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Bunda | Mara |
| 43. | Utawala Bora | Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu | Simiyu |
| 44. | Kilimo | Mradi wa kudhibiti Sumukuvu - Itilima | Simiyu |
| 45. | Utawala Bora | Ujenzi wa nyumba mbili za makazi ya askari polisi Wilaya ya Meatu | Simiyu |
| 46. | Ujenzi | Ujenzi wa barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 121.9) | Simiyu |
| 47. | Viwanda | Ujenzi wa viwanda vya chaki na vifungashio katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa. | Simiyu |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 48. | Viwanda | Kuimarisha Uwezo wa Kituo cha Uendelezaji Teknolojia - SIDO | Lindi |
| 49. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Nachingwea - Liwale (km 130) | Lindi |
| 50. | Utawala Bora | Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama ya Wilaya Kilwa | Lindi |
| 51. | Utawala Bora | Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Ruangwa | Lindi |
| 52. | Maji | Ujenzi wa Miundombinu ya Maji katika Mitaa ya Cheleweni, Narunyu, Tandangongoro na Muungano katika Manispaa ya Lindi | Lindi |
| 53. | Maji | Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji Safi katika Mji wa Kilwa Masoko | Lindi |
| 54. | Kilimo | Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhi Mazao - RUANGWA | |
| 55. | Uvuvi | Ukarabati na upanuzi wa Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji - Nyengedi | Lindi |
| 56. | Viwanda | Ujenzi wa Majengo Mawili ya Viwanda Eneo la SIDO - Mtwara | Mtwara |
| 57. | Ujenzi | Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara; | Mtwara |
| 58. | Utawala Bora | Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Nanyumbu | |
| 59. | Maji | Mradi wa Maji Mwena - Liloya | Mtwara |
| 60. | Viwanda | Uendelezaji wa Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara (Mtwara Freeport Zone) | Mtwara |
| 61. | Uchukuzi | Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mtwara | Mtwara |
| 62. | Afya | Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini Mtwara | Mtwara |
| 63. | Viwanda | Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songea | Ruvuma |
| 64. | Ujenzi | Ujenzi wa Daraja la Ruhuhu na Barabara za Maingilio | Ruvuma |
| 65. | Maji | Mradi wa Maji wa Liparamba | Ruvuma |
| 66. | Maji | Mradi wa Maji Mkongo Gulioni - Nahimba | Ruvuma |
| 67. | Biashara | Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi Songea | Ruvuma |
| 68. | Nishati | Mradi wa Ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Msongo wa kV 220 Makambako - Songea | Ruvuma |
| 69. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya Kilindi | Tanga |
| 70. | Biashara | Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Kitega Uchumi katika Kituo cha Mabasi Kange | Tanga |
| 71. | Uchukuzi | Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Tanga | Tanga |
| 72. | Uchukuzi | Ununuzi na Ufungaji wa Mashine za Ukaguzi wa Mizigo ya Abiria (x – ray machine) katika Uwanja | Tanga |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| | | wa Ndege Tanga | |
| 73. | Ujenzi | Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 245) | Tanga |
| 74. | Uchukuzi | Mradi wa Ufufuaji wa Njia ya Reli ya Tanga - Arusha (km 437) | Tanga |
| 75. | Utawala Bora | Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Wavulana Awamu ya Tatu Katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto | Tanga |
| 76. | Kilimo | Mradi wa Shamba la Kuzalisha Mbegu za Chikichi Mwele - Tanga | Tanga |
| 77. | Viwanda | Kiwanda cha Kusindika Majani ya Chai - Lushoto | Tanga |
| 78. | Viwanda | Mradi wa Ukarabati wa Kiwanda cha Kuchakata Tangawizi | Tanga |
| 79. | Biashara | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Kimataifa Moshi | Kilimanjaro |
| 80. | Elimu | Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Ushirika Moshi | Kilimanjaro |
| 81. | Viwanda | Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Bidhaa Ngozi cha Kilimanjaro | Kilimanjaro |
| 82. | Viwanda | Mradi wa Kufufua Kiwanda ha KMTC | Kilimanjaro |
| 83. | Ujenzi | Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) | Kilimanjaro |
| 84. | Afya | Mradi wa Ujenzi wa Maabara Daraja la Tatu katika Hospitali ya Kibong’oto | Kilimanjaro |
| 85. | Maji | Ujenzi wa Bwawa la Maji katika Kijiji cha Ikozi; | Rukwa |
| 86. | Maji | Mradi wa Maji - Sakalilo | |
| 87. | Maji | Ujenzi wa Miundombinu ya Maji - Mpasa | Rukwa |
| 88. | Maji | Mradi wa Maji Muze - Group | Rukwa |
| 89. | Utawala Bora | Ujenzi na Ukarabati wa Mahakama Kuu ya Sumbawanga | Rukwa |
| 90. | Nishjati | Kusambaza Umeme Vijijini Mkoa wa Rukwa – REA III | Rukwa |
| 91. | Maji | Mradi wa Maji Ikolongo II | Katavi |
| 92. | Maji | Mradi wa Maji Manga na Kasokola | Katavi |
| 93. | Elimu | Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wa Kike wa Shule ya Sekondari Sitalike katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo | Katavi |
| 94. | Uchukuzi | Ukarabati wa Njia ya Reli wa Kati (Kaliua - Mpanda) | Katavi |
| 95. | Ujenzi | Ujenzi wa Barabara ya Tabora - Koga – Mpanda (km 321.4) | Katavi |
| 96. | Ujenzi | Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 517.4) | Katavi |

| NA. | SEKTA | JINA LA MRADI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 97. | Maji | Ujenzi wa Bwawa la Maji - Wanging'ombe | Njombe |
| 98. | Maji | Ujenzi wa Mradi wa Maji Igando – Kijombe, Wanging'ombe | |
| 99. | Maji | Mradi wa Maji Kidegembye | Njombe |
| 100. | Utawala Bora | Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya Njombe | Njombe |
| 101. | Utawala Bora | Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya Wanging'ombe | Njombe |
| 102. | Afya | Ujenzi na Upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe. | Njombe |
| 103. | Nishati | Mradi wa Kufua Umeme Julius Nyerere MW 2,115 | Pwani |
| 104. | Uchukuzi | Ujenzi wa Reli ya Kati kwa *Standard Gauge* | Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza |
| 105. | Elimu | Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO 19 (Tanzania Covid Relief Plan - TCRP) - Vyumba vya madarasa | Mikoa yote Tanzania Bara |